Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 27 Juni, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 120

**Elimu ya Maumbile na Afya ya Uzazi Itolewe Darasani**

**MHE. HALIMA O. KIMBAU (k.n.y. MHE RHODA L. KAHATANO)** aliuliza:-

Kwa kuwa fahari ya nchi yoyote ile ikiwemo Tanzania ni pamoja na kuwa na vijana wenye afya njema na elimu ya kutosha itakayowawezesha kujitegemea na kwa kuwa kumekuwa na taarifa mbalimbali za vyombo vya habari juu ya vijana wanavyoathirika na magonjwa yatokanayo na ngono zisizo salama katika umri mdogo licha ya jitihada za Serikali kuhimiza matumizi ya kondomu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha elimu ya maumbile na afya ya uzazi kwa vijana wenye umri wa kuanzia miaka 9 - 20 ili waweze kuyaelewa mabadiliko yao, elimu itakayowasaidia kujizuia hasa wanapohisi hamu ya tendo la ngono wakumbuke waliyofundishwa darasani badala ya kusikia tu kwenye vyombo vya habari?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Rhoda Kahatano, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafanya juhudi ya kutoa elimu bora kwa kila Mtanzania, ili kumwezesha kila anayeipata aweze kumudu maisha anapomaliza shule. Kuhusu elimu ya maumbile na afya ya uzazi, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Idadi ya Watu *(UNFPA)*, inatoa mafunzo ya elimu ya familia. Aidha, Wizara yangu inachukua hatua zifuatazo:-

- Kuingiza elimu dhidi ya ukimwi katika mitaala ya elimu msingi, sekondari na vyuo;

- Kuingiza mada za elimu ya familia katika masomo ya maarifa ya jamii na sayansi katika shule za msingi na *Biology*, *Geography*, *Civics* na *Home Economics* kwa shule za sekondari na vyuo;

- Kutoa mafunzo kwa wakufunzi na walimu wa shule za sekondari ili wafundishe masomo chukuzi kwa kuzingatia elimu ya familia;

- Kuendesha warsha za elimu dhidi ya ukimwi kwa wakaguzi wa shule, walimu wa shule za sekondari na shule za msingi;

- Kutoa na kusambaza vitabu vya elimu ya familia;

- Kuanzisha kamati za malezi na ushauri katika shule zote za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu;

- Kuandaa na kutoa mwongozo wa malezi, mafunzo na ushauri nasaha kwa wanafunzi na wakufunzi; na

- Kuendesha warsha ya Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya kuhusu malezi na ushauri.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zimechukuliwa kwa lengo la kumwezesha kijana kufanya uamuzi wa busara na hivyo kulinda afya yake na kuepuka maambukizi ya magonjwa yatokanayo na ngono.

Na. 121

**Kuwepo kwa Chombo cha Walimu cha Majadiliano na Waajiri**

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA** aliuliza:

Kwa kuwa kazi ya walimu ni nyeti sana katika nyanja zote za maendeleo; na kwa kuwa asilimia 49 ya watumishi wa Serikali ni walimu; na kwa kuwa walimu wanazo sifa za kupewa chombo chao cha majadiliano *(Negotiation Machinery)* na waajiri wao juu ya maslahi yao; je, ni lini sasa watapatiwa chombo hicho badala ya kuendelea kugandamizwa na waajiri wao kwa mishahara midogo bila kuwa na uwezo wa kujitetea?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwalimu Faustine Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uchambuzi wa kina kuhusu utaratibu wa majadiliano ya pamoja na watumishi wake. Uchambuzi huo umebainisha kuwa Sheria Na. 52 ya mwaka 1962, inayohusu chombo cha majadiliano (*Negotiating Machinery)*, baina ya Serikali na Watumishi inayosimamiwa na Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi, haishirikishi makundi yote ya watumishi. Serikali sasa imeandaa utaratibu mpya wa ushirikishwaji wa makundi yote ya watumishi, ikiwa ni pamoja na kundi la walimu. Kwa hiyo, Muswada umeandaliwa ambao utawasilishwa Bungeni muda wowote kuanzia sasa kwa lengo la kufanyia marekebisho Sheria Na. 52 ya mwaka 1962, ili iweze kukidhi matakwa ya walimu ambao awali sheria hiyo haikuwahusu.

Muswada wa marekebisho ya sheria hiyo utakapopitishwa, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi, itakuwa tayari kuyapokea na kuyafanyia uchambuzi mapendekezo yatakayoletwa na walimu kama kundi mojawapo la utumishi wa umma kuhusu uwezekano wa wao kuwa na chombo cha kundi lao peke yao, cha majadiliano na waajiri wao juu ya maslahi yao. Hata hivyo, napenda nilimalizie kujibu swali hili kwa kufafanua kuwa walimu wana uwezo wa kujitetea kupitia chama chao huru cha wafanyakazi kiitwacho Chama cha Walimu Tanzania *(CWT)*. Kwa hiyo, suala la kugandamizwa halipo.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Kwa kuwa Miswada mingi mara nyingi inapoandaliwa inakuwa imeegemea sana upande wa Serikali. Je, ili kuondoa *biasness* ni kiasi gani Chama cha Walimu Tanzania kinashirikishwa katika kuandaa Muswada huo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kusema kweli haitakuwa na ugumu wowote wa kuwashirikisha walimu. Siku hizi katika taratibu zetu kuna uwezekano kabisa katika ngazi ya Kamati, kualika kundi lolote kuweza kuwa na mjadala. Kwa hiyo, kama walimu wangependa

kuwa na mjadala katika hatua za kupitisha Muswada huo katika ngazi hiyo ya Kamati ambapo fursa hiyo hutolewa, mimi nina hakika haja hiyo inaweza kutekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa iko kero sugu katika nchi nzima na hasa katika shule za sekondari, walimu wapya kukosa mishahara karibu miezi sita na mifano ninayo na majina ninaweza nikayataja. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa tatizo la walimu hawa ambao mishahara ni haki yao, ili waweze kupata mishahara mara tu wanapoajiriwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, tatizo hili la kuchelewa kulipa mishahara Serikali tunalifahamu na tunafanya jitihada kuhakikisha kwamba ule muda unapungua. Ni katika taratibu kwamba kuna mambo yanayotakiwa yamitizwe kabla jina halijaingia katika orodha ya mishahara. Kwa hiyo, tatizo nakubali lipo, lakini tunaweka kila aina ya jitihada kulighulikia ili walimu wasisubiri muda mrefu kuanza kulipwa mishahara yao.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika nchi nyingi zilizoendelea huajili walimu wale ambao wana vipaji maalum ili watoe elimu bora kwa watoto wao katika nchi na kwa kuwa katika nchi yetu tunaita ualimu ni wito. Je, si njia ya kuhalalisha kutoa malipo duni kwa walimu na haipunguzi uzuri wa elimu hapa nchini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba katika kujibu swali hili nikubaliane na Profesa Maghembe, Mbunge wa Mwanga kwamba, ualimu ni kazi ya wito na tukitaka walimu wetu wafanye kazi nzuri tunahitaji kuwalipa mishahara. Lakini lazima tuelewe kwamba, huwezi ukalichukua kundi la walimu peke yake tofauti na watumishi wa umma kwa ujumla. Kwa hiyo, Serikali inajitahidi kuangalia mishahara ya wafanyakazi wote wakiwemo walimu, waweze kulipwa mishahara inayowavutia na waweze kufanya kazi vizuri. Nilikwishawahi kusema hapa kwamba, Serikali ilikuwa katika zoezi la kuitazama upya mishahara ambayo inajulikana kwamba iko chini mno. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, awe na subira kadri Bajeti inavyoendelea pengine tutakuwa maelezo ya ziada. *(Makofi)*

Na. 122

**Ajali za Barabarani**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa ajali nyingi za barabarani zikiwemo ajali za magari ya abiria zinatokana na sababu nyingi ikiwa ni pamoja na mwendo wa kasi kwa madreva wengi; na kwa kuwa Serikali ilikwisha endesha zoezi kamambe la kufunga *speed governors* kwa magari yote ya abiria; na kwa kuwa magari hayo hayakuchukua muda mrefu yakarudia mwendo wa kasi bila kujali roho za Watanzania wanaokuwemo ndani ya magari hayo; je, Serikali ina mpango gani wa kukagua magari hayo kuona kuwa hizo *speed governors* kama zinafanya kazi yake au zimefunguliwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba, ajali nyingi za barabarani ikiwa ni pamoja na za mabasi ya abiria husababishwa na sababu nyingi mojawapo ikiwa ni mwendo wa kasi. Serikali inalijua tatizo hili na ndiyo maana ilianzisha hatua za kufunga vidhibiti mwendo kwenye mabasi na kutunga Sheria ya Vidhibiti Mwendo iliyoanza kutumika Aprili, 1997. Madhumuni ya kufunga vidhibiti mwendo katika mabasi ni kuyafanya mabasi haya yasizidi mwendo wa kasi wa km 80 kwa saa. Mara baada ya vidhibiti mwendo kufungwa katika mabasi na Sheria ya Vidhibiti Mwendo kuanza kutumika, tatizo lilianza kujitokeza kwa baadhi ya wamiliki wa mabasi na madreva kuanza kuvilegeza au

kuviharibu vidhibiti mwendo na mabasi haya yakaanza kwenda kwa mwendo wa kasi zaidi ya km 80 kwa saa.

Mara baada ya Serikali kugundua zoezi hili, ilichukua hatua za kuendesha zoezi la ukaguzi wa mara kwa mara kwa mabasi ya abiria ili kuona kama mabasi hayo yamefungwa vidhibiti mwendo na vinafanya kazi. Ukaguzi huo hufanywa kwenye kituo cha mabasi kabla basi halijaanza safari au katika *check points* au katika sehemu zingine za kuvizia. Kutokana na ukaguzi huo, kati ya Aprili, 1997 na Aprili, 1998 mabasi 1,002 yalikamatwa na kati ya Januari, 2002 na Juni 2002 mabasi 238 yalikamatwa kutokana na kuharibu vidhibiti mwendo.

Mheshimiwa Spika, wamiliki na madreva wa mabasi yanayokamatwa kwa kosa la kuharibu vidhibiti mwendo, wanachukuliwa hatua za kisheria kwa kutozwa faini ya shilingi 20,000/= kwa kila kosa. Taarifa za wahalifu wa mabasi hayo hupelekwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kupitia Mamlaka Kuu ya Leseni za Usafirishaji, ili Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi akiona inafaa, aweze kuchukua hatua nyingine ikiwa ni pamoja na kufuta au kusimamisha kwa muda leseni za usafirishaji kwa manufaa ya umma kutokana na mamlaka aliyopewa kisheria. Kwa kuwa adhabu ya faini ya shilingi 20,000/= ni ndogo sana kwa kosa la kuharibu vidhibiti mwendo, Wizara yangu imependekeza kwa mamlaka husika kwamba, adhabu ya faini iongezwe hadi 150,000/= kwa kila kosa. Aidha, Serikali itaendelea kwa nguvu zote na zoezi la ukaguzi wa mabasi wa mara kwa mara na kisha kuwachukulia hatua wote wanaobainika kuviharibu vidhibiti mwendo. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa inafahamika wazi kwamba madreva wengi wameharibu vidhibiti mwendo na kwa kuwa wanaostahili kufuatilia mienendo ya madereva ni askari wa usalama barabarani. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu kila Mkoa kuwa na vyombo vya kupima mwendo wa magari barabarani kuliko ilivyo sasa ni Mikoa michache tu, maaskari wa usalama barabarani wanavyo hivyo vyombo kwa mfano Mkoa wa Pwani tu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hivi sasa vifaa vya kupimia kasi ya mwendo (*Speed Radar),* vipo katika barabara kuu na huku kusema kweli ndiko kwenye *speed* kali kuliko barabara zingine hasa kule sehemu anakotoka Mheshimiwa Diana Chilolo na mimi, ambapo barabara zenyewe jinsi zilivyo tayari ni *speed governor.* Hata hivyo, katika Bajeti ambayo wiki chache zijazo tutaomba muipitishe, tumeongeza vifaa kama hivi katika maeneo yale ambayo hasa *speed* ni kali na vile vile vifaa hata vya kupima ulevi kwa sababu baadhi ya ajali zinatokana na watu ambao wanakunywa pombe halafu wanaendesha magari. Sheria inasema ukinywa pombe usiendeshe gari. Kwa hiyo, vile vile tutaongeza vifaa vya *speed radar*. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Je, kulewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Hapana hata kunywa, siyo kulewa tu. Kwa hiyo, tutaongeza *speed radars*, tutaongeza vile vile na vifaa vya kupimia *alcohol* na tutavisambaza nchi nzima ili tuweze kupambana na madreva wanaokunywa pombe halafu wanaendesha magari na kusababisha ajali. *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa imethibitika wazi kwamba kuongeza ukali wa adhabu wakati mwingine hakusaidii kupunguza idadi ya makosa. Lakini pia sheria ile inatamka kwamba mwendo wa mwisho wa mabasi ni km 80 kwa saa, mwendo ambao kwa kweli ni mdogo sana kutokana na hatua za Serikali za kuboresha barabara.

Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu wa kubadilisha kiwango cha chini cha mwendo wa mabasi angalau kifikie km 100 kwa saa ili wavunjaji wa sheria wasiwe wengi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Malangalila kwamba, wakati mwingine ukali wa udhabu unawezekana usiwe dawa, lakini kwa hili la shilingi 20,000/= kwa tajiri wa mabasi, nadhani ni hela ndogo mno kiasi ambacho wanaona kwamba watazilipa tu wakati wowote. Kwa hiyo, kwa hili ningependa kushawishi Bunge kwamba, tukileta pendekezo hili tulikubali ili waone uchungu kidogo kwa kufanya kosa hili.

Kuhusu kuongeza kasi ya mwendo kutoka km 80 kwenda 100 kwa saa, kwanza km 80 kwa saa hatuko mbali sana hata katika nchi zilizoendelea, nchi nyingi zilizoendelea ziko kati ya km 80 na km 100 kwa saa. Lakini hata hivyo, kama hoja hii ikija nafikiri inazungumzika. *(Makofi)*

Na. 123

**Tatizo la Ajira kwa Vijana**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua juhudi gani za makusudi za kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu ili waepukane na uzururaji na hatimaye wapate shughuli za kufanya na kukuza sekta ya uzalishaji?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kama ifuatavyo:-

Ili kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana, Serikali imekwisha chukua hatua mbalimbali ambazo zitasaidia kupanua ajira kwa vijana ili hatimaye waondokane na uzururaji. Moja ya hatua ambazo Serikali imekwishazichukua ni pamoja na kuwaelimisha na kuwahamasisha vijana ili waweze kujiunga katika vikundi vyao vya ushirika na uzalishaji mali ili kurahisisha utoaji wa elimu na stadi za kazi na pia kutilia mkazo ajira binafsi, ambayo inaweza kuwaajiri vijana wengi zaidi katika shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji, ufundi na kadhalika. Serikali itakuwa karibu na Halmashauri, Manispaa na Jiji ili kuhakikisha kuwa sehemu ya mapato yanatumika katika kutunisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kuanzisha rasmi Mfuko wa Maendeleo ya Vijana *(Youth Development Revolving Fund)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendeleza ushirikiano wa karibu na taasisi zisizo za Kiserikali, pamoja na wadau mbalimbali wakiwemo vijana wenyewe kuweza kuainisha matatizo na njia za ufumbuzi wa matatizo ya vijana ikiwa ni pamoja na kukamilisha uundaji wa Baraza la Vijana Tanzania, ambalo kimsingi litawezesha vijana kupanga, kutekeleza na kutathmini shughuli zao mbalimbali zikiwemo za kijamii, kiutamaduni na kiuchumi.

Aidha, kwa sasa Wizara imekuwa karibu sana Taasisi za Vijana na wadau wengine ili kwa pamoja kuweza kushirikiana katika kupambana na matatizo yanayowakabili vijana.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba vijana hawana ajira na Serikali inafanya mpango wa kuhakikisha kwamba wanakuwa na shughuli za kufanya. Kwa kuwa kuna Mikoa ambayo vijana wengi wanatoka vijijini kwenda Mjini na hasa vijana wa kike ukiwemo Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Singida na Mkoa wa Arusha. Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi za kuweza kuweka mikakati ya kusaidia mikoa hii ili vijana wasiondoke kwenye mikoa hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, jukumu la kuelimisha vijana pamoja na wazazi kwamba mijini wanakokimbilia hakuna neema ila balaa ni jukumu la kila mmoja wetu, tukiwemo na sisi na Waheshimiwa Wabunge. Ni bahati mbaya sana kwamba tumefikia mahali sasa hivi kuamini kwamba, Mkoa fulani hutoa wafanyakazi wa ndani mijini, Mkoa fulani ni maarufu labda wa kutembeza bakuli barabarani, hii ni tabia ambayo siyo ya kuiendekeza na

ingefaa kupigwa vita na sisi sote kama Viongozi, Mashirika ya Dini na wazazi wenyewe. Ninaomba kutoa rai kwa Viongozi mbalimbali, Mashirika ya Dini na *NGOs* kwamba, wakati huu tunapopambana na ajira mbaya kwa watoto zikiwemo za majumbani, basi ni muhimu kila mmoja wetu kutambua kwamba, haki ya watoto kwanza ni kuwapatia elimu na siyo kuwakimbizia mijini kwenda kufanya kazi ambazo zinadhalilisha jinsia, vile zinadhalilisha na utu. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa asilimia 70 ya nguvu kazi inatokana na vijana, je, Serikali ipo tayari kujenga Vyuo vya *VETA* kwa kila mkoa ili vijana wapate elimu ya kujitegemea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo nia ya Serikali kuhakikisha kwamba, kila mkoa unapata Chuo cha *VETA*, ndiyo hivi sasa tupo Kigoma, tunatarajia mwakani kumaliza ujenzi huo. Tunatarajia baada ya hapo kuelekea Mkoa wa Lindi. Mkoani Mara tunatanua sasa kile chuo. Kwa hiyo, ndiyo sera yenyewe ya Wizara kuhakikisha kwamba, kila Mkoa unapata chuo. Lakini bado tuwapongeze taasisi binafsi ambazo bila kujali kama Mkoa huo una Chuo cha *VETA*, wao wanaendelea kujenga na kuimarisha zaidi vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi na sisi kama Serikali huwa tunatenga fungu maalum kupitia Mamlaka ya *VETA*, kusaidia vifaa lakini vile vile na elimu kwa walimu wa vyuo hivyo binafsi. *(Makofi)*

Na. 124

**Kuendeleza Michezo**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA (k.n.y. MHE. VENANCE M. MWAMOTO)** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingi za Afrika kama vile Ghana, Nigeria, Cameroon, Gabon na kadhalika zinajipatia fedha nyingi kwa njia ya michezo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga uwanja wa kisasa wa michezo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mpira wa kulipwa?

(c) Je, katika mwaka wa fedha wa 1999/2000 Serikali ilitenga kiasi gani cha fedha katika kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kujenga uwanja wa kiasi wa michezo na tayari imekwishatiliana sahihi na msimamizi na mshauri wa ujenzi wa uwanja huo. Hivi sasa taratibu zinaendelea za kumpata mjenzi wa uwanja huo. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza Novemba, 2003 na kumalizika Mei, 2005.

(b) Serikali kupitia Sera ya Maendeleo ya Michezo 1995, imeruhusu kuwepo kwa michezo ya kulipwa na Wizara yangu inaendelea kuhamasisha watu binafsi, vilabu na vyama vya michezo yote kuendesha shughuli za michezo ya kulipwa kwa lengo la kuinua kiwango cha michezo. Hata hivyo, mchezo pekee ambao hivi sasa umeanzisha Chama cha aina hiyo ni mchezo wa ngumi. Bado hazijaanzishwa klabu za kulipwa katika mpira wa miguu. Serikali inatoa wito kwa vilabu vyote vya michezo kuunda klabu za kulipwa kwa kuzingatia Sera ya Maendeleo ya Michezo ya 1995 ili kuendeleza michezo nchini.

(c) Katika mwaka wa fedha wa 1999/2000, Wizara yangu ilitumia kiasi cha shilingi 101,743,000/= kwa ajili ya kuendeleza michezo. Wizara haitengi fedha kwa ajili ya mchezo mmoja mmoja bali inatenga kwa ajili ya maendeleo ya michezo kwa jumla.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa vurugu zinazoendelea kwenye vilabu mbalimbali zinapelekea kuyumba kwa michezo:-

(a) Je, Serikali inaweza kufanya lolote kupunguza vurugu hizo?

(b) Kwa kuwa nchi nyingi za kiafrika zilizoonyesha kufanya vizuri katika mpira wa miguu ni kwa sababu ya wachezaji wake ambao huuzwa nje na baadaye kurudi kuimarisha timu za Taifa. Je, Wizara inafikiri inaweza ikafanya lolote kuweza ku-*promote* wachazaji wetu wazuri wakaenda nje na baadaye wakarudi kuweza kuziimarisha timu zetu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunakuwa na misukosuko ya vurugu ndani ya vilabu vyetu hasa vinavyoshiriki *Vodacom League.* Lakini vurugu hizi zingeweza kupatiwa ufumbuzi kama kichwa kinachosimamia vilabu hivi chenyewe kingekuwa kimetulia. Lakini kwa bahati mbaya kichwa hakijatulia kwa hiyo, si ajabu sana kuona na mabega na miguu nayo inayumba hivyo hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

(a) Kwa hiyo, Serikali kwamba tunafanya nini kutuliza vurugu hizo kwenye vilabu? Tunajitahidi sisi pamoja na BMT, kujaribu kukaa na hawa watu kuwaambia madhara ya mwenendo wao, lakini kwa bahati mbaya sana watu wametanguliza mno ubinafsi kuliko maslahi ya mchezo wenyewe. *(Makofi)*

(b) Wachezaji tunafanya nini kuwa-*promote* ili kwenda nje? Unaweza ku-*promote* biashara nyingine yoyote kupitia vyombo vya habari kama vile *television* na magazeti, lakini mchezaji lazima aende mwenyewe *physically.* Njia pekee ya kumtangaza mchezaji labda tunatarajia kupitia *Simba Sports Club*, ambayo kama wataweza kufanya vizuri wakaingia kwenye fainali za Kombe la Afrika, wale wanaochukua wachezaji kutoka nje ya Bara hili wanaweza wakawaona na kuwachukua. Lakini namna nyingine kwa kucheza mpira wa *Vodacom*, Uwanja wa Jamhuri, Uwanja wa Kariokoo, hatuwezi tukapata wachezaji wa kwenda nje. Kwa hiyo, naomba uongozi wa vilabu mbalimbali nchini, wajue kwamba umuhimu wa ku-*promote* wachezaji wetu ni kuhakikisha tunaleta utulivu ndani ya vilabu ili wachazaji hao waweze kushiriki katika makombe ya Afrika ili waonekane na waajiriwe Bara la Ulaya na sehemu nyingine Duniani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kuzingatia muda. Mheshimiwa Waziri wa Michezo ya Simba. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa niongezee kidogo kuhusu namna ambavyo tunaweza tukasaidiana kushughulikia vurugu za michezo zilizoko katika vilabu na hususan katika michezo fulani fulani ambayo inatokea kupendwa sana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la vurugu katika vilabu linahitaji nguvu za pamoja hasa kutoka kwa Wabunge kwa sababu wanaowachagua wale viongozi wa Kitaifa wanatoka Mikoani kwetu. Kama sisi Wabunge tukilivalia njuga huko huko Mikoani kwetu kwa kuwaambia Wawakilishi wanaokuja kupiga kura huku kwamba kataeni rushwa, mimi nina hakika tutapata viongozi wa Kitaifa wa vilabu wazuri. *(Makofi)*

Lakini vile vile kwa sababu kwa bahati nzuri Wakuu wa Mikoa wako hapa, wao kule ni wasimamizi wakubwa kupitia Ma-*RAS* kwa Kamati za Michezo za Mikoa na hao nao watusaidie sana kupambana na rushwa zinazojitokeza huko ili wawakilishi wao wanapofika katika ngazi ya Kitaifa wachague viongozi wa vilabu au viongozi wa Vyama vya Kitaifa wa Michezo wanaokuwa na malengo ya kuendeleza michezo badala ya kusimamia ubinafsi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Na.125

**Kujihami na Uhaba wa Chakula**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2002/2003 Serikali ilitenga fungu maalum la kuinua Sekta ya Kilimo na katika kujibu swali Na.67 katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge Serikali ilifafanua kuwa fungu hilo pamoja na mambo mengine lilitumika kununulia chakula cha Hifadhi ya Taifa:-

Je, ni kiasi gani cha mazao kilinunuliwa katika lengo la kujihami na upungufu wa chakula ambao unaweza kuikumba nchi yetu kwa msimu wa mwaka 2003/2004?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2002/2003 Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilitengewa shilingi bilioni 4.63 zilizotumika kununua mahindi tani 28,475 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.82, kutoka kwa wakulima wa hapa nchini. Kiasi hicho cha mahindi kilichonunulia mwaka 2002/2003, kilifanya Hifadhi ya Chakula ya Taifa kuwa na akiba ya tani 75,522. Aidha, shilingi bilioni 1.29 zilitumika kununua vifaa vya kutunzia akiba, uendeshaji na usimamizi.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri na mafupi kabisa ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza swali dogo kutokana na jibu kwamba; Je, tani hizi 75,000 zinaweza zikakidhi mahitaji ya chakula ambayo yameanza kujionyesha kwa msimu huu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, haitaweza kukidhi mahitaji yote yanayojitokeza sasa hivi. Serikali imechukua tahadhari mbalimbali, mojawapo ni kwanza kuhamasisha wananchi kuingia mabondeni kulima chakula kusudi waweze kuzalisha chakula kwa muda mfupi ujao.

Pili, tumejitahidi katika mashamba yetu ya *NAFCO* kuagiza nao walime kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji.

Tatu, tumehamasisha Makampumi binafsi yaingize chakula. Kwa mfano wakati wa mwezi Mei, *Export Trading Company* imeingiza tani 750 za mahindi na yamepelekwa Lindi na sasa hivi yanasambazwa katika Wilaya ya Kilwa na Wilaya ya Ruangwa na bado kuna Makampuni nane yanashirikishwa katika kuagiza vyakula, tunategemea nao wataagiza kama tani zipatazo 580,500. Tunafikiri kwa jitihada hizi zote itasaidia.

Hapo hapo tungependa kukumbusha kuwa maeneo yote ambayo wamejishughulisha na kuhimiza kilimo cha muhogo hawajaathirika. Hivyo napenda kutoa wito kuwa tukazane kuhimiza kilimo cha muhogo nchini. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kweli kuwa hali ya chakula mwaka huu ni mbaya ikiwa ni pamoja na Wilayani Kongwa na amesema kwamba ziko tani 75,000 kwenye Akiba ya Chakula ya Taifa. Sasa swali langu ni kwamba; je, chakula hicho kitawafikiaje wananchi hasa wasiojiweza, wazee, wagonjwa na wengine wa makundi maalum? Kwa kununua, kwa kufanya kazi au watapewa bure au kuna utaratibu gani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, yote haya yatatumika. Kama alivyosema Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ni kwamba sasa hivi, tuseme katika wiki ijayo inatumwa timu mpya kufanya tathmini upya nchini kote. Hivyo, tathmini itatupa jibu la kina kuhusu mahitaji ya karibuni hivi. Kutokana na hilo tutajua nani wanahitaji chakula cha bure na nani watabidi wauze mifugo na wengine inawezekana wakapewa bure. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ulikuwa hujasimama. Sasa nimekuona. Mheshimiwa Christopher Wegga. *(Kicheko)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona kama nimesimama. Naomba tu kuuliza swali moja dogo.

Kwa kuwa katika Jimbo la Mikumi kuna miradi miwili ya umwagiliaji ambayo sasa bado ni hai na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, alishaitembelea Malolo na *Kilangali Farm;* je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kupeleka nguvu zote pale wakalime yale mashamba kwa sababu kuna umwagiliaji ili tuepushe njaa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Christopher Wegga, kwamba tutajitahidi au tumeagiza mashamba yote kuotesha chakula kukabiliana na tatizo lililojitokeza na sio hilo la Mikumi tu, ni mashamba yote pamoja na Ruvu na yale yote yaliyopo Mbeya, mashamba yote ya *NAFCO* yajitahidi kukabiliana na tatizo hili la njaa nchi nzima. *(Makofi)*

Na.126

**Madai ya Wafanyakazi wa Mashamba**

**MHE. MUSA A. LUPATU** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo na Chakula alipotembelea mashamba ya Chai ya Balangai/Dindira na Ambangulu Wilayani Korogwe mwaka wa 2002 alielezwa juu ya kuwa na madeni makubwa wanayodai wafanyakazi wa mashamba hayo na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alijionea mwenyewe jinsi shamba la Balangai/Dindira lilivyotelekezwa na mmiliki wa shamba hili ambaye yuko nje ya nchi:-

(a) Kwa kuwa Meneja Mkuu Mkazi anayesimamia Kampuni inayomiliki mashamba hayo aliahidi kulipa madeni ya wafanyakazi na kuyamaliza katika kipindi cha miezi 12 na kwa kuwa ahadi hiyo haijatimizwa na wala hakuna dalili yoyote ya kufanya hivyo; je, Serikali inachukua hatua gani kwa mwekezaji huyo ili wafanyakazi husika walipwe madai yao?

(b) Je, kwa nini Serikali imekaa kimya bila kuingilia kati utendaji mbovu na wa dhuluma unaofanywa na mwekezaji huyo asiye na huruma kwa wafanyakazi wake?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kulitwaa shamba hilo na kuwagawia wananchi wa Kata ya Dindira?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musa Lupatu, Mbunge wa Korogwe Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba ahadi ya kulipa madeni ya wafanyakazi wa shamba la Balangai/Dindira haijatekelezwa kama ilivyoahidiwa. Serikali, imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kikao cha pamoja kati ya Mbunge wa Korogwe Magharibi, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mbunge wa Rungwe Magharibi, Uongozi wa Bodi ya Chai na Meneja Mkuu wa Kampuni ya *George Williams (T) Limited* kilifanyika tarehe 31 Mei,2002. Katika kikao hicho matatizo yanayokabili mashamba ya mwekezaji huyo yalijadiliwa kwa kina.

(ii) Mwezi Oktoba 2002 mtaalam kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula alitumwa kufuatilia na kutathmini kero za wafanyakazi wa mashamba ya Dindira na Balangai. Ufuatiliaji huo ulibaini kuwepo kwa madai ya malimbikizo ya mishahara ya kuanzia Januari, 2000 hadi Julai 2002 yenye thamani ya shilingi milioni 81.9.

(iii) Meneja wa mashamba ya *George Williamson* aliitwa Wizarani tarehe 31 Desemba, 2002 na kuonana na Naibu Waziri ili kutoa taarifa kuhusu maendeleo yaliyofikiwa katika kutatua matatizo ya

wafanyakazi wa Balangai/Dindira. Mahojiano na Kampuni ya *George Williamson* yalidhihirisha kuwa tatizo hili halikupatiwa ufumbuzi hadi wakati huo. Aidha, Meneja huyo aliahidi kwamba kufikia mwishoni mwa mwezi wa Juni, 2003 atakuwa amelipa malimbikizo ya mishahara na madai yake yote yaliyokuwa wakati huo.

(b) Kwa mtiririko wa hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Wizara hadi sasa, ni dhahiri kwamba Serikali inayashughulikia matatizo ya shamba hilo ili mgogoro uliopo umalizike na wafanyakazi walipwe haki zao ifikapo mwishoni mwa mwezi Mei mwaka 2003 kulingana na ahadi zilizotolewa. Iwapo hadi wakati huo Meneja huyo atakuwa hajalipa malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi hao, watashauriwa kuchukua hatua za kisheria dhidi yake.

(c) Suala la Serikali kulitwaa shamba la Balangai/Dindira kwa sasa na kuligawa kwa wananchi wa Dindira sio jawabu mbadala la kutatua matatizo yaliyopo. Iwapo mwekezaji wa shamba hilo ataendelea kutoliendeleza kwa mujibu wa masharti ya hatimiliki, itabidi hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake. Uamuzi juu ya matumizi ya baadaye ya shamba hilo utategemea matokeo ya hatua za kisheria zitakazochukuliwa.

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba bado yapo malimbikizo na hakuna hatua kutoka kwa mwekezaji; je, Serikali itakubaliana nami kwamba ni wakati muafaka kutoa kibali ili wafanyakazi waliopo waweze kumiliki shamba hilo kwa muda mpaka watakapoweza kujilipa mishahara yao?

Pili, kwa kuwa kazi kubwa ya mwekezaji huyu ni kuhamisha raslimali fedha kwenda Ulaya na hivyo kuikosesha mapato Serikali; je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu ufisadi huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, natambua haya yote aliyoeleza Mheshimiwa Musa Lupatu, lakini kama nilivyosema ni kwamba yote haya yatategemea ahadi zilizotolewa hadi mwisho wa mwezi huu. Hatuwezi kuchukua hatua yoyote sasa hivi mpaka muda utakapoisha ambayo ni tarehe 30 Jumatatu ijayo. Kutoka hapo tutaweza kuchukua hatua vilivyo. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa chai inapokaa kwa muda mrefu bila kuchumwa au kukatwa inakuwa ni pori; je, Waziri haoni kwamba lile shamba la Balangai lililoko katika Jimbo la Bumbuli na Dindira katika Jimbo la Korogwe Magharibi, yatakuwa mapori na hivyo tutapoteza chai ile? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tunatambua hilo. Hata hivyo lile shamba ni la mtu binafsi, sio shamba la Shirika la Umma *(SU)*. Hivyo hatuwezi kuingilia moja kwa moja. Lakini kwa kuwa tunajali sana masuala yote ya uchumi na masuala ya wananchi ndio maana tumelishughulikia kwa karibu sana na ninaamini kuanzia Jumatatu tutajua la kufanya. *(Makofi)*

Na.127

**Umeme Iyula**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme sio anasa Tanzania bali ni kwa maendeleo na kukabiliana na umasikini hasa Vijijini na kwa kuwa Kijiji cha Iyula kilikubalika na *TANESCO* kupelekewa umeme:-

(a) Je, ni nini kinachozuia umeme usifikishwe Iyula wakati upimaji tayari na nguzo zimelundikwa njiani bila kutumika?

(b) Je, kama *TANESCO* ililundika nguzo tu bila maandailizi mengine, haoni hali hii ni kuwakatisha tamaa wananchi kwa kebehi?

(c) Je, kama mchwa watakula nguzo hizo zilizolundikwa, nani alaumiwe kwa hasara itakayotokea?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edson Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kusimamisha nguzo katika Kijiji cha Iyula imeshaanza na inaendelea vizuri ili kukipatia umeme Kijiji cha Iyula.

*TANESCO* ililundika nguzo katika maeneo mbalimbali kwenye njia ya umeme kwenda Kijiji cha Iyula yakiwa maandalizi ya awali na baada ya kukamilika kazi ya kupima njia ya umeme, kazi ya kusimika nguzo ilianza na bado inaendelea. Mradi huu utaendelea kutekelzwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nguzo zinazotumiwa na *TANESCO* zimewekwa dawa za kuzuia madhara ya wadudu waharibifu wakiwemo mchwa. Hata hivyo kwa kuwa nguzo hizi sasa zimeanza kusimikwa katika njia ya umeme hakuna matarajio tena kwamba nguzo hizo zitaliwa na mchwa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa imeonekana katika Wilaya ya Mbozi nguzo nyingi zimesimikwa na hata nyaya kutandazwa, sasa ni miaka zaidi ya mitatu hakuna kinachofanyika kule kwa kisingizio kwamba hawana vifaa; je, haoni kwamba huku ni kupoteza muda na kuwalaghai watu tu?

Pili, kwa kuwa Wilaya ya Mbozi ni ya uzalishaji wa kahawa na inategemea sana kuweza kutumia umeme ili ipate kuzalisha kahawa yenye ubora zaidi na kwa faida ya uchumi wa nchi hii; kwa nini Serikali isitumie muda huu kuwasaidia wananchi hawa ili kuinua Pato la Taifa katika maeneo yanayozalisha kahawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna maeneo mbalimbali ambapo nguzo inawezekana zimewekwa na kuna nyaya ambazo zimetandazwa, lakini sababu yake sio kuwalaghai wananchi. Ni kweli kwamba usambazaji wa umeme Vijijini na usambazaji wa umeme kwa ujumla ni kazi yenye gharama kubwa na ni kazi inayohitaji fedha nyingi na wakati mwingine inajitokeza kwamba Shirika linaweza likaanza mradi lakini hapo baadaye likashindwa kuendelea na ule mradi kama ilivyotarajiwa kutokana na ukosefu wa fedha. Kwa hiyo, sababu sio kwamba inataka kuwalaghai wananchi.

La pili, ni kwamba tunafahamu kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge umuhimu wa umeme katika maeneo haya yanayopandwa kahawa, lakini kama nilivyosema awali usambazaji wa umeme katika maeneo haya utategemea pia na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, napenda niseme tu kwamba Wizara imewaelekeza wenzetu wa *TANESCO* kwamba kwa miradi ile ambayo imo katika uwezo wao wa kuitekeleza, baada ya mapato ya Shirika kuongezeka basi waendelee kuitekeleza ile ambayo tayari imeshaanza kwa mfano nguzo zimeshawekwa, nyaya zimeshatandazwa lakini bado umeme haujafikishwa. Kwa hiyo, utaratibu huu na kadri mapato ya Shirika yanavyoongezeka tunaamini kwamba miradi hii mingine inaweza ikakamilika katika muda si mrefu sana. *(Makofi)*

Na.128

**Umeme Kijiji cha Soya Wilaya ya Kondoa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (k.n.y. MHE. PASCHAL C. DEGERA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa kupitia Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* ilipanga kukipatia umeme Kijiji cha Soya, Wilaya ya Kondoa ifikapo Desemba mwaka 2002 na kwa kuwa hadi sasa Kijiji hicho hakijapatiwa huduma hiyo:-

(a) Je, kwa nini mpango huo bado haujatekelezwa?

(b) Je, ni lini sasa mpango huo utaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme *(TANESCO)* lilipanga kuvipatia umeme Vijiji vingi katika mpango wa Mradi wake unaoitwa Umeme awamu ya Nne, sehemu ya Pili yaani *Electricity IV Phase II.* Kati ya Vijiji vitakavyopata huduma ya umeme katika Mardi huu, kimo Kijiji cha Soya kilichopo Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa awali wa mradi huu yaani upimaji wa awali kwa njia za laini za umeme ulikwishafanyika toka mwaka 2002 na hatua inayofuata sasa ni kuchagua na kuingia mkataba na wakandarasi wa kuleta vifaa vya ujenzi kwa laini za umeme. Baada ya kukamilisha taratibu zote za upimaji halisi katika maeneo husika na kumpata Mkandarasi wa kuleta vifaa vyote vinavyohitajika, ndipo kazi ya ujenzi wa mradi huo itakapoanza. Kufuatana na makubaliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika, kazi ya ujenzi inatakiwa ifanywe na vikosi maalum vya *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, mradi huu unategemewa kukamilika mwezi Machi, 2004.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linauliza kwamba Kijiji cha Soya, Wilaya ya Kondoa ingepata umeme ifikapo Desemba, 2002 na kwa kuwa mara nyingi tunajibiwa maswali kwamba ufinyu wa Bajeti ndio unasababisha kutokupeleka umeme na *TANESCO* wanakusanya fedha kila mwezi; kwa nini fedha hizo zisitumike kupeleka umeme katika maeneo hayo ya eneo la Soya, Burwe, Kiseyu na maeneo mengine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri. Nadhani hakusikia vizuri jibu lako.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, si visingizio vya Bajeti finyu. Ni ukweli kama nilivyosema awali kwamba mpango wa kusambaza umeme unahitaji fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali la msingi nilisema kwamba umeme katika Kijiji cha Soya na Vijiji vingine utapatikana kutokana na mradi uliopo wa *Electricity IV Phase II* na labda niseme tu kwa faida ya Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba kuna Vijiji kadhaa ambavyo vitanufaika na mradi huu wa *Electricity IV Phase II* katika Mkoa huu wa Dodoma yaani kwa maana ya Kondoa, Babati, Karatu, Arusha, Moshi na maeneo mengine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la msingi ni umeme kwa Kijiji cha Soya. Sasa Mheshimiwa Philip Marmo, tuone kama una nyongeza ya Kijiji cha Soya. *(Kicheko)*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, kwa vile mradi wa umeme wa awamu ya nne uliokuwa unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika hadi ulipokamilika mwaka 1994/95 ulikuwa umetumia fedha asilimia 75 ya fedha iliyokadiriwa na miradi asilimia 75 na miradi iliyobaki ikiwa ni pamoja na Soya na miradi mingine katika Wilaya alizotaja ingawa Mbulu hakuitaja lakini ipo; je, hiyo

asilimia 25 iliyobaki ya fedha za *Electricity IV* itakamilisha miradi yote ambayo imeshapimwa na ilishakadiriwa wakati ule wa kuandaa mradi huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza fedha ambazo zimebaki katika mradi huu ni Dola za Kimarekani milioni sita, sawasawa na shilingi bilioni sita. Kama nilivyojibu awali ni kwamba kuna Vijiji kadhaa, ni vingi katika Mikoa ambayo nimeitaja. Lakini mradi huu wa *Electricity IV Phase II* unashughulikia ujenzi wa substation za umeme katika Mikoa ya Arusha na Tanga kwa mfano Lushoto, Tanga Mjini imeshajengwa, Moshi - Majengo na maeneo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwa mujibu wa taarifa tulizokuwanazo na kwa mujibu wa mpango uliopo, tunatarajia kwamba Vijiji vilivyoorodheshwa katika mradi huu ambao orodha yake ninayo na nitakuwa tayari kumpatia Mheshimiwa Mbunge Vijiji hivyo, tunatarajia kwamba miradi hiyo itakamilika. Kwa mujibu wa mpango uliopo hivi sasa kama kutatokea mambo ambayo hayakutabiriwa au hayakutegemewa sasa hilo litakuwa ni suala ambalo litakuwa ni nje ya mpango.

Na.129

**Kiwango cha Pensheni**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa kiasi cha fedha ya pensheni inayolipwa kwa wastaafu haitoshi kukidhi mahitaji yao; na kwa kuwa wengi wa wastaafu huwa bado wana majukumu ya kusomesha watoto wao:-

(a) Je, si busara kwa Serikali kufanya mipango ya kuwalipa fedha yao wastaafu ya kila miezi sita; mwezi Januari, mwanzoni ili waweze kulipia ada za watoto wao badala ya fedha hizo kulipwa mwezi Februari na Machi ili watoto wa wastaafu wasinyanyaswe?

(b) Je, Serikali, kupitia Hazina, haioni ni busara kuweka utaratibu wa kuwaarifu wastaafu mapema kuhusu malipo yao ili kuwaondolewa kero ya kwenda kwenye Ofisi za Hazina mara kwa mara kuulizia kama hundi zao zimefika au la?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, naomba nitoe maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mtumishi wa Serikali anapostaafu kama anastahili pensheni ya kila mwezi anatakiwa apewe pensheni hiyo kila mwisho wa mwezi husika kama vile mtumishi wa Serikali anapopata mshahara alioufanyia kazi mwisho wa mwezi husika. *(Makofi)*

Kiasi cha pensheni anachopata mstaafu kinategemeana na kiwango cha mshahara aliokuwa anapata wakati alipostaafu. Hata hivyo, kutokana na ugumu wa maisha na uwezo mdogo wa Serikali, pensheni anayopata mstaafu kwa sasa ni kidogo na haikidhi mahitaji muhimu kama vile gharama za kusomesha watoto na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua udogo wa kiwango cha pensheni ya kila mwezi, Serikali iliamua pensheni itolewe mara mbili tu kwa mwaka badala ya kila mwezi. Hivyo, pensheni sasa hutolewa katika mihula miwili ya miezi sita sita, yaani kila mwezi Januari na mwezi Julai kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ulipaji wa pensheni ya kila mwezi hulipwa mwisho, sio mwanzo wa mwezi husika. Kwa utaratibu wa sasa, muhula wa malipo ya pensheni ya miezi sita, sita, hulipwa mwishoni mwa miezi ya Januari na Julai. Kila ifikapo tarehe 31 Januari au 31 Julai ya kila mwaka, hundi zote za pensheni zinatakiwa ziwe zimekwishawasilishwa

kwenye Vituo vya Mabawana Fedha nchi nzima ambapo wastaafu huchukulia pensheni zao. Hundi hizo zisipochukuliwa na wahusika hurudishwa Hazina baada ya miezi sita. Nyingi ya hundi zinazorudishwa zimechacha ni za wastaafu waliofariki. Bila kufanya marekebisho haya kuna hatari ya kuwalipa wastaafu waliofariki na hundi hizi huangukia mikononi mwa watu wasio waaminifu.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kuwaarifu wastaafu mapema kupitia Ofisi za Hazina Ndogo, juu ya malipo hayo badala ya kuwaacha wastaafu wenyewe waje Hazina, tutachunguza zaidi uwezekano huo.

Hata hivyo, tunazidi kukumbusha kwamba utaratibu wa malipo ya mstaafu ni kwa mtumishi anayekaribia kustaafu kutoa taarifa ya kustaafu miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu kufika. Muda huo wa miezi sita kabla ya tarehe unamwezesha mwajiri na Hazina kukamilisha mafao yake ili yawe tayari mara tu anapostaafu, kwa kutumia anuani iliyomo katika taarifa zilizoletwa na mwajiri wa mstaafu mhusika.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa wale wastaafu waliochukua fedha zao kwa mkupuo, wengine wameshaishi zaidi ya miaka 12 ilivyo kisheria na bado wanaendelea kuishi na kwa kuwa wao pamoja na Serikali kuamua kwamba sasa inapandisha kiwango cha pensheni cha chini kwa hawa wastaafu, watajiona kwamba ni kama watu ambao walidanganywa na wanabaguliwa hivi sasa.

Je, Serikali haioni ni busara kuona ni jinsi gani ya kuweza kuwarudisha katika mpango huu ili na wao waweze kunufaika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati nilipokuwa najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuwasilisha Bajeti ya mwaka 2003/2004 kwamba suala hilo tunaliangalia. Sasa tunatafuta namna itakavyoweza kufanyika ili tuweze kuwasaidia hata wale wastaafu. *(Makofi)*

Kama nilivyoeleza, tuna wastaafu aina hiyo 35,700. Kwa hiyo, tunaangalia *Financial Implications* zake, tuangalie na vipi tunaweza kufanya na wapi na *record* zao kama zote hizo zipo, ili tujue Serikali namna ya kuwasaidia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Kabla sijaendelea kuna matangazo mawili ya Vikao ya leo. Sio yote ya vikao, la kwanza ni la Semina ya kesho. Kama nilivyoeleza mwanzoni mwa Mkutano huu kwamba kila Jumamosi itakuwa na Semina. Kwa hiyo, Jumamosi ya kesho ina Semina ambayo inadhaminiwa na Wizara ya Kilimo na Chakula, kuanzia saa tatu asubuhi kama kawaida. *(Makofi)*

Tangazo la Kikao linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya *Commonwealth Parliamentary Association (CPA),* Tawi letu la Tanzania. Tunaomba Wajumbe wa Kamati ya Utendaji *(Executive Committee),* ikutane leo saa 7.00 mchana baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, kwa kikao cha asubuhi. Mwisho wa matangazo. Tunaendelea na *Order Paper.*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004**
**Ofisi ya Rais, Tawala za Mitaa na Serikali za Mitaa**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kwa kifupi hoja iliyoko mbele yetu ya Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kufuta kodi ya maendeleo, kodi ambayo ilikuwa kero sana kwa wananchi wetu. Wananchi wetu wengi waliumia, wengi walikuwa wanahama majumba yao kuogopa kufukuzwa na Mgambo waliokuwa wanadai kodi hii. Kwa kweli tunaishukuru sana Serikali kwa kuchukua hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo niunganishe na mapato ambayo Halmashauri zetu zilikuwa zinapata. Halmashauri nyingi zilikuwa zinategemea kodi ya maendeleo na sasa hivi mapato yao yatarudi nyuma kwa kiasi kikubwa sana. Jana wakati Mheshimiwa Waziri anasoma hotuba yake alisema kwamba, utaratibu utakaofanywa ni kufidia Halmashauri hizo kutokana na kodi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri hapo Serikali itabidi ifikirie upya. Halmashauri zetu zina haki ya kupata fedha za matumizi na siyo kufidiwa. Umefika wakati ambao Serikali lazima ikae chini ifikirie jinsi ya kugawa Pato la Taifa. Halmashauri zetu zilikuwa zinategemea kodi. Kodi imefutwa. Kwa hiyo, mkusanyaji mkuu wa fedha ni Serikali ambayo inaunganisha na zile za Halmashauri ni Serikali Kuu. Kwa hiyo, hili suala la kusema wanafidia hilo pengo si sahihi. Halmashauri zetu zina haki ya kupata mgao sawa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza hizi fedha zigawiwe sawasawa. Serikali Kuu na Halmashauri zetu na zipate fedha za kutosha. Kwa sababu fidia hizi fedha hazitatosheleza kuendeleza Halmashauri hizi. La sivyo itakuwa ni njia ya kuziua na kufuta hizi Halmashauri. Lakini sasa hivi Watanzania hatukubali hizi Halmashauri zifutwe tena. Hizo ndiyo ziko karibu na wananchi na ndiyo zinawaletea wananchi maendeleo. Kwa hiyo, isiwe kufidia zile kodi tu. Ni lazima fedha za kutosha ziende kwa Halmashauri kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, niongelee kero ya mshahara kwa watumishi wa Halmashauri hasa Walimu. Walimu wetu wanapata tabu sana kufuata mishahara. Narudia kusema kwamba natoa mfano kwenye Jimbo langu, Walimu hufuata mishahara Wilayani. Aidha, aende kwa miguu ambapo atatumia zaidi ya siku tatu kwa baiskeli au azunguke Singida ambako atatumia siku nne mpaka tano. Serikali imeanzisha mpango, imesema, Walimu na watumishi wengine wa Serikali wafungue *account* kwenye Benki ya *NMB* na wote wamefanya hivyo mpaka sasa. *(Makofi)*

Nashangaa, kwa nini mpaka sasa hivi mishahara haipitii *NMB*. Sasa ni wakati wa kupunguza hiyo kero ipitishie mishahara benki. Mimi ningeomba kwa walimu wa Iramba Mashariki pamoja na kwamba wamefungua *account* zao *NMB* Kiomboi, naomba Waziri na Watendaji wake wasaidie hizo *accounts* zihamishiwe Singida ambako walimu na watumishi wengine walioko Iramba Mashariki wanaweza kwenda asubuhi wakachukua hela zao na mchana wakarudi kwenye vituo vyao vya kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatapoteza muda na wanafunzi wetu hawatachelewa kwenye masomo. Sasa hivi wanachukua siku nne, tano mpaka sita na ni kila mwezi. Kwa hiyo, wanafunzi wetu wamekuwa wameachwa nyuma kimasomo. Hilo naomba Mheshimiwa Waziri alizingatie na lifanyiwe utaratibu wa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, niongelee fedha zinazotoka Serikali Kuu kwenda Halmashauri zetu. Fedha za Elimu, *Basket Fund, Road Toll* mpaka sasa sehemu ya fedha hizi haitumiki kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Hizi ni fedha nyingi sana. Nianze na *Road Toll*. Katika Wilaya nyingi zinazopata hizi fedha za Mfuko wa Barabara mpaka inapofika mwisho wa mwaka wanakuwa hawajatumia hizi fedha. Sehemu fulani ya fedha inabaki na hiyo fedha kufuatana na utaratibu wa Halmashauri inatakiwa ihamishiwe mwaka unaofuata. Lakini Halmashauri nyingi hazifanyi hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumegundua Halmashauri nyingi hazifanyi hivyo na mpaka sasa hatujajua hizo fedha zinakwenda wapi. Kuna Halmashauri haijulikani shilingi milioni 125 zimekwenda wapi na siyo moja, ziko nyingi. Kwa hiyo, hizi fedha hazifanyi kazi inayokusudiwa. Sisi tunaomba kuwe na uangalizi na usimamizi wa karibu. Halafu hizi fedha za barabara, kuna Wilaya zingine zinakuwa zinapata hela za barabara kutoka Serikali Kuu na zinapata hela zingine kutoka kwa wafadhali. Unakuta hizo fedha za *Road Toll* zimejenga barabara kutoka *point A* mpaka *point B* na zile za wafadhili zimejenga barabara hiyo hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna hela nyingi sana hazitumiki inavyotakiwa. Mifano ipo na tutampa Mheshimiwa Waziri na hatua za haraka zichukuliwe. Hii ni sawasawa na *Basket Fund* wanapewa hela nyingi. *Basket Fund* hela zinabaki na zingine zinatumika isivyokasimiwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili. Hata ujenzi wa madarasa, tunadanganywa kwa ripoti hizi, lakini ukienda huko kwenyewe madarasa aidha hayakujengwa kwa *standard* inayotakiwa. Wengine hawajajenga kabisa, wanajua nani atakwenda kutughasi, hawaendi huko. Kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie hili.

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi za Halmashauri hazitumiwi ipasavyo kwa sababu Wakaguzi wa ndani, aidha, hawapo au wapo pale wananyimwa nafasi ya kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Kuna baadhi ya Wakurugenzi wanawanyanyasa sana hawa *Internal Auditors* na kwa sababu hawajitegemei, wengi wanakata tamaa na wengine wanatoroka. Wameajiriwa wengi na wengi wametoroka. Kwa hiyo, sisi tunaomba Mheshimiwa Waziri uangalie hilo. Vile vile Maafisa Ugavi kule Wilayani, mambo ya *stores* yako nyuma sana na Wilaya nyingi hazina watu kama hawa. Ndiyo maana wananunua bidhaa kienyeji.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hela nyingi za Serikali zinakwenda Wilayani. Kwa hiyo, tusipofuatilia na kweli ni jukumu la Serikali kuwaajiri watalaam wake wanaojua kazi zao. Tuna waweka Hazina wengi hawafanyi kazi inavyotakiwa kwa sababu hawana ujuzi. Maofisa Ugavi na Wakurugenzi wengine, Mkurugenzi anakuwa kila mwaka mahesabu yake yakienda kwa Wakaguzi yanarudishwa na bado Wizara haichukui hatua. Kwa hiyo, mimi kwa niaba ya Wabunge wenzangu naomba sana utaratibu huu uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru Wilayani kwangu kuna programu ya usafiri na uchukuzi vijijini. Kuna programu ya usafiri na uchukuzi vijijini. Huu mradi ulikuwa na ulianza vizuri na unawasaidia sana wananchi na lengo la mradi huu ilikuwa ni kuwashirikisha wananchi, akinamama, Halmashauri inatoa vifaa wanaajiriwa watu kule vijijini na barabara zilivyotengenezwa kwa mpango huu mwanzo mpaka leo bado ni nzuri sana.

Lakini Wakurugenzi wakabadilisha, wakaanza kutoa *tender* kwa kuwanyima haki wananchi ambao walikuwa wafanye hizi kazi. Halmashauri ilikuwa inatakiwa itoe magreda kama yako lakini kazi zingine zote zifanywe na wananchi hasa akinamama. *(Makofi)*

Naomba Mheshimiwa Waziri ufuatilie suala hili. Kuna barabara moja jimboni kwangu ya kutoka Mwangeza mpaka leo imesimama. Wananchi wanajitolea lakini Halmashauri bado inazungusha na fedha ziko nyingi na zinatakiwa ziishe mwaka huu. Kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afuatilie hiyo.

La mwisho, Mheshimiwa Waziri wenzangu wamelalamika juu ya mipaka, hata kule kwangu kuna tatizo la mpaka, kati ya Wilaya ya Mbulu, Hanang na Karatu. Tulikuwa tumeomba wataalam waende wakutanishe hizi Wilaya zote husika waangalie *beacons*, lakini sasa hivi wenzetu wa Mbulu wanaweka *beacons* kinyume na mapatano tuliyokuwa nayo. Wananchi walikuwa tayari kwenda kung'oa. Mimi nikawaambia hapana, ngojeni nitapeleka hii.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri jambo hili lichukulie kwa uzito wake. Nilipomwandikia barua, walikuwa wanaweka hizo *beacons* kwa kisingizio kwamba wanafanya hifadhi ya wafanya pori. Nilipowaandikia barua *DC* akanijibu kwamba huo ndio mpaka. Mpaka ulioko kati ya Wilaya yangu na Mbulu ni wa Mkoa.

Kwa hiyo, ni lazima Wakuu wa Mikoa washirikishwe, wataalam wa mipaka kutoka Makao Makuu waje waangalie hili. Sisi hatutaki kugombana na majirani zetu. Lakini kuna watu wachache wanataka kutugombanisha. Kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri hilo ulifuatilie na ikiwezekana lipatiwe ufumbuzi kwa nia njema kabisa.

Mheshimiwa Spika, wananchi kule Wilayani wako tayari kujitolea kwenye kazi za maendeleo, wako tayari kusaidia Halmashauri, kusaidia Serikali. Wanatakiwa washirikishwe tu, lakini pale ambapo ushirikishwaji unakuwa duni mambo hayaendi vizuri. Naomba Watendaji wa Halmashauri waende kwenye Kata, waende Vijijini wasaidie wananchi ili kujiletea maendeleo yao. *(Makofi)*

Fedha zinazotolewa kwa ajili ya kazi kwenye Kata au Kijiji fulani, wananchi wajulishwe mapema na fedha hizo zikafanye kazi hiyo. Sasa hivi fedha nyingi zinabaki Wilayani badala ya kufanya kazi za maendeleo kule kulikotakiwa zinabaki Wilayani na ndiyo hiyo zinaleteleza zihamishwe toka fungu fulani kwenda fungu fulani kwa kazi ambayo haikukusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninashukuru kwa kupata nafasi ya pili kuzungumzia hotuba ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri na Watendaji wote katika Wizara yake na niseme kwamba hotuba ilikuwa nzuri. Maelezo yake ni mazuri. Muhtasari ulikuwa unaeleweka vizuri na umetolewa kwa muda uliopangwa na kwa kweli kwa uangalifu mkubwa. *(Makofi)*

Zaidi ya hilo nimshukuru Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ya kuonyesha mfano wa kuzunguka nchi nzima kuyaona matatizo na kutoa ushauri. Naibu Waziri amefika Lushoto na kwa kweli wananchi walifurahi sana kwa jinsi alivyozunguka na kuyaona matatizo ya wananchi kwa vitendo na Waziri mwenyewe anakufahamu vizuri. Ninapenda kusema mchango wake ni mzuri sana katika Wilaya ya Lushoto na Jimbo la Lushoto kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia katika maeneo yafuatayo. Kwanza, mfuko wa barabara. Napenda kusema kwamba kwa kweli mfuko wa barabara umefanya kazi nzuri sana. Wabunge wote ni mashahidi kwamba leo ukiizungumzia Serikali ya Chama Cha Mapinduzi iliyoko madarakani katika suala la barabara kwa kweli wananchi wanakubali kwamba imefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Nijielekeze katika kero ambazo ziko katika jimbo langu. Nina barabara mbili ambazo ni muhimu sana na huko nyuma niliwahi kumwomba Waziri kwa kuandika barua ili aweze kunisaidia kwa sababu kushinda kwangu na kuendelea kwangu kuwa Mbunge ni pale ambapo kwa kweli matatizo ya barabara hizi yatatatuliwa.

Kwanza barabara ya Ngwelo, Mlola kwenda Makanya hadi Milingani nilikwishaandika na nikapewa matumaini. Nikawapa wananchi matumaini kwamba Serikali inaliangalia suala hili na wananchi wamejitahidi sana kwa juhudi zao kuponda mawe, kutumia mikono yao, kulima barabara na kwa kweli kutengeneza barabara milimani ni kazi kubwa sana. Ninamwomba Waziri hili kiasi chochote kitakachoweza kupatikana hata kutokana na dharura naomba ahadi ile ambayo tumewapa wananchi itekelezwe.

Barabara nyingine ni kutoka Dochi kwenda Mombo. Barabara hii ndiyo barabara pekee ambayo tunaitegemea, kama itatokea dharura katika Wilaya ya Lushoto. Ndiyo barabara ya dharura. Kwa muda mrefu hii barabara ilikuwa inatumika hata wakati wa Ukoloni. Kwa sababu Wizara inalielewa tatizo ninaomba kwa kweli barabara hizi mbili katika jimbo langu zichukuliwe hatua angalau mwaka huu nipewe hata kutokana na dharura ili barabara hizi ziweze kujengwa.

Lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la Zahanati na Vituo vya Afya. Naishukuru sana Serikali. Kwa kweli juhudi za Serikali hasa TAMISEMI kuonyesha uwezo wa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kufanya kazi zinaonekana wazi. *(Makofi)*

Zahanati pamoja na Vituo vya Afya vinakarabatiwa na ninashukuru kwa mipango mizuri. Lakini pengine niombe tatizo ambalo ninalo katika jimbo langu. Tarafa nzima ya Lushoto haina Zahanati, inategemea hospitali ya Wilaya. Ninaomba uwezekano wa kupewa Zahanati katika Kata za Dare, Ubiri pamoja Kwai, angalau kama ingepatikana Zahanati ingesaidia sana wananchi wanaokwenda masafa marefu kufuata huduma katika hospitali ya Wilaya.

Lingine ambalo nitalizungumzia ni kuhusu mazingira. Tatizo la mazingira kwa kiasi kikubwa nalishukuru sana Shirika linaloitwa *SECAF* ambalo lilikuwa linafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani. Kwa bahati mbaya mkataba wa shirika hili sasa hivi umekwisha. Kwa hiyo, Serikali ya Ujerumani haitoi fedha kwa ajili ya *SECAF*. Pamoja na juhudi za Serikali kuimarisha kitengo cha kutunza mazingira katika Wilaya ya Lushoto hiki cha *SECAF* bado tatizo lipo.

Kwa hiyo, naiomba Serikali katika suala la upandaji miti, utunzaji wa misitu ni suala ambalo lazima lipewe umuhimu wa kwanza. Najua kunahitajika sana ushirikiano na Wizara ya Maliasili na Utalii. Nilimwandikia Waziri wa Maliasili na Utalii, ili kuona kama kuna uwezekano wa kuangalia utunzaji wa misitu ambayo kwa kweli ni michache sana katika Wilaya ya Lushoto. Bado mbao au miti inakatwa ovyo, misitu inapungua na hatimaye mazingira katika Wilaya yanaanza kuwa mabaya sana. Mvua hazitabiriki na hali si nzuri.

Kwa hiyo, ninachokiomba kwanza, ni kuimarisha juhudi za kulinda misitu hiyo ya asili. Pili, kusimamia kwa nguvu zaidi misitu ambayo iko chini ya Halmashauri ya Wilaya. Ninajua kwamba mimi ni Mbunge, nahusika moja kwa moja. Lakini lazima tukubali kwamba katika misitu ya asili siyo rahisi kwa sababu wizi umekuwa mkubwa sana. Iangaliwe uwezekano wa kufanya *TANAPA* isimamie maliasili hizi ambazo kwa kweli ni chache Wilaya ya Lushoto na misitu hii ndiyo pekee inayolinda Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia katika hotuba ya Waziri, ni suala la kilimo. Huduma za ugani bado ni duni sana. Wataalam kwa kweli hawaonekani vijijini. Matokeo yake ni kwamba bado kwa maeneo ambayo sisi tunategemea kilimo na hasa kilimo ambacho kinategemea kulima katika maeneo madogo madogo. Kinahitaji sana utalaam wa kilimo ili uzalishe zaidi. Sasa kama huduma za ugani ni dhaifu mara nyingi wananchi, wakulima wale wadogo wadogo hawawezi kuzalisha kwa kiwango kikubwa katika eneo dogo. Kwa hiyo, utaalam na ushauri unahitajika sana.

Sasa naomba wataalam walioko katika Wizara ya Kilimo na Chakula na ambao sasa hivi wamerudishwa kwenye Halmashauri, wajaribu kumotishwa. Huko nyuma historia inaonyesha wazi Wizara ya Kilimo na Chakula ndiyo kati ya Wizara ambazo ilikuwa na matatizo makubwa sana kujali watumishi. Mishahara ilikuwa ni midogo, posho ilikuwa hakuna, wafanyakazi walikuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Sasa naliomba hili, pamoja na juhudi za kuboresha maslahi kwa watumishi wa Wizara ya Kilimo na Chakula, mimi nashauri pia wahimizwe kutekeleza wajibu wao. Kwa kweli tatizo la ushauri kutokana na wataalam wa kilimo ni dogo sana. Kwa hiyo, naliomba hili ichukuliwe kama eneo muhimu ambalo linahitaji msisitizo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi nisingependa sana kuzungumzia suala la malipo kwa Madiwani. Hiki ni kilio ambacho ni lazima sote tuiangalie kwa uaminifu na kwa kweli kwa uzito unaotakiwa. Madiwani ni wenzetu katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na ni viongozi muhimu sana. Sasa ngazi zote zimeangaliwa kwa jicho la huruma. Wabunge tumeangaliwa, Watendaji wa Vijiji wameangaliwa, Watendaji wa Kata wameangaliwa, waliobaki ni Madiwani. Tusipowaangalia Madiwani, tutafanya nguvu zetu ziwe na kasoro. *(Makofi)*

Naomba hili lizingatiwe kama lilivyozingatiwa na wenzangu, nalisisitiza utafutwe utararatibu, hata kama Halmashauri itachangia basi kiwepo kiwango kama ilivyopendekezwa ambavyo Serikali Kuu itatupa ili Madiwani nchi nzima wajulikane wanapata nini na kile kidogo kinachotoka kwenye Halmashauri kisipingwe na Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili nisingependa nilizungumzie kwa undani zaidi. Lakini lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu mapato ya Halmashauri. Kwanza, nichukue nafasi hii kama wenzangu walivyoipongeza Serikali kwa kufuta kodi mbalimbali zenye kero. Azma na nia ya Serikali ni nzuri sana na hakuna mtu anayetutendea kheri katika nchi hii atakataa kupunguza kodi zenye kero. Lakini ni wajibu wa Serikali pale inapokata kodi, itafute chanzo kingine cha kodi ili shughuli za maendeleo zisisimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumepunguza kodi nyingi kutoka 60 mpaka nane. Ni kazi kubwa sana imefanyika na hili ni pengo kubwa sana litatokea. Waziri amelizungumzia kwa undani na amezungumzia kwa uzito unaostahili. Lakini lazima tukubali kwamba pamoja na juhudi za wananchi, uwezo wa kujaza pengo hili kutokana na juhudi za wananchi wenyewe vijijini kupitia Halmashauri zetu utakuwa si mkubwa kiasi cha kuziba lile pengo lote. *(Makofi)*

Kwa hiyo naomba Serikali itamke rasmi kila Wilaya ije na *schedule,* ni kiasi gani itafidiwa na Serikali Kuu kutokana na upungufu wa kodi, kutokana na kodi zilizopunguzwa ili mwanzoni kabisa kila Halmashauri ione upungufu wake. Madiwani pamoja na Serikali wakae na kuona mapengo haya yatatekelezwaje, vinginevyo badala ya kwenda mbele tutarudi nyuma. Kwa hiyo, nashauri kwamba ifahamike wazi Serikali Kuu itasaidia kiasi gani ili pengo lililopo tujue litazibwa kwa kiasi gani.

Lingine ambalo nitalizungumzia ambalo ni la mwisho ni suala la ukosefu wa ajira. Suala la vijana wetu vijijini na suala la vijana kutoroka vijijini kukimbilia mijini ni tatizo ambalo ni zito sana. Hili linahitaji kuangaliwa kitaalam. Lakini kwa mtu wa kawaida aliye na mawazo ya kawaida ukitaka uweze kuondoa kwamba vijana wasikimbilie mijini, ni kuboresha huduma za vijijini.

Huduma za Vijijini haziwezi kuboreshwa kama hakuna maamuzi ya makusudi na maamuzi ya makusudi yanaweza kuja kwa utaratibu kwa mfano, tunapozungumzia kilimo, lazima ikubaliwe wazi kabisa kwamba ruzuku pamoja na misaada yoyote inayotolewa kwa ajili ya kilimo vijana wanaifahamu, ili wapewe hamasa warudi wakalime.

Kwa mfano, mimi katika Jimbo langu leo vijana wangekuwa na uhakika wa kupata mbolea kwa bei nafuu pia madawa ya kilimo kwa bei nafuu, nawahakikishieni kwamba vijana wengi wangekubali kurudi Vijijini na wangekubali kuishi Vijijini wasiende Mijini kwa sababu ana uhakika akilima mboga mboga pia akirutubisha matunda yake ataweza kupata pato kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini leo sasa hakuna uwezekano wa kurudi kule kwa sababu hizi zana zote ni ghali, atakimbilia Mjini ili akazitafute akirudi anaweza akazalisha kidogo sana na matokeo yake ni kwamba harejeshi ile gharama yake ya kilimo kutokana na ughali wa madawa na kutokana na ughali wa pembejeo za kilimo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kweli ili tuweze kuliondoa tatizo la vijana kwenda Mijini, ni lazima tuboreshe kwa dhati na tuwe na mpango rasmi katika kila eneo, kuanzisha miradi ya vijana Vijijini na Serikali ikubali kuigharamia miradi hii aidha, kwa kutoa ruzuku, kuisimamia au kutoa vitendea kazi, vijana watakubali kukaa Vijijini. Vinginevyo tatizo hili litakuwa ni kubwa na tunaunda jeshi lisilo na kazi, tutakuja kushindwa kuwadhibiti vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi napenda kushauri kwamba suala la ajira kwa vijana ni suala ambalo ni *sensitive* na bahati nzuri Wakuu wa Mikoa wapo, majeshi haya yapo huko Mikoani. Wajaribu kutengeneza ratiba na programu za kuwafanya vijana wakubali kukaa Vijijini na Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa, tukae ili tufikirie ni vipi tunaweza kuiboresha hiyo miradi ili vijana wakae Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nashukuru kwa hotuba nzuri. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu kwa wakati huu, Waheshimiwa Wabunge wa Vyama vyote na hasa wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nami niungane na wenzangu kutoa pongezi za dhati kwa Serikali katika kuondoa kodi ya maendeleo kwa wananchi. Kodi hii ilikuwa ni kero kubwa na hasa kwa wanawake.

Wanawake walibeba mzigo mkubwa tukizingatia kwamba ndiyo walezi wa familia lakini pamoja na kulea familia wakiwemo watoto yatima walikuwa na mzigo wa kulipa kodi, matokeo yake wanawake wengine walikuwa wanakimbia kuwakwepa watoza kodi, sasa wameona kwamba Serikali yao inawajali.

Sasa kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Iringa, napenda niipongeze sana Serikali na wameniletea taarifa kwamba niipongeze Serikali kwa juhudi hizi za kufuta kodi na pia kwa kuamua kwamba pembejeo zitatolewa kwa bei nafuu kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambako ndiko kuna kilimo kikubwa cha zao la mahindi. Wameahidi kwamba wao wakipewa pembejeo watazalisha mazao kwa wingi na wangependa pia kuona masoko ya mazao yao yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie suala la Madiwani. Naomba nianze kwanza na posho za Madiwani kama walivyozungumza wenzangu. Kwa kweli kama tunapenda kuangalia maendeleo na tunajua kwamba maendeleo yaliyoko Vijijini kazi kubwa inafanywa na Madiwani hasa katika kuwahamasisha wananchi, lakini Madiwani hawa wengi wao walioko Vijijini hawana hata baskeli ya kuendea kwenye hayo maeneo. Madiwani hawa, nikichukulia Madiwani wa Viti Maalum ambao wao badala ya kusimamia Kata wanasimamia mpaka Tarafa, wamegawiwa Tarafa, Tarafa moja au Tarafa mbili ili kuhakikisha kwamba kila eneo wanawake wanafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Madiwani hawa hawana kitendea kazi chochote na wala mkopo unaoweza kuwasaidia kufanya hizi kazi. Nafikiria kwamba sasa wakati umefika wa kuangalia, Wizara iangalie upya jinsi ya kuweza kuwamotisha hawa Madiwani ili waweze kufanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kutoa mafunzo kwa Madiwani. Mafunzo haya yametolewa ili kuboresha utendaji wa kazi za Madiwani. Lakini kama tukiboresha mafunzo haya bila kuwaangalia na kuwapa motisha, mafunzo haya yatakayokuwa yametolewa hayatazalisha matunda yale yanayostahili kuzalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo, naomba pia nizungumzie suala la huduma za afya. Napenda kuipongeza Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara nyingine zinazohusika ikiwemo Wizara ya Afya, kwa kazi nzuri wanayoifanya ili kuboresha huduma za afya Vijijini na hasa Huduma ya Mama na Mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nilete kilio changu kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu Hospitali ya Wilaya ya Ludewa. Wanawake wa Wilaya ya Ludewa, wanawake wajawazito, hawana chumba cha kujifungulia. Matokeo yake *clinic* ambayo ilipangwa kwa ajili ya huduma za mama na mtoto pamoja na huduma za kutolea uzazi wa mpango, chumba hicho ndiyo kinachotumiwa kama chumba cha kujifungulia.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri aitazame Hospitali ya Wilaya ya Ludewa ili tuweze kujenga *Labour Ward,* kwa kweli mazingira ya chumba kile hayafai kwa mwanamke kujifungulia pale. Naomba Wizara ilitazame hili kwa jicho la pekee ili wanawake wa Ludewa nao waone kwamba Serikali yao inawajali na kuwaona kwamba wana mahali pazuri pa kujifungulia. Hii pia itaboresha utoaji wa huduma za uzazi wa mpango, sasa hivi chumba cha huduma za uzazi wa mpango badala ya kuwa karibu na *clinic* kiko mbali wakati tunategemea kwamba wakipata mafunzo ya *clinic* pale wakati wa huduma ya upimaji wa watoto wapate pia mafunzo ya uzazi wa mpango lakini sasa inabidi yatenganishwe kwa sababu ya upungufu wa vyumba. Kwa hiyo, naomba nilete kilio hicho cha wanawake wa Wilaya ya Ludewa kama walivyonituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hilo naomba sasa pia nizungumzie suala la wataalam wa ugani. Wataalam wa ugani wanafanya kazi katika mazingira magumu. Hawa wataalam wa ugani ni pamoja na wataalam wa Wizara ya Kilimo, wataalam wa Maendeleo ya Jamii na pia naweza kuwaweka na wataalam wa Idara nyingine ikiwepo na Idara ya Maliasili. Wataalam hawa wanafanya kazi Vijijini kwenye ngazi ya Kata mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya na mara nyingi inapofika mwisho wa mwezi wanakuja kudai mishahara yao Wilayani. Mara nyingine mishahara inachelewa kutoka kwa hiyo wanakaa kwa muda mrefu pale Wilayani bila kupata huduma na wakati mwingine hata kwa kujitegemea wao wenyewe. Sasa tunategemea ni motisha gani hii wanayoipata ya kufanya hii kazi ngumu huko Vijijini wakati wanatumia hela yao ya mfukoni ili kuweza kulala hadi mishahara itakapotoka.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nafikiria ya kwamba sasa ni wakati wa kuangalia upya huduma ambazo zitakuwa bora, njia ambayo inaweza kuwawezesha hawa wataalam wakapata mishahara yao kwa wakati na kwa utaratibu mzuri uliopangwa ili kuwapunguzia kero ya kufuatilia mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie suala la watoto wa kike, ajira za watoto. Suala hili ningelizungumza kwenye Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, lakini sina uhakika kama nitapewa nafasi ya kuchangia. Kwa kuwa hii Wizara ndiyo inayohusika na shughuli zote kama Mratibu, naomba nizungumzie suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya ukosefu wa shughuli za kufanya Vijijini, zile ambazo zinaweza kuwapatia kipato wengi wa watoto na hasa watoto wa kike wamekuwa wanaondoka Vijijini na hii nazungumzia kwa Mkoa wangu wa Iringa na kwenda Mijini, katika Miji ambako sasa ndiyo wanakokuwa kwenye kazi ambazo ni za ajira mbaya ikiwemo kwenda kuwekwa kwenye madanguro. Hizi hadithi tumezisoma sana kwenye magazeti na hali halisi ndiyo hivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba elimu inayotolewa inakuwa ni vigumu kuwazuia hawa watoto kubaki Vijijini, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Mkoa wa Iringa hasa Mkuu wa Mkoa wa Iringa na timu yake, kwa kuweza kuihamasisha jamii kuhusu tatizo la ajira ya watoto na hasa watoto wa kike wanaotoka katika Mkoa na kwenda sehemu mbalimbali nchini ili kutafuta ajira hata mpaka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kusaidia nguvu hizi za uhamasishaji zinazofanywa na viongozi mbalimbali wa Mkoa wakiwemo na Waheshimiwa Wabunge, Serikali inatakiwa kuliangalia upya ili kuhakikisha kwamba shughuli mbalimbali zinapatikana Vijijini, ambazo zitawafanya vijana wasiondoke. Shughuli hizi ni pamoja na sehemu za michezo, viwanja vya michezo na shughuli mbalimbali za michezo Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kama elimu ya michezo inatolewa mashuleni na shule zimejitahidi kutoa elimu, basi hiyo elimu pia irudi kwenye jamii ili watoto walioko nje ya shule waweze kuwa na sehemu mbalimbali za kuchezea. Lakini si hilo tu, pia tufikirie sasa kuwa na sehemu za *recreation*, vituo vya maendeleo, kwa mfano zamani Mijini kulikuwa na *Community Centers*. Tufikirie pia Vijijini kuwa na *Community Centers* ambako wananchi pamoja na vijana wanaweza kupumzika jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo langu mahala pa kupumzikia ni vilabuni. Sasa tutazuiaje hata madawa ya kulevya wakati hakuna sehemu maalum ya vijana kwa ajili ya kupumzikia, ambako wanaweza kupewa elimu maalum, utawapataje vijana kama hawako nje ya shule na hakuna mahala popote wanapokutana, hakuna viwanja vya michezo na pia hakuna vituo ambavyo vinawafanya wakutane pale ili waweze kujadili masuala mbalimbali na kupewa elimu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naiomba Wizara sasa ianze kuangalia kwa kushirikiana na Wizara nyingine zinazohusika, kuanzisha vituo Vijijini ambavyo vitakuwa ni vituo vya mahala, kama *recreation* wanakoweza kubadilishana mawazo na kucheza michezo mbalimbali ikiwemo michezo ya ndani kama tennis na michezo mbalimbali iweze kuchezwa pale na kuwafanya vijana wawe na shughuli za kufanya tukizingatia kwamba Serikali yetu sasa imepunguza bei za pembejeo, nina uhakika kwamba vijana watashiriki katika shughuli za kilimo.

Lakini pia baada ya kazi wapate mahala pa kujiburudisha badala ya kuishia vilabuni na kwenye vijiwe, kwenye kona ambako wanafundishana mambo mbalimbali yakiwemo matumizi ya dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba pia nizungumzie suala la uhusishwaji wa Madiwani wanawake pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanawake katika Kamati mbalimbali. *(Makofi)*

Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano imetoa nafasi sawa kwa wote, wanawake na wanaume na imetoa nafasi za uwakilishi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wanawake na wanaume, Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo na Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nchi yetu ni ya nne katika nchi zote zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa kuwa na uwakilishi wa wanawake, naomba niipongeze Serikali yetu kwa kuliangalia hili, kwa kuwa na umuhimu wa kuangalia masuala ya jinsia. Mheshimiwa Rais wetu amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba wanawake wanakuwa katika nafasi za maamuzi. Naomba nimpongeze kwamba hivi karibuni amewateua pia Wakuu wa Wilaya wanawake, naomba nimpongeze na kuwapongeza wanawake wote walioteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa utakuta maagizo yanayoelekezwa kutoka kwenye Wizara ndiyo yanayobagua, yanaacha kuwa na misingi ya kijinsia. Ninaomba niliseme hili nikiangalia muundo wa Kamati za Ukimwi zilizoundwa huko na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika Kamati za Ukimwi naipongeza Wizara kwa kuhakikisha kwamba kuna uwakilishi wa wanaume na wanawake. Lakini ilipokuja kwenye Kamati za Ukimwi kwenye ngazi ya Kata, wamesema mwakilishi atakayekuwa mle ni Diwani wa Kata, je, yule Diwani wa Viti Maalum aliyeko kwenye Kata ile hayumo kwenye huu uwakilishi? Wamekuja kwenye Kamati za Wilaya, Wajumbe wanaotakiwa wawe mle ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo, je, yule Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum aliyeko kwenye Wilaya ile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hili Wizara iliangalie, kama tunazungumzia kwamba Ukimwi haubagui kwa nini sasa inapokuja kwenye uwakilishi wale wawakilishi wa wanawake wasiwe mle ndani na tukijua kwamba mwanamke ndiye aliyeathirika zaidi na Ukimwi. Naomba hili Mheshimiwa Waziri aliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati nyingine zikiwemo pia Mfuko wa Barabara na nyingine ambazo tumekwishazizungumzia wakati wa maswali ya mwezi Aprili. Naomba Wizara iangalie upya muundo wa Kamati mbalimbali kwa kuangalia usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la kuangalia Wilaya zenye matatizo. Naomba Wizara iangalie vizuri Wilaya ambazo zinaonekana ni zenye matatizo. Kila nikizungumza humu ndani nimekuwa naleta kilio changu kwa Wilaya ya Makete. Tarehe 1 Desemba, ilitangazwa rasmi Wilaya ya Makete na Umoja wa Mataifa kwamba ni Wilaya ya janga kwa kuwa na tatizo kubwa la Ukimwi tukitilia maanani kwamba asilimia 40 ya watoto wote wa chini ya miaka 18 ni yatima.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iitazame hii Wilaya. Iitazame kwa kuipatia wataalam, iitazame pia kwa sababu vifo vingi vinavyotokea ni vya wataalam wakiwemo walimu na wataalam wa ugani. Naomba hii Wilaya iangaliwe kwa jicho la pekee. Tunapozungumza sasa hivi watoto wengi wanajilea wenyewe na tukizingatia pia kwamba Wilaya ile ni ya baridi, watoto hawana nguo.

Nimechangia hapa kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimelizungumzia hili. Naomba Wizara ilitazame.

Mheshimiwa Spika, namalizia sasa kwa kumpongeza Ndugu Betty Mkwasa, kwa kuweza kushinda katika shindano la *CNN* la waandishi bora na ninampongeza kipekee kwa sababu ameshinda katika mada ya kuzungumzia tatizo la Ukimwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niungane na wenzangu kwa kuipongeza Serikali tena na kwa hotuba nzuri ya Ofisi hii ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na niseme awali kwamba ninaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono ningependa kugusia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ituwekee bayana hizi fedha wanazogawa kwa Mikoa, wanagawa kuangalia vigezo gani vya kisasa. Ninasema hivyo kwa kuangalia Mkoa wangu wa Lindi ambao mwaka hadi mwaka mgao wake wa fedha ni mdogo sana.

Katika Kitabu cha Umaskini, Mkoa wa Lindi unaorodheshwa kama Mkoa maskini, kama kigezo ni idadi ya watu, nafikiri Lindi tunastahili kupongezwa kwa sababu tumezingatia nyota ya kijani. Lakini nilikuwa nawaambia wenzangu inawezekana kabisa sisi hatuongezeki kwa wingi kama mnavyoangalia kwa sababu ya mazingira yaliyopo na ukubwa wa eneo la Mkoa wa Lindi. Sasa mimi ningeomba sana waangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hapa *other charges* katika *Vote* ile ya *Regional Administration*, Mkoa wa Lindi umepewa shilingi milioni 573. Mimi nilikuwa naomba Serikali iangalie ugawaji huu kwa kuzingatia geographia ya Mkoa ulivyo na ukubwa wa eneo. Mkoa wa Lindi sehemu kubwa ya Liwale ni *Selous* lakini Mkuu wa Mkoa ni lazima afike Liwale ambapo kutoka Lindi Makao Makuu ya Mkoa mpaka Liwale kwenda na kurudi si chini ya kilometa 900. Sasa *unless* mseme hamtaki Mkuu wa Mkoa aweze kuzungukia katika maeneo hayo. Lakini vile vile Mkoa wa Lindi tunalo tatizo kwamba Mkuu wa Mkoa akitaka kuzungukia Wilaya zote hawezi, atatoka Lindi aende Lindi Vijijini, aende Ruangwa - Nachingwea - Liwale akitaka kwenda Kilwa ni lazima arudi tena Lindi ili aanze safari ya Kilwa kwa sababu hakuna barabara inayo-*connect* sasa ya uhakika kutoka Liwale kwenda Kilwa.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sana Serikali iangalie kwa sababu tatizo moja kubwa la Mkoa wa Lindi ni hizo *other charges*. Kama kigezo ni *contribution* katika Pato la Taifa Mkoa wa Lindi unazalisha korosho ambayo inaleta fedha za kigeni, Mkoa wa Lindi unazalisha ufuta ambao vile vile unaleta fedha za kigeni na pia Mkoa wa Lindi tunazalisha mbaazi ambazo vile vile zinaleta fedha za kigeni. Nilikuwa naomba mliangalie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Waziri ameeleza umuhimu wa kupeleka fedha katika Wilaya, nilikuwa ninaomba waangalie. Ninapongeza hatua hiyo kwamba itasaidia Wilaya sasa inaweza kusimamia fedha zake. Lakini vile vile nilikuwa ninaomba katika kugawa muangalie ukubwa wa eneo iwe kigezo kinachozingatiwa. Ukubwa wa eneo ni muhimu sana. Kwa mfano, Wilaya ya Liwale katika Mkoa wa Lindi imepewa fedha kidogo sana lakini mimi nafikiri hatuelewi Jiografia ya Wilaya ya Liwale. Wilaya ya Liwale ukitaka kutembelea eneo lolote, ukitoka Liwale kwenda Mpigamiti ambayo iko mwishoni mwa *Selous* pale inapakana na Wilaya ya Songea Vijijini, ukitaka kwenda Barikiwa ni lazima urudi tena Liwale ili uende Barikiwa, ukitoka pale urudi tena Liwale kwenda Mbaya, ukitoka pale unataka kwenda Nguja ni lazima urudi tena Liwale.

Sasa ni lazima muelewe Jiografia hiyo kwa sababu robo tatu ya Wilaya ya Liwale ni *Selous* lakini hatuwezi tukawaacha wale wananchi wanaokaa karibu na *Selous* eti kwa sababu wako pale porini. Kwa hiyo, ninaomba sana Wizara hii mtembelee Wilaya hizi na Mikoa ili mfahamu Jiografia yake ilivyokaa ili mkigawa fedha mjue watu hawa wanafanya kazi katika mazingira gani.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ningependa kulizungumzia, ni suala la kodi zilizopunguzwa. Ninaipongeza sana Serikali lakini niungane na wenzangu katika kutoa duku duku langu juu ya athari ambazo zinaweza kutokea katika Halmashauri.

Kwa mfano katika eneo la Masoko. Masoko ni lazima yatunzwe, yasafishwe. Kama nilimsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema, wale wanaokuja kuchuuza pale wasitozwe tena ushuru wowote. Ni kweli watakuwa wameishatozwa kule wanakotoka lakini hili soko litatunzwaje? Kwa mfano, soko la Kariakoo, pale ndiyo vitu vingine vinaingia na kuna wachuuzi wengi, kama wale watu hawatatozwa ushuru soko la Kariakoo litajiendeshaje? Pia soko la Lindi Mjini litajiendeshaje?

Naomba Serikali iliweke hili bayana maana tusije tukafika mahali tukasema Halmashauri hizi ni chafu, hazifanyi kazi vizuri kumbe tumewakata baadhi ya maeneo ambayo yanawapatia fedha.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo ningependa kuligusia, ni suala la madeni ya Halmashauri. Mheshimiwa Waziri ameainisha vizuri sana katika hotuba yake. Pamoja na juhudi wanazofanya mimi

nilikuwa naomba uliangalie hili kwa makini kwa sababu sehemu kubwa ya madeni ni mapato ya watumishi wenyewe wahusika kwa mfano mchango wao huu wa *PPF* na pia mchango wao katika *WADU,* sasa kama fedha hizi hazijafika kunakohusika na mtumishi imefikia wakati wa kustaafu inakuwaje? Anastahili kulipwa haki zake, sasa tusije tukajenga adha ambayo itasababisha watumishi wakajenga manung'uniko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile liko lalamiko kubwa la walimu wa shule za msingi ambao kwa miaka mingi hajalipwa fedha zao za likizo. Walimu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu, wanastahili kulipwa haki zao za likizo, waende majumbani kwao kupumzika, sasa wanaponyimwa haki hii mwaka hadi mwaka wanakosa gani? Wanafanya kazi, wanatekeleza wajibu wao. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iliangalie suala hilo.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni suala la wataalam. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa *concern* yake kwamba tunahitaji kuongeza wataalam katika maeneo mbalimbali. Ninaomba nieleze hapa tatizo ambalo tunalo sisi katika eneo letu la Mkoa wa Lindi juu ya wanyamapori, ndovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo letu la Mchinga katika Kijiji cha Narunyu ndovu wanafika mpaka mlangoni kwa mwananchi, Afisa Wanyamapori yuko mmoja, walivyomfuatilia Wilayani hakupatikana. Katika Wilaya ya Lindi Vijijini ukizingatia kwamba tunazo hifadhi za misitu na ndovu wako pale, tunaomba wanyama wasiwaachie kuja kuwatia adha wananchi.

Tunaomba suala hili lizingatiwe kwa haraka ili wananchi wale wasiendelee kupata adha ya kufuatwa na ndovu. Ukienda Liwale simba mpaka Liwale Mjini, Afisa Wanyamapori yuko mmoja. Kweli wapo watu wa *Selous* pale tunashirikiana nao lakini eneo lile ni kubwa. Kwa hiyo, mimi napenda kulipongeza wazo hili lakini naomba hatua za haraka zichukuliwe ili wananchi wetu wapunguziwe adha hii ya kufuatwa na wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika suala la utumishi upo upungufu mkubwa wa watumishi Hospitalini. Nimewahi kutembelea katika Hospitali ya Kilwa nikawakuta manesi wengi ambao ni *Auxiliary* ambao siyo *properly trained, one year training.* Ninaomba basi Serikali iangalie uwezekano wa kuwapeleka watumishi wanaotakiwa hasa manesi maana huduma ya afya ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kwamba ningependa kuzungumzia suala la vituo vya afya. Katika Mikoa yetu hospitali kuu ziko mbali lakini vituo vya afya ndiyo viko karibu na wananchi. Lakini hali ya vituo vya afya vingine ni mbaya na vinatia huruma. Kituo cha Afya cha Masoko Kilwa kinatia huruma, kiko katika *pathetic situation.*

Mheshimiwa Spika, nilitembelea pale *ceiling-board* zinadondoka, huduma zenyewe unakuta nesi ni mmoja tu hakuna waganga wa kutosha. Sasa vituo vya afya hivi vikiachiwa ni hatari. Nichukue mfano wa Kituo cha Afya cha Rutamba, hiki kituo tumekirithi kutoka kwa kambi ya wakimbizi iliyokuwepo, lakini mimi sidhani kama Serikali imekwishafanyia *maintenance* yoyote, hali yake ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke mpango wa makusudi wa kuweza kuvihudumia vituo hivi vya afya ili viweze kutoa huduma ambayo inastahili na wananchi wawe na matumaini.

Mheshimiwa Spika, Mikoa yetu mingi hasa sisi Kusini hatuna umeme. Sasa kama mnashindwa kutupa kituo cha umeme pale Wilayani basi angalau mpeleke umeme kwenye kituo cha afya ili huduma kama za *X-ray* na mengine yaweze kutolewa.

Sisi Lindi tuko jirani sana na Kidatu lakini umeme wa *grid* hauwezi kufika kwa sababu ambazo hazieleweki na pia umeme wa Songosongo hauwezi kufika Lindi kwa sababu ambazo hazieleweki. Basi tunaomba mtupelekee umeme wa *solar,* Serikali iweke mpango, iombe hata msaada kwa wafadhili, tushirikiane ili tupate umeme wa *solar* katika vituo vyetu vya afya.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ningependa kuungana na msemaji aliyepita kwamba kweli kuna vijana wengi wanahama Vijijini na kwenda Mijini.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya vijiji vyetu, nichukue mfano wa Ruponda kule Nachingwea, vijana wameungana wanalima bustani wanazalisha nyanya nzuri lakini kwa sababu hakuna barabara nzuri bei wanayolipwa ni ndogo, wanapunjwa mwaka hadi mwaka, tenga la nyanya shilingi 5000/=, sasa huyu ataendelea lini? Ndio maana anafikiria ngoja nikimbie niende mjini nitapata akifika mjini anapatikana.

Kwa hiyo, naishauri Serikali mpango wake wa kutengeneza barabara uwe makini na ikiwezekana fedha za *Fuel Levy* ile asilimia ambayo inapelekwa Mikoani basi iongezwe ili tuweze kuzihudumia hizi barabara za vijijini. Tuwape matumaini vijana na wanawake hawa ambao wanashinda mashambani, wanalima lakini mavuno yao bei wanayopata ni ndogo kwa sababu mlanguzi anakuja na gari lake, asipouza gari yenyewe inayokuja ni ile moja kwa hiyo anauza kwa kukandamizwa.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho kinawahamisha vijana hawa ni kwa sababu hakuna burudani ya aina yoyote ile. Sinema inakuja mara moja kwa mwaka na kama barabara ni mbovu hiyo mara moja kwa mwaka yenyewe unaweza usiione. Wakati wa *World Cap* vijana wanahama kuja vituo ambako kuna umeme ili waone mpira maana na wenyewe wanakuwa na hama ya kuona vitu hivi.

Kwa hiyo, mnawavutia waje mijini. Sasa hebu tuangalie kuna *waterfalls* ndogo ndogo ambazo zimekaa huko zizalishe umeme. Siku moja kwenye *Television* niliona kuna kijana amebuni *turbine* yake kwa kutumia *waterfall* kijijini. Mbunifu kama yule angeendelezwa ili ile *knowledge* yake iweze kusambaa na kuweza kutumia vyanzo vile vidogo tulivyonavyo kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGOBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, labda nianze na suala la posho kwa ajili ya Madiwani. Wabunge wenzangu waliopita wamezungumzia suala la posho kwa ajili ya Madiwani, hivi karibuni Serikali imetangaza kuwapa mishahara Maafisa Watendaji na Maafisa Watendaji wanafanya kazi kwa usimamizi wa Madiwani na Madiwani ndio hasa wanafuatilia maendeleo ya Kata zao, leo hii kama tutakuwa tunawapa mishahara Maafisa Watendaji Madiwani wakaendelea kupata posho zile zile ambazo wanazipata mpaka sasa hivi ni kutowatendea haki na ni kuwanyima haki za kibinadamu.

Kwa hiyo, naomba Madiwani wafikiriwe upya. Kama wenzangu walivyosema, kama kuna sheria ina tatizo ya kuongeza posho au kuwapa mishahara basi hizo sheria ziletwe hapa Bungeni ili ziweze kurekebishwa na hatimaye Madiwani wetu wapate hela kwa sababu hawa Madiwani ndio wanatusaidia kusimamia maendeleo na hatimaye tunajiona kama tuna viongozi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni jambo ambalo si la haki kama nilivyosema, kwanza Wabunge waliwahi kupiga kelele suala la kuwapa usafiri Madiwani wetu kwa sababu Madiwani wetu wanakwenda maeneo ya mbalimbali ya Kata zao na Kata nyingine ni kubwa mno kiasi ambacho kwa kutembea kwa mguu na ukizingatia posho wanayopata haikidhi mahitaji ya yule Diwani. Naomba kama inashindikana kuwanunulia Madiwani magari basi tuwape pikipiki za kuwawezesha kuzungukia maeneo yao na kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la wataalam, Manispaa nyingi zinapewa wataalam ambao wanasimamia shughuli mbalimbali kama vile za ujenzi wa barabara, nyumba na vitu kadhaa. Lakini kuna maeneo wanapewa ma-*engineer* ambao kwa kweli sio wataalam ni kama wababaishaji. Anafanya *estimation* ya kutengeneza daraja kwa shilingi milioni 40 wakati kumbe daraja hilo linaweza kutengenezwa kwa shilingi milioni 20, *engineer* kama huyo hatumuhitaji kwa sababu anatutia hasara.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu katika Manispaa yangu ya Temeke tunaye-*engineer* ambaye tuna matatizo naye muda mrefu. Pamoja na kupiga kelele lakini inaelekea kikwazo kiko Ofisi Kuu ambayo nadhani ndio inatoa wataalam hao kwa shughuli za maendeleo yetu. Kwa hiyo, nashauri wale ma-*engineer* ambao tunaona hawafai tunapoleta ripoti zetu zifanyiwe kazi na wale ma-*engineer*

waondolewe kabisa au kupewa mafunzo zaidi lakini kama tunang'ang'ania ma-*engineer* hao hao kila wakati ambao tunajua kabisa wanatutia hasara inakuwa haitusaidii.

Mheshimiwa Spika, hata mwaka 2002 niliwahi kusema kule kwangu kuna daraja moja linaunganisha Kwamangaye na Mtaa wa Nyoka na Sokoine, daraja hili mara ya kwanza lilijengwa kwa shilingi milioni 28 na mpaka leo hii halipitiki kwa sababu unajenga daraja wakati unajua kabisa barabara haitapitika.

Sasa kwa ni nini tupoteze hela kufanya vitu kama hivyo ambavyo tunakuwa hatuna kazi navyo baadaye. Kwa hiyo, nashauri Waziri mwenye dhamana anapopewa ripoti ya watu kama hao aifanyie kazi na kutusaidia sisi tusipige tu kelele kila wakati hapa tunaonekana kama hatuna maana. Kwa hiyo, naomba atusaidie katika hilo kwa kuwaondoa wale ambao tunawaona ni wabovu tupewe ma-engineer wengine ambao wanaweza kutusaidia katika maendeleo ya kuinua Taifa letu katika hadhi ambayo inatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Uhasibu, naipongeza Manispaa yetu ya Temeke katika mahesabu yake imekwenda vizuri nadhani ni watu wa tatu au wa kwanza katika kupata *Clean Certificate* lakini maeneo mengine Wahasibu wengi wamekuwa ni wababaishaji kama ulivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba kuna Halmashauri nyingi ambazo hesabu zao hazikwenda vizuri kwa sababu ya kukosa wataalam wazuri katika maeneo yao. Cha msingi Mheshimiwa Waziri hawa Wahasibu wetu tukiona kwamba hawafanyi vile tulivyokusudia wapewe nafasi ya kwenda kusoma zaidi ili wasituharibie mahesabu yetu.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia kwa kirefu kidogo suala la Manispaa yangu. Toka nimeingia madarakani mwaka 2000 na Baraza letu la Madiwani kwa kweli nadiriki kusema naipongeza Manispaa kwa kazi kubwa na nzuri inayofanyika katika Manispaa hiyo. Kwa kipindi cha miaka miwili na nusu Manispaa hiyo imejitahidi kukusanya hela nyingi, kujenga shule mbalimbali mbali na pesa ambazo zimetolewa na Serikali Kuu, imejitahidi pamoja na mradi wa *TASAF* kusimamia miradi mbalimbali ambayo imeletwa katika Manispaa yetu, sasa hivi tumejenga Ofisi nzuri ya kisasa ambayo hivi karibuni tunakusudia kumwomba Rais pamoja na Waziri waje kuifungua Ofisi hiyo mpya.

Mheshimiwa Spika, lakini nasikitika kusema baadhi ya viongozi, Waziri mwenye dhamana, Waziri Mkuu hata Rais anafahamu, kuna baadhi ya viongozi wa zamani ambao walikuwa viongozi, wengine walikuwa Mameya na Wabunge, katika maeneo haya wameleta chokochoko katika Manispaa ya Temeke bila sababu ya msingi na ni aibu kwa kiongozi maarufu kama yule ambaye CCM inamwita maarufu nadhani mimi sioni sababu ya kumwita maarufu mtu ambaye anachochea kusiwepo na maendeleo, sitegemei kama huyu mtu naweza kumwita maarufu. Sitaki kumtaja jina lakini mtu huyu anajijua ameanzisha utaratibu ambao sisi hatukuutegemea tulitegemea yeye angekuwa kama kiongozi wetu wa zamani angetupa ushauri jinsi ya kufanya kazi lakini kiongozi huyo amekuwa mstari wa mbele kuleta mambo ya mitaani Ofisini au kwenye Baraza la Madiwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nitakayosema naomba uniwie radhi, huyo mtu ameleta mambo ya mapenzi ambayo yanatoka mitaani na kuyaleta kwenye Baraza la Madiwani. Anajaribu kuandika barua za uchochezi kwamba sisi tumwondoe Meya kwa kutumia baadhi ya Madiwani, kwa kweli kutokana na umaskini wao nadhani anatumia hela kuwashawishi Madiwani wale wamkatae Meya aliyekuwepo kwenye madaraka.

**MBUNGE FULANI:** Chokochoko.

**MHE. FRANK G. MAGOBA:** Hiyo ni chokochoko ya kutuletea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu huyo bila aibu, nasema wazi, kama alivyosema anafanya mapenzi huko mitaani sasa bahati mbaya katika mambo yao nadhani wamekutana kwa mwanamke mmoja mtu huyo analeta hoja Ofisini kwenye Baraza la Madiwani kwamba tumwondoe Meya kwa sababu Meya ametembea na huyo mwanamke mambo kama hayo wasituletee Ofisini ni mambo ya mitaani hayo. Nimesema nizungumzie wazi ili hata Rais ajue kwamba hatukupendezewa. Nilitegemea sisi watu wa Upinzani ndio

tungekuwa tunazungumza vitu hivyo lakini watu wa CCM ndio wanaunga mkono mambo hayo. Hili ni jambo la aibu, sisi tunaona Manispaa inafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri kwenye Baraza langu la Madiwani kuna Wapinzani kama kumi lakini tuna ushirikiano mzuri. Napenda kusema wazi kwamba katika Jiji la Dar es Salaam Manispaa ya Temeke inapaswa kupata sifa kwa sababu kwanza ndio Manispaa pekee yenye Madiwani kutoka Upinzani na ndio inayofanya vizuri kuliko hata Manispaa nyingine. Lakini huyu mtu ningeshauri Serikali, Waziri unafahamu na Waziri Mkuu anafahamu adhibitiwe na Chama chake cha CCM, asituharibie sisi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Manispaa yetu inafanya vizuri, Mkurugenzi wetu ni mzuri, Meya ni mzuri na Madiwani ni wazuri japo kuna Madiwani wachache ambao wanatumiwa na mtu huyo kwa sababu ya umaskini wao. Naomba sana suala hili Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Waziri Mkuu na Rais, juzi juzi nasikia kwamba mtu huyo baada ya kusikia tumepiga kura ya kumuunga mkono Meya ameona haitoshi na katika mahojiano amesema yeye hana ugomvi na Manispaa isipokuwa ana ugomvi wake na Meya sasa anataka tuvunje Manispaa kwa sababu yake, kwa sababu ya starehe zake, hatuwezi kukubaliana na suala hilo. Nasema kabisa hatuwezi na tutasimama imara kama Wapinzani kuhakikisha kwamba yule Meya aliyekuwepo hata kama ni wa CCM anafanya kazi nzuri, kitu kama kinafanyika vizuri tunakubali kitu kama hakifanyiki vizuri tutasema, yule Meya hana tatizo. Tatizo ni watu ambao wanajifanya wao ni wazoefu, ni wa siku nyingi na wana umaarufu, umaarufu hatuwezi kuuleta kwenye kazi.

Mheshimiwa Spika, yeye ana Ofisi yake akafanye kazi zake, kazi zake zinamshinda anakuja kufanya kazi kwenye Manispaa kwa sababu gani? Naomba sana suala hili liangaliwe, Waziri mwenye dhamana unanisikia, Waziri Mkuu ananisikia na juzi juzi Rais ameandikiwa barua na huyu mtu kutokana na umaarufu wake anafikiri kumwandikia Rais barua atavunja Manispaa ya Temeke hatavunja na sisi hatuko tayari katika hilo. Naomba sana suala hili lichukuliwe kwa uzito mkubwa kwa sababu ni vitu vya aibu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mitaa yangu mingi ya kule Mbagala, Charambe, Tuangoma na maeneo kadhaa kwa kweli barabara zake bado si za kuridhisha sana japo mipango ipo lakini inakwenda polepole.

Naomba pia suala hili lifanyiwe kazi kwa sababu sasa hivi maeneo hayo yamevamiwa na watu wengi, si kuvamiwa *in such* kwamba baada ya Waziri wa Ardhi kutangaza kutoa ardhi kwa Watanzania mbalimbali barabara zinahitajika pamoja na miundo mbinu ya maji kwa sababu ya kutoa huduma kwa watu ambao wamenunua viwanja vyao.

Hivi karibuni nadhani wengi ambao wamenunua viwanja kule wanahitaji kujenga nyumba zao ili kuliweka Jiji la Dar es Salaam katika hadhi ya Kitaifa lakini mpaka sasa hivi mambo mengi bado hayajafanyiwa kazi.

Kwa hiyo, naomba Wizara inayohusika ifanyie kazi hata kama suala hili litakuwa halihusu Wizara hii lakini kwa kuwa nimesimama na kuchangia ni moja ya hoja ya kuiambia Serikali kwamba maeneo mengi tunahitaji maji, barabara na miundombinu ya umeme kwa sababu maeneo mengi umeme hakuna.

Mheshimiwa Spika, ya kwangu ni hayo ilikuwa lazima nifoke kwa sababu sikupendezewa na hilo lakini kwa kuwa nimefoka najua Serikali imesikia na huyo mtu ambaye anatuharibia Manispaa yetu naomba adhibitiwe ili aendelee na shughuli zake asiingilie Ofisi za watu wengine, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nyingine tena katiba Bunge hili la Bajeti ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri Brigedia Mstaafu Hassan Ngwilizi na Naibu wake, Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu yetu Mmari, tunamfahamu sana pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii ambayo ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Kifungu cha 34 kinachozungumzia sekta ya huduma za kiuchumi, nilisema kwamba Manispaa yangu ya Temeke hupokea fedha za miradi ya maendeleo kupitia Wizara hii ya TAMISEMI. Fedha hizo za maendeleo ni kama vile fedha za barabara, elimu, Hospitali *(Basket Fund)* na fedha nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Manispaa yangu ya Temeke kwa kazi nzuri inayofanya. Fedha hizi jinsi tunavyozipata kwa mafungu yake huzifanyia kazi kama zilivyopangwa na si vinginevyo. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Ndugu yangu Iddi Nyundo, pamoja na watendaji wote wa Manispaa ya Temeke bila kuwasahau Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali kwamba fedha hizi sisi tunapoletewa tunazifanyia shughuli zilizopangiwa bila kukiuka taratibu za kisheria. Kwa kufanya hivyo, kama alivyozungumza Mheshimiwa Magoba, Mbunge mwenzangu kutoka Jimbo la Kigamboni sasa hivi ukifika Temeke sio Temeke ile ya zamani Temeke ina mabadiliko makubwa sana. Mabadiliko haya kwanza tumejenga jengo la utawala kubwa kabisa la Ofisi ya Manispaa ya Temeke na tumeshatoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais ili aje kutufungulia Ofisi hiyo. Ofisi hiyo iko karibu na barabara ya Mandela karibu na sehemu ambayo kutajengwa Uwanja wa Taifa wa kisasa. Kwa hiyo, Manispaa ya Temeke itapendeza kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yote niliyoyaeleza yamekuja kutokana na dhana kubwa ya ushirikishwaji ndio maana nimeona niwapongeze sana viongozi wa Manispaa ya Temeke wakiwemo Madiwani kwamba tunafanya kazi *as a team work* na ndio maana tumeweza kupata mafaniko haya mazuri ninayoyaeleza hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nina maombi mawili. Ombi la kwanza kama nilivyosikia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anayo azma ya kutaka kuwapunguzia Waheshimiwa Madiwani majukumu yao, mimi nasema ni kutaka kuwapunguzia kwa sababu nimesikia kwamba anataka kutowahusisha katika Kamati za Zabuni. Niliposikia hili kwa kweli nilishtuka sana kama azma hii ipo kabla ya kufanya azma hiyo, nina ombi hili.

Mheshimiwa Spika, wakati sisi tukizungumzia dhana ya ushirikishwaji wa wananchi ambao ndio wadau wakubwa tunapofikia kwenye masuala ya maamuzi hususani hayo ya kuingia katika Kamati hizi za Zabuni, Waheshimiwa Madiwani ndio wawakilishi wa wananchi wanapoingia katika *tender* hizi ama Kamati hizi wanawawakilisha wananchi kwa ujumla. Sasa haliniingii akilini kama kweli Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anayo dhamira hiyo huu uwakilishi utakuwa vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninao mfano, ninatoka Mkoa wa Dar es Salaam, katika kumbukumbu miaka kama mitatu ya nyuma Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliwahi kuvunjwa na wananchi walikosa uwakilishi. Wakati ule ninakumbuka Mheshimiwa Charles Keenja, Waziri sasa wa Kilimo na Chakula, ndiye aliyepewa dhamana ya kusimamia Jiji la Dar es Salaam mara baada ya kuvunjwa alifanya kazi nzuri sana Mheshimiwa Keenja na kwa kweli nampongeza sana. Kazi ile aliyoifanya katika Mkoa wa Dar es Salaam ndio iliyofanya hasa tumtambue Keenja ni nani, alifanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi ile aliyokuwa akiifanya mimi nasema ni nzuri lakini wapo watendaji waliotumia nafasi ile ya kukwepa na kufanya vitu vyao, wapo watendaji ambao walikuwa wanamzunguka Mheshimiwa Charles Keenja wakafanya vitu vyao kwa maana ya kufanya matumizi mabaya ya pesa. Mimi napatwa na wasiwasi na azma hii ya Mheshimiwa Waziri kama kweli hilo anataka kulifanya naomba akaliangalie tena kwa makini ikiwezekana basi ajaribu kutumia washauri ili kuangalia kwani wakiwemo Madiwani katika Kamati ya *Tender* ni katika kusaidia na kuelekeza kwamba hapa tufanye hivi au la na kuna madhara gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika suala ambalo wenzangu wamelizungumza, unisamehe sana Mheshimiwa Spika usije ukanipiga na kile kifungu kinachokataa kurudiarudia. Kwa nini nasema hivi?

Mimi nimewahi kuwekwa kiti moto na Madiwani wa Temeke, bahati mbaya sana Mheshimiwa Magoba siku hiyo hakushiriki sisi Temeke tuko Wabunge wawili tu kwa hiyo huwa tunashiriki kikamilifu katika vikao vyote kwa kweli bila tatizo. Nilikwenda kwenye mkutano siku hiyo ulikuwa ni wa Kamati ya Fedha na mimi naingia. Bahati nzuri siku hiyo tulikuwa tumetembelewa na Waheshimiwa Madiwani kutoka Mkoa wa Mara sasa tukawa tuko kwenye mazungumzo basi nilijikuta nimefungwa ninaulizwa wewe kama Mbunge unasaidia nini kumwelezea Waziri kuhusu posho za Waheshimiwa Madiwani? Nilishindwa kujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nakumbuka na Mheshimiwa Waziri nadhani atakumbuka kama siyo yeye ni Naibu wake sisi Temeke tumemfuatilia sana kuhusu masuala ya maslahi ya Madiwani wetu. Katika mazungumzo ya kawaida tulifikia mahali Mheshimiwa Waziri ametuahidi kwamba kama kuna Halmashauri au Manispaa itafanya vizuri katika makadirio yake ya mapato itavuka basi wanaweza kuwafikiria kuweza kuongeza posho za Waheshimiwa Madiwani. Hili nalikumbuka na Mkurugenzi wangu tulikuwa tunafuatilia sana suala hili lakini bado tulikuwa hatujaweza kupata uamuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri lakini Temeke tumefanya vizuri katika makusanyo ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hili maana najua nitaulizwa umesema nini kuhusu hilo nilishawekwa kiti moto, watu wa Mara wamesikia na Waheshimiwa Madiwani wa Temeke watakuwa wamesikia.

Mheshimiwa Spika, naomba nije katika ombi langu la pili kuhusu hili suala ambalo sisi tunalishangilia sana na wananchi nchi nzima wanalishangilia la kufuta Kodi ya Maendeleo. Pamoja na Kodi hii ya Maendeleo kufutwa sisi Mkoa wa Dar es Salaam sijui wengine kwa kiasi fulani tumeathirika katika mapato yetu. Nalisema hili kwa sababu mimi ni Diwani katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, nafahamu vyanzo vya mapato yetu kimojawapo kilikuwa ni kodi hii. Sisi tulikuwa hatupati nayo tatizo kwa sababu tulikuwa tunaichukua kwa asilimia kutoka kwa wafanyakazi moja kwa moja ilikuwa inaingia Jiji tulikuwa hatumfuati mtu mmoja mmoja na mapato haya tulikuwa tunayapangia matumizi.

Nashukuru Serikali imefuta kodi hii na nishukuru sana Mheshimiwa Waziri amesema kwamba atatoa ruzuku, naomba hizo ruzuku zitoke kwa uwazi isiwe kwa upendeleo ama kwa kufuatilia kwa muda mrefu tutaathirika sana katika matumizi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, nizungumzie suala la Walimu. Wenzangu wamelizungumza lakini naomba na mimi nilizungumze kwa aina yake. Humu Bungeni wengi wa Waheshimiwa Wabunge ni Walimu na ndio maana unaona michango ya Waheshimiwa Wabunge inakuwa mizuri kwa sababu mimi namwogopa sana mtu anayeitwa Mwalimu. Mwalimu ana uzoefu anakuangalia kuanzia ulivyovaa, unavyozungumza kisha anatoa maksi kwamba wewe unafaa au hufai. Mwalimu tumekuwa tukimtumia katika masuala mbalimbali kwenye uchaguzi tunawatumia Walimu kusimamia na juzi wamefanya kazi ya kusimamia shughuli za sensa lakini inapofika kwenye kudai maslahi yao, Walimu tunawasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninalisema hili kwa uchungu, juzi nilikuwa kwenye sherehe za Mei Mosi nadhani na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwepo Walimu walipita pale na bango lao ambapo ujumbe wao ulikuwa haupendezi kwa sisi viongozi. Wameandika bango linasema : “Kauli za Mawaziri,” sasa tupo pale kwenye *high table* na Mheshimiwa Rais anaona kwa kweli inasikitisha. Ni kwa nini wanasema hivi? Ni pale wanapoona wanadai haki zao wanasahauliwa lakini tuelewe kwamba Walimu ndio wanaotufanya sisi tuzungumze hapa bila Walimu mimi nisingeweza kufika hapa hata na wewe Mheshimiwa Spika, nisamehe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Walimu wamefikia mahali pa kusema kwamba kama sisi haki zetu na kwa kweli wamenituma, walikuwa wananialika katika shughuli zao kila ukienda wanakosomea suala hili hawataki kudharauliwa wanataka haki zao. Wamefikia kusema kwamba kama sisi hamtujali na kuona sisi hatuna mchango wowote mkubwa katika Taifa hili basi tutumie elimu yetu hii ya Ualimu kulifanya Taifa hili lizalishe wanafunzi ama watu hafifu?

Nadhani mnanielewa ninapozungumza namna hii. Wagomee tu katika kufundisha *production* iwe mbovu mbovu watu wana feli na nini. Mimi nikasema hapa tusifikie huko. Hili nalisema nina uhakika na

nimetumwa na Walimu, kwa kweli ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri Walimu wanasema hivi sisi hatuna baba? Wanaposema hawana baba sio baba wa kuwazaa baba kwa maana ya Waziri anayehusika kwa sababu kilio chao hakisikilizwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja hii, nadhani Mheshimiwa Waziri atakuwa amesikia na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi ya pekee kumshukuru sana Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI lakini pia nimpongeze Naibu wake. Timu hii ya Askari wa Miamvuli kwa kweli mara baada ya kushika mianvuli yao ilianza kazi kwa kukabidhiwa majukumu makubwa sana ya kusimamia utendaji wa kazi katika maeneo ya Serikali za Mitaa ambapo mpango wa maendeleo ya nchi ya Tanzania ulipelekwa moja kwa moja, naomba niwapongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mawaziri hawa hawakuwa wakifanya kazi peke yao. Kwa kweli hatuna budi pia kuchukua nafasi ya pekee kuwapongeza sana Wenyeviti wa Halmashauri zetu, Ma-*Mayor* wanaoongoza Halmashauri zetu na Miji yetu katika maeneo yote ya Serikali za Mitaa, lakini wakishirikiana bega kwa bega na Waheshimiwa Madiwani katika mipango yote ya maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. Mimi naomba niwapongeze wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upo usemi unaosema kwamba mara zote harusi ikifana sana ina maana harusi hiyo imekuwa na chakula cha kutosha, imekuwa na vinywaji vya uhakika, lakini pia imekuwa na waimbaji na chereko chereko za namna mbalimbali. Lakini msiba ukisema msiba ule ulifanikiwa ni kwamba ulikuwa na watu wengi lakini pia vilio vilikuwa vingi sana na vya namna tofauti. Sasa vilio vinapokuwa vingi na vya namna tofauti ina maana kwamba huyo marehemu aliyefariki ama mwenye msiba ana mahusiano ya namna yake, ana umaarufu wake ama ana hali ya namna ya pekee inayopelekea kila mhudhuriaji katika tatizo hilo anaguswa kwa kiasi cha karibu sana.

Mheshimiwa Spika, jana jioni nilikuwa naongea na Mheshimiwa Stephen Kahumbi, tunajaribu kubadilishana mawazo. *(Kicheko)*

Wakati tunabadilishana mawazo na Mheshimiwa Stephen Kahumbi jana jioni kwa kweli tuligundua kwamba kilio kikubwa cha Bunge letu hili katika kuchangia hoja ya Waziri wa TAMISEMI ni jinsi gani Waheshimiwa Madiwani wataangaliwa kwa macho mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoanza mwanzo kwamba kama kilio hicho kimekuwa cha watu wengi na chenye sauti kubwa basi ina maana kwamba lipo jambo katika kutoa maslahi ya mishahara ama posho kwa Waheshimiwa Madiwani.

Kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba ni lazima tufikie wakati tukubaliane kwamba umefika muda muafaka wa kuzingatia matokeo ya kilio hiki ambacho kimepigwa kelele sana katika Bunge letu katika kikao chako hiki cha Bunge hili la bajeti la mwaka huu. Hapa sitaki kuendelea kuzungumza zaidi, nafikiri ujumbe wangu umefika na nimeeleweka inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niendelee kwa kusema kwamba tumekuwa na kada mbalimbali za viongozi katika nchi yetu ya Tanzania. Katika suala zima la kupeleka madaraka katika Serikali zetu za Mitaa kada hizo za viongozi mbalimbali wamejitahidi sana kuhakikisha ushirikishwaji wa jamii na utawala bora unafika katika maeneo husika. Kabla sijaendelea naomba nichukue nafasi ya pekee kuwapongeza Wakuu wa Mikoa wote katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haitoshi sisi kuendelea kujivuna na kusema kwamba tumekuwa na mafanikio ya kimaendeleo bila kuwakumbuka Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa yetu. Wamekuwa wahimili wazuri. Mimi ninayo mifano kadhaa kutoka katika Mkoa wangu wa Ruvuma. Kwa kweli Mheshimiwa Mkuu wetu wa Mkoa akisaidiana na Katibu Tawala wetu wa Mkoa, Ma-*DC* na viongozi wengine mbalimbali wamesaidia sana katika kuhakikisha maendeleo yanafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Msingi kama siyo ushirikishwaji wa pamoja wa nguvu hizo za viongozi mbalimbali basi Wilaya yetu ya Mbinga isingevuka lengo la kuwa na madarasa 121 kwa Wilaya hiyo kufanikiwa kujenga madarasa 334 na ni madarasa 12 tu ndiyo yanayoendelea kujengwa lakini katika mpango huu huu wa Serikali, kwa hiyo huo ni ushirikishwaji ambao lazima uonyeshwe na lazima tuweze kujipongeza.

Mheshimiwa Spika, katika jedwali Na. 16 mpaka mwaka 2003 ripoti ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha kwamba Wilaya ya Songea Mjini haina madeni. Lakini pia Wilaya ya Mbinga nayo haina madeni. Haya ni maeneo ambayo yanaonyesha upo ushirikishwaji wa uongozi pamoja na chombo chetu cha Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, miradi kama ya *TASAF* imefanya kazi kubwa sana Songea Vijijini na Wilaya ya Tunduru. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba tunayo nafasi ya kutembea kifua mbele na tunasema kwamba sisi sasa hivi hatufuati nyayo bali tunafuata mwelekeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu anayefuata nyayo hawezi kujua aliyetangulia alikanyaga kwenye moto ama kwenye takataka. Lakini anayefuata mwelekeo ni yule anayeangalia maendeleo na mahitaji ya binadamu katika kuona kwamba kumekuwa na maendeleo yenye kuwa viashirio yako wapi na hivyo basi Wizara hii inafuata mwelekeo katika kuleta maendeleo na siyo kufuata nyayo ambazo unaweza ukajikuta unakanyaga moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya pongezi na kueleza hayo niliyoyasema ninaomba sasa nizungumze mambo mawili au matatu ambayo nafikiri yananitia kigugumizi kidogo kwa kuona uhalisia wa shughuli zenyewe katika Wizara hiyo. Nilikuwa najaribu kupitia suala zima la kuipongeza Serikali kwa kuondoa kodi ya maendeleo, ni wazo la msingi na linapongezwa na mimi nalipongeza kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Ruvuma na jamii nzima.

Lakini mimi nilikuwa nataka tu kufahamu asilimia kumi ya mapato yakiwemo ya kodi za maendeleo yalikuwa yanatumika kuendeleza Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake. Je, kama ruzuku haitatolewa haraka ule umaskini wa kipato kwa wanawake si utaanza tena kwenda juu? Kwa sababu misimu ya miradi na biashara yao imefika na kiasi cha pesa ambacho kingeweza kukidhi mahitaji yao hakitaweza kupatikana kwa karibu na kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, wakati napitia majedwali nimeona kabisa kwamba makisio ya mapato katika Halmashauri zetu yamekuwa yakiwiana toka mwaka 1999 mpaka mwaka huu wa 2003 kwa maana ya kwamba mpaka sasa hivi kwenye jedwali la makisio kodi ya mapato haijaondolewa katika makisio yale. Kwa maana hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aone lile pengo litakuwaje na litafanyiwaje kazi kwa haraka sana ili kuweza kutetea kada hiyo ya ajira kwa vijana na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nichukue nafasi ya pekee kushukuru Wizara kuona kwamba hata sisi Wilaya zetu kama vile Tunduru, Mbinga na Namtumbo zimeingizwa katika programu ya Miji midogo midogo endelevu. Lakini mara nyingi tunapoingiza neno la Mji mdogo miradi mingi ya maendeleo inakuwa ikiepushwa kwamba watu hao tayari wapo kimjini mjini, kwa hiyo, miradi mingi iende kwenye Vijiji. Pamoja na kwamba Miji hiyo inaitwa Miji lakini naomba mipango yote ya maendeleo bado ipelekwe kwenye hiyo Miji midogo ili iweze kuboresha zaidi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba pia ushirikishwaji wa Halmashauri kwa maana ya kwamba tunacho chombo chetu cha *ALAT* kipo katika ngazi za Mikoa lakini pia katika ngazi za Taifa.

Mimi nilikuwa nafikiri kwamba masuala haya ya uboreshaji wa Serikali za Mitaa basi nadhani kuwe na ushirikishwaji wa karibu baina ya chombo hiki cha *ALAT* ambacho kinaelewa na kusimamia sana kwa karibu masuala yote ya Serikali za Mitaa ili kiweze kuunganisha nguvu kwenye Serikali Kuu na hivyo mipango yote ya maendeleo iweze kueleweka vizuri. Pia kwa sababu Madiwani ndiyo watekelezaji wakubwa basi nafikiri kazi hizo zitakwenda kwa urahisi zaidi kuliko kama hatutakuwa na ushirikiano wa karibu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na tatizo lingine kidogo kwenye suala zima la uanzishaji wa Vijiji. Nimejaribu kupitia kwenye jedwali linaloonyesha Kata na Vijiji vilivyopo. Naamini sasa hivi tunataka kutoa ajira mpya kwa Watendaji wa Kata, Vijiji, Vitongoji, Mitaa na kadhalika. *Data* nilizo nazo hapa zinanichanganya kidogo, ipo Mikoa mikubwa kieneo, ipo Mikoa yenye *population* kubwa na ipo Mikoa inayoonyesha kabisa ongezeko la watu linakwenda kwa kasi sana.

Pamoja na hayo yapo maeneo yenye uchumi ambao unafanya kazi au upo motomoto, kwa maana hiyo kwamba ongezeko la watu katika maeneo hayo litaendelea kukua kwa haraka. Lakini Vijiji vilivyosajiliwa na kuruhusiwa kupata jina la Vijiji ni vichache na bado Vijiji vingine havijasajiliwa na huko tunakokwenda ninaamini kwamba kwenye ajira ya Utendaji Vijiji hivyo havitakuwa na hiyo kada ya Watendaji wa kazi hizo. Mheshimiwa Spika, sasa ninahisi Utawala Bora utachelewa kufika katika maeneo hayo kama suala hili halitaangaliwa na kuzingatiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona pia tuna tatizo la Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi. Jedwali linaonyesha bado waajiri wengi sana hawalipi na kama wanalipa basi wanapeleka michango hiyo bila nyaraka za wachangiaji. Hawa wachangiaji watakapotaka mafao yao itakuwa ni tatizo la nani? Mimi nilikuwa naomba sana Wizara iliangalie tatizo hilo ili kupunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kuiomba sana Wizara kwa kupitia hiyo Mikataba ya Huduma Bora kwa Wateja basi hebu sasa waangalie, wenzangu wamezungumza sana kwamba bado tuna matatizo makubwa sana ya huduma bora kwa wateja wetu ambao ni wadau wakubwa wa maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, watu hawapandishwi vyeo kwa wakati unaotakiwa, watu bado hawapati malimbikizo ya mishahara yao kwa wakati unaotakiwa na watu bado wanahangaika na mambo yao mengi mengi yanayowafanya washindwe kufanya kazi kama wafanyakazi bora katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Waziri amesema ni wakati wake mwingine wa kushughulikia suala hili la Mkataba wa Huduma Bora kwa Wateja, namwomba sana awaangalie hao Walimu, Manesi, Madaktari na kada zile zote ambazo zipo chini ya Wizara yake ili kuweza kuondoa kero hiyo na kusaidia sana kulijenga Taifa letu katika nguvu moja ya kupambana na umaskini kwa kupitia kazi zetu mbalimbali ambazo kila mtu ameajiriwa nazo.

Mheshimiwa Spika, mwisho na mimi naomba kusisitiza tunapozungumza suala la viongozi wa wawakilishi, tukizungumza suala la Madiwani tujue tunazungumza pia suala la Madiwani wa Viti Maalum. Madiwani wa Kata wanafanya kazi kwenye Ofisi za Kata, Madiwani wa Viti Maalum hawajui hata wakakae kwenye kiota gani ili waweze kufanya hizo shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee ninawashukuru sana wale viongozi wa Mikoa ambao wamezingatia uwepo wa ofisi za Wabunge katika maeneo yao. Sisi katika Mkoa wetu tunashukuru sana uongozi ingawa bado kuna matatizo madogo madogo, lakini tunashukuru kwani hata mimi tayari ninayo ofisi. Lakini yale mengine ambayo bado hayajakamilika basi tunaomba waendelee kutusaidia ili Wabunge tupate ofisi za kufanyia kazi ambazo kweli zinaweza kufaa, lakini na Madiwani waendelee kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuendelea kusema kwamba tufuate mwelekeo wa maendeleo na tusifuate nyayo, tusije tukaingia kwenye vichaka vya moto na tukashindwa kuvuka katika hii mikakati yetu tunayoiandaa ya kujiletea maendeleo halisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ili nisikiuke Kanuni ya kutukataza kurudia rudia yaliyosemwa na wenzangu na mimi niingie kwenye rekodi kwamba nawapongeza Mawaziri wote walioleta hotuba nzuri ikiwa ni pamoja na Waziri Mkuu lakini pia na Ndugu yetu Betty Mkwasa, aliyetuletea tuzo la Mwandishi Bora wa *CNN*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiangalia *Hansard* kati ya mwaka 1986 hadi leo mimi nimebahatika kujadili hoja ya Wizara hii ikiwa katika *portfolio* mbalimbali na muda huo wote aidha nilikuwa nikikosoa sana au nikitoa mapendekezo mbalimbali. Lakini kwa hii hotuba ya leo siyo kwamba naogopa usemi wa mwanafalsafa na mwanasheria mashuhuri wa Amerika na Rais wa tatu, Jafferson kwamba mwanasiasa anayekosoa muda wote na anapozidi kukosoa tu baadaye atakuwa ni mjinga, la hasha. Isipokuwa hali tuliyofikia sasa katika mchakacho wa sera na sheria za Serikali za Mitaa sasa umefika mahali pazuri na pa kutufanya sisi sote tusifu maendeleo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalazimika kwa hili lakini nisingependa kukosana kidogo na rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai juu ya nafasi ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya katika mchakacho huu wa mabadiliko ya sheria na sera katika Serikali za Mitaa. Kwa hali tuliyofikia Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa sasa wamefikia nafasi yao nzuri ya kufanya kazi yao nzuri ya kumwakilisha Rais katika maeneo yao. Sasa hivi hawana haja ya kuwa sehemu ya maamuzi ndani ya Baraza la Madiwani kwa sababu wakiwa sehemu ya maamuzi katika Baraza la Madiwani baadaye matatizo yatakapotokea Rais mwenyewe ndiye atakuja kuyashughulikia matatizo haya?

Kwa hiyo basi, katika hali kama hii tuliyofikia sasa huu mpango wa sasa wa kuelimisha Madiwani na hasa huu utaratibu wa maboresho ambao bila shaka kwa maoni yangu sasa utakamilisha mchakacho wa mabadiliko ya sera na sheria za Serikali za Mitaa ambapo Madiwani watakuwa na upeo mkubwa wa kuendesha Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Wizara imetugawia vitabu saba vya mafunzo ya Madiwani. Mimi naomba sana wenzangu msome vile vitabu. Mimi nimehudhuria mafunzo haya kwa Madiwani wa Halmashauri yangu na nimewafuatilia kwa karibu, nao wamegundua kwamba kwa hali ya sasa na baada ya mafunzo haya baadhi yao pengine watajiona kwamba wao hawatakuwa sehemu ya mabadiliko haya kwa sababu hawataweza kuwa na uwezo na upeo ambao unatakiwa uwepo katika uendelezaji wa Serikali za Mitaa katika karne hii. Hayo yote yamejitokeza katika hotuba ya Waziri ndiyo maana kwa mara ya kwanza katika miaka kumi na saba nafikiri siwezi kukosoa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 13 Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba: "Hatua ya kufuta kodi mbalimbali zinazotozwa na Halmashauri zinapunguzia Halmashauri mapato kwa kiasi kikubwa na pamoja na fidia zitakazotolewa kwa Halmashauri ambayo haitajitosheleza, suala la wananchi kushiriki kikamilifu katika kujiletea maendeleo yao haliwezi kuepukika." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumkumbusha Waziri mambo matatu muhimu sana. Kwanza, hii nchi ni kubwa na tuna tofauti kubwa sana. Pengine kodi ya maendeleo kuondolewa haitakuwa na athari kubwa kwa Wilaya kama Masasi kwa sababu ilikuwa inatoka kwenye korosho na mapato yake yalikuwa zaidi ya shilingi bilioni moja, Wilaya ambayo ilikuwa inakusanya vizuri sana. Lakini nenda Mafia mapato yake shilingi milioni 50, Mbunge wa Mafia kama yupo hapa ni shahidi, Temeke ni mashahidi wanakusanya bilioni nne na zaidi, Ilala pia bilioni nne na zaidi pamoja na Kinondoni. Sasa angalia Mbulu milioni 450 ni kodi ya maendeleo. Sasa katika Halmashauri zaidi ya 117 lazima kazi kubwa ifanyike kuziba pengo hili kwa sababu athari yake itakuwa kubwa. Kwanza fedha hizi zilikuwa zinasaidia kama *counterpart fund* kwa miradi ya wa fadhili ambao walikuwa wanafanya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, fedha hizi zinaingia kwenye akaunti inaitwa *general fund. General fund* pamoja na wengi wanailaani hiyo akaunti nzuri katika Halmashauri. Itakuwa siyo akaunti nzuri kama itatumika vibaya, lakini kama itatumika vizuri ni akaunti nzuri sana na mimi nashangaa itakuwaje akaunti hii ni mbaya kama kila mwezi Kamati ya Fedha na Mipango inakaa kujadili akaunti hii na matumizi yake. Nasema hivi kwa sababu hali hii itadhoofisha kwa kiasi kikubwa kwa asilimia zaidi ya sabini uwezo wa Wilaya na kwa Wilaya kama sabini. Hofu yangu Vijiji vitakuwa ni visiwa.

Mheshimiwa Spika, wengi hapa tunatoka Vijijini, karibu asilimia tisini. Utawala uliopo Vijijini bado upo katika *hangover* ya zamani na ya kimila. Kuna baadhi ya Wenyeviti wa Vijiji wanataka wawe kama wale viongozi wa kimila ambao huletewa chakula, vinywaji au walimiwe. Mwenyekiti wa sasa anatakiwa naye asaidiwe badala ya watu kumjia Mwenyekiti wa Kijiji, imekuwa ni tofauti kabisa.

Sasa ndiyo maana Utawala Bora hapa hautawezekana kwa sababu akili ya huyu Mtendaji wa Kijiji na Mwenyekiti wa Kijiji na Kitongoji na Balozi na hali halisi kule Vijijini hailingani na mchakacho wa sera na sheria zetu za Serikali za Mitaa za sasa. Ndiyo maana Wilaya ni kiungo muhimu sana. Afisa Wilaya, Mkurugenzi, Afisa Utumishi, Afisa Mipango akienda Kijijini pengine kwa miezi sita maajabu yatatokea, pengine watajitawala kwa namna ambayo itakuwa ni karne iliyopita. Ndiyo hii akaunti inayoitwa *general fund* ndiyo ilikuwa inatumiwa na Wilaya kujaribu kudhibiti Vijiji na Vijiji vyetu ni vingi, kuna Halmashauri hapa zina Vijiji zaidi ya mia tatu. Kwa hiyo naomba Mhshimiwa Waziri aliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulisema lakini limesemwa kwa uchungu sana na Mheshimiwa Benedict Losurutia, kuhusu mpaka na pia Mheshimiwa Mgana Msindai hapa amelisema. Mimi naamini Waziri wetu hisia zake za uzalendo ni za hali ya juu kwamba mipaka ya ndani haina maana yoyote kwake. Lakini siyo hisia za Watanzania wote, maana sehemu kama Kiteto na Kondoa watu wanauana, maisha ya watu yanaondoka, kwa hiyo, siyo jambo la kupuuzia na migogoro hii inapoteza fedha nyingi.

Mheshimiwa Mgana Msindai ameongelea mgogoro kati ya Mbulu na Iramba. lakini kwangu mimi nina mgogoro kati ya Mbulu na Karatu, Mbulu na Babati na hatujui sababu yake ni nini wakati kuna *beacons*. Kwa mfano, mpaka kati ya Mbulu na Iramba, *beacons* zimeshawekwa toka miaka mia moja iliyopita. Kama zilikuwa mbali basi Serikali ijitahidi ziwe karibu karibu. Kama kutoka *beacon* moja mpaka ya pili ilikuwa kilomita labda mia moja basi iwe kilomita hamsini, hamsini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Waziri kwamba mimi sijawahi kuona mwananchi akilalamikia kuhusu mpaka. Mheshimiwa Mgana Msindai ni shahidi hapa, uhamaji wa watu, biashara, mifugo hakuna hata siku moja tumesikia malalamiko hayo.

Mimi nafikiri kuna lingine zaidi ya haya. Nafikiri baada ya kuondolewa sasa kodi mimi na ndugu yangu Mheshimiwa Willbrod Slaa, sasa hatutakuwa na ugomvi kwa sababu upande wake kwa vile walipunguza kodi watu wa upande wangu walikuwa wanahamia kule. Kwa upande wa Babati pengine ni ugomvi tu wa ardhi. Bwana mmoja anataka kugawa ardhi toka upande wa pili wa Wilaya, kwa hiyo hili aliangalie sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo limeongelewa ni kuhusu Katibu Tarafa, katika hali tuliyotoka tumepiga hatua kubwa. Mimi nafikiri hatimaye upende usipenda Katibu Tarafa atakuwa sehemu ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sitaki kuongelea hilo, hivi kazi yake hasa ni nini pale kwenye Tarafa na pikipiki yake ambayo haipati mafuta? Lakini hata akipata mafuta, nitoe mfano wa Tarafa moja kule kwetu inaitwa Dongobesh. Dongobesh ina watu karibu 120,000. Kutoka Magharibi mpaka Mashariki ni kilomita 120, kutoka Kusini mpaka Kaskazini ni kilomita mia moja tisini na ana Vijiji karibu arobaini. Angetaka kufanya kazi angefanya vipi? Kwa hiyo, mimi nafikiri mnamwonea tu pale, watu laki moja na ishirini, Wilaya nyingi zina watu chini ya 100,000. Maombi haya Waziri anayafahamu, naomba ayashughulikie.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, Waziri anafahamu Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa inafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na Kamati hii tumeelewa Wilaya zetu zote na tumeweza kufanya malinganisho na tumejua udhaifu ni nini na tumejua pia maana ya kuwa na Mkoa katika maeneo fulani fulani kwa maana ya Mkoa kusaidia Wilaya.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Spika, la kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wenzake wote kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu watendaji, nashukuru kuwa ajira Wilayani mnajitahidi, lakini katika kata na vijiji bado kuna pengo kubwa hususan Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi hizo.

Nashauri hao waajiriwe kwani wana umuhimu kwani ni Mtambuka *(cross-cutting)*. Hawa wana uwezo wa kuziba pengo kubwa kati ya Wilaya na Vijiji juu ya suala zima la utandawazi. Pamoja na ufinyu wa Bajeti, kuna matatizo ya usafiri. Lakini kwa vile hawa ni waajiriwa Halmashauri ziweze zikawafanyia mipango ya mikopo ili angalau wapate baskeli . *They must be mobile.*

Leo hii mimi nafikiri naweza kusema kwamba *RAS* wa Rukwa anafanya kazi kubwa sana kusaidia Halmashauri za Rukwa na ndiyo maana Halmashauri yake hata moja haiwezi kurudi tena mbele ya Kamati ya *LAAC*. *RAS* wa Kagera tulikuwa tunawashauri Ma-*RAS* wengine waende kuchukua mfano kule.

Kwa hiyo, tusichukulie kwa ujumla kwamba Mkoa hauna wajibu wala mchango wowote katika kuzisaidia Halmashauri. Pale ambapo pana nia na dhamira safi imewezekana Mkoa ukazisaidia Wilaya zake vizuri na kwa mwaka huu mfano mzuri ni Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Kagera, tunawasifu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, fedha hizi tunazopeleka huko Wilayani naomba Wizara yake Mheshimiwa Waziri iige mfano wa Wizara ya Ujenzi, tupewe nakala ya mgawo, tusisome kwenye magazeti tu. Hasa kwa sasa ambapo utaratibu wa tenda umebadilika. Inawezakana fedha zikakaa ofisini kwa Afisa Elimu kama ni za MMEM au Ofisi ya Kilimo kama ni za kilimo kwa muda wa miezi minne wakitafuta *tenderer*, lakini Mbunge akijua na nakala ya fedha zilizotumwa Wilayani kwake akiwa nayo anaweza akasukuma haraka na fedha zikatumika haraka iwezekanavyo na taarifa ikatolewa kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache kwa mara nyingine nakushukuru na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Spika, la kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wenzake wote kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu watendaji, nashukuru kuwa ajira Wilayani mnajitahidi, lakini katika kata na vijiji bado kuna pengo kubwa hususan Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi hizo. Nashauri hao waajiriwe kwani wana umuhimu kwani ni Mtambuka *(cross-cutting)*. Hawa wana uwezo wa kuziba pengo kubwa kati ya Wilaya na Vijiji juu ya suala zima la utandawazi. Pamoja na ufinyu wa Bajeti, kuna matatizo ya usafiri. Lakini kwa vile hawa ni waajiriwa Halmashauri ziweze zikawafanyia mipango ya mikopo ili angalau wapate baskeli . *They must be mobile.*

Mheshimiwa Spika, la tatu, ushirikishwaji wa wanawake kwenye *Dar es Salaam International Trade Fair (DITF)*. Tunashukuru wengi wanashiriki lakini bado kuna udhaifu. Dhana ya *cost sharing* kati ya *EOTF* na Halmashauri imeaanzishwa. Nashauri Wakurugenzi wote wahakikishe kwamba hao wanawake wanashiriki kikamilifu labda tuanze mwaka huu. Namshukuru sana Mama Anna Mkapa, kufanikisha jambo hili. Tumuunge mkono.

Mheshimiwa Spika, la nne, ni kuhusu Mikopo *WDF*. Katika kuboresha mfuko huu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imewapanga Halmashauri kama mawakala. *Agreement forms were signed between the two parties.* Walitakiwa kuleta marejesho *by 30th June, 2003.* Ninafurahi kusema hadi leo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mtwara Mikindani tu ameleta. Nampongeza! Wengine bado waagizwe la sivyo watabanwa.

Mheshimiwa Spika, la tano, tunahitaji *desegregated data no generalization!* Takwimu zote ziwe *me* na *he.*

Mheshimiwa Spika, suala la sita ni kuhusu Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi. *(FDCS)* viko 58 na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii viko 4 *(C.D.T.Is)*. Bodi za Chuo, Wenyeviti ni Wakurugenzi wa Halmashauri wahusika. *Almost 90 percent* hawaitishi Bodi. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ilipeleka fedha kwenye Vyuo vyote kuwezesha kuitisha hivyo vikao. Hazikuitishwa, twenda mbali hata hapa *FDC* Arnatoglue hawakufanya tusaidiane.

La saba, Mheshimiwa Spika, asilimia 10 kwa mikopo ya wanawake na vijana, tunashukuru. Lakini bado haijafikia asilimia 10. Tuwasisitize labda agizo la Waziri Mkuu, sasa liwe sheria!

Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, *keep it up,* wananchi wako nasi. Hongereni

Mheshimiwa Spika, nimepitia orodha zote katika kitabu cha orodha ya majedwali mlichotupatia, Ahsante sana. Lakini sioni orodha ya mifuko ya wanawake na vijana. Mheshimiwa Waziri naomba ufafanuzi.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, la kwanza ili tuwasaidie vijana wa vijijini kupambana na umaskini, napendekeza kwamba vijana wa Singida vijijini wapewe ajira katika kila ujenzi wa barabara za vijijini ambazo zinaweza kutengenezwa kwa vifaa vya mikono kama beleshi, majembe na kadhalika.

Pili, Wakandarasi walazimishwe chini ya makubaliano na Halmashauri, kuajiri vijana kama sehemu ya Mkataba.

Tatu, Fedha za mikopo asilimia 5 kwa wanawake na vijana zitolewe kwa njia ya vitendea kazi badala ya *cash*. Kama majembe, ngombe Maksai, nyavu, mbegu na kadhalika ili vijana na wanawake wazalishe mali.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, napongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara hususan Wakurugenzi wa Wilaya katika kusimamia kazi na huduma ya jamii huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Tabora Vijijini kwa wakati huo, wananchi kupitia Halmashauri yao, tuliomba Jimbo la Igalula ziongezwe Kata mbili kwa kuzigawa Kata ya Igalula na ya Kizengi, Kata hizo zilikuwa na vigezo hususan vya kukubaliwa kugawanywa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000 wananchi waliipokea Kata ya Loya iliyotoka katika kata ya Kizengi. Mheshimiwa Waziri, Kata ya Igalula ikabakia kitendawili. Pamoja na kushukuru sana kupata Kata ya Loya, naomba kama mwakilishi wao, uwaonee huruma watu wa Kata ya Igalula watendaji wanapata taabu kuhudumia wananchi masafa ni marefu na usafiri hawana. Mheshimiwa Waziri, wakomboe wananchi hawana ili wapate huduma kutoka kwa watendaji ni kuwapatia idhini ya kupata Kata.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika wananchi wa Wilaya hii waliomba katika Jimbo la Igalula tupate Tarafa mbili yaani Tarafa ya Igalula itakayojumuisha Kata ya Igalula, Goweko na Kigwa ninayoiombea igaiwe katika Kata ya Igalula. Halafu Kata ya Kizengi, Loya na Lutende iwe Tarafa moja ya Kizengi. Yapata mwaka wa tatu sasa ninakerwa na swali hili ambalo, Mkoa wala Wilaya hawatoi jibu. Mheshimiwa Waziri, raha na faraja ya wananchi wa Jimbo la Igalula na ukombozi wao, wasikilize kilio chao kabla ya chaguzi za mwaka 2004 za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili wapige kura za uhakika juu ya uongozi wao.

Mheshimiwa Spika, pengine Wizara inasita kutoa tamko kwa kutokujua eneo lenyewe lilivyo kubwa na wananchi wanahitaji utawala wa karibu. Tarafa ya Igalula pamoja na kuwa kubwa kiasi hicho na ingawa juhudi za kupata Tarafa mbili bado inasuasua yapata sasa zaidi ya mwaka, Tarafa hii haina Afisa Tarafa pamoja na kuwa Wizara inasubiri Muundo mpya wa utawala wa eneo hili, lakini hamuoni kuwa hamuwatendei haki wananchi wa Jimbo la Igalula kwa kuwanyima kiongozi muhimu katika Tarafa hii?

Mheshimiwa Spika, je, Wizara itakuwa tayari kutamka leo ni lini Afisa ataripoti Igalula mara moja ili akaanze kazi hii kati ya wale waliosailiwa, ili nikimaliza kazi za Bunge tarehe 7 Agosti, 2003 nikute anafanya kazi kituoni kwake. Mheshimiwa Waziri, viongozi wa Kata, Tarafa na Vijiji, ni muhimu sana katika kutoa huduma kwa wananchi. Nitashukuru hayo yote niliyoeleza hapo juu yakitiliwa maanani na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naendelea kuunga mkono hoja ili fedha zipatikane na watendaji niliowaomba wapatikane na kufanya kazi katika Jimbo la Igalula.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha hali ya utawala na usimamizi wa karibu katika utoaji wa huduma. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Ibara ya 16 ukurasa wa 7.

Kwanza, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Pili, je, kwa kuwa Maafisa Watendaji wa vijiji na mitaa wataajiriwa moja kwa moja na mamlaka za Serikali za Mitaa na kulipwa, sababu ipi iliyoashiria kutofikiriwa Waheshimiwa Madiwani nao pia kufikiriwa kulipwa mshahara na mamlaka hiyo? Hasa ukizingatia uzito wa shughuli za Waheshimiwa hao!

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa kuipongeza sana Wizara hii kwa jinsi ambavyo inajitahidi. Moja, kuendesha mafunzo kwa viongozi ambayo imekuwa chachu kwa maendeleo. Pili, kuboresha mtandao wa mawasiliano. Tatu, tendo la kuajiri watendaji wa kata na vijiji, litapunguza matatizo kwa ujumla; kwa kuwa watendaji hawa watashugulikia tu masuala ya maendeleo na kuepusha dhana ya chuki, baina ya wananchi na watendaji hao.

Nne, kupandisha madaraja, toka vijiji kuwa miji midogo, toka miji midogo kwenda Halmashauri za miji na kadhalika. Hili ni suala jema kwa kuinua na kuleta maendeleo ya haraka katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuliweka wazi suala la wananchi kushiriki kikamilifu katika suala zima la kujiletea maendeleo yao wenyewe. Kuanzisha *One Stop Center,* nalo ni jambo ambalo litadhibiti rushwa. Suala hili litapunguza usumbufu kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, napenda nirudie kuishukuru Wizara hii hususan Mheshimiwa Brigedia Mstaafu Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Kwa ujumla mambo mengi yanaenda vizuri katika Halmashauri nyingi kwa sababu ya hekima na busara ya viongozi hawa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuandaa hotuba ya Bajeti yenye mwelekeo mahususi. Aidha, pamoja na pongezi hizi napenda pia kuainisha baadhi ya masuala muhimu kwa ajili ya kuangaliwa na kuzingatiwa kwa kipindi hiki na kijacho.

Moja, mlolongo wa kodi kwa wananchi. Ninashauri Wizara ifanye utaratibu wa kupunguza kodi nyingi wanazotozwa wananchi zikiwemo kama kodi ya baiskeli, kodi ya mikokoteni na biashara ndogo ndogo. Hii itawapatia nafuu wananchi katika kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Wananchi hawa hadi sasa wamechangia shughuli nyingi za maendeleo.

Pili, tatizo la ukosefu wa ajira. Ni vema Wizara ikaandaa mpango maalumu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa makundi ya vijana na akinamama wanaendelea kusaidiwa katika kuanzisha/kujishughulisha na uzalishaji mali ili kuondokana na msongamano wa vijana wengi kukaa bila kazi. Aidha, mpango wa kutenga asilimia 10 kwa kila Halmashauri ya Wilaya uzingatiwe na litekelezwe badala ya hivi sasa kuwa katika baadhi ya Halmashauri za Wilaya chache.

Tatu, upungufu wa watumishi wenye sifa. Kuna baadhi ya Halmashauri za Wilaya nyingi mpaka sasa hazina watumishi wenye sifa za kuwa Wakuu wa Wilaya. Kwa mfano, katika Wilaya ya Magu hakuna Mhandisi wa Maji mwenye sifa, hivyo hupelekea miradi yote ya maji kushindwa kutekelezeka.

Nashauri Wizara ifanye kila namna kuzisaidia Halmashauri zenye matatizo kama hayo. Pia Wizara ifanye mpango wa kufuatilia kuona kila Halmashauri ya Wilaya inazingatia hilo.

Nne, Makatibu Tarafa/Watendaji wa Kata na Vijiji. Nashauri sana majukumu ya watendaji hawa yaainishwe vema na wapatiwe elimu sambamba na majukumu pamoja na ajira zao. Aidha, Sheria namba 6 ya 1999 ifanyiwe marekebisho ili nafasi za Makatibu Tarafa ziwekwe wazi.

Tano, Ofisi za Wabunge. Nashauri Halmashauri za Wilaya zirudishiwe moja kwa moja katika kuhakikisha upatikanaji na ukarabati wa ofisi za Wabunge.

Sita, Mahesabu ya Fedha za Halmashauri za Wilaya. Nashauri watendaji wote wenye Halmashauri zisizofanya vema katika kuandaa mahesabu wachukuliwe hatua ikiwa ni pamoja na kuondolewa katika nyadhifa zao ili liwe fundisho na kutoa nafasi kwa vijana wenye sifa na *commitment* ya kazi kupata nafasi hiyo. Aidha, Wakurugenzi wote waliokwisha kupatikana na makosa ni vema wakaadhibiwa bila ya huruma ili kutoa fundisho kwa wengine.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa maandishi. Naomba kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nawapongeza kwa kazi nzuri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na wataalam kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakifanya na kuleta mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuona umuhimu wa kuwaunga mkono na kuwapunguzia mzigo wananchi wa Mbarali kwa kutenga shilingi 100,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Boma. Nashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Mbarali na nashukuru sana ukizingatia kuwa umeenda sambamba na kufutiwa kodi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie kuhusu Madiwani, Wilaya, Halmashauri, Kata zinatofautiana sana kwa ukubwa. Mzigo wanaoubeba Madiwani katika kuhimiza maendeleo ya Kata na kuwatembelea wananchi wao ni mkubwa sana. Naomba kupendekeza kuwa angalau kiwango cha shilingi 30,000/= kiongezwe kusudi waweze kumudu kusafiri na kuhimiza maendeleo na kuwaongezea motisha.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa ukusanyaji wa mapato hautakuwa kigezo tena. Uandikishwaji wa vijiji, Wilaya ya Mbarali ina vijiji vingi ambavyo havijasajiliwa na maombi ya uandikishaji yameletwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Naomba ajira ya Afisa Watendaji wa vijiji iende sambamba na uandikishwaji wa vijiji vyote ambavyo maombi yameletwa Wizarani.

Meshimiwa Spika, ili kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Mbarali namwomba Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, aone umuhimu wa kushirikisha Wizara zingine kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ili waweze kukamilisha Ofisi za Polisi, Magereza, Mahakama kama ahadi zilivyotolewa na Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, katika mpango ambao kilimo kinatiliwa kipaumbele kwa njia ya kuleta fedha za kilimo moja kwa moja kwenye Halmashauri atuboreshee Idara ya Kilimo. Aidha, kwa kuongeza watalaam au kwa kutoa elimu kwa waliopo ili lengo la kuboresha kilimo liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo ambayo ilikuwa ikitolewa kwa vijana na akinamama kwa asilimia 10 kwenye mapato ya Halmashauri naomba ufafanuzi wa utaratibu utakuwaje.

Mheshimwia Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, ninawapongeza watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Kwanza, kuhamia Dodoma, ila hapa naomba sana maboresho ya *PR* hasa Katibu

Mkuu, mengi nitasema wakati wa kuchangia jinsi alivyo nipokea na wazee wenye matatizo ya Mgongola hadi leo sijapata watu alioahidi kuja Morogoro wakati vielelezo vya hoja hii vipo. Ahadi kama hizi siyo vizuri kwani wakulima wanaishi kwa tahadhari. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, hongera sana.

Pili, kuhusu kutembelea Mkulazi, Kidunda. Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri niliwaalika kutembelea Morogoro Vijijini hasa Kata ya Mkulazi ili waone ubovu wa barabara ya Ngerengere hadi Kidunda ambayo tangu 1995 Wizara yako ilitoa fedha lakini barabara hiyo haijachongwa. Naomba mje mimi nimeishachoka na hali hiyo.

Tatu, kuhusu *VEO* kulipwa mishahara. Nashukuru sana kwa hili, lakini kabla ya Januari, 2004 Wizara ije na Waraka unaotoa sifa, upatikanaji wao, jinsi ya kuondolewa, hadhi za *VEO* wa maeneo tofauti yaani *Main Trading Centers,* vijiji mji na vijiji vidogo vidogo.

Nne, Mfuko wa Pensheni na mafao ya Madiwani. Ipo haja Wizara hii kuandaa mfuko maalum wa mafao ya Madiwani pindi wanapofikia ukomo wa muda wao ili walipwe kiasi cha kutosha na kwa heshima.

Tano, viwango vya posho za Madiwani. Madiwani ni kiungo muhimu sana kati ya wananchi na Wabunge hivyo wanastahili kurekebishwa *sitting allowance,* posho za kujikimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi ya maendeleo, utaratibu ufanywe ili kuziba pengo la kodi hii ambayo imefutwa. Ombi ni kwamba ilipwe kwa mkupuo na nakala za kiasi kinachopelekwa kimaandishi tupewe Waheshimiwa Wabunge wote kwa kila Mheshimiwa Mbunge apewe ya Halmashauri yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi za viingilio na mageti barabarani. Kwa nini viingilio vinashamili ukifika *stand* nyingi ambazo zimejengwa kwa kodi za wananchi, wanaweka viingilio. Mfano Maili Moja Morogoro, *Ubungo Terminal,* naomba sana utoe tamko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utawala Bora. Je, Wizara ina kitengo cha Utawala Bora ili kuona hali ya Halmashauri zetu nchini?

Mwisho, naomba sana kama mtumishi yeyote wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, *DED, DC, RC* na kadhalika wanapoharibu Mkoa, Wilaya, wasihamishiwe kwenda maeneo mengine.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Napenda kukumbushia kama Manispaa yetu pia imewekwa katika mradi wa kuboresha barabara za Manispaa ya Shinyanga kama ilivyo kwenye miradi ya Manispaa zote nchini. Nitashukuru kupewa maelezo kwenye majumuisho.

Hali ya barabara na madaraja ndani ya madaraja iko duni sana. Tunahitaji daraja la Mushikamano na la Ndala ambayo huunganisha Kata za mjini Ngololo na Ndala. Wakati wa mvua watu huteseka sana. Zaidi ya hayo naitakia utekelezaji mwema Wizara yako kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, nazidi kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, katika jedwali linaloambatana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 72 sisi Waheshimiwa Wabunge wa Tabora mbona hatukupangiwa fedha za ofisi za Wabunge ikizingatia kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge wengine hatuna ofisi za Serikali tumepanga nyumba binafsi na tunazilipia na *stationeries* tunajinunulia, tunaomba ufafanuzi.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, ni fupi lakini imegusa maeneo yote muhimu. Pia nawapongeza kwa kuamua kuwa baadhi ya vijiji viwe mji. Natumaini Makambako imo hasa ushauri wangu kwenu unahusu.

Moja, dhana ya kijiji, niliwahi kutoa ushauri katika suala hili, leo nasikia *VEO* watalipwa mishahara na Serikali Kuu. Pia utawalipa viongozi wa mitaa ? *This is strange* kwa miji tuanzie ngazi ya kata na siyo mitaa. A ma sivyo tutaangamiza fedha kwa watu wasio na kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijiji mahali pengine vimegawanywa kwa kuangalia idadi ya watu hata kama mkusanyiko wa watu wasiona na ardhi. Njia ni kuunganisha baadhi ya vijiji ili *VEOs* wawe na kazi za kufanya. Halmashauri zetu za Wilaya hazitajali kuongeza vijiji katika mazingira haya. Kijiji nini hasa katika karne ya 21? Vipi mawazo yangu kuhusu vijiji kuna haja ya kuimarisha Idara ya Maendeleo ya Vijiji ili kushughulikia vijiji na hatma yao. Vijiji vimepuuzwa.

Pili, Miji na Vijiji ni mingi, kuna haja ya kuimarisha Idara ya Mji kutokana na kuongezeka kwa miji midogo 80 isiwe kama Buguruni au Manzese au Mwanjelwa.

Tatu, kodi ya maendeleo imefutwa kwa sababu mbalimbali. Lakini ni vizuri sote tuelewa kuwa kero kubwa ni umaskini. Kwa nchi maskini kama Tanzania sijui mchango gani wa umma hauna kero. Nashauri Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa lengo la kuondoa kero isirudishe nyuma kasi ya maendeleo. Kujitawala ni kujitegemea. Nia njema iambatane na njia sahihi na endelevu. *Timing is important.* Wapi tutapata fedha ya kuwalipia ada vijana tuliwasamehe ada?

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Naibu Waziri wake. Aidha, nawapongeza pia watendaji wote wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, tulipeleka ombi kwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa katika kuanzisha Mamlaka za Miji Midogo Handeni nayo iangaliwe. Tunashukuru hili limefanyika. Lakini tuliomba kutoka Wilayani, kupitia Mkoani Tanga kuwa mamlaka hiyo ya Mji mdogo isiitwe Mamlaka ya Mji Mdogo wa Chanika bali iitwe Mamlaka ya Mji Mdogo wa Handeni. *Please do the needful* .

Mheshimiwa Spika, narudia tena naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu kulikuwa na ahadi ya Serikali ya kuanzisha Programu ya Elimu ya Sekondari *(SEDEP)* nashauri ianze haraka iwezekanavyo ili kupunguza matatizo na kupanua Elimu ya Sekondari. Ada ya shilingi 40,000/= kwa mtoto wa sekondari ya umma ni kikwazo kikubwa cha kuelimisha watoto wetu; Serikali iangalie uwezekano wa kuiondoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MEMKWA, walimu wa MEMKWA bado hawalipwi naomba Serikali ione uwezekano wa kutoa ruzuku ya posho. Walimu wa Elimu ya Watu Wazima wamekuwa hawalipwi kwa kitambo kirefu sasa walipwe. Pamekuwa pakitolewa masharti na maagizo ya kukanganya kutoka Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Halmashauri za Wilaya. Kwa mfano, masharti kedekede ya matumizi ya fedha za MMEM, kwa mfano, kutaka vifaa vya ujenzi vinunuliwe katika maduka ya walioorodheshwa *VAT* sasa hao wa maduka hayo vijijini watoke wapi? Ajira za walimu wapya umekuwa ni usumbufu kwao mkubwa sana.

Pili, baada ya Serikali kuondoa kodi ya maendeleo na kuanza kuwalipa ma-*VEO* na ma-*WEO* na kadhalika. Naomba sana Madiwani nao watazamwe kwa vile maslahi yao ni duni sana.

Tatu, Serikali iliahidi kuangalia uwezekano wa Makatibu Tarafa kuhamishiwa Halmashauri mbona safari hii Serikali haijasema lolote? Wanahamishiwa huko lini ili kuweka hali vyema ya utendaji Wilayani.

Nne, pamekuwa na tatizo la Halmashauri za Wilaya ya Kongwa kukosa nembo na hati ya kuandikishwa tokea Halmashauri ya Wilaya hiyo ianzishwe. Tunaomba kero hii imalizike ili kuzipa Halmashauri mpya uhalali wa kisheria.

Tano, iko haja ya kuangalia *composition* ya Kamati za Fedha, Mipango na Uchumi na Kamati za ajira. Kwa maana ya kuwaondolea Wenyeviti na mameya Uenyekiti wa Kamati hizi muhimu wakapewa *responsible retired Civil Servants* au watu wengine kama ambavyo Serikali itaona inafaa.

Sita, Wilaya au Halmashauri ya Kiteto imekuwa ikitoza kodi ya ardhi ya shilingi 500/= kwa ekari. Kwa kuwa wakulima wengi wa huko wanatokea Kongwa; kero hii ni kubwa sana sana. Baada ya Serikali kupunguza kodi hiyo hadi shilingi 200/= tu kwa wenye hati ya ardhi kwa ekari. Naomba sana kodi hii isiendelee kudaiwa.

Saba, Wilayani Kongwa, wananchi wanaomba sana huduma ya umeme kwa vijiji vya *NARCO* - Chamae - Hogoro - Songambele A na B - Mkoka - Matongolo na Norini. Vijiji hivi ni vikubwa vyenye wakulima wazuri wa mahindi, karanga, alizeti, zipo sekondari na Taasisi kadhaa. Eneo hili ndiyo lenye uzalishaji mkubwa sana Mkoani Dodoma; wanaomba sana wapelekewe umeme.

Nne, Miji midogo. Katika Wilaya ya Kongwa kuna miji midogo minne.

Mlali
Kongwa } *GN 9/8/200*
Mkoka *198*
Kibaigwa } *GN 2002.*

Mheshimiwa Spika, tunaomba zoezi la kuanzisha rasmi Miji Midogo (Mamlaka) lihusishe Miji Midogo niliyoitaja hapo juu.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu akiongoza watendaji wake kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara yake. Naunga mkono hoja yake mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aone uwezekano wa kutupatia watumishi wenye uwezo na wenye uzoefu katika kupanga mipango ya wananchi katika ngazi ya vijiji na kata. Hatua hii ni muhimu katika maandalizi yote muhimu ya kufuta au kupunguza umaskini. Tuandaa dira ya maendeleo kwa kila kijiji, kata, Wilaya na kadhalika. Halmashauri za Wilaya/Miji zitakiwe zote kupeleka watendaji wao kwenye mafunzo katika Chuo chetu cha Mipango Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliombwa na Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga kupatiwa Mkuu wa Idara ya Maji ambaye atasimamia masuala yote ya maji katika vijiji zaidi ya 25 ambavyo havihudumiwi na Mamlaka ya Maji Safi na Taka ya Mji wa Sumbawanga. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atusimamie hilo kwenye Idara ya Utumishi ambayo ilikwishajulishwa na kuombwa. Tungeomba kupitia kwa Mheshimiwa Waziri akishirikiana na Waziri wa Fedha atoe maelekezo kwa Halmashauri zote kuhusu kodi zilizoondolewa ili kuwa na mtizamo unaofanana kwa kila Halmashauri ya Wilaya au Miji /Jiji. Hii ni muhimu ili kuondoa vurugu zinazoweza kujitokeza kutegemea na kila Halmashauri itakavyosimamia utekelezaji wake. Tusipende kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ikaingia doa. Hatua zote za kisheria, zitumike kuhalalisha maamuzi hayo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, michango ya watumishi kwenye *LAPF* isionekane kuwa ni ya hiari. Bado wapo Wakurugenzi wanaopuuzia agizo hili na kuwafanya watumishi wakose haki zao wakati wa kustaafu au kuacha kazi. Kazi hii ipewe kipaumbele pamoja na kuwabana wahusika na waweka Hazina kuendeleza jitihada za uwajibikaji katika kusimamia vizuri fedha za Halmashauri. Kuendelea kuwa na Halmashauri za Wilaya au Miji zinazopata Hati Chafu za Hesabu ni dalili za uzembe. Hatua kali ziendelee kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kuanza kuwalipa Watendaji wa Vijiji. Lakini kwa msingi huo, sasa tutumie nafasi hii tuwapate Watendaji wazuri zaidi, kwa sababu wale wenye uwezo

hawakuweza kuingia kwenye kazi kama hizi kwa kuwa hazikuwa na maslahi yoyote. Hali hii itavutia wasomi wengi pia itaboresha utendaji mzuri vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia pia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Moja, naomba katika jedwali la I, yafanyike marekebisho katika idadi za Tarafa. Karatu ina Tarafa 4 na siyo 3. Ningependa Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi wa kina kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka za Miji Midogo 88 kuanzia Januari 2004. Naogopa iwapo tafsiri pana ya hatua hii haitaeleweka, kutatokea matatizo makubwa hasa ya uendeshaji katika Miji hiyo Midogo. Sheria ilikuwa inataka wahusika waombe kupandishwa hadhi na hivyo kuwa wanajiandaa kikamilifu; ikiwa ni pamoja na kupanga vianzio vya mapato. Je, tumejiandaa kwa kiasi gani kufanya mabadiliko haya makuu na hasa tafsiri yake ni nini kutakuwa na uchaguzi upya wa Madiwani, kutakuwa na uteuzi wa Wakurugenzi na watendaji?

Pili, katika jedwali la 4, Karatu inaonekana kuwa na deni la mkopo toka Bodi ya Mikopo. Kisheria, mkopo huo ulichukuliwa wakati Karatu haikuwa Halmashauri kisheria, na waliochukua ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ya wakati huo. Pamoja na hayo, Karatu tumeomba Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, isaidie kusimamia ugawaji wa mali na madeni baada ya Wilaya kugawanywa. Jambo hili pamoja na kufuatilia limesimama na hadi sasa hakuna hatua inayojulikana na ninaona riba inaongezeka. Hili litaleta athari tuendako, ninaomba suala hili sasa lipatiwe hatma yake. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imefanya kazi kubwa katika kuboresha Serikali za Mitaa. Kwa mfano, uamuzi wa kuwalipa mishahara Maafisa Watendaji wa Kata na vijiji utaleta maendeleo mema katika kuendesha Utawala Bora vijijini. Lakini Waheshimiwa Madiwani hawajawekewa utaratibu ulio bora, wazi na wa kumwezesha Diwani kutimiza wajibu wake kwa wananchi. Diwani ni mwakilishi wa wananchi wa Kata yake katika Halmashauri ya Wilaya/Mji/Jiji. Uhalali wa mamlaka wa Halmashauri hizo ni kwamba Waheshimiwa Madiwani wamechaguliwa na wananchi, hivyo sauti yao ni sauti ya wananchi.

Pili, demokrasia ina gharama zake. Hivyo Waheshimiwa Madiwani wanapohudhuria vikao vya Halmashauri au Kamati za Halmashauri walipwe posho inayowiana vema na gharama za usafiri, malazi, chakula na matumizi mengine yanayowiana na hayo.

Tatu, wakati Diwani akiwa kwenye kata yake anafanya kazi nyingi za kutembelea vijiji na kuhamasisha maendeleo. Yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata. Anapofanya kazi hizi Diwani halipwi kitu chochote ili kumwezesha akabili gharama zinazoendana na majukumu yake.

Nne, hivyo, napendekeza kuwa, Mheshimiwa Diwani, zaidi ya kulipwa posho za vikao, alipwe pia mshahara. Akiwa analipwa mshahara itawezekana Madiwani kukopa pikipiki ili kuwawezesha kutembelea kata zao bila matatizo. Vinginevyo Madiwani watengewe malipo maalum kwa shughuli hizo, yaani watengewe *OC* maalum *(other charges).*

Tano, naelewa kuwa ushauri huu utaleta gharama kubwa. Lakini hizi ni gharama zisizokwepeka. Lazima tufanye hivyo.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri , Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa namna ya pekee Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa ufuatiliaji wa kero za wananchi Majimboni kwetu na kuzifanyia kazi na kutoa taarifa za

utekelezaji huo kwa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine wa ngazi za Wilaya hadi vijijini kwa mfano, Wenyeviti wa vijiji. Hii ndiyo tafsiri sahihi ya dhana ya uwazi na uwajibikaji. Hata hivyo, nitoe mawazo machache katika kuboresha hotuba hii.

Moja, nafasi ya Katibu Tarafa ni muhimu sana katika kuratibu na kusimamia shguhuli za amendeleo ndani ya Halmashauri. Nashauri Katibu Tarafa apewe nafasi rasmi kisheria ili aratibu kazi za watendaji ngazi ya kata na kijiji. Ni vyema Katibu Tarafa pia akawa na nafasi ya kumsaidia Mkuu wa Wilaya na akawajibika kwake kama ilivyo sasa.

Pili, pamoja na kumlipa *VEO* mshahara, ningependekeza Serikali pia iweke utaratibu wa kuhakiksha *WEO* wanapata mishahara yao kutoka katika Halmashauri kwa hakika. Kwa sasa, baadhi ya Halmashauri huwalipa watendaji kata kwa wasiwasi, na mara nyingi huchelewa kuwalipa na hivyo kuamua kujilipa kwa njia zisizo halali. Hali hii inasababisha kishawishi cha rushwa.

Tatu, napendekeza Chuo Kikuu Kishiriki cha *UCLAS* kishawishiwe kuchukua changamoto ya kukubali zoezi la kupima (ku-*design*) ramani za Makao Makuu ya Wilaya mpya zilizotangazwa Juni mwaka 2002.

Nne, Wilaya mpya pamoja na Kilindi zipendekezwa kwa kuwekwa katika programu nyingi kama *TASAF* na Mashirika mengine ya ufadhili ili zipige hatua za haraka kuzikuta zile za zamani na kupunguza utegemezi kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia na Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote wapewe fedha walizoomba.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima, kwa kutayarisha hotuba nzuri na safi kabisa.

Moja, kwanza napenda kuipongeza Wizara hii na Serikali kwa kuwaondoa Waheshimiwa Madiwani wote kuhusika na kugawa *Tender*. Hii ilikuwa inawapa mianya ya rushwa na ilikuwa inawapa nafasi kubwa Wenyeviti wa Halmashauri kuwa mabosi zaidi kwa Watendaji na hata kuwaona Wabunge wa maeneo hayo kana kwamba hawana maana. Kwa kuwa Mwenyekiti anaitisha vikao Wabunge wakiwa hawapo na hata kutowapa taarifa Wabunge hao. Kwa hili naipongeza Serikali kwa dhati.

Jambo la pili, Mheshimiwa Waziri na Watendaji wako Wakuu. Kuna barabara moja Jimboni kwangu ilisahaulika kwa miaka mingi na iko chini ya Halmashauri, na kutokana na kuharibika kwa kiwango kikubwa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema haiwezekani kukabili gharama kubwa za kuitengeneza barabara hii yenye urefu wa kilomita 33, barabara hii inatokea Nyakarilo hadi Lushamba na ni sehemu ambayo ina uchumi mkubwa kuna mazao mbalimbali, samaki na kadhalika. Watu wanalazimika kusafiri kwa njia ya maji, yaani kupitia Ziwani ambako ni hatari kubwa kwa maisha ya binadamu. Ninaomba Wizara hii iliangalie suala hili kwa upana wake na unyeti wake. Na ningependa kupata jibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi kwa mujibu wa Kanuni ya 49(7). Aidha, nitamke kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kufuta kodi ya maendeleo na ushuru wa bidhaa na biashara ndogo ndogo ambayo ilikuwa ni kero kubwa kwa wananchi. Wananchi wa Wilaya ya Arumeru, wanaishukuru Serikali yao kwa kufuta kodi ya maendeleo ambayo kwa muda mrefu hawakuona maendeleo yaliyoletwa na kodi hii.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu ubadhirifu na wizi wa fedha na mali katika baadhi ya Halmashauri za Wilaya zetu, kama inavyothibitishwa na taarifa za ukaguzi wa

Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali *(CAG).* Naipongeza Serikali kwa kuanza kuchukua hatua za kurekebisha kasoro hizi kwa kutuma Tume za Uchunguzi na hatimaye kuwachukulia hatua za kisheria na kinidhamu wale wote watakaohusika na vitendo viovu vya ubadhirifu wa mali za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa wa watumishi wenye ujuzi na sifa za Uhasibu katika Idara za Serikali na Halmashauri za Wilaya, upungufu huo umechangia kwa kiasi kikubwa kuzorota kwa usimamizi bora wa fedha na mali za Halmasahuri zetu. Ninashauri Serikali iajiri watumishi wenye fani ya Uhasibu na pale inapowezekana, wale wenye uzoefu wa Uhasibu waendelezwe waweze kufuzu katika Uhasibu kwa nia ya kuboresha utendaji wao katika Idara za Serikali na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu ukosefu wa ajira kwa vijana wetu. Ukosefu wa ajira kwa vijana wetu unakuwa mkubwa sana. Vijana wasio na ajira halali ni wengi na wanaongezeka kila mwaka na bila matumaini yoyote ya kuwa na ajira ya kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikiweka sera ya kuwapa vijana nyenzo na kuwawezesha vijana hawa wawe na shughuli halali za kilimo na biashara ndogo ndogo ili waweze kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Mfuko wa Pembejeo. Kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu jinsi Mfuko huu wa pembejeo unavyoendeshwa. Utaratibu wa sasa unaelekea kuongeza gharama za pembejeo husika. Ni vema usimamizi wa Mfuko huu ukawa katika Halmashauri za Wilaya ambako ndiyo wanaoelewa wakulima wao pamoja na mahitaji yao ya pembejeo husika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalizie kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya mwaka 2003/2004.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa utendaji mzuri na Bajeti safi.

Pili, kuhusu ajira ya Maafisa Watendaji wa Mitaa na Vijiji, ningependekeza vigezo *(qualifications)* za kuajiriwa watu hawa, zilingane na matarajio *(output)* ya utendaji wao. *WEO's* Mkoa wa Dar es Salaam ilibidi wawe *Graduates.* Napongeza hatua hii. Ajira hii ifanywe kwa makini, waliopo wachunjwe barabara ili nchi iwe na Maafisa Watendaji wa Mitaa na Vijiji ambao ni *qualified, committed* na *competent.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye dira ya mwelekeo wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba nzuri kuna maeneo machache yanayohusu kuboreshwa. Nianze na eneo la Madiwani. Madiwani wanafanya kazi ngumu katika mazingira magumu sana. Kwanza, wao ndio watangazaji sera katika jamii wao wako karibu na wananchi kuliko Mbunge na pili, wao ndio wasimamizi wakuu wa miradi yote inayotekelezwa vijijini na mijini. Tatu, wao ndio wanaohakikisha kama Ilani ya Uchaguzi inatekelezwa kutoka ngazi ya Kijiji, Mtaa, Kata hadi Wilaya na nne, wana jukumu la kusimamia mapato na matumizi kuhakikisha kuwa matumizi yanatumika kama yalivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Diwani ni Mbunge wa Kata majukumu yake hayana tofauti sana na Mbunge wa jimbo alichozidi Mbunge wa jimbo ukubwa wa eneo na ukubwa wa uwakilishi. Diwani anawakilisha Wilayani kutoka Kata na Mbunge anawakilisha Wilayani, Mkoa na Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima namwomba Mheshimiwa Waziri Madiwani walipwe mishahara. Kama Mtendaji wa Kijiji analipwa Diwani halipwi hayo maendeleo hayatapatikana kwa sababu Mtendaji hawezi kuhimiza maendeleo au kubuni miradi bila kumshirikisha Diwani. Kwa hiyo, Diwani atakuwa mnyonge katika kushiriki.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Madiwani wapatiwe usafiri kwa maana wakopeshwe walipe kupitia mishahara yao.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kufuta kodi ya maendeleo kwani hii kodi ilikuwa kero kubwa sana kwa wananchi hasa wa jimbo langu wenye kipato cha chini. Pia ningeiomba Serikali ifidie hiyo kodi bila kufidia basi Halmashauri zetu zitakuwa na hali ngumu na kusababisha Wilaya yangu ya Kilwa kushindwa hata kulipa posho za vikao.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vingi vya mapato vimechukuliwa na Serikali Kuu. Tulikuwa tunategemea katika mazao huko nako kuna tatizo toka tutekeleze amri ya kuondoa vizuio barabarani hatupati ushuru wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, tafadhali rejea toleo la Mheshimiwa Waziri, Orodha ya Majedwali yanayoambatana na Hotuba yake kuhusu Makadirio ya Matumizi 2003/2004. Ukurasa wa 72 na 73 (Ofisi za Wabunge) No. 7:-

(a) Idadi ya Wabunge Kilimajaro ni 10.

(b) Idadi ya Wabunge wenye Ofisi ni 8 tu.

(c) Fedha zilizotengwa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kutoa fursa hii ya kuchangia kwa maandishi kwani si rahisi Wabunge zaidi ya 200 kupata fursa ya kuchangia kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninampongeza Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa hotuba yake nzuri mno na ya kihistoria kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2003/2004.

Kwa mchango wangu ulio makini ninamwomba na kumshauri Mheshimiwa Waziri achukue *Hansard* ya Hotuba yake, maoni ya Msemaji Kambi ya Upinzani na yale yote waliyochangia Waheshimiwa Wabunge iwe ni dira ya kumwongoza katika shughuli zote za Wizara hii kwa mwaka 2003/2004 na Juni-Julai 2004 aweze kuliambia Bunge lako Tukufu mafanikio na upungufu wa utekelezaji wa yote yaliyotamkwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa uwezekano wa majukwaa ya siasa kuzungumzia zaidi kuhusu msamaha wa kodi ya maendeleo ni vizuri sana, na ni Utawala Bora, kumwomba Mtukufu Rais kutangaza msamaha wa kuachiliwa kwa wale wote waliofungwa Magerezani kutokana na Kodi ya Maendeleo. Hii itapunguza msongamano wa mahabusu na wafungwa kwenye Magereza hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ubadhirifu wa fedha za umma ni sawa na wizi na ujambazi ambapo hatma ya mwizi au jambazi ni kuuawa kwani yeye anaua.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nashauri kwa nguvu zangu zote Mheshimiwa Waziri asimamie Bajeti hii kwa uwezo wake wote, kama Afisa Mkuu Mtukuka wa *JWTZ* mfano Brigedia Jenerali na pale anapobaini ubadhirifu wowote kila baada ya miezi mitatu ampe mhusika adhabu itakayotoa onyo kwa wengine. Huu ndiyo Utawala Bora na siyo Udikteta.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nikimtakia Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na serikali za Mitaa, kazi njema na afya njema.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima natoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mitaa na Serikali za Mitaa, pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wake walioshiriki katika maandalizi ya Bajeti hii kwa umahiri mkubwa. Hongera sana.

Nianze na kuunga mkono Bajeti hii mia kwa mia kwa sababu nyingi, lakini hasa suala la kuondoa kodi mbalimbali ambazo ni kero kwa wananchi pamoja na kodi ya maendeleo. Nimepokea salamu nyingi kutoka kwa wananchi wa kawaida Wilayani Mbunge wakiipongeza Serikali kwa kuchukua uamuzi wa kishujaa.

Hata hivyo wapo watu ambao wana wasi wasi sana na maamuzi hayo hasa Viongozi wa Halmashauri. Wasiwasi huo unatokana na ukweli kwamba, mabadiliko haya hayakutegemewa na kwamba yametingisha mfumo uliozoeleka.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba mabadiliko haya hayawi kikwazo cha maendeleo napendekeza Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

Kwanza Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na wasaidizi wao, wafanye kazi ya kusimamia maendeleo na sio kazi ya utawala kama inavyofanyika sasa hivi. Muda mwingi wa Watendaji wa Halmashauri umekuwa unatumika maofisini. Watendaji wa Kata wanaendesha mambo yao watakavyo kwa sababu hakuna mfumo wa ufuatiliaji wa karibu na wa mara kwa mara unaofanywa na Viongozi wa Wilaya. Huu ni wakati muafaka kwa Wakurugenzi kujihusisha zaidi na shughuli za maendeleo na badala yake masuala ya utawala akaachiwa Katibu Tawala wa Wilaya. Katika maeneo ambayo Tarafa ni kubwa kuliko maeneo ambayo Tarafa ni kubwa kuliko baadhi za Wilaya ipo haja ya kuwa na kiungo cha kuwaunganisha Watendaji wa Kata mbalimbali, Katibu Tarafa angeweza kuwa kiungo kwa Kata zilizopo chini yake licha ya majukumu yake ya kiulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusu utata ambao umekuwa unajitokeza katika kutoza ushuru wa mazao *(Crop Cess)* ya asilimia tano katika zao la kahawa hasa Mbinga, ambako wanunuzi binafsi wale wanaonunua moja kwa moja kahawa kutoka kwa mkulima wanatozwa 5% *at source*. Lakini vyama vya ushirika ambavyo hukoboa, kuisafirisha na kuiuza kwenye mnada hutozwa 5% ya mauzo ya mnada tena kwa dola. Kwa utaratibu huo ni dhahiri kabisa wakulima wanaopeleka kuuza kahawa mnadani wanatozwa kiasi kikubwa zaidi kuliko mnunuzi anayenunua kahawa ya maganda.

Mheshimiwa Spika, suala la manunuzi ya bidhaa, zabuni na mikataba katika ngazi za Halmashauri zetu ni tatizo kwa sababu huko ndiko kwenye tuhuma za ulaji na mianya ya rushwa. Utaratibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri, kuwa pia Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango, Fedha na Utawala na hatimaye Kamati hiyo kujigeuza kuwa Bodi ya Zabuni na kisa kutoa taarifa zake kwa Baraza la Madiwani chini ya Mwenyekiti wa Halmashauri ni kuhalalisha uhalifu wa kimfumo. Pamoja kwamba, Serikali imefanya mabadiliko kidogo ambayo yamewaudhi baadhi ya Waheshimiwa Madiwani, bado mabadiliko haya hayatoshi. Ili kuboresha mfumo kuwa wa ufanisi zaidi nashauri na kupendekeza mambo yafuatayo:-

(i) Mwenyekiti wa Halmashauri (Wilaya au Mji) abaki na kazi yake ya msingi ya kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani tu.

(ii) Kutokana na uzito wa masuala ya fedha Kamati iwe ya Mipango na Fedha Mwenyekiti wake awe mmoja kati ya Madiwani mwenye uwezo na elimu nzuri.

(iii) Bodi ya *Tender* isiwahusishe Madiwani kama Serikali ilivyofanua, lakini marekebisho zaidi yanahitajika kwa kupanua chombo hicho ili kihudumie zabuni zote za Serikali Wilayani yaani Magereza, Mahakama, Polisi na Kurugenzi ya Halmashauri. Ikibidi Mwenyekiti wake anaweza kuwa hata kutoka nje ya Serikali. Utaratibu huo ni muhimu hasa ikizingatiwa kuwa fedha nyingi zinatoka Serikali Kuu, lakini vile vile vyanzo vingi vinatokana na walipa kodi waliopo katika sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko kama haya yatawaudhi Waheshimiwa Madiwani hasa wale waliokuwa wana bahatika kunufaika na mfumo huo. Lakini naamini Waheshimiwa Madiwani watakuwa huru zaidi kufutilia utendaji, kwani hawatakuwa na *conflict of interest.*

Mheshimiwa Spika, kwanza, suala la Ofisi za Waheshimiwa Wabunge, bado lina utata, Hivi *fully furnished* inazingatia mambo gani. Nashauri Viongozi wanaotoa taarifa kuhusu matumizi ya fedha kwa ajili ya Ofisi ya Waheshimiwa Wabunge, wawe wanafanya mawasiliano kwanza na Wabunge. Ofisi ya Mbunge Mbinga Mashariki ni chumba kimoja haijawahi kupata hata senti kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, pili, tunahitaji ufafanuzi Ofisi za Wabunge zinatakiwa ziwe wapi. Kwenye Makao Makuu ya Jimbo au Makao Makuu ya Wilaya.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Spikwa, kwanza kabisa napenda kusema kuwa naiunga mkono hoja iliyo mbele ya meza yako mia kwa mia.

Baada ya hilo basi nimpongeze Waziri mtoa hoja kwa Bajeti nzuri ambayo inastahili kuitwa Bajeti ya watu kwa kuwajali hasa kwa kuwapunguzia mzigo wa kodi mbalimbali ikiwemo kodi ya maendeleo. Kodi hii ilikuwa ni chanzo kizuri cha Mapato ya Halmashauri , lakini ukusanyaji wake ulikuwa na kero kiasi cha baadhi ya wanaume kutoroka familia zao wakiogopa kukamatwa. Hongera sana.

Eneo lingine ni ule uamuzi wa Serikali kupeleka fedha zinazokatwa watumishi wa Serikali za Mitaa moja kwa moja kwenye Mfuko wa *LAPF.* Halmashauri nyingi uzalendo ulikuwa unawashinda kuziwasilisha wakati hali za makusanyo yao yanapowawia magumu. Fedha hizi ni mali ya mfanyakazi, hivyo kutozipeleka kwenye mfuko husika ni sawa na kumnyang'anya haki yake ya msingi bila ridhaa.

Mheshimiwa Spika, katika maboresho yanayoendelea ndani ya Halmashauri zetu, Manispaa ya Morogoro iliwahi kuomba Serikali iridhie kukabidhi Hospitali ya Mazimbu na zahanati ya Sabasaba pale mjini ili zigeuzwe kuwa Hospitali ya Wilaya. Najua bado Serikali ingali inalifanyia kazi lakini nimeona nisichoke kukumbushia kama mwakilishi wa wananchi wa jimbo langu. Kuna wakati nilileta hili kama swali katika Bunge lilijibiwa lakini sikuridhika na jibu, hasa baada ya kuwasiliana na uongozi wa Mkoa akiwemo Mganga Mkuu wa Mkoa ambaye amesema hana matatizo ya kukabidhi na kwa kweli anasubiri idhini tu kutoka TAMISEMI wakati alipoitwa kutoa ufafanuzi ndani ya Kikao cha Baraza la Madiwani yaani *Full Council.*

Hivyo basi ni imani yangu kuwa Wizara itaridhia kauli hii ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro kuwa ombi hili sasa linaweza kupata mkono wa baraka.

Mwisho nirejee tena kusema kuwa naiunga mkono Hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa mia kwa mia.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Naibu Waziri, TAMISEMI, Katibu Mkuu, Ndugu Mmari na wataalamu wote walioitayarisha Bajeti hii kwa kazi nzuri sana. Mmetuletea Bajeti nzuri na imewasilishwa kwa umahiri sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Waziri alikuwa anahitaji muda zaidi wa kuisoma na kufafanua maeneo mengi ya hotuba yake nzuri na hakuwa na muda wa kutosha. Ni imani yangu kuwa Wizara hii imepewa siku mbili za mjadala kwa ukubwa na unyeti wa shughuli zake. Ingekuwa vyema basi, Waziri akapewa saa nzima ya kuitoa hotuba yake ili apate nafasi ya kuelezea kila hatua ambayo Serikali imeamua kuchukua na mikakati ya kuitekeleza. Suala hili nalipigia debe na nitahitaji uelewa wako na kulifurahia kama utalikubali.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati yako ya Katiba, Sheria na Utawala, hivyo nimechangia mawazo yangu yale ya ujumla na nimehusika katika kutengeneza hotuba iliyowasilishwa Bungeni na Kamati leo asubuhi. Hivyo mchango wangu huu wa maandishi unahusu jimbo langu na hasa matatizo ya Maji katika

Mji Mdogo wa Mwanga na maombi yetu maalum kwa utengenezaji wa Barabara ya Kikweni mpaka Usangi na Lomwe.

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Mwanga hauna Maji safi na salama tangu Septemba, 2002. Matatizo haya ni makubwa mno na yanavunja imani ya wananchi kwa Serikali yao ya CCM.

Matatizo haya niliyafikisha Serikalini kwa barua yangu ya tarehe 19 Oktoba, 2002 niliyomwandikia Mkuu wa Wilaya ya Mwanga na kuwapa nakala moja, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Katibu Mkuu, TAMISEMI.

Katika Barua hiyo nilieleza kwa undani kuwa tatizo la Maji katika Mji wetu halikutokana na ukosefu wa fedha, bali kutokana na ubadhirifu mkubwa na wa wazi wa fedha za Serikali unaofanywa na Mhandisi wa Maji wa Wilaya akishirikiana na Msaidizi wake ambaye ni ndugu yake wa karibu kwa kuzaliwa na *cashier* na mboharia wa Idara ya Maji Mwanga.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maji Wilayani imekuwa inapata fedha za ruzuku ya Serikali Kuu vizuri na kama ilivyopitishwa kwenye Bajeti ya mwaka 2001/02 na 2002/03. Katika mwaka wa fedha 2001/2002, Idara ya Maji, Mwanga ilipata shilingi 29.6 milioni zikiwa ni fedha za maendeleo kwa ajili ya kutengeneza na kupanua huduma ya maji mjini Mwanga.

Pia kiasi cha shilingi 6 milioni kilitolewa kutoka Serikalini kwa ajili ya kununulia vifaa vya kuchimba visima Wilayani. Idara pia ilipokea shs. 1.5 milioni zikiwa ni msaada kutoka *NGO* ya pamoja Mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji mjini Mwanga. Hivyo, fedha zote zilizopelekewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya maji katika Mji Mdogo wa Mwanga pekee katika kipindi hicho ni shilingi 37.1 milioni.

Haikubaliki kuwa kwa fedha zote hizi, watu wa Mji Mdogo wa Mwanga hawana Maji ya kunywa. Bila ya kujali kitu chochote, ukweli ni kuwa fedha ilitolewa lakini hakuna maji. Sioni Serikali inahitaji ushahidi gani kwa kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, katika barua yangu kwa Serikali, nilitoa mapendekezo yafuatayo ya kutatua matatizo ya Maji Mwanga:-

Serikali ichukue hatua ya dharura na kuyatengenezea maji ya Mjini Mwanga mara moja ili kuondoa matatizo makubwa yanayowakabili wananchi, Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Mwanga Bwana Kibakaya Senkoro aondolewe kwenye madaraka hayo mara moja na Mtanzania mwingine mwenye uchungu na nchi hii apewe nafasi hiyo na timu ya Wakaguzi wa Mahesabu ya Serikali kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI iitwe mara moja ikague mahesabu ya Idara ya Maji Mwanga na kuhakiki ununuzi, upokeaji na utoaji wa vifaa. Halafu timu iende kwenye miradi husika ihakiki utekelezaji wake kulingana na matumizi.

Ili kuwatia moyo wananchi katika kutoa sehemu yao ya uchangiaji wa miradi, sheria ichukue mkondo wake kama kuna ubadhirifu wowote.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuchukua hatua kubwa na za nia njema ya kutatua matatizo haya. Baada ya barua yangu ya 19 Oktoba, 003 kupokelewa. Serikali ilitoa sehemu ya shilingi 12 milioni zilizokuwa zimepangwa kwa maendeleo ya Maji Mjini hapo mwaka 2002/2003 kununua *motor* mpya ya pampu kama hatua ya dharura. Ikanunuliwa *motor* lakini tukaambiwa imeungana baada ya kufungwa kutokana na kutokuwepo na fundi wa kuaminika. Lakini hili ni mbali sana na ukweli. Imebainika kuwa tatizo la Maji Mwanga sio ubadhirifu wa fedha peke yake, bali wizi wa *motors* na *spare* zingine pamoja na kubadilisha vipuri *genuine* kwa vifaa feki. Hivyo, tatizo la maji likaendelea kama lilivyokuwa licha ya hatua ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge la Januari 2003, tulikwenda tukamwona Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo tukamwomba atunusuru na tatizo hili la Maji Mjini Mwanga. Kwa ukarimu wa Serikali, tukapewa shilingi 15 milioni kununulia pampu moja kubwa. Nasi kama Halmashauri tukatoa shilingi 15 milioni ili tununue pampu mpya ya pili, nia ikiwa ni kumaliza kabisa tatizo hili. Pampu moja imeshawasili Mwanga na inasubiri kufungwa wakati ya pili iko bandarini inatolewa.

Mheshimwa Spika, Baraza la Madiwani liliunda Kamati yake ya kuchunguza tatizo hili, Januari 2003; lakini Kamati hii ikashindwa kufanya kazi hiyo kwa maelezo kuwa Serikali imeunda Kamati ya kuchunguza tatizo hili tangu Desemba 2002. Hatimaye Kamati ya Uchunguzi ya Serikali ilifika Mwanga mwezi Machi 2003.

Kamati hii ya Serikali ilichukua muda mrefu sana kufika Wilayani kwetu. Hiki ndio kitendawili kikubwa. Kumbe Kamati ilichagua kufika Wilayani wakati Mkurugenzi wa Halmashauri hayupo na Kaimu Mkurugenzi ni Bwana Kibakaya Senkoro. Mhandisi wa Maji. Japo nilikuwepo wakati wote Kamati hiyo haikuongea nami, wala kuongea na Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji ya Baraza la Madiwani. Kamati pia haikuongea na wananchi. Ilitosha kwa Kamati hiyo kupokelewa na Mhandisi wa Maji, ikaongozwa na Mhandisi wa Maji na ikamchunguza kwa siri na ikasindikizwa na Mhandisi wa Maji, ikaondoka.

Mheshimiwa Spika, hatujaiona Ripoti ya Kamati hiyo katika Baraza letu la Madiwani na wala hakuna Kiongozi wa Serikali aliyeweza kunieleza uchunguzi huo uliona nini. Niliambiwa siku moja kuwa ripoti iko tayari lakini hakuna karatasi hivyo haijachapwa.

Lakini njia zinasema ripoti imeona kuwa kazi ya Mhandisi wa Maji Mwanga ni nzuri sana. Kwani ukizingatia mwenendo wa kazi wa Kamati yenyewe ungetegemea nini? Mazingira yote ya kuchagua wakati wa kufika Mwanga, utendaji kazi, mwenendo na hofu ya kutoa taarifa ya Kamati hii unanuka rushwa. Natamka wazi kuwa sioni ni vipi hatua hizi za Serikali zikizaa matunda wakati hakuna hatua za msingi zilizochukuliwa kudhibiti wizi na ubadhirifu katika Idara ya Maji ya Wilaya ya Mwanga.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mwanga wamenituma niiombe Serikali iwanusuru na tatizo hili la maji. Na kwa niaba yao naishukuru sana Serikali kwa hatua iliyochukua. Hata hivyo, mimi na wananchi wa Mwanga tunaamini kuwa pamoja na hatua hizo, maji ya Mwanga yataendelea kuwa tatizo kama Viongozi Wakuu wa Serikali watafumbia macho na kuonea aibu ubadhirifu na hujuma za wazi zinazofanywa na wafanyakazi wa Idara ya Maji Mwanga. Wanamwanga wanataka tamko rasmi la Serikali kuhusiana na tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 Desemba, 2002 nilimwomba Mheshimiwa Brigedia Jeneral Mstaafu Hassan Ngwilizi, atupatie msaada maalum wa utengenezaji wa barabara ya kilomita 18 kutoka Kikweni mpaka Usangi, Lomwe. Tuliomba msaada wa shilingi 110 milioni ili kuichonga barabara hii, kufungua mifereji, kuweka makalivati na kumwaga changarawe. Barabara hii inaunganisha Wilaya nzima ya Mwanga na Hospitali ya Wilaya iliyoko Usangi. Mwisho Barabara ilitengenezwa mwaka 1997 na sasa ina hali mbaya sana.

Katika kufuatilia suala hili, niliahidiwa na Waziri kuwa utaratibu umefanywa ili barabara hii itengenezwe mwaka huu wa 2003. Matengenezo yangu na ya watu wote wa Mwanga ni kuwa Barabara hii itatengenezwa kwa fedha zilizotengwa katika Bajeti hii. Naomba Mheshimiwa Waziri atuhakikishie hilo kwa kuwa ombi hili ni muhimu sana kwa wagonjwa wanaohitaji huduma ya Hospitali ya Wilaya na watu wote wanaoishi Usangi kwa ujumla wake.

Mwisho napeda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa naunga mkono hoja hii ya Ofisi ya Rais, kwa 100%. Ahsante sana.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kuipongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba nzuri inayolenga hasa ni nini imekusudia kutufahamisha Wabunge wote ili tuwe na ufahamu wa kina juu ya yale yote yanayohusika na mamlaka na madaraka ya wananchi na Viongozi wao katika kuziendesha shughuli za Tawala za Mitaa na Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii Kikatiba haipo katika Muungano, lakini kusema kweli kwa lugha ya kikwetu ninaihusudu. Kwa maana ya kuwa ninaionea choyo jinsi inavyopanga mambo yake kwa utaratibu unaoeleweka vizuri tu katika kuendesha Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na imani yangu ninayo mambo mawili, matatu ambayo ningependa kuchangia katika hotuba au mwongozo wa kusaidia katika kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambayo ni moja ya Serikali katika nchi yetu hii ya Tanzania kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika muundo wa Halmashauri za Wilaya za Zanzibar, Waheshimiwa Wabunge si wajumbe wa Halmashauri hizo, sasa ningeiomba sana Wizara hii, hasa Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano uliopo kati ya SMT na SMZ kushauriana na kuona kuwa Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar na wao wawe wajumbe kamili katika Halmashauri za Wilaya na kuweza kuchangia kikamilifu katika shughuli za kujenga nchi yetu hii ya Tanzania kwa kusaidiana na Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni suala la Ofisi za Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar. Roho yangu imeingia wivu kuona kuwa Waheshimiwa Wabunge au kila Mkoa, wenye Ofisi zao Mikoani, wanatengewa fedha kwa ajili ya Ofisi zao hizo. Hivyo kuna sababu gani za kimsingi ambazo zinaifanya SMT kutotenga fedha kwa Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar kuwa na kasma za kudumisha au kuendeleza Ofisi zao katika Mikoa wakati Wabunge wa Zanzibar ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama walivyo Wabunge wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, ikiwa shughuli za Wabunge wa Zanzibar zipo chini ya Ofisi ya Waziri Kiongozi wa SMZ ni kiasi gani fedha kutoka SMT ambazo zimepelekwa Ofisi ya Waziri Kiongozi mbona sikuziona katika orodha ya jedwali yanayoambatana na hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu makadirio ya matumizi kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu haya ninatumai Mheshimiwa Waziri atanipatia maelezo japo kidogo ili nipate kutuliza roho yangu.

Naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalamu wa Wizara hii. Mimi mchango wangu ninaomba Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Majimbo ya Zanzibar mpaka mwezi huu hatuna Ofisi za Wabunge ninaomba nipate taarifa ni lini Ofisi hizo zitajengwa.

Kuhusu kuondoa umaskini, ninashauri Serikali ipambane na watu wanaozurura ovyo ambao hawana kazi za kufanya na wanategemea sana wazee wao ambao hawana uwezo wa kuhudumia watu wengi, hivyo basi ni vizuri iwepo sheria ya kuwabana wale wote wasio na kazi watafutiwe mashamba huko Vijijini walime, Serikali ikifanya hivyo huenda umaskini ukapungua. Wakulima wapewe elimu ya kutosha kuhusu kilimo, kwa sababu wakulima wengi wanalima bila kutumia utaalam, hivyo Mabwana shamba waanzishe vi-*plot* vya mashamba katika mashamba ya wakulima wadogo wadogo ili waone tofauti ya kulima kwa utaalamu na kulima bila ya utaalamu. Lingine iwepo taaluma kwa njia ya *Television* ili wakulima wajionee wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu adui maradhi napendekeza kuwa ziongezwe zahanati Vijijini na hatimaye kwa wale wananchi ambao hawana uwezo wapatiwe matibabu bure. Vita dhidi ya Ukimwi, naomba elimu hii sehemu maalum ya masomo ya darasani kwa wanafunzi wa shule wa ngazi zote. Vile vile fedha za misaada au zilizopangwa kwa Wizara, mbali na kufanya semina lakini fedha zingine wapewe wagonjwa wa Ukimwi na warithi wa marehemu waliofiwa na wazazi wao, vipeperushi vigawiwe mara kwa mara kwa wananchi vyenye kufahamisha madhara ya Ukimwi.

Mwisho, naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja.

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu kwa kutoa kauli Bungeni ninaomba nitoe kilio cha wanakijiji wa Kijiji cha Makiidi Mkuu Rombo.

Mheshimiwa Spika, Kijiji hicho kilijenga Ofisi ya Mifugo na nyumba za wafanyakazi wa Idara hiyo kwa nguvu zao. Walisaidiwa mabati na Serikali. Sera ya Wizara ya Ujenzi ya kuuza nyumba za

Serikali Kuu kwa wafanyakazi wake imeeleweka vibaya na uongozi wa Wilaya ya Rombo na nyumba hizo zimeuzwa kwa yule Afisa Mifugo aliyeko na kulikuwa na harakati za kumpimia eneo hilo apewe hati.

Wanakijiji wanaheshimu sana eneo hilo kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, ni eneo la jadi la utawala wa Kijiji, pili, nyumba hizo zimekuwa kwenye kesi kwa zaidi ya miaka 6 na uongozi wa Wilaya haukufanya lolote kusaidia kijiji katika juhudi zake za kuzitetea, tatu, eneo hilo ni sehemu inayotumika kama Ofisi ya Tiba za mifugo. Wanakijiji wana wasi wasi huduma hii itaathirika ikiwa itakuwa mikononi mwa watu binafsi, hasa ikizingatiwa kuwa sehemu hiyo ina uhaba mkubwa sana wa ardhi na nne, kuna nguvu za wananchi katika nyumba hizo na siyo busara kuwanyang'anya.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mmoja wa wanakijiji, ninaomba uingilie kati utuokolee hii mali yetu.

Tano, eneo hilo ni sehemu inayotumika kama Ofisi ya Tiba za mifugo. Wanakijiji wana wasi wasi huduma hii itaathirika ikiwa itakuwa mikononi mwa watu binafsi, hasa ikizingatiwa kuwa sehemu hiyo ina uhaba mkubwa sana wa ardhi na sita, kuna nguvu za wananchi katika nyumba hizo na siyo busara kuwanyang'anya. Nikiwa kama mmoja wa wanakijiji, ninaomba uingilie kati utuokolee hii mali yetu.

**MHE. IDDI M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, baada ya salaam za pongezi na kuunga mkono hoja, ninayo yafuatayo:-

Kwanza, uzoefu umeonyesha kwamba uhusiano wa Wakuu wa Wilaya na Mkoa, kwa upande mmoja na Madiwani haueleweki sawa sawa. Mara kadhaa wakuu hawa wanaonekana kama ndio wanaosimamia kazi za watendaji ambao wanahisi wanawajibika kwao badala ya kuwajibika kwa Halmashauri. Pengine ipo haja ya kufikiria mawazo aliyetoa Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, ya kuwaingiza Wakuu wa Wilaya katika Manispaa, na Mkuu wa Mkoa aingie katika Halmashauri ya Jiji.

Pili, napendekeza Mheshimiwa Waziri aangalie uwezo na uhuru wa Halmashauri wa kuamua aina na idadi ya wafanyakazi wanaoajiriwa na Halmashauri. Madiwani, kama wawakilishi wa wananchi, wanawanyima nafasi ya kupanga vyama zaidi mipango ya kutekeleza ilani za Uchaguzi. Desturi ya kupeleka maombi Wizarani juu ya jambo hili, ambalo liko mbali na Wizara, kwa maana ya kutambua mahitaji halisi ya Manispaa au Jiji, imeonyesha udhaifu katika kufikia maamuzi sahihi. Kwa mfano, iwapo Manispaa inaomba ajira ya watumishi 20 wa aina mbalimbali na Wizara inaruhusu idadi ya watumishi 16 tu, haiwezi kueleweka vigezo vinavyotumiwa katika kufikia maamuzi ambayo hata hivyo yanachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tatu, maslahi ya Madiwani, uzoefu umeonyesha kwamba Waheshimiwa Madiwani wanatumia muda mrefu sana katika kazi za umma. Mshahara wa shs. 30,000 kwa mwezi na posho ya shilingi 25,000 za vikao ni ndogo mno. Waheshimiwa hawa wanadhalilika mno. Napendekeza Wizara iliangalie suala hili vyema na kujenga uwiano baina ya kazi inayofanywa na maslahi na nne, vitendea kazi kwa Madiwani, napendekeza suala zima la kuwawezesha Madiwani kufanya kazi zao liangaliwe pamoja na mikopo ya kununua vyombo vya usafiri.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi na watalamu mbalimbali wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa hotuba nzuri waliyoiandaa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu mwenyewe na wananchi wa Wilaya ya Korogwe, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe pamoja na wataalam wako kwa kuipatia Korogwe Mji hadhi ya Halmashauri ya Mji.

Kwa kuzingatia kutupatia Halmashauri ya Mji *(Town Council)* tunaomba sana tupatiwe watendaji wanaolingana na hadhi ya Mji. Hivi sasa watumishi waliopo hawalingani au hawana sifa. Halmashauri za Mji hizi zinazoanza zinahitaji watumishi wenye uwezo ili kazi zifanyike kwa ufanisi.

Kwa muda mrefu sana Wilaya yangu ya Korogwe, tumeleta Wizarani kwako Vijiji vipya ambavyo kwa muda mrefu vinaomba na kufuata taratibu zote za kuandikishwa kuwa Kijiji kamili. Vijiji hivyo ni Magungu ya Cheke - Kata ya Kwagundo,Lusanga - Kata ya Karenge, Magunge Pole Pole - Kata ya Mnyuzi na Matondo - Kata ya Ngombezi

Niliwahi siku moja kuzungumza na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Naibu Waziri TAMISEMI, akanieleza kulikuwa na tatizo la Daftari la Vijiji halionekani, kwa hiyo, nivute subira. Kwa muda mrefu nimevuta subira lakini bado wananchi wa Magungu ya Cheke wananisumbua. Kero hii sasa imekuwa ya kisiasa.

Naomba sana ikiwezekana baada ya Bunge hili niondoke na usajili wa Vijiji hivyo hasa kwa kuanzia na Kijiji cha Magungu ya Cheke na Lusanga. Kama tatizo ni daftari ninashauri lianzishwe jipya.

Kuhusu watumishi wabovu, wabadhirifu na wezi, nashauri sana Wizara isiwalee watendaji wabovu, wabadhirifu na wezi, katika Halmashauri zetu. Kuendelea kuwalea watendaji wabovu wa aina hii kuleta mgongano usio wa lazima kati ya Watendaji na Madiwani.

Wizara inapoona Mtendaji ni mwizi ni mbovu ni vizuri wakamwondoa mara moja. Mtu anayejulikana ni mwizi ni vizuri haraka sana mtu huyo au hao wakaondolewa. Inashangaza Wizara inafahamu mtu fulani ni mwizi au ana tabia mbaya lakini anahamishiwa Halmashauri nyingine. Hivi ni kwa nini inakuwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, hali hii inapotokea huleteleza kutesa wasiohusika ambao ni wananchi wenye Halmashauri yao. Nashauri Wizara iwe macho kuteua Watendaji wenye uwezo waadilifu na wenye nia kweli ya kuendeleza wananchi wa maeneo waliyokabidhiwa. Wizara itafute namna ya kukomesha tabia ya Ma-*DED* wanaokwepa vikao na kuwa na tabia ya kukaimisha Wakuu wa Idara wote katika Wilaya. Matokeo yake haieleweki sasa anayestahili kukaimu mwenye uwezo ni nani. Haiwezekani katika Wilaya kila Mkuu wa Idara ana uwezo wa kukaimu. Nimshauri sana anayetakiwa kukaimu kama Mkurugenzi amesafiri Wizara imetambua hii inamarisha aina ya cheo fulani, mfano Afisa Mipango au Afisa Utumishi ndio awe kaimu. Hivyo itajenga *consistence.* Lakini ni tabia ya kila Kiongozi kukaimu ni tatizo, sio Utawala Bora.

Kuna umuhimu wa *DED* na *DC* kuheshimiana. Ma-*DC* wapewe uwezo wa kisheria wa kuwashauri Ma-*DED* na kuona Halmashauri zinatimiza wajibu na majukumu yake na Madiwani waelimishwe zaidi ili wawezeshwe kuwa na uwezo wa kuishauri na kuisimamia Halmashauri. Wazo la kuwapatia posho ya kima cha chini cha mshahara Madiwani lifikiriwe.

Kuhusu Walimu wapya kukaa zaidi ya miezi sita bila kupata mishahara lipatiwe ufumbuzi wa kudumu.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Spika, naomba *status* ya maombi yote ya fedha za *Road Fund* yaliyoletwa na *District Council* ya Nachingwea. Baadhi ya maombi hayo yana zaidi ya miaka miwili, kama Nachingwea, Ntila-Nkonjela-Namikango. Naomba wakati wa kikao hiki nipatiwe miradi iliyopitishwa na kupatiwa fedha na orodha ya maombi yaliyo *pending since 2000 to date.*

Mheshimiwa Spika, maombi yaliyoletwa huko nyuma ya kuanzisha Tarafa ya Mnero yamefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *DED, Mr*. Nelson Mwasaga, alisimamishwa. Je, uamuzi umekwishachukuliwa. Kama umechukuliwa ukoje? Mbona sioni fedha za Serikali kuchangia ujenzi wa Boma ya Nachingwea kuunga mkono wananchi.

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2003/2004 TUMITAA inaombewa jumla ya shilingi 681,486,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Nasema fedha hii ni ndogo sana pamoja na kuwa fedha iliyoombwa itapita kwa kura nyingi za Waheshimiwa Wabunge. Lakini eneo hili liangaliwe upya ili eneo hili liongezewe fedha kwa utendaji kwa sababu TUMITAA imejipangia mambo mengi na muhimu kama ilivyo katika aya 35 ya hotuba ukurasa 16.

Mheshimiwa Spika, sheria Na. 3 ya 1970 kifungu cha 4(b) na 5(i) mtu anayetoa siri afungwe jela miaka ishirini (20). Adhabu hii ni kubwa sana na inahitaji ifanyiwe marekebisho sababu sheria hii inaweza ikatoa tafsiri mbaya ya maana ya siri.

Mheshimiwa Spika, kipando cha Mwenyekiti. Mwenyekiti hakupewa uwezo wa kulitumia gari hilo kwa shughuli zake binafsi. Swali, je, kutumia gari kwa ajili ya dharura kwa mfano wagonjwa wake anaruhusiwa ? Kama jibu ni laa!!! Kwa nini? Huu ni udhuru.

Nakutakia kila la kheri katika kufanikisha majukumu ya Taifa hili na shughuli zako za kawaida. Nimeelewa madhumuni ya hotuba.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii nzito na kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo inawalenga wananchi walio huko chini ya nchi hii. Wananchi wengi wanaitegemea sana katika kuwaletea maendeleo kupitia Halmashauri zao. Kuna kero nyingi zinafanyiwa na watendaji wengi, hivyo napendekeza sasa hivi Waziri utume haraka sana Waraka kuhusu kufutwa kwa kodi ili wasitozwe wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naleta tatizo kubwa linalofanywa na Wakurugenzi wetu wa Halmashauri za Wilaya. Serikali iliamua Halmashauri zote zichangie asilimia 10% kwa vijana na wanawake. Lakini watendaji hawa wamepuuza maagizo haya wanayofanya wanavyotaka wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sera ya CCM ni kupunguza umaskini kwa kukopesha vikundi vya vijana na wanawake. Je, Serikali imewajibishaje hawa watendaji wasiotii amri za Waziri?

Mheshimiwa Spika, mimi sina mengi zaidi ya kuwapongeza sana kwa kazi wazozitekeleza Waziri na Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hasa kwa kujibu maswali yetu kwa makini.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ipewe fedha zote walizoomba katika Bajeti ya mwaka 2003/04 kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Brigedia Mstaafu Hassan Ngwilizi, Katibu Mkuu, Ndugu Mmari na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii yenye mwelekeo wa kuleta ufanisi katika utendaji ndani ya Serikali za Mitaa na Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kutoa pongezi nyingi kwa Serikali ya CCM kwa niaba ya wananchi wa Singida kwa tendo zito, kubwa na la kiungwana kwa kufuta kodi ya maendeleo, kodi ya mifugo na kodi ndogo ndogo ambazo zilikuwa kero kubwa kwa wananchi kwani baadhi ya ndoa zilivunjika kwa ajili ya wanaume zao kukimbia kodi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ya kufuta kodi hizi kwa wananchi wetu sasa ikumbukwe kwamba kuna upungufu mkubwa wa fedha za kuendeshea Halmashauri zetu pamoja na miradi ya maendeleo iliyoendeshwa kwa fedha za kodi zilizofutwa. Hivyo basi naiomba Serikali ihakikishe kuwa imefidia upungufu huo kwani Halmashauri nyingi zitashindwa kujiendesha kutokana na upungufu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, vile vile naipongeza Serikali kwa dhati kabisa kwa kuwaajiri Maafisa Watendaji wa Vijiji naMitaa kwa kufanya hivyo imekuwa ni ukombozi kwa watendaji hawa kwani walifanya kazi kwa mazingira magumu kwa kusukumana na wananchi kwa kufukuzia asilimia ya posho zao zinazotokana na makusanyo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watendaji hawa walidhani kuwa kazi yao kubwa ilikuwa ni kukusanya kodi tu, naishauri Serikali kwa kuwa ina mpango wa kutoa mafunzo ama semina kwa watendaji

kwa ngazi mbalimbali basi iwakumbuke na wale wa ngazi ya Vijiji na Mitaa kwa lengo la kuwaboresha utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kuona Serikali inafahamu kuwepo kwa watendaji wasio na uwezo na kuamua kuanza kutoa semina, warsha na kozi fupi na mitihani kwa lengo la kupata watendaji wenye uwezo na kufahamu wasio na uwezo. Naitaka Serikali isiwafumbie macho wale watakaobainika kutokuwa na uwezo iwaondoe kwenye nafasi hizo na kuwapa nafasi zinazolingana na uwezo wao.

Mheshimiwa Spika, napenda nikumbushe Serikali kwamba inawaacha Watendaji Wakuu wa Mikoa, Wilaya pamoja na Wakurugenzi na Wakuu wa Idara mbalimbali za Serikali kwa muda mrefu hadi wanafikia hatua ya kuwa Miungu watu katika Ofisi zao na kufanya shughuli za maendeleo kuzorota, katika maeneo yao kitu ambacho ni kero kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu wa watumishi ni kukaa miaka mitatu hadi mitano kwa ngazi ya juu, niiombe Serikali basi izingatie utaratibu huo iliyojiwekea yenyewe, ili kuondoa ukiritimba kwa watendaji hawa wanaolowea hasa Makatibu Tawala wa Mikoa *(RAS)*.

Mheshimiwa Spika, lingine ninaloliona kwa upande wangu ambalo si zuri sana ni lile la viongozi kuwepo, madarakani kwa mkataba. Hivi kuna sababu gani za msingi za kuendeleza utaratibu huu wakati sasa hivi Taifa linao wasomi wengi, wenye ujuzi na uwezo wa hali ya juu. Wapo wanamangamanga mitaani bila ajira.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba Serikali hutumia fedha nyingi kwa ajili ya kupambana na rushwa kazi ambayo imezaa matunda kwa kiasi kidogo sana. Katika utafiti wangu nimeona kuwa rushwa chanzo chake hasa ni kutokana na kipato kidogo kwa watumishi na huduma mbaya kwa wananchi. Ni vizuri Serikali iboreshe vipato kwa watumishi na huduma nzuri/bora kwa wananchi ili kuondoa usumbufu au ucheleweshaji kwa wananchi na kuondoa tamaa kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la utoaji wa zabuni kwa wafanyabiashara katika Taasisi mbalimbali na Idara za Serikali. Baadhi ya wafanyabiashara walikuwa wakitoa huduma na kucheleweshewa malipo au kutolipwa kabisa hadi sasa wengi wao ni wazee sana au marehemu suala ambalo si haki kwa wazabuni, kwani wamekata tamaa na kuwa hohehahe hadi familia zao kuathirika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali imalize tatizo hili kwa wakati muafaka sasa ili kurudisha imani kwa wazabuni.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hotuba ya Bajeti ya Wizara hii kwani imezingatia na kukidhi matarajio mengi ya wananchi.

Pamoja na kuunga mkono, napenda kuishauri na kusisitiza kuhusu mambo yafuatayo:-

Kwanza, kufufua Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata. Mabaraza hayo bado sheria inayotambua *(Ward Tribunals)* na yana madaraka makubwa ya kusikiliza kesi ndogo ndogo Vijijini na kutoa hukumu. Lakini katika Halmashauri nyingi Mabaraza hayo hayafanyi kazi hivyo kusababisha mlundikano wa kesi ndogo ndogo kwenye Mahakama za Mwanzo ambazo tayari zina upungufu wa Mahakimu. Nashauri Wizara isimamie Halmashauri zote zifufue Mabaraza hayo ili kupanua wigo wa vyombo vya kutoa haki Vijijini

Pili, matumizi ya Fedha za Barabara Vijijini. Fedha za Barabara ambazo zimeletwa kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya Barabara za Vijijini nashauri badala ya zote kupelekwa kwa Mkandarasi, sehemu zitumike kwa mtindo wa *TASAF* yaani wanavijjiji wanaohusika na barabara hizo waajiriwe kutengeneza barabara hizo chini ya mtaalam wa barabara kama *TASAF* wafanyavyo. Utaratibu huu uliwezesha Barabara za Vijijini kutengenezwa kwa haraka na kwa gharama nafuu na kwa kuzingatia viwango. Kazi za kitaalamu kama madaraja, kuweka vifusi na kushindilia ndizo zipewe mkandarasi. Lakini kazi za kuinua tuta la barabara, mifereji, na kadhalika zinaweza kufanywa na wananchi na walipwe ili kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuanzisha Vijiji Vipya na Kata Mpya, hivi sasa kwenye *pipeline* yapo mapendekezo ya kuanzisha Vijiji na Kata mpya kutoka Halmashauri mbalimbali pamoja na Halmashauri ya Manyoni. Nashauri kwamba katika kipindi cha maandalizi ya Serikali Kuu kuanza kumlipa mishahara *VEO* na *WEOs* itafaa Wizara ya TAMISEMI ikatazame maombi haya na kuyafanyia uamuzi kabla ya Januari, 2004.

Namalizia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii. Pongezi kwa Wizara ya TAMISEMI kwa kazi nzuri mnayoifanya.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Brigedia Jenerali Hassan Ngwilizi, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hiyo. Wizara hiyo sasa imetulia na mizozo ya hapa na pale haipo tena. Kama ikiwepo inashughulikiwa mara moja kwa umakini mkubwa. Natoa shukrani na pongezi kwa Naibu Waziri Mheshimiwa *Comrade* Mizengo Peter Pinda, kwa kazi nzuri anayoifanya hasa anayojibu vizuri kwa makini maswali ya Wabunge na amekuwa karibu sana na sisi Wabunge. Wizara imefanya busara kubwa kujenga hoja hadi Serikali sasa kukubali kuwalipa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa. Hili ni eneo muhimu katika kusimamia maendeleo. Kwa hatua hii tumekamilisha mtiririko wa utawala.

Pili, naunga mkono jinsi ambavyo sasa inapeleka pesa moja kwa moja Ofisi ya *DC*. Ma-*DC* wamekuwa omba omba kwenye Halmashauri. *DC* ni mtawala, lazima aonekane kweli ni mtawala. Sio mtawala ombaomba pia atashindwa kufanya kazi ya ulinzi na usalama. Akitaka kwenda Vijijini, lazima aombe mafuta Halmashauri. Wizara kwa makusudi ili kuimarisha Ofisi za Ma-*RC* na Ma-*DC*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kazi nzuri sana. Kwa hali hiyo naiunga mkono hotuba na hoja yao.

Ombi langu ni kuhusu Wilaya ya Dodoma Vijijini ndiyo Wilaya yenye Kata nyingi kuliko Wilaya nyingine zote nchini. Ziko Wilaya 48 na bado kuna Kata zetu mbili za Segala na Fufu ni kubwa sana. Mwaka 2000 tuliomba zigawanywe ili tupate Wilaya nyingine mbili. Ombi hilo halikukubaliwa kwa maelezo kwamba tungeendelea kuzidisha Kata hadi 50. Kwa hiyo, tukashauriwa tuombe kugawa Wilaya yetu ili tuwe na Wilaya mbili. Tumekwishaleta ombi Wizarani kwako tunaomba lizingatiwe.

Sambamba na ombi hilo la kugawa Wilaya yetu ya Dodoma Vijijini, yale maombi yetu ya mwaka 2000 ya kugawa Kata zile mbili za Segala na Fufu lizingatiwe pia kwani Kata hizo ni kubwa sana. Kata ya Segala tulipendekeza izae Kata mbili za Segala na Zajilwa na Kata ya Fufu tulipendekeza izae kata mbili za Fufu na Chiboli.

Liko suala la kuondoa umaskini kutumia Vyama vya Ushirika hususan *SACCOS* na Vyama vya Msingi imara vyenye kuundwa na wanachama waliokwishahamasishwa na kuelewa dhana ya ushirika. Kwa Mkoa wa Dodoma jambo hili linaweza kufanikiwa iwapo Serikali za Mitaa hususan Halmashauri za Wilaya zitatoa kipaumbele kinachostahili kwa kuitengea Idara ya Ushirika fedha za kufanyia kazi hiyo.

Suala la jumla ni kuhusu matumizi ya watumishi wachache wa Idara ya Ushirika, baadhi ya Halmashauri haziwatumii kwa kazi za Idara ya Ushirika na badala yake hupangiwa kazi nyingine kama vile kufunga Mahesabu ya Halmashauri. Hali hiyo inafifisha jitihada za kuimarisha ushirika nchini. Nawatakieni kila la kheri kwa kazi nzuri sana mnazofanya Wizarani.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hotuba yake nzuri na ya uelewa. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nianze na barabara kati ya Mtama - Kitangari - Newala. Barabara hii ina muda wa miaka mitano (5) haijafanyiwa ukarabati. Tarafa ya Kitangari ndiyo inayoongoza katika

uzalishaji wa korosho, hivyo, kwa barabara hii kuwa mbaya, uchumi wa Wilaya yetu ya Newala unadumaa ukizingatia Wilaya ya Newala tunategemea sana zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vituo vya Afya, tuna matatizo ya usafiri wa magari katika Kituo cha Afya cha Chilangala na Kitangari ukizingatia Vituo hivyo vyote viko mbali na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Watendaji wetu wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala, kuna Watendaji ambao wamekaa miaka mingi pale Halmashauri, mfano ni Afisa Elimu, yuko pale takriban miaka 20 au zaidi. Afisa Ushirika naye yuko pale kwa takriban miaka 20 au zaidi. Watendaji hawa sasa wanashindwa kufanya kazi! Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala pamoja na matatizo aliyonayo pia ni mgonjwa, kazi zote anafanyia nyumbani kwake na si ofisini!

Mheshimiwa Spika, ninapenda kupata jibu kwa nini Mtendaji anakaa miaka yote hiyo bila kuhamishwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, narudia kusema naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa Bajeti yao nzuri. Aidha, napenda kuchangia mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuna umuhimu wa kuweka vigezo vya kuliita eneo Kijiji, tafsiri ya watu 250 haitoshi hasa kama Kijiji hakijiwezi kiuchumi *(Economic/social Viability)*. Ilivyo sasa hivi Vijiji vingi vinahudumiwa na Mtendaji *(VEO)* mmoja kati ya Kijiji kimoja hadi vitatu). Hii inazorotesha maendeleo Majimboni.

Mheshimiwa Spika, pili, *VEOs* wengi elimu yao ni darasa la saba. Hii ni elimu ndogo mno kuwa kichocheo cha maendeleo Vijijini. Elimu ya darasa la 12 iwe kigezo cha kuajiriwa katika Karne hii ya 21.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni muhimu *VEOs* wakapewa *orientation* yenye mwelekeo wa *Community Development* ili wawe chachu ya maendeleo Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nne, *VEOs* sharti wawe wanatoa taarifa ya kazi ya kila mwezi, wasiwe wanazagaa Vijijini bila shughuli rasmi/inayoelezeka. Taarifa zipelekwe kwa *DED*. Hii ina maana pawe na *Job Description* inayoeleweka. Aidha, ni vizuri pakawa na *Scheme of Service* yao. Mwenye bidii aweze kupanda hata kufikia ngazi ya Katibu Tarafa.

Mheshimiwa Spika, tano, ningefurahi kuona *VEOs* hawapangiwi kufanya kazi mahali walipozaliwa. Inawawia vigumu kuwa makini *(efficient)* kazini katika maeneo wanayoishi, walipo jamaa zao.

Mheshimiwa Spika, sita, hesabu za Vijiji zikaguliwe kila mwaka. Mapato mengi ya Kijiji yanatumika vibaya na Viongozi kulewa tu! Hii inawakatisha tamaa Wananchi kuchangia maendeleo yao. Hatua kali zichukuliwe kwa Viongozi wezi, walevi na hasa wafujaji fedha. Tusikazanie hesabu za *District Councils* peke yake, usafi wa hesabu za Vijiji ndiyo kichocheo cha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, narudia kutoa hongera kwa Bajeti nzuri na vile vile kwa umakini wa Waziri na Naibu wake, kusikiliza maoni ya sisi Wabunge. Tafadhali waendelee kuwa na spirit hiyo hiyo.

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spikal kwanza, naomba nieleze kuwa Jimbo langu lina Tarafa tatu na kuna Vituo viwili tu vya Afya. Vituo hivyo vipo mbali na hospitali ya Rufaa ya Mbeya, hawana gari la wagonjwa, Wananchi wanapata tabu wanazalia njiani na kama ni bahati mbaya ana *complications*, basi anapoteza

maisha. Chonde chonde, naomba magari mawili ya wagonjwa kwa ajili ya Tarafa ya Santilya na Tembela. Ombi hili ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, *Engineers Registration Board (ERB)* walifanya utafiti kwenye Halmashauri zote kujua ni Wahandisi wangapi wamesajiliwa na Bodi. Waligundua kuwa Mbeya (Mkoa) ni Mhandisi mmoja aliyesajiliwa. Fedha za barabara hazitumiki vizuri au kama zinatumika barabara hizo ni mbovu. Wahandisi wengi ni *fake,* hawafai kuwa Wahandisi, wanatakiwa waondolewe. Kwa kusaidiana na Wizara ya Ujenzi, tupate Wahandisi kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. HUSSEIN A. MWINYI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nauelekeza kwenye hoja moja tu nayo ni Uchaguzi wa Watendaji wa Halmashauri. Katika Wilaya yangu. Tulikuwa na mgogoro mkubwa juu ya utendaji wa *DED.* Tulilalamika na hatimaye aliondolewa baada ya mambo mengi kuharibika. Fedha nyingi za ushuru na zinazoletwa na Serikali kwa Idara mbalimbali kutumika vibaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuondoka *DED,* mambo yanakwenda vizuri sana kiasi kwamba Halmashauri kupitia kikao halali cha *Full Council* kiliazimia kuomba Kaimu Mkurugenzi athibitishwe kiazini na Mamlaka husika. Kaimu huyu ambaye ni Afisa Mipango anafanya kazi nzuri sana ambayo imeturidhisha sisi kama Madiwani na ameweza kuondoa kero nyingi za Wananchi sambamba na Ilani ya Uchaguzi inavyosema.

Mheshimiwa Spika, tunachomwomba Mheshimiwa Waziri ni Mamlaka hii ya Uteuzi (TUMITAA) wasikilize mawazo na maamuzi ya vikao halali kwani ndiyo walio karibu na Watendaji. Tatizo kubwa imekuwa kuletewa Watendaji ambao siyo wazuri bila kujali maoni ya vikao vya Madiwani. Ni mategemeo yangu kwamba, suala hili litaangaliwa na Mamlaka husika itasikiliza maoni ya wadau katika kuteua Watendaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu ushuru ambao ni kero kwa Wananchi na *agent* anayetumia pesa kuwarubuni Viongozi na kunyanyasa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, *stand* ya Maili Moja imekuwa ni mateso kwa wafanyabiashara hasa wenye magari, kwani mabasi makubwa hulazimika kuingia *stand* hiyo ili wakaguliwe na *traffic,* lakini wanapotoka hulazimishwa kutoa Sh.500/= hata kama hawakupakia abiria! *DED* katika kikao cha Kamati ya Fedha alisema hilo si kero bali baadhi ya mabasi ya Tanga yanatumia nafasi ya kumfahamu Mheshimiwa Waziri na kumlalamikia. Kwa hiyo, *DED* na Madiwani hawaoni kama ni kero.

Mheshimiwa Spika, mabasi madogo hulazimika kutoa Sh.200/= kila linapoingia *stand.* Mabasi ya Kongowe na Mlandizi kwa siku hutoa Sh.1,600/=. Pia, taxies hulazimika kutoa Sh.200/= wanapotoka stand na kwa siku hutoa Sh.2,000/= hadi Sh.3,000/=.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa magari na ushuru mwingine unaotozwa kwa magari haya humfanya Mtanzania mmiliki/wamiliki kuendelea kuwa maskini na kunufaisha Halmashauri tu!

Mheshimiwa Spika, kero nyingine ni kuhusu *agent* aliyepewa *tender* ya kutoza ushuru. Niliwaeleza Wadiwani wasimpitishe mtu huyo kwa sababu ana matatizo, lakini sikusikilizwa! Baadhi ya Madiwani walimpitisha huku wanajua matatizo yake! Tabia yake mbovu ya kuhonga Viongozi ilianza kujulikana alipokuja kutaka kufanya biashara eneo la CCM. Kwanza, alimrubuni Mwenyekiti wa Tawi la CCM Maili Moja aliyekuwpo mpaka akawa mlevi, akanyanyasa familia yake na kuoa mke mwingine. Pia, Mwenyekiti wa Tawi akataka CCM Wilaya ihamie kwenye Tawi lake kwa mdomo na maandishi.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti alidiriki kuwafukuza baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Siasa wa Tawi waliochaguliwa na kuweka watu wake, ili waweze kutimiza azma yake na kumweka huyu Bwana.

Vile vile, aliamua kuvunja mlingoti wa CCM uliojengwa ili aweke biashara yake na alipoulizwa na Katibu na CCM Wilaya alimtolea maneno ya kashfa na kusema ana kinga ya Mwenyekiti wa Tawi.

Mwenyekiti wa CCM Tawi alimpa *meter* ya *TANESCO* ambayo ilikuwa inatumiwa na Ofisi ya CCM na maduka yaliyokuwepo eneo la CCM na yeye *(agent)* akaamuru kila Ofisi ya CCM na maduka walipe Sh.30,000/= kila mmoja kwa mwezi. Hii imefanya Ofisi ya CCM isiwe na umeme. Pia, maduka yaliyokuwa yanailipa CCM kodi ya pango kulazimika kutafuta umeme sehemu zingine na wengine kuhama.

Mheshimiwa Spika, CCM Wilaya ilikuwa haina hadhi mbele ya huyu Bwana *(agent)*. Kwa sababu hiyo Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi walilazimika kumsimamisha Mwenyekiti huyu na kuwarudisha Wajumbe wa Kamati ya Siasa waliofukuzwa. Mwenyekiti huyo hivi sasa sio Kiongozi. Baadhi ya Madiwani walikuwa Wajumbe wa Kamati ya wakati huo, lakini walifumbia macho matatizo hayo na kumpa tender ya kukusanya ushuru Maili Moja, kulikoni?

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata *tender* ya kukusanya ushuru, manyanyaso yameanza kwa wenye magari. Hivi sasa ameshawarubuni Maaskari Polisi, naamini utasoma kwenye *Hansard* yangu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa haki ya madereva ameishika yeye kwa kutumia Polisi. Imefikia Polisi kuwaweka ndani madereva bila ya kufunguliwa kesi na wakitaka kutolewa inabidi watoe Sh.10,000/= na kama madereva wahusika wahataki kuwekwa ndani, hulazimika kumpa Polisi Sh.5,000/=. Nilipokwenda kumpa taarifa *RPC* akasema, sina haja ya kumwona yeye ila nikatoe malalamiko Bungeni. Alijitetea kuwa, kuweka mtu ndani kwa saa mbili ni haki ya Polisi, la sivyo niliambie Bunge lifute Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa faida ya Serikali ya CCM na Chama chake huyu *agent* aliyepewa *tender* hiyo atolewe. Hivi sasa CCM inasemwa vibaya kwa sababu ya kero anayoisababisha agent huyo *stand*. Kampuni yake inaitwa *SALU Investment*, *agent* huyo ni kiburi sana na mnyanyasaji mkubwa, anapewa kichwa na kiburi na *DED*, Madiwani na Askari kwa uwezo wake wa kuwahonga. Pesa sabuni ya roho, humtoa nyoka pangoni, ilimsaliti Yesu, itaisaliti CCM 2005.

Mheshimiwa Spika, ninakumbusha kuwa, vijana hawa wa stand ya Maili Moja, walifanya kazi kubwa katika uchaguzi wa mwaka 1995 mpaka CCM kushinda. Kibaha ilikuwa ichukuliwe na Upinzani (CHADEMA), lakini kwa juhudi kubwa za vijana wa *stand* ya Maili Moja, Kata ya Tumbi ambayo ndiyo ilikuwa moja ya ngome ya Upinzani, walifanya CCM kushinda Kata hii. Leo vijana hawa waliokuwa wanategemea kuenziwa sasa wananyanyaswa!

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Waziri atumie uwezo wake *agent* huyu atolewe. Hautaamini kwamba *stand* iliyojengwa kwa fedha nyingi ili Wananchi wapumzike wakisubiri magari au kujikinga na jua au mvua imevunjwa na kuwekwa *container* la *agent* huyu, hii siyo kuwanyanyasa raia? Ikumbukwe kuwa, *agent* huyu ni Mweka Hazina wa Kampuni iliyokodi Kiwanda cha Korosho, yeye na wenzie wamewakimbia Wananchi bila ya kuwalipa mishahara yao. Wenye Kampuni hii hawajulikani walipo, lakini *SALU Agent* huyu yupo Kibaha! Wafanyakazi wameomba akamwite ili awataje wenzie walipe fedha za wafanyakazi. Polisi hawamkamati na hawajaandika mashtaka dhidi yake. *Taxi* namba 40 ya *OCD* haisumbuliwi!

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri awanusuru Wananchi *stand* ya Maili Moja kunyanyaswa kwa sababu ya *agent* huyu anayekusanya ushuru *stand* ya Maili Moja. Pia, naomba Waziri atume Wataalam wake wachunguze tuhuma hizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Wataalam wake kwa hotuba hii ambayo imefafanua kwa kina suala zima la utendaji katika Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuchukua jukumu la kuwalipa mishahara Maafisa Watendaji wa Kata, Vijiji na kuanzisha cheo cha Afisa Mtendaji wa Mtaa. Vile vile, naipongeza Serikali kwa kufuta kodi ya maendeleo na ushuru mdogo mdogo wa baiskeli, mboga na ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuangalia upya posho za Waheshimiwa Madiwani ziongezwe na wakopeshe baiskeli na pikipiki. Pia, mafunzo ya Waheshimiwa Madiwani yanayoendelea sasa yamechelewa kuanza, nashauri mafunzo haya yawe yanaanza mara baada ya uchaguzi kumalizika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi bora ya ardhi na ili Wananchi waelewe mwongozo uliotolewa na Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, semina zitolewe kwa Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Wabunge, ili waweze kuwaelimisha Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya kisiasa, nashauri Serikali kuwafanyia semina Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa mwezi Mei, 2003 kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni za Bunge hasa Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafi katika Miji na Jiji, Serikali izisaidie kuzipa fedha za kuwezesha kufanya usafi hasa kuchimba mitaro ya maji machafu na Halmashauri na Manispaa zibuni njia za kusafisha Miji ili kuzuia milipuko ya magonjwa kama kipindupindu. Mabwawa ya maji machafu ya Ipagala Dodoma yaongezwe na kuboreshwa. Vile vile, Wananchi wanaweza kushirikishwa katika kazi hizi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi za Wabunge wa Majimbo na Viti Maalum katika Mikoa zijengwe au ziboreshwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pili, Sheria za kuteua ma-*RC* na ma-*DC* itazamwe upya. Pia, ma-*DED* wanaonekana kutokuwa na udhibiti halisi. TUMITAA huchangia utendaji mbovu kwani iko *headquarter* tu. Hivyo, hoja ya mhimili ni lazima iwepo.

Mheshimiwa Spika, Madiwani walio wengi hawana semina za kutosha, hivyo, hupenda kuamua bila kufuata taratibu.

Mheshimiwa Spika, suala la Jimbo la Kigoma Kusini bado ni baya kijiografia kwa Mbunge kuweza kulitembelea kwa muda wa mwezi moja. Barabara ya kwenda mpaka mwisho wa Ziwa Tanganyika (Kalya) ni mbaya.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu kwenye Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza, namshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wataalam na Watendaji wote wa Wizara hii muhimu kwa taarifa nzuri ambayo imewasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imeleta hoja ambayo baada ya kuijadili tutafikia Azimio la kupitisha Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2003/2004. Mchango wangu kwenye hoja ya Wizara ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwanza, utumishi na utendaji katika Halmashauri zetu hususan kwenye Halmashauri ya Jiji la Mwanza kama mfano si mzuri. Kuna uzembe mwingi, kutotekeleza majukumu kwa viwango vya kutoridhisha, mazingira ya kutoonyesha kuwajibika kikamilifu (*laiss'ez-faire)* mapungufu ya utii wa Watendaji kwa wanaowaongoza, tija ndogo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaleta sura ya mapungufu ya taaluma, ujuzi na Sheria legelege za kazi ambazo zinawafanya Watumishi kuonekana wanashindwa sana, kwa hiyo, kuwa vichwa maji. Kwa

mfano, Mhandisi wa Jiji la Mwanza ambaye mpaka sasa ana matatizo kazini hana sifa za kutosha kwenye kazi hiyo. Pia na wengine kwenye Idara za Uhasibu, Utumishi, Biashara na kadhalika. Kwa nini Wizara inafumbia macho na kuendelea kulinda hali hii wakati sasa nchi inao Wataalam wa fani zote hizi na wanapatikana?

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, Wizara inachukua muda mrefu sana kutoa adhabu kwa wenye makosa. Waliosababisha ujenzi wa kituo cha mafuta kwenye eneo la barabara ya Makongoro Mwanza Jijini na pia matumizi mengine ya ardhi kinyume na taratibu mashauri yao yamalizike. Kwa vile ushahidi unaonekana wazi, hawa waondolewe kazini ili wawe funzo kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, tatizo la rushwa bado ni kubwa kwenye Halmashauri zetu na kwa kiwango kikubwa inaathiri sana utendaji kazi kwenye maeneo haya. Inapunguza tija, inaharibu imani kwa Wananchi na kuonyesha kwamba haki haitolewi kwa raia na Chombo chao hicho. Kwenye maeneo ya Miji na Majiji, zoezi la ugawaji viwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi, biashara viwanda na kadhalika, unazungukwa na wimbi kubwa la rushwa. Mambo mengi kwenye Halmashauri zetu yanafanyika mwenye mazingira ya rushwa. Wizara inashauriwa kuwa na mkakati wenye nguvu juu ya kudhibiti rushwa. Watumishi wa kuhamishika wawe wanapelekwa kwenye vituo vingine kila baada ya miaka miwili na nusu.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano kati ya Makao Makuu ya Wizara na Halmashauri kuhusu maamuzi mbalimbali si mazuri. Ukamilishaji wa maamuzi kati ya Wizara na Halmashauri huchukua muda mrefu sana kufikiwa. Uchelewaji huu unasababisha hata haya matatizo ya Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri zinapoleta hoja ya kumkataa Mkurugenzi Mtendaji Wizarani kwamba wameshindana naye, basi Wizara inapaswa kutoa jibu haraka.

Wizara inapaswa kuiarifu Halmashauri husika maamuzi yake kama inakubaliana na ombi/pendekezo la Halmashauri au la. Kama Wizara inakataa pendekezo hilo basi pia itoe sababu zake mara moja. Zaidi ya hapo itoe maelekezo sahihi kama funzo na kuikumbusha Halmashauri hiyo namna ya kuchukua hatua zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Pamoja na mipango/maelezo na mikakati mizuri katika hotuba yake hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri afanye maboresho katika maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu Baraza la Madiwani. Kulingana na taratibu za TAMISEMI inaelekea Serikali inakosa au imepungukiwa na imani kwa wawakilishi wa Wananchi kama kutokuwa huru kutembelea miradi ya maendeleo bila idhini ya *DED*, kutoshirikishwa katika *tender* na pia kutokuwa na mazingira wazi ya kumdhibiti *DED* watendaji walioko chini yake. Hali hii inapaswa iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu Shule za Sekondari za Wananchi. Shule hizi kimsingi zinamilikiwa na *DED* kwa niaba ya Wananchi wa maeneo husika, maendeleo yake na uendeshaji wake haufahamiki kwa Baraza la Madiwani wala *DED*. Hata muundo wa Bodi za Shule hizi hauhusishi Madiwani wana uwakilishi wa *DED*. Hati ya maendeleo ya Shule hizi yamekuwa duni na yakimtegemea Mkuu wa Shule peke yake, jambo ambalo ni hatari sana. Pia, inabidi TAMISEMI ihusike na Shule hizi kama zile za Msingi ndani ya miliki yake, vinginevyo iwekwe bayana kuwa Shule hizi ni za Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kuhusu ruzuku ya Serikali za Mitaa kutoka Serikali Kuu. Utaratibu huu wa Serikali Kuu ni nzuri na unahitaji kupongezwa katika Sekta za maji, afya, elimu na barabara na sasa kilimo. Kikwazo kikubwa ni Halmashauri zetu kubweteka na ruzuku hizo badala ya kubuni/kukuza vyanzo vyake vya mapato ndani ya Halmashauri ili Wananchi wao wachangie maendeleo yao katika Halmashauri zao. Kila Halmashauri ingepaswa iwajibishwe katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, nne, ni kuhusu Asasi/*NGOs* katika Halmashauri zetu, kwani ni wachangiaji wakubwa katika maendeleo ya watu. Asasi zinadai Halmashauri haziwapi ushirikiano, lakini Halmashauri nazo hazijui na hazijishughulishi kutaka kujua taarifa/mipango ya kazi ya Asasi/*NGOs* hizi. Ipo haja ya TAMISEMI, sasa kuweka uratibu wa Asasi/NGOs hizi katika kila Halmashauri, vinginevyo zitakuwa za mifukoni mwa watu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ROBERT K. MASHALLA: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii ili nitoe mchango wangu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano wao wa kuanda bajeti nzuri yenye matumaini kwa Watanzania. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Bajeti hii ni nzuri, naomba nitoe ushauri tu kwa maeneo mawili ambayo yanaonekana kuwa kero endapo hayatachukuliwa hatua haraka.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni suala la madai sugu ya Walimu wa Shule za Msingi. Kuna malalamiko ya Walimu hao juu ya madai yao kutolipwa kwa muda mrefu. Madai hayo ni mapunjo ya mishahara, uhamisho, marekebisho ya ikama na mishahara kwa ajira mpya.

Mheshimiwa Spika, madai haya yamekuwa yakilalamikiwa na Walimu kwa muda mrefu sasa bila mafanikio. Kwa Wilaya ya Bukombe pekee, Walimu wanadai jumla ya Shilingi 176 milioni na madai haya nimeyawasilisha *Local Government,* lakini mpaka sasa hayajapatiwa ufumbuzi, kitu ambacho kinawafanya Walimu wetu wapunguze ari ya uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, pili, nashauri Serikali itoe ufafanuzi jinsi gani inashughulikia madai ya Walimu ili Walimu wetu waendelee kuwa na imani na Serikali yao na ufafanuzi utolewe na Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nizungumzie fedha za *capitation* zinazopelekwa kwenye Shule za Msingi. Fedha hizi zinapelekwa, lakini hazizingatii uwiano wa idadi ya wanafunzi walioko kwenye Shule husika, hivyo, kushindwa kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa. Naomba Serikali irekebishe hali hii ili fedha zinazopelekwa ziwiane na idadi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHAN H. KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa ufanisi mkubwa alioutumia katika kuwasilisha hoja yake.

Mheshimiwa Spika, vile vile, niwapongeze Wataalam wote ndani ya Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Deotrephas Mmari. Pongezi maalum pia napenda kuzitoa kwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Naibu Waziri, ambaye sote humu Bungeni tunatambua umahiri wake katika kuiongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, hotuba tunayoijadili inayo ndani yake mambo mengi mazuri, hivyo, nalazimika kuiunga mkono kabla sijaenda mbali katika kuchangia.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la mafunzo kwa Viongozi na Watumishi (ukurasa wa 4 kifungu cha 9/10) ni jambo zuri sana na la msingi kabisa. Napenda kuishauri Wizara ilitie maanani na kutoa kipaumbele kutoa mafunzo zaidi na maalum kwa Maafisa Utumishi katika Halmashauri zetu. Wengi wa

tulionao sasa hivi ni wenye taaluma ndogo sana na wengine hawana kabisa fahamu ya utawala wa Watumishi.

Mheshimiwa Spika, chanzo kikubwa cha malumbano na migogoro isiyo na maana katika Halmashauri zetu ni kwa sababu ya kukosa Watumishi wazuri katika utawala wa Watumishi na kutojua au kuzingatia Sheria za Kazi. Afisa Utumishi aliye mahiri katika fani ya utawala na utumishi na Sheria za Kazi ni kiungo muhimu katika uendeshaji mzuri wa Halmashauri zetu na ni mshauri mzuri katika upande wa uongozi na Madiwani katika masuala ya Wafanyakazi/Watumishi.

Mheshimwia Spika, mapungufu mengi yanayojitokeza katika ajira na utoaji adhabu kwa Watumishi inapobidi inaleta migongano na tafrani nyingi kwa sababu tu Maafisa Utumishi waliopo wengi kabisa hawafai. Napenda kutoa mwito maalum kwa Wizara kulifanyia kazi eneo hili na kwa sisi wa Bagamoyo ni mfano hai wa kuwa na Afisa Utumishi mwenye uwezo wa chini sana kikazi na upeo duni kabisa wa uelewa wa Sheria za Kazi na utumishi. Wizara itusaidie haraka.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ninalopenda kulichangia ni lile la Mfuko wa Barabara (ukurasa wa 35 vifungu 74/75) Wizara imeliweka vema sana suala la Mfuko huu. Kwa kipindi cha mwaka mzima Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ilifungiwa kupata fedha za mgao wake na kusababisha adha kubwa sana kwa wakazi wa Wilaya nzima ya Bagamoyo Mjini na Vijijini kote. Wizara inavyo Vijiji 68 na Vitongoji 657, vimeachwa katika hali mbaya kabisa kimawasiliano ya miundombinu ya barabara kutokana na makosa yaliyo nje kabisa ya uwezo wao kuyazuia.

Mheshimiwa Spika, tarehe 19 Juni, 2003, Waziri wa Ujenzi akijibu swali la nyongeza Bungeni, alikiri bayana na kulifahamisha Bunge rasmi kwamba, katika Halmashauri 114 ambazo zilikaguliwa zilikuwa na jumla ya Wahandisi 211. Kati ya hao, Waziri wa Ujenzi alilifahamisha Bunge kwamba, Wahandisi 20 hawatakiwi kabisa kuitwa Wahandisi kwa sababu hawana sifa *(qualifications)* zozote. Aliendelea kulieleza Bunge kuwa, Wahandisi watano (5) wako Mkoa wa Pwani, Mkoa wenye Wilaya sita (6). Tazama Hansard ya tarehe 19/06/2003, ukurasa wa tano.

Napenda kumwomba rasmi Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa awavue Wananchi wa Bagamoyo mzigo huu wasiostahili kuubeba, lakini wamebebeshwa kwa miaka kadhaa sasa. Pamoja na kuchoka, lakini pia sitaki kuwaacha wakiumizwa kiasi hiki. Wizara ichukue hatua za haraka katika kulipatia ufumbuzi suala hili ambalo halina hadhi ya kuzusha mjadala wa aina yeyote ile.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuzungumzia kuhusu TUMITAA. Idara hii isiachwe ikachafua heshima iliyojengeka katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. TUMITAA ijisafishe na isafishe safu ya utumishi katika Halmashauri zote. Waachane kabisa na hulka ya upendeleo katika kuajiri na isitishe tabia yake inayowafanya waonekane ni walinzi wa waovu na Mababa wa Ubatizo *(Godfathers)* wa Watumishi wabovu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga tena hoja mkono.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia kwangu kwa kuongea, napenda kuchangia machache kwa maandishi, kuhusu Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza, nawapongeza kwa juhudi kubwa waliyoifanya katika kurekebisha matatizo mengi yanayofanywa na Watendaji wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kutoa fedha za mikopo kupitia Mifuko mbalimbali, lakin imipango ya utoaji wa mikopo hiyo ni mbaya sana. Kwanza, wanapewa vikundi kwa upendeleo na Vijiji vilivyoko mbali havipati. Pia, ufuatiliaji wa kuhamasisha ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa masahihisho kwenye majedwali ambayo yameandikwa. Kwanza, Vijiji vya Wilaya ya Monduli ni 71 na siyo 69. Pia, majengo ya shule yalizojengwa siyo 24 kama ilivyoandikwa kwenye jedwali namba 15, bali ni ni majengo 176, lakini baadhi ya majengo hayo hayakumalizika. Taarifa za Wilaya ya Monduli kila mara zinaandikwa kwa kubuni tu! Naomba ufuatiliaji wa takwimu za Halmashauri ya Monduli.

Mheshimiwa Spika, narudia kuunga mkono hotuba hii.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii adhimu ili nami niweze kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri mwenyewe Mheshimiwa Brigedia Jenerali (Mstaafu) Hassan Ngwilizi na Naibu wake, Mheshimiwa Kayanza Mizengo Peter Pinda, kwa umahiri wao katika kuendesha Wizara hii kubwa na nyeti katika ujenzi wa Taifa hili na hasa katika kipindi hiki ambapo nchi inasogeza Serikali na maamuzi ya maendeleo karibu zaidi na Wananchi kupitia Halmashauri zao, katika mkakati mzima wa kuondoa umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mafanikio yaliyopatikana katika miaka hii miwili kwenye nyanja za elimu ya msingi, katika ujenzi wa miundombinu kama barabara, maji na kadhalika, Waziri anastahili pongezi za pekee na kwa kweli kama tungekuwa tumeanza namna hii miaka ya nyuma, sasa hivi tungekuwa tumepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mafanikio yaliyokwishapatikana, napongeza mpango uliopo wa kuteua Watendaji bora wa Tarafa na hata wenye upeo mkubwa na pia watakaokuwa na ngazi ya mishahara. Hii itaongeza sana uwajibikaji wa Watendaji hawa katika kusimamia maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini hapo hapo, napenda kutoa ushauri kwamba, ingekuwa vema na uamuzi wenye manufaa zaidi utakaoimarisha zaidi Serikali katika ngazi ya chini kama Madiwani ambao si wengi sana kama Watendaji nao wangeingizwa katika mfumo wa mishahara. Naelewa fika uwezo wa Serikali, lakini nafahamu pia umuhimu wa Serikali ya CCM kurudishwa na kuendelea na madaraka ya Dola mwaka 2005 kwa kigezo cha mafanikio makubwa kabisa katika maendeleo ya nchi hii hasa katika kipindi cha miaka ya uhai wa Bunge hili.

Lakini uzoefu unaonyesha kwamba, hata mafanikio ni lazima yasemwe na msemaji wetu mkubwa katika ngazi ya chini yaani Kata na Vijiji ni Diwani. Naomba tusipoteze fursa hii, kumbuka katika kampeni ya kushika Dola huwa tunawanadi wagombea watatu muhimu yaani Diwani, Mbunge na Rais. Jambo hili ni la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kuzungumzia majedwali yanayoletwa kutoka Mikoani kwetu. Katika jedwali la kutoka Tabora, halina makadirio yoyote kwa ajili ya Ofisi za Wabunge, hii inadumaza sana maendeleo ya Wabunge katika Majimbo yetu. Ninapendekeza *allocation* ifanyike hata kama ni kidogo ni mwanzo mwema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia zote. Ahsante.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ili niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Waziri wa hotuba nzuri, hususan kwa vile Serikali imeondoa kodi ya maendeleo, jambo ambalo lilikuwa ni kero kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri afanye kila linalowezekana ili wafanyakazi wenye sifa na uzoefu waajiriwe kwenye Halmashauri zetu. Hivi sasa kuna upungufu wa Wafanyakazi wenye sifa za Sheria, Uhasibu na Uhandisi. Ukosefu huu unazorotesha ufanyakazi wa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ndogo zinazotungwa na Halmashauri, nashauri Waziri ashirikiane na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba ili kutengeneza *model formats* za Sheria kwa mfano mifugo, mashamba na kadhalika, maana Sheria hizi zinafanana kwa Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za kuhudumia Ofisi za Waheshimiwa Wabunge, mbona Mkoa wa Tabora haukutengewa fedha hizo katika Bajeti hii? Namwomba Waziri arekebishe kasoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa juhudi zake za kuwaelimisha Waheshimiwa Madiwani kuhusu wajibu wao. Nashauri zoezi hili liendelee maana linaleta tija kwa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wataalam wa Wizara kwa kuandaa hotuba iliyotoa dira na maelekezo ya utendaji katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hotuba imejaribu kutosheleza nitaelekeza mchango wangu katika sehemu chache kwa madhumuni ya kuboresha tu. Kwanza, ninaipongeza Wizara kwa kuanzisha *program* ya mipango shirikishi jamii ambayo huwashirikisha Wananchi kupanga, kutambua vikwazo vya maendeleo yao na kutafuta ufumbuzi wa vikwazo hivyo wakati wa kutekeleza mipango yao.

Mheshimiwa Spika, nimeona kiasi cha mafanikio ya *program* hii Wilayani Masasi nilipotembelea Wilaya hiyo Mei, 2003. Kwa vile ni program nzuri, nashauri kasi ya kuieneza nchi nzima iongezwe ili Wananchi waone kuwa maendeleo yataletwa au yatategemea ushiriki wao mkamilifu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kubuni mbinu za jinsi ya kutatua tatizo la madeni ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, *TALGWU, WADU* na kadhalika, kwa sasa fedha zitakatwa moja kwa moja toka Hazina. Uamuzi huu ni wa busara kwa sababu utaondoa kabisa kero kwa Wafanyakazi walio wengi kama si wote kwa vile wengi walikuwa wanakosa fedha zao pindi kwa mfano *WADU* inapoiva, lakini Serikali (Wizara) imewashughulikiaje waliosababisha madeni hayo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa MMEM, naipongeza Serikali na Wananchi kwa ujumla kwa kufanikisha mpango huu kwa awamu ya kwanza, lakini ninashauri Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ishirikiane kikamilifu na Wizara ya Elimu na Utamaduni ili kuhakikisha kuwa vikwazo vya kielimu vinavyowapata watoto wenye ulemavu kwa mfano mazingira ya majengo ya madarasa, vyoo, vifaa vya kujifunzia *(braille machines)* na *(braille papers)* kwa watoto wasioona, matumizi ya lugha za alama kwa watoto viziwi na kadhalika vinaondolewa. Ninaamini bila kushirikiana vizuri kwa Wizara husika MMEM haitawakomboa watoto wengi wenye ulemavu wa hapa nchini, hivyo, watabaki bila elimu na kuendelea kukuza kundi la jamii ya watu maskini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kubuni utaratibu mpya katika jitihada za kuimarisha Utawala Bora Wilayani wa kupeleka fedha za *OC* kwa Ofisi za Wilaya na hivyo fedha kwa ajili ya Ofisi za Wabunge hapo baadaye. Hata hivyo, naomba ufafanuzi wa fedha hizo kwa ajili ya Ofisi za Wabunge ni kwa ajili ya Wabunge wa Majimbo peke yao? Naomba ufafanuzi huo kwa sababu Wabunge wa Viti Maalum hawana ofisi. Kama nao wanahusika, fedha hizo zitatumikaje?

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia suala la kuwaongezea uwezo Waheshimiwa Madiwani. Ni kweli wao ndiyo wanaishi na Wananchi na kuanzia ngazi ya Mtaa mpaka Kata nzima na ndiyo wahamasishaji wa ngazi za awali kabisa za muundo wa Serikali. Kwa msingi huo, matatizo, mafanikio na matarajio ya Wananchi yanawaelemea wao katika kutoa ushauri na kutekeleza kwa kushirikiana na Wananchi. Hivyo, suala la kupewa posho ya kutosha liangaliwe kwa kuongeza ruzuku kwa Halmashauri ili ziweze kuwalipa Waheshimiwa Madiwani posho zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ukosefu wa ajira ni kweli kwamba makundi mbalimbali yameathirika, lakini Wanawake na Vijana wanajaribu kujishughulisha na biashara ndogo ndogo Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo inasikitisha kuona kwamba, Watendaji wa Halmashauri nyingi hupenda kutumia Wanamgambo wa Halmashauri hizo kuwafukuza na kutupa vifaa vya Wafanyabiashara hao kutoka kwenye maeneo wanayouzia kwa kisingizio cha usafi wa Miji, lakini hakuna asiyetaka usafi, ila nashauri kuwa kila Halmashauri iandae kwanza sehemu za kuuzia kwa hao wafanyabiashara ndogo ndogo kabla ya kuwabughudhi Wananchi hao ambao wanajiajiri.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, ni jambo la kiungwana kupongeza na kusifia kazi nzuri. Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inafanya kazi nzuri sana na inastahili pongezi za dhati. Tatizo kubwa ambalo ninaliona si ukubwa wa Wizara kama wasemavyo Waheshimiwa Wabunge wengi, bali tatizo kubwa ni uduni wa miundombinu ya utawala na uaminifu mdogo wa Watendaji katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatakiwa itenge kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya mafunzo ya Watumishi wake hasa katika ngazi ya Uhasibu, Uchumi na Utawala. Suala la msingi ni elimu na matumizi ya kompyuta, Wizara ikiwekeza katika miundombinu ya kompyuta na mafunzo sahihi kwa wafanyakazi wake, utendaji wa wafanyakazi utaboreka sana na Wizara itaonekana ndogo na hakutakuwa na haja ya kuigawa.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la uaminifu mdogo wa Watendaji katika Halmashauri zetu, hasa katika matumizi mabaya ya fedha za umma. Tatizo linakuwa kubwa zaidi kama Madiwani hasa Mwenyekiti wamejiunga katika mchezo mchafu wa wizi wa fedha za umma. Tume nyingi zinazoundwa na Wizara kuchunguza tuhuma za wizi katika Halmashauri mbalimbali zinafanya kazi nzuri, lakini zipo Tume zingine ambazo washiriki wake ama wanapokea rushwa ili wafiche na wapindishe mambo/ukweli au hawajui kazi waliyotumwa kuifanya.

Suala lingine ni ucheleweshwaji wa matumizi juu ya mapendekezo ya Tume hizo pale Wizarani. Aidha, kwa sababu ya kazi nyingi au kwa sababu za udhaifu wa Utawala Bora, Kyela ni mfano mzuri.

Hoja inayotolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi kutaka kuwapa uwezo wa kisheria Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya katika uendeshaji wa Halmashauri au Serikali za Mitaa itazamwe kwa makini sana. Wakuu wa Mikoa na wa Wilaya wana kofia mbili, wao ni Wanasiasa na vile vile, ni Wasaidizi wa Rais Kiserikali. Nionavyo, Waheshimiwa hawa wana kazi nyingi za kuongoza shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao na haitakuwa jambo la busara kuwaingiza katika shughuli za Serikali za Mitaa, wataleta vurugu tupu! Tatizo la matumizi mabaya ya fedha litaongezeka mara kumi, waachwe kama walivyo kama *watchdogs.*

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Kyela lina Mito minne mikubwa ambayo haikauki. Mito hiyo ni Songwe, Kiwira, Mbaka na Lufilyo, ukiacha Mto Songwe ambao ni mpaka wa Kimataifa na nchi ya Malawi. Mito mingine mitatu inaleta matatizo makubwa ya mawasiliano kwa Wananchi na wanafunzi. Kuvuka Mito hiyo ni matatizo makubwa sana. Mamba wamezagaa katika Mito hiyo na Wananchi wengi wamepoteza maisha yao kwa kuliwa na mamba.

Mheshimiwa Spika, njia pekee ya kuwasaidia Wananchi hawa ni kujenga supervision bridger katika sehemu muhimu za mito hii mitatu. Ninaishukuru Serikali kwa madaraja mawili ya aina hiyo yaliyojengwa kwenye mito ya Kiwira (Ngana) na Lufilyo (Kagera). Hivi sasa daraja lingine la aina hiyo linajengwa katika Mto Kiwira likiunganisha Mji wa Kyela na Vijiji vya Kata za Ikolo na Katumba Songwe. Ombi langu ni kujenga daraja lingine la aina hiyo katika Mto Mbaka kuunganisha Kata ya Ipande na Kata ya Ipinda.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hotuba yake nzuri, ya wazi na inayolenga kuondoa umaskini katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na uongozi mzima wa Wizara hii. Pongezi za hakika zimwendee Katibu Mkuu, kwa ushauri wake mzuri kwa wasimamizi wa Sera ya CCM ambao ni Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na usimamizi imara wa utendaji Wizarani. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imeonyesha umahiri wake katika kusimamia na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi hadi Vijijini. Naomba iandae mikakati kwa ushauri, ninaoutoa hapa chini:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu afya (Ibara ya 64 - 68). Hakuna ubishi kwa Wizara kuwa imefanya Mapinduzi makubwa kuimarisha afya za Wananchi. Kitu kimoja muhimu sana ambacho kimesahaulika au kimebaki ni usafiri kwa Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya. Watu wako Vijijini mbali na Miji na sehemu nyingi ni pembezoni mwa nchi kusiko na miundombinu ya uchukuzi na mawasiliano. Haya bado ni maeneo yenye umaskini uliokithiri kutokana na mazingira na ukosefu wa elimu, masoko na msuguano na wageni kwa utamaduni wa *evolution* na *revolution*.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngara inaomba magari matatu kwa Vituo vya Afya vya Mabawe (km. 20), Bukiziro (km. 80 hivi) na Murusagamba (km. 130 - 140) ambavyo kwa miaka zaidi ya 25 havina usafiri vinanyanyaswa na wakimbizi, wizi, mauaji na kadhalika kwa maana ya raia wa Ngara waishio sehemu hiyo kutoka Hospital ya Wilaya. Umaskini hautaondoka bila Wananchi kufanya kazi kwa muda mrefu mashambani kila siku kwa sababu ni wagonjwa, ni dhaifu na wanyonge. Naomba Serikali ifahamu kuwa uchumi hujengwa na watu wenye nguvu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utawala Bora (Ibara 14 - 18), namuomba Waziri mwenye dhamana hiyo ashirikiane na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kuhusu kupatikana Mahakimu, hususan wa Mahakama za Mwanzo. Wilaya ya Ngara ina Vituo 13, lakini ina Mahakimu watatu tu wanaofanya kazi katika Kata 17 zenye Vijiji 73! Ngara ni Wilaya ya wakimbizi tangu 1948, hivi sasa makimbizi yamejaa wakimbizi, nafasi haitoshi. Mahakimu hao wachache hawana usafiri ikiwa ni pamoja na Hakimu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii mama itoe Mahakimu na usafiri wa kutosha kwa Wilaya ya Ngara, bila hivyo rushwa haitakwisha na haki haitatolewa. Wakati wa Bunge la Bajeti 2002/2003 nililalamika kwamba, kesi nyingi Vijijini hughughulikiwa na Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji ambao ni dhahiri kuwa wanapotosha dhana ya Utawala Bora. Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba ametembelea Ngara hivi karibuni alishuhudia hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu (Ibara ya 61 - 63), nchi nzima inaishukuru Serikali ya CCM kwa kuboresha elimu. Napenda kusema kwamba MMEM italeta maana pale tu mambo mawili muhimu yatakaposhughulikiwa kikamilifu. Kwanza, ni Ujenzi wa Nyumba za Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari huko Vijijini ambako hakuna nyumba za kupanga kama ilivyo Mijini. Hii ni kero kubwa mno na ndiyo sababu ya elimu ya msingi kudidimia. Walimu wamekuwa kama wawindaji kwa kutembea masafa marefu kwenda na kutoka kazini na pengine wasiende kabisa wakati wa majira ya mvua na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa *(LAPF)* (Ibara ya 36 - 42), Kitengo hiki kina menejimenti adilifu kweli kweli. Matatizo yanatatuliwa kwa uwazi na Halmashauri inawasilisha makato ya wadau ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa CCM ipo kumsaidia mwananchi pale uwezo ulipoishia, nashauri Mikoa ifungue ofisi imara na kumbukumbu za Watumishi ziwekwe huko ili wadau wapate mafao yao kwa urahisi kutokana na ukaribu wa huduma. Hii ni hali itakayoongeza kutambulika Sera ya CCM ya kupeleka madaraka kwa Wananchi na kufikisha huduma kwao kwa haraka na kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mafunzo kwa Uongozi na Watumishi (Ibara ya 10), naomba kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri ya kuwapa Viongozi na Watumishi mafunzo kwa miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa tahadhari kwamba, wakati sasa umefika Serikali itambue kuwa zipo kada nyingi katika Wizara hii na zile muhimu zilizo karibu sana na umma wa Watanzania zilizo na maarifa au hata elimu ya kadri. Viongozi na Watumishi hawa muhimu ni Madiwani, Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji na hata baadhi ya Makatibu Tarafa.

Mheshimiwa Spika, Viongozi na Watumishi hawa ndiyo hasa Wanasiasa, Watawala, Wakaguzi wa Shughuli na Miradi ya Maendeleo, wanaendesha vikao na Mikutano Vijijini, wanasuluhisha/patanisha migogoro ya kawaida Vijijini, hasa ya kuandaa na kupokea wageni/Viongozi toka ngazi zote za juu.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ishauriane na Wizara ya Fedha kupata fungu la kutosha kuendesha mafunzo ya kutosha, siyo semina, ili watu hawa waweze kumudu madaraka yao vizuri zaidi kwa faida yao na Taifa pia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliojumuika nasi hivi karibuni. Pili, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu Waziri na *team* yao yote kwa matayarisho mazuri ya Bajeti iliyoambatana na vielelezo vingi, lakini muhimu na fasaha sana kwa Bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa Wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nianze kwa kuipongeza Wizara kwa namna ambavyo wamezingatia elimu na mafunzo kwa Watumishi wake wa ngazi mbalimbali. Katika ulimwengu huu wa soko huru ambalo linabadilika kwa haraka haraka kutokana na utandawazi unaofanya dunia kuwa Kijiji kutokana na teknolojia ya mawasiliano na habari, Tanzania hatuna budi kujifunza kwa haraka namna ya kufanya shughuli zetu kwa ufanisi. Ufanisi huo hautakuja bila ya mafunzo na elimu ambayo inatoa ari, uelewa na ujuzi wa kutawala mazingira na kwa namna hiyo kutoa huduma inayostahili kwa umma.

Mheshimiwa Spika, binafsi nimefurahi sana kusikia na kusoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri waliochukua mafunzo wakirudi watapimwa kutokana na tija na ufanisi wao wa kazi. Endapo itabainika kuwa kuna ambao tija yao ni ya chini basi waondolewe na wale wenye uwezo wathibitishwe. Huu ni utaratibu mzuri, *"Gone are the days where nepotism, favouritism etc, used to be a criteria for performance."* Kila mtu avune anachopanda na kila mtu abebe msalaba wake. Tumefika mahali kila mtu awajibike na ale jasho lake. Kwa namna hii, nchi itazidi kupata ufanisi na hivyo kukuza tija na uchumi kwa jumla. Utaratibu huu ukiendelea Wakurugenzi na Ukurugenzi utakuwa ni *performance oriented* na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuonyesha appreciation yangu kuhusu kuundwa kwa cheo cha Afisa Mtendaji wa Mtaa na ambaye atalipwa. Hii ni hamasa na changamoto nzuri katika ngazi hii ya mwisho ambayo ndiyo inayoishi na umma wa watu wetu. Mtu huyu ndiye muhimu sana, maana akielimika yeye kwa jambo lolote la maendeleo basi na mtaa wake utakuwa umeelimika. Wakielimika Maafisa Mtaa wote wa Kijiji, Kata na kadhalika, basi maendeleo yataenea haraka.

Mheshimiwa Spika, ninathubutu sasa, baada ya hotuba ya Waziri wa Fedha, Waziri Mkuu na sasa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kusema kuwa Tanzania tunakwenda.

Mheshimiwa Spika, ninatoa shukrani kwa fursa hii na ninaunga hoja mkono.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Wataalamu wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa kutegemewa na kila Mtanzania. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbinga ina Kata 37, Vijiji 179 na Vitongoji 1,127 na ni Wilaya ya milima milima. Ili mpango wa kuboresha kilimo na mifugo uweze kufanikiwa vizuri, Serikali inatakiwa kuongeza idadi ya Wataalam wa Kilimo na Mifugo, kwa sasa wapo 85 na pungufu ni 166. Tunaomba sana Serikali iongeze hawa Wataalam.

Mheshimiwa Spika, pili, ni juu ya upungufu wa vitanda vya kujifungulia na mipira ya kuvaa mikononi na kama zahanati ina kitanda, basi kipo katika hali mbaya sana na hakifai kabisa kutumika!

Zahanati zenye matatizo haya ni Kwambe, Chiudu, Lundo, Mkili, Mbaha, Ngingama na Litumbakuhamba. Kwa hiyo, nashauri sana Serikali inunue vifaa hivyo kwa ajili ya zahanati hizo.

Naipongeza sana Serikali kwa kufuta kodi ya maendeleo, hatua hii imepunguza kero moja kubwa sana iliyokuwa inawasumbua Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna kero nyingine ya ushuru wa mitumbwi, sea boats na ushuru wa kuchuuza samaki. Kodi za namna hii pia zingefutwa kwani hazileti mapato yanayoeleweka, zaidi huleta usumbufu tu kwa Wananchi wenye mitumbwi na kwa wachuuzi. Maafisa wa samaki waliopo badala ya kuwasaidia wavuvi ushauri wa kitaalam wa kuvua ili waongeze uzalishaji, mara zote wao hukimbizana tu na wavuvi na wachuuzi kwa ajili ya kukusanya ushuru. Ushuru wa namna hii hauongezi tija bali kero kwa Wananchi, nashauri ufutwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Matuta - Mango na barabara ya Mikavanga - Lundo, Wananchi wamejitahidi sana kutengeneza wenyewe, lakini sasa wamekwama wanahitaji msaada wa kitaalam na fedha ili barabara hizi ziweze kukamilika. Naiomba sana Serikali iwaunge mkono hawa Wananchi ili nguvu zao zisipotee bure.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba pia barabara ya Mbinga - Ngumbo itengenezwe hadi mwisho, yaani Ngumbo. Mara nyingi barabara hii hutengenezwa mwisho Litoho na hakuna hata mara moja imetengenezwa hadi mwisho, yaani hadi Ngumbo.

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo naomba sana Mheshimiwa Waziri akayafanyie kazi kwa faida ya Wananchi. Ahsante sana naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pili, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kazi kubwa kabisa wanayoifanya katika kuhakikisha kuwa nchi hii, inapata maendeleo makubwa na kuhakikisha kuwa yale yaliyolengwa na Serikali katika kuyapeleka katika Halmashauri kwa masuala ya kuboresha jamii na maendeleo yake yanafika na yanasimamiwa na kufanikisha. Naomba pia kuchukua fursa hii kuwatakia kila la kheri na mafanikio mema katika shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo naomba sana Mheshimiwa Waziri akayafanyie kazi kwa faida ya Wananchi. Ahsante sana naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, lingine naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge, wengine waliochangia kwa kusema kuwa watumishi waliokaa katika Halmashauri kwa zaidi ya miaka 8 au zaidi kwa kipindi kirefu sana basi ni bora wapate uhamisho kwa sababu hata akili zao zinakuwa zinadumaa hazitoi michango mizuri kwa ajili ya kuboresha Halmashauri au wanakuwa wanajiona kama ndiyo pekee wanaoweza kuleta maendeleo katika Halmashauri hizo na wanakuwa chanzo cha migogoro katika maeneo hayo kwa sababu huwa wanakuwa wanaegemea upande mmoja wa kundi ambalo huwa mara nyingi huwapiga vita viongozi waliokuwa madarakani.

Lakini kwa Mafia naomba niwapongeze kwanza Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wangu wa Mkoa Bwana Ditopile Ukiwaona Mzuzuri, Mkuu wangu wa Wilaya ndugu ali Mohamed Libaba, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mafia ndugu Amiri Swaleh Gwakirayi kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kuleta maendeleo katika kisiwa cha Mafia, japokuwa vita ni vikali wanavyopigwa. Lakini maendeleo sasa yanaonekana wazi, Wilaya inakua kimaendelea hasa ya elimu, afya, maji nakadhalika. Na mi katika kuwapa moyo wananchi wa Wilaya yangu nimeanzisha mradi wa kuhakikisha kuwa vijana wote waliomaliza kidato cha nne hawazururi ovyo na nimeamua kuwapeleka katika vyuo maalum ili Mungu akipenda wajisaidie wenyewe. Mwaka 2003 nimepeleka vijana 31 amb ao wanasoma katika Chuo cha Ualimu Vikindu na nategemea mwezi septemba mwaka 2003 kupeleka vijana 10 katika Chuo cha Unesi (ukungu) Newala na pia mwaka 2004 Januari watakwenda vijana 50 katika Shuo cha Ualimu Vikindu na vijana hao wote ofisi yangu ya Mbunge Jimbo la Mafia ndiyo nawagharamia. Hiyo yote ni katika kuhakikisha tunatokomeza kabisa suala la kuondoa umaskini, maradhi, ujinga na hata kukisaidia chama changu kilichonipatia nafasi

hii ili nikijengee Imani kwa wananchi kuwa viongozi wao si viongozi wa kulala na kuongea tu bali ni viongozi waochapa kazi haswa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwapongeze Waheshimiwa Madiwani wangu kwa kusimamia vizuri shughuli zote za maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia. Mwisho ninaomba tupatiwe haraka *D.T.* katika Halmashauri yetu au basi apandishwe daraja (cheo) yule kijana anayekaimu nafasi hiyo anaitwa Kessy Mpakata. Ni kijana mzuri mpole mwadilifu, lakini inatakiwa atiwe moyo tu na naamini atakuwa kijana mzuri. Baada ya kusema hayo machache naomba tena kurudia kwa kukupongezeni tena viongozi wote wa Wizara hii TAMISEMI na kuunga mkono hoja hiyo.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Brig. Gen. Mstaafu Hassan Ngwilizi Mbunge, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda Mbunge, Katibu Mkuu na watumishi wengine Wizarani humo kwa kazi nzuri hasa kwa kutuletea hotuba muafaka ya bajeti ya Wizara. Naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Kituo cha Afya Mlalo. Pamoja na jitihada za ukarabati wa vituo vya afya nchini kikiwemo cha Mlalo bado kituo hicho kina shida kubwa ya ukosefu wa usafiri. Kutoka Mlalo hadi Lushoto ni zaidi ya km 40 hivyo rufaa ya mgonjwa kwenda katika Hospitali ya Wilaya ni matatizo makubwa bila usafiri wa kuaminika. Tunaomba Kituo cha Afya Mlalo kipewe gari.

Pili, vile vile kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mlalo naishukuru sana Wizara kwa ukarabati wa Kituo cha Afya Mnazi pamoja na kupatiwa gari la wagonjwa. Hata hivyo kituo hicho kiko mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya. Kutoka Mlalo hadi Mnazi ni kama km 100 hivi, hakuna umeme hakuna simu. Kwa sababu hiyo naomba kituo hicho kipatiwe *Radio Call* pamoja na *generator* ya umeme.

Tatu, kuhusu ajira ya *Revenue Collectors.* Kufuatana na maagizo ya Wizara ziko baadhi ya Wilaya au Halmashauri ambazo tayari zimekwisha kuajiri *Revenue Collectors* na wako kazini hivi sasa ikiwemo Wilaya ya Lushoto. Swali ni kwamba kwa kuwa sasa Serikali imekwishaondoa kodi ya maendeleo na kodi nyingine zenye kero kwa wananchi hawa vijana sasa watafanya kazi gani?

Nne, maombi ya Wilaya mpya Mlalo. Suala hili kama yalivyo mengine ni la muda mrefu sana. Nimetumwa na wananchi wa Jimbo la Mlalo kuendelea kuomba Wilaya mpya ya Mlalo kwa maana ya kuigawa Wilaya ya sasa ya Lushoto. Jambo hili lilijadiliwa sana nyakati za *RDC* na mapendekezo ya wakati huo ni kwamba Mkoa wa Tanga waliweka kipaumbele cha kwanza Handeni na Kilindi. Hii limetekelezwa tunashukuru sana. Kipaumbele cha pili kilikuwa Lushoto na Mlalo kwa maana ya kuigawa Wilaya ya Lushoto. Maana yake ni kwamba vigezo vyote vya kitalaam vilizingatiwa mapendekezo yote hayo yalipelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo kwa sasa ni Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Tano, Madiwani kuhusu posho ni kweli haitaeleweka kama Mtendaji Kata, Mtendaji Kijiji na Mkusanyaji mapato wanalipwa lakini kiongozi wao Mkuu wa Kata hana kitu. Naomba wafikiriwe nao vile vile.

Sita, vilevile nimetumwa kuishukuru sana Wizara kwa msaada wa matengenezo ya barabara ya Mtae - Langoni (MNAZI) na mlalo - Mng’aro ahsante sana. Hata hivyo tuna tatizo kubwa na daraja la Kwemaramba ambalo lilichukuliwa na mafuriko miaka ya nyuma. Daraja hilo ni muhimu sana kwa vile kuondoka kwake kumetenganishwa shule ya Sekondari Kwemaramba na pia Shule ya Msingi Kwemaramba. Eneo hilo liko katika kijiji cha Handeni, Kata ya Mwangoi na Tarafa ya Mlalo.

Suala la Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, hivi kiungo chake ni nini na ni wapi kule chini? Kama Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Makatibu Tarafa hawaonekani popote kushiriki kwenye masuala ya Serikali za Mitaa kisheria mnataka wananchi wakubali kwamba tunazo Serikali mbili zinazofanya kazi sambamba?

Kwa maoni yangu naamini Tanzania ni moja na kuwepo kwa Serikali Kuu na pia Serikali za Mitaa ni utaratibu tu. Muafaka wa kurahisisha utawala wa nchi pamoja na kupeleka madaraka karibu na wananchi. Ili ukweli huu udhihirike ni lazima ionekane dhahiri kuwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa

kweli ni Serikali moja. Ili hili lionekane hivyo ni lazima viongozi hao niliowataja hapo juu waonekane kuwa na madaraka kisheria kushiriki katika shughuli za Halmashauri za Wilaya, miji, Manispaa za Majiji. Hali ilivyo hivi sasa haionekani hivyo, Serikali Kuu za Serikali za Mitaa zinaonekana kama Serikali mbili zinazofanya kazi sambamba.

Mheshimiwa Spika naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. AISHA OMAR KIGODA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mikoa, (TAMISEMI) Mheshimiwa Brigadia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri. Nawapongeza pia wale watendaji wote walio chini ya Ofisi yake. Pongezi nyingi sana. Naomba pia niunge mkono hoja hii kwa asilimia asilimia mia moja. Baada ya hapo nichangie kama ifuatavyo:-

Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri kwa nia ya kuhakikisha mwananchi anapata huduma nzuri katika Halmashauri na Mikoa kwa ujumla. Tatizo kubwa ni jinsi watumishi wa idara mbalimbali hasa vijijini wanavyopata adha kiasi ambacho kinaathiri utendaji wao.

Watumishi wa Wizara ya Elimu, Walimu na Afya (waganga/wauguzi wanapata shida sana hasa inapofikia suala la kupata mishahara yao. Wanachukua siku nyingi wakiwa wanagaragara katika Ofisi ya Halmashauri kusubiri mishahara inayochelewa na wakati huo huo kuacha wazi vituo vya kazi. Tunaomba suala hili lifanyiwe utafiti ili kutafuta njia ya kulitatua kabisa tatizo hilo.

Naipongeza Serikali kuhusu mfuko wa barabara. Kwa kweli kazi nzuri tunaiona. Mheshimiwa Waziri, tatizo la barabara Mkoa wa Tanga hususan ya kwenda Handeni - Kilindi kupitia Korogwe na Mkata. Barabara hii umuhimu wake ni mkubwa kwani Handeni/Kilindi ni kati ya Wilaya zinazotoa mazao mengi kama mahindi kwenda mikoa na Wilaya mbalimbali. Tunakuomba sana ulipe uzito suala hili kwa uwezo wako Mheshimiwa Waziri barabara iwe na kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu posho za madiwani ni lazima kulipa mtizamo mpya ili kuweza kuwapatia malipo kama wenzao watendaji na Wabunge. Ingawa sifa za kuwa Diwani ni kwamba uwe na kipato na asiwe muajiriwa lakini tukubali mchango wao kisiasa na Serikali. Ikibidi kama sheria haikubali tuirekebishe ili uwepo utaratibu wa kuwapatia walao posho inayoeleweka na Serikali ichangie.

Mheshimiwa Spika, mengine yamechangia na wenzangu hakuna haja ya kurudia lakini huduma za jamii kama afya, elimu, barabara bila kuzifuatilia, umaskini utaendelea.

Narudia kuwapongeza na nawatakia kila la kheri ili muweze kuboresha Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono tena hoja. Ahsante.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Brigadia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hotuba yake nzuri, inayoeleweka na yenye takwimu muhimu.

Aidha napenda pia kumpongeza Naibu Waziri wa Wizara hiyo Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Mbunge, Katibu Mkuu, bwana D. Mmari na wasaidizi wao kwa kazi nzuri wanayofanya ya kumsaidia Waziri kuongoza Wizara hiyo vizuri sana na kuandaa hotuba nzuri sana. Naunga mkono hoja hii kwa dhati. Hata hivyo naomba kutoa mchango wangu mdogo kuhusu Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo. Chuo hiki ni muhimu sana kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uongozi na utendaji katika Serikali za Mitaa.

Pamoja na maelezo hayo hapo juu *impact* yake tangu chuo kianzishwe mwaka 1994 wakati huu nikiwa kama KM (WN) mpaka sasa haijaonekana. Ushauri wangu ni kwamba Serikali wakati huu ambapo Chuo cha Mzumbe sasa kinatoa *Academic Studies* zaidi kuliko *Professional Studies and Training in Local Government*. Chuo kipatiwe nyenzo muhimu za mafunzo ikiwa ni pamoja na walimu na kadhalika.

Serikali iaanzishe ajira ya mkataba wa muda mfupi miezi sita, mwaka mmoja, miaka miwili na kadhalika. Ili itumie *Retired Local government and Rural Development Experts. Some of these Experts are retired but not tired.* Vile vile Chuo kiwe na mpango wa *Extension Training Services* ili mafunzo kama ya watendaji wa kata yafanyike huko huko Mkoani, badala ya kuwaleta Hombolo hasa kwa ajili ya *short courses* za miezi miwili, mitatu, na kadhalika. Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kama Mabugali Lushoto vitumike kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Uchumi Mbelei - Baga - Mgwashi - Mayo - Bumbuli km 50. Nilileta ombi kwa Waziri ili ipewe allocation maalum na *survey report.* Napenda kupata maelezo. Barabara hii ni ya uchumi wa mazao ya chai, kahawa, mboga, maharage, viazi.

**MHE. TALALA BANA MBISE:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimwia Brigadia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi na *team* yake kwa hotuba yake nzuri. Ninaunga mkono hoja hii. Napenda kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa fedha. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri anakiri kuwepo na usimamizi wa fedha usioridhisha kwenye Halmashauri zetu. Hotuba inasema hatua zinachuliwa/zitachukuliwa kuboresha hiyo hali. Nashauri kama ifuatavyo; mpango/utaratibu wa sasa wa kila idara kuwa na account yake inayosimamiwa na Mkuu wa Idara peke yake na fedha kutumwa moja kwa moja kwenye hizo accounts za idara una kasoro nyingi zinazosababisha usimamizi kuwa mgumu, hasa kwenye Halmashauri ambazo wakurugenzi siyo makini sana. Idara ambazo ni notorious ni pamoja na elimu, ujenzi, afya. Kungojea *Audit Reports* kutambua matatizo ya utunzaji wa fedha baada ya zaidi ya mwaka haisaidii sana. *System* ya *internal audit performance ni poor and ineffective.* Je, Serikali (TAMISEMI) inaweza kuwa na mpango/utaratibu wa kufanya *external review* ya *finacial accounts* za Halmashauri kila baada ya miezi sita? Utaratibu huu unaweza kutumia huduma za *private financial cum audit services* kwa utaratibu wa mkataba. Hii huduma itagharimu fedha kidogo. Lakini inaweza kuokoa fedha nyingi ambazo zingepotea kwa njia nyingi. Mkataba ungekuwa kati ya TAMISEMI na watoa huduma.

Mheshimiwa Spika, vile imezungumzwa Hazina ya Ardhi kwenye hotuba ya budget. TAMISEMI inahusikaje kwenye hili suala? Halmashauri je? Dhana ya Hazina ya Ardhi ni nzuri. Lakini bado haijaeleweka hata kidogo. TAMISEMI ina mkakati gani wa kueneza elimu juu ya suala hili? Kwa vile hazina ya ardhi inalenga kuanzishwa kwa maeneo ya uwekezaji. Je, itakuwaje kwenye maeneo yenye msongamano mkubwa wa watu kama vile Arumeni? Tunaomba Serikali kupitia TAMISEMI ifikirie kutwaa maeneo yaliyo kwenye *lease* Arumeru (hasa Arumeru Mashariki) ili yawe kwenye Hazina ya Ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hii pekee ndiyo itakayohakikisha wakazi wa Arumeru ambao hawataki kuhama, uhakika wa kupata fursa ya ajira kwenye maeneo watakaowekeza hazina ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa kuondoa kodi ya maendeleo, kodi ya mifugo kama Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alivyotamka kwenye hotuba yake. Kero ambayo bado ni *outstanding* ni namna ya kufidia Halmashauri. Tunaomba tamko litoke la ni jinsi gani Halmashauri zitafidiwa *formula* ipi itatumika, *short run, long term*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. JAMES A MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalamu wote katika Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya. Ninaunga mkono hoja ya Wizara. Hata hivyo naomba kuchangia hoja ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza ninashauri pale ambapo fedha itapelekwa kwa matumizi mengineyo huko Wilayani, basi Waheshimiwa Wabunge wapewe nakala ya barua juu ya tendo hilo ambapo barua pia itaonyesha kiwango cha fedha zinazopelekwa kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Mbunge. Uwazi katika hili utaondoa mgongano usio wa lazima baina ya Mbunge wa *DAS* na pia utadumisha uongozi bora na ushirikiano wa dhati.

Pili, napenda kufahamishwa kwa maandishi, maendeleo ya uandikishaji wa vijiji vipya viwili Kijiji cha Chali na Kijiji cha Imala Mihayo, vilivyoko katika Kata ya Ndono Wilayani Uyui. Maombi hayo ya kuandikisha vijiji hivi yamekuwa ya muda mrefu sasa yapata miaka 2 bila mafanikio wala hata taarifa ya maendeleo ya uandikishaji wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, tatu napenda kufahamu bayana fungu (kiwango) lililotengwa katika mwaka huu wa fedha kwa ajili wa ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Wilaya ya Uyui. Vile vile napenda nifahamishwe ni majengo yapi au ofisi zipi ambazo zitajengwa na Serikali Kuu kupitia bajeti au mpango mwingine wowote ule katika ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui. Je, inawezekana kukawa na mpango/*program* kwa ujenzi huo? Ninaweza kupewa nakala ya mpango huo? Suala la malipo zaidi au mishahara kwa madiwani haliwezi kuendeleza kuachwa bila kushughulikiwa ipasavyo, hasa kwa kuzingatia umuhimu wao Madiwani na mizigo mikubwa wanaobebeshwa na wananchi huko katika Kata zetu. Ukweli kwamba posho zao ni kidogo kiasi cha kuwawezesha kutekeleza majukumu yao mengine yoyote yale yatakayokuwa ni za nyongezi tu katika kujenga hoja ya kuongeza posho au hata kuwalipa mishahara kabisa. Shilingi 100,000/= kwa mwezi itasaidia sana.

Tano, katika kuendeleza makazi na kusisitiza matumizi mazuri ya ardhi yetu kwa makazi ninashauri kuwe na mipango mahsusi iliyoandaliwa na wataalamu wa mipango miji, wakishirikiana na wataalam wengine. Mipango hii *(Master Plans)* iwepo na ihamike na ifuatwe na wasimazi wote, kuanzia *VEO* hadi wale wa ngazi ya Wilaya na hata Mkoa. Vile naipa changamoto Wizara yako katika kuhakikisha kuwa makazi yanapangwa na msisitizo unatolewa katika kutumia *materials* bora na rahisi kwa ajili ya kujenga makazi bora na ya kupendeza. Hii pia itapendezesha vitongoji, vijiji, miji midogo Manispaa na hata Majiji yetu. Naisisitiza miji ipangwe kwa kutumia watalaam sahihi.

Kuhusu ujenzi katika miji yetu, wakati sasa umewadia wa kutambua kwamba haikubaliki tena kujenga vijengo vidogo vidogo mijini. Kufanya hivyo kunasababisha miji yetu kupanuka kwa kasi kubwa na mara nyingi, bila mipangilio mizuri. Makosa haya hufanya gharama za kuishi mijini ziongezeke na pia huongeza shida/gharama za upelekaji wa huduma utilities kwa wakazi wa miji hiyo. Usambazaji wa kiholela wa miji yetu pia inatusababishia matatizo makubwa ya uendelezaji wa barabara yetu na hata kupelekea kero ya kulazimika kuvunja majengo ya wakazi kitu ambacho tunaweza kukiepuka. Ukimwi bado haujapatiwa nyenzo kama inavyostahili cha ajabu zaidi ni kule kutokuwepo kwa *urgency* katika kupeleka nyenzo za mapambano dhidi ya ukimwi. Kwa kweli hakuna juhudi za kutosha katika Serikali Kuu zinazoelekezwa katika kupambana na ukimwi ambao umetangazwa na Mheshimiwa Rais kuwa ni janga la kitaifa. Inaonekana hata ndani ya Serikali yenyewe kwamba kila mmoja wetu, kila idara, kila wizara wanadhani kuna mtu/wizara/idara fulani ambayo ndiyo inatakiwa kuendesha vita hivi dhidi ya ukimwi huku wengine waliobakia kama washangiliaji tu.

Kama hivyo ndivyo kwa kweli taifa hili linatishiwa kuangamia na kufutika. *TACAIDS* imekuwa kama ndiyo watendaji pekee badala ya kuwa waratibu kama ilivyotarajiwa. Wilaya zetu zinachukulia Ukimwi kama ni suala la warsha na mikutano ya wateule wachache tu. Kwa kweli *we yet have to face the HIV/AIDS pandemic more deservedly. We need more and extended involvement of every body. The best body to coordinate this is of course TACAIDS down through our Council structures, for they are the only Organized bodies that can well compliment the role of TACAIDS and at the same time, spear head the fight against HIV/AIDS in the District Councils. While our Councils need to be assited in preparing some write ups that will enable them se cure some funds from TACAIDS and other relevant donors, schools, church/mosque congregassions, cultural troups and other groupings need to be treated and indeed encouraged to actively play their party in the fight against this pandemic.*

Mheshimiwa Spika, napendekeza Jimbo la Tabora Kaskazini ligawanywe na kuzaa Majimbo ya uchaguzi ya Kolangulu na Uyui kwa kufuata mipaka ya Tarafa za Ilolangulu na Uyui zilizopo hivi sasa. Sensa ya 2002 imezalisha vigezo vya kupeleka ombi hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi na Wataalamu wao wote kwa kukaa na kuandaa bajeti ambayo ni nzuri na yenye kufahamika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuhusu suala Ofisi za wabunge na kuanisha kiasi cha fedha ambacho Waheshimiwa hao wanapata. Lakini kwa upande wetu Wabunge wa Zanzibar ukweli tuko katika masikitiko makubwa sana kwa kuwabagua Wabunge wa Zanzibar ambao pia tukiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tupo tu bila ya kufikiriwa kuwa kwa kupatiwa Ofisi kwa ajili ya kufanyia shughuli zetu za kazi na tunapolieleza suala hili hujibiwi liko Zanzibar kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Kiongozi ambako hakuonyeshi hata dalili za kuweza kupatiwa Ofisi hizo kwani wengi katika Ofisi hii ni mambo ya shughuli za SMZ kwa hiyo hatujui tushike wapi kwani tumekaa kama Popo si ndege wala si mnyama kwani anaruka kama ni ndege lakini wakati huo huo anazaa kama mnyama.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la msingi sana kuwapa heshima na vitendea kazi watendaji wetu katika ngazi mbalimbali hasa kwa madiwani wetu kwenye majimbo. Waheshimiwa Madiwani ni watu muhimu na Watendaji Wakuu wa Waheshimiwa Wabunge, katika kazi za kila siku ndani ya Majimbo yetu kwa hiyo tunaomba wapatiwe angalau pikipiki ili waweze kufanikisha kazi zao na kuwapatia posho ili waweze kupata utulivu na kuweza kupata nafasi nzuri ya kufanya shughuli zao bila kuwa na mashaka yoyote.

Mheshimiwa Spika, suala la kupata wataalam ni zuri lakini tuangalie kwanza wataalamu wetu walio ndani ili wapewe elimu zaidi nao waweze kulingana na hao wa nje au hata kuwakaribia katika utendaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nawapongezi Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji katika (TAMISEMI) kwa maandalizi ya hotuba hii nzuri yenye kuonyesha mwelekeo thabiti katika kusogeza maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia usimamizi wa maendeleo katika maeneo yetu kazi ya msingi *(grass root level)* hufanywa na watendaji Ofisa watendaji vijijini na katani. Napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi huu wa busara wa kuwalipa mishahara kwa ajira ya mkakati watendaji hawa. Kazi zao ni nyeti na muhimu kwa maana ya kwamba katika dhana ya ushirikishaji tunayoenda nayo katika uendeshaji wa nchi hii, mipango yote inatakiwa ianzie vijijini kwa wananchi wenyewe na waratibu wakuu huko ni watendaji hawa. Uamuzi wa kuwaajiri ni wa busara sana.

Mheshimiwa Spika, lakini tuna matatizo makubwa katika ngazi ya kata ambako kamati ya maendeleo mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Diwani. Madiwani ndiyo wanaotarajiwa kupitia kwenye baraza na kamati za kudumu za Halmashauri kusimamia utendaji na utekelezaji wa ilani yetu ya uchaguzi 2000 katika ngazi ya Halmashauri. Kwa kiwango inashindikana kwao kuepuka vishawishi vya kurubuniwa na watendaji ili kufumbia macho maovu mengi yanayoambatana na ubadhirifu na wizi miongoni mwa watendaji. Tunajua kwamba hali halisi kutegemea Serikali ilimalize tatizo hili linalohusisha uadilifu wa watu wetu wenyewe ila ni kweli kabisa kwamba kiwango cha posho wapatayo Waheshimiwa Wabunge kwa sasa hivi ni kidogo sana, hata kama tunakubaliana kwamba kinachotolewa ni posho tu na hutegemea pia uwezo wa Halmashauri yenyewe.

Ningeshauri utolewe mwongozo wa Kiserikali kuanisha viwango vinavyofanana kwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji ukiwemo pia uwezekano wa Serikali kutoa nyongeza top up itakayohitajika kuziba mapengo ya uwezo kifedha wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, la pili linahusu kanuni inayozuia waajiriwa kugombea udiwani kwenye maeneo yao. Kanuni hii kwa kiwango kikubwa inawabana wananchi wenye uwezo na elewa wa kutosha kuingia katika uongozi ngazi ya udiwani na hivyo kukosa kutoa mchango unaohitajika katika kusukuma

maendeleo vijijini. Tatizo la kudanganyika kwa urahisi linatoka na pia na ukweli kwamba kwa kuzingatia kanuni hii fursa ya kugombea udiwani huwaendea watu wenye kiwango cha chini mno kielimu na kitaaluma kuweza kukabiliana na wataalamu wanaoletwa Wilayani na Serikali Kuu. Hali hii inajitokeza mahali pengi kwenye Halmashauri zetu na ndiyo msingi wa hoja hii. Katika hali hii wizi na ubadhirifu haviepukiki, japo rekodi sasa inaonyesha Halmashauri zinazopata hati safi za ukaguzi zimeongezeka sana. Lakini sharti ukumbukwe kwamba hati safi pekee yake siyo kigezo thabiti cha ubora wa kazi inayotendwa na maofisa husika kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kimsingi mawasiliano ya Bajeti ya Wizara hii ni ya kupongezwa na kuungwa mkono ili kupitia kwenye utekelezaji wa yote haya Halmashauri, Wilaya na taifa letu lisonge mbele.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. DAMAS PASCAL NAKEI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Wizara hii ni Wizara inayogusa jamii yetu katika nyanja zote na kwa ukaribu sana. Kama tunazungumzia kuondoa umaskini nchi hii, basi Wizara hii ndiyo mhusika mkuu.

Mheshimiwa Spika, utawala bora ni msingi mojawapo katika kuleta maendeleo. Naomba Serikali ihakikisha kuwa katika Wilaya kunakuwa na uongozi wa pamoja, uongozi unaoheshimiana na unaojali. Hali ilivyo hivi sasa ni kwamba katika Wilaya uongozi hauendi pamoja. Nashukuru kwamba katika Wilaya yangu ya Babati tumeanza kujenga uongozi mzuri ingawa bado kuna matatizo. Tulikwama kumpata Mwenyekiti wetu wa Halmashauri kwa zaidi ya miezi 6 kwa sababu tu ya kukataa au kusita kutambua maamuzi ya walio wengi. Wale walioelezea hali halisi na kuunga mkono mabadiliko kuelekea kuzuri tulionekana kana kwamba tuna maslahi binafsi. Naomba maslahi ya umma yawekwe mbele kuliko jambo lingine lolote, tusiruhusu tabia ya kulindana kwa gharama ya wananchi wetu walio wengi kama ilivyotaka kujionyesha wilayani kwetu Babati.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na utawala bora Mheshimiwa Spika, ajira ya watendaji wa vijiji na wa kata zizingatie au ziwe na ushindani, uwazi, sifa na uwezo. Watendaji wa vijijini wasilazimike kufanya kazi katika vijiji walikozaliwa wawe huru kuhamishwa. Hatuwezi kuzungumzia Halmashauri za Wilaya katika ujumla wake bila Waheshimiwa Madiwani. Waheshimiwa Madiwani ndiyo walioshika usukani wa maendeleo katika kata na Wilayani. Mimi ninaishauri Serikali iboreshe hali ya madiwani na kuwawezesha kufanya kazi yao ya udiwani vizuri. Hali ya Madiwani kwa sasa ni duni na inaathiri ufuatiliaji wao katika kazi. Walipwe mishahara kwa namna inayofaa.

Mheshimiwa Spika, upande wa afya wananchi wanapata shida kufuatilia huduma za matibabu kusafiri masafa marefu. Kuna upungufu wa zahanati, upungufu wa watumishi pia. Hali ilivyo sasa ni kwamba zahanati moja inahudumie watu 10,000. Mimi ninashauri Serikali isije - limit hapo badala yake Serikali iangalie/izingatie hali ya kujiografia kwani wagonwa wanakuwa mbali mno na zahanati. Kwa sababu hiyo naomba sana Serikali ikubali kusajili zahanati za Merr, Dohom, Duru, Ufani na Mandi zilizoko katika Wilaya yangu hususan jimbo langu la Babati Magharibi kwa mfano Zahanati ya Merr iko zaidi ya km 12 kutoka Madunga ambako kuna dispensary.

Mheshimiwa Spika, upande wa elimu ya msingi inaenda vizuri mpaka sasa. Lakini elimu ya msingi katika dunia ya leo haitoshi kwa mtu kujitegemea. Zipo jitihada za kufungua sekondari za kutwa kwa kila kata. Lakini wananchi wanaelemewa na mzigo huu wa ujenzi naomba kuishauri Serikali itoe majukumu kwa Halmashauri ili zisimamie zifuatilie ujenzi wa shule za sekondari. Halmashauri zihusike katika kusaidia ujenzi wa madarasa, maabara nakadhalika katika shule za sekondari za kutwa. Labda nifahamishwe kwa nini isiwe hivyo?

Mheshimiwa Spika, para ya 72 na 74 zinazungumzia usafiri/usafirishaji na mfuko wa barabara. Hali ya usafiri vijijini ni mbaya sana. Bado wananchi wanasafiri masafa marefu kwa miguu kwa sababu hakuna barabara zenye hupitika kwa magari. Nashauri Serikali iboreshe *accessibility* vijijini na namna pekee ni kufanyia grading mtandao wote wa barabara za vijijini zilizo za udongo. Ukisha *grade* barabara hizi utapata *roadshape* na hapo ndipo wanavijiji wanaweza kuingia kuilinda barabara hiyo kwa kujengea mifereji na matengenezo ya mara kwa mara itawezekana!

Mheshimiwa Spika, kuwe na *Capacity* ya kutosha Wilayani na hata kwenye Wizara. Mimi bado naamini hali ya sasa Makao Makuu ya TAMISEMI kwa upande wa miundombinu ya barabara haitoshelezi, haiwezekani ukawa na wahandisi wawili tu kufanya *management* ya mtandao mzima wa barabara za vijijini na Wilaya nchi nzima. Lazima uwe na *staffing* ya kutosha katika kitengo hiki na mimi nilikwisha shauri kuwe na kurugenzi ya barabara katika TAMISEMI na Mkurugenzi wake awe Mhandisi. Hii itasaidia kujenga uwezo *Capacity Building* huanzia Wizarani hadi Wilayani. Mfano mzuri ni Wizara ya Ujenzi hususan *TANROADS* wahandisi wamefunzwa *on the job training* wanaelewa vizuri kazi yao.

Mheshimiwa Spika, naomba eneo hili la barabara lipewe umuhimu mkubwa kwani ni eneo mojawapo katika kuondoa umaskini kuelekea mwaka 2025 na ushauri wetu naamini utachangia kusaidia.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza Waziri kwa hotuba yako nzuri yenye maelezo ya kina. Hongera sana wewe pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wako wote. Waziri mimi naomba kuchangia kwenye maeneo matatu tu.

Kwanza kabisa maslahi ya Madiwani, hili kwa kweli umefika wakati wa kuangalia maslahi ya viongozi hawa. Baadhi ya Wilaya zetu kwa mfano Mafia posho ya kikao ni 10,000/= tu. Sasa ukiangalia kweli haya mambo yanafanana na shughuli wanayofanya viongozi hawa. Mimi naomba Madiwani wa Nchi nzima posho ifanane na pia posho ya mwezi iongezwe.

Pili, suala la kuchagua mazaola chakula na moja la biashara kila Wilaya. Mimi binafsi naona kwa baadhi ya Wilaya ni tatizo. Nikiongelea mfano wa Mafia hivi sisi tukiongelea suala la Nazi ni tatizo suala la korosho ni tatizo. Ukiondolea mbali suala la soko na bei tuongelee hata suala tunasafirisha vipi. Ukija kwenye chakula hivi tuseme mpunga au viazi vitamu, tunalima maeneo gani ya kutosha. Je, tukisema zao letu kubwa linalokidhi pande zote mbili ni mazao ya baharini Serikali itakuwa tayari kwa hili?

Tatu, kuhusu Halmashauri yetu, naomba Mheshimiwa Waziri hii Halmashauri unajua ilivyokuwa maskini. Sasa mimi ningeomba ukizingatia mazingira yetu kimawasiliano, kielimu nakadhalika. Ipo haja ya kuipa upendeleo maalum wakati wa kugawa ruzuku na pia wakati wa kutupa watumishi. Mheshimiwa Waziri tunaomba utupe fungu kubwa na pia mtupe watumishi wenye ujuzi na afya nzuri li itupunguzie matatizo ya kiutendaji. Nadhani Mheshimiwa Waziri umenielewa. Matatizo yetu mafia unayaelewa na hivyo sina sababu ya kuendelea kukuchosha kwa kurudia rudia.

Mheshimiwa Spika, mwisho nakutakia kazi njema Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote ndani ya Wizara yako. Naomba upate nafasi ya kuja kutembelea Mafia karibu sana.

**MHE. EMMANUEL ENOCK KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napongeza jitihada zote zinazofanywa na TAMISEMI katika harakati zote za kuondoa umaskini. TAMISEMI imekuwa kiungo kikubwa katika shughuli zote za maendeleo mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madiwani na utawala bora. Kada ya Madiwani katika suala la utawala bora limekuwa kikwazo kikubwa sana. Kada hii hasa wale wachache sana wanaoingia katika kamati ya uongozi, fedha na mipango imekuwa ni genge la wala rushwa, watumiaji wabaya wa dhamana na madaraka waliyopewa.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na wataalam wake kwa kuliona hilo na kufanya maamuzi ya kuwaengua katika Kamati. Hizo hasa katika eneo la Tenda, eneo hili lilikuwa limegeuzwa duka la jumla na Waheshimiwa Madiwani hawa hasa wakati wa kuteua wazabuni na makandarasi, hakuna haki wala vigezo vilivyokuwa vinatumiwa bali ni kiasi cha rushwa kilichotolewa. Hili lina maelezo kwa Halmashauri ya Kahama na yanadhibitika.

Nampa hongera Mheshimiwa Waziri kwa kuwaondoa waharibifu hawa lakini naomba ujaribu kuwafikiria suala la mshahara ili ulafi uliodhibiti usije kuhamia kwenye eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, naomba nielekeze mchango wangu kuhusu Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Naomba Waziri wakati anajumuisha atueleze kuhusu bodi hii kwani inaonekana kuwa ngeni kwangu na kwa baadhi ya Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Spika, kama kweli bodi hii ipo, basi naomba ielekezwe kwa Halmashauri zote na iwe na ufuatiliaji wa karibu. Isije bodi hii ikawa kama mfuko unaotokana na michango wa asilimia 10% ya mapato ya Halmashauri kwenda kwa wanawake na vijana.

Mheshimiwa Spika, mfuko huu wa wanawake na vijana hauchangiwi. Ni Halmashauri chache zinazochangia na kwa kuwa hakuna adhabu inayotolewa kwa wale wasiochangia basi ahadi hii ya kushindia wanawake na vijana imekuwa ni ndoto. Naomba Waziri atueleze ni hatua gani zitachukuliwa dhidi ya Halmashauri zisizochangia.

Mheshimiwa Spika, ili madiwani wafanye kazi zao vizuri, nami naomba waongezewe posho kwani kwa posho ya shilingi 11,000/= kwa kikao cha na shilingi 20,000/ kwa mwezi kwa diwani anayefanya kazi kila siku kuhimiza maendeleo ya kata ni ndogo mno. Naomba wafikiriwe sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na madiwani kuongezewa posho, naomba wapewe na vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri na ofisi hata kama ni kwa mtendaji wa kata, kusudi wananchi wenye shida wajue ni wapi waonane nao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba nzuri waliyotoa. Napenda kushauri yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa mapato ya Halmashauri ya Wilaya yangu ya Singida yatapungua kwa takribani asilimia 60 kufuatia kufuta kodi ya maendeleo na ile ya mifugo, hivyo tatizo langu la Kituo cha Afya cha tarafa ya Sepuka itabidi vishughulikiwe na Wizara hii narudia kueleza kuwa Tarafa ya Sepuka ni tarafa pekee ambayo haina kituo cha afya wala hospitali. Mazungumzo yangu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda yahusika. Naomba sana Wizara/Serikali itimize ahadi yake iliyokwishatoa kupitia swali langu Bungeni.

Pili, aidha kufutia upungufu huo wa fedha katika Halmashauri nashauri barabara za Wilaya na Vijijini sasa zitengenezwe na *TANROAD* au vinginevyo *Road Fund* iongezwe kwa TAMISEMI kutoka aslimia 30 hadi asilimia 50 kuwezesha barabara hizo kujengwa ipasavyo. Tatu, suala la usafiri kwa madiwani ni muhimu sana. Nasisitiza Madiwani wakopeshwa baiskeli kuwawezesha kufanya kazi zao sawaswa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMISI JUMANNE NGULI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kuunga mkono hoja hiyo hapo juu. Nampongeza sana Waziri na Naibu Waziri, pamoja na watumishi wa Wizara hii kwa kazi nyingi na nzuri wanazofanya. Pamoja na pongezi hizo naomba nichangia machache ili kuboresha bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, zahanati nyingi katika Halmashauri zetu zimejengwa muda mrefu wakati idadi ya watu ni chache pia watu wachache walikuwa wanatumia zahanati hizo. Tangu wakati wote hakuna upanuzi au ujenzi upya unaofanywa na Serikali. Napendekeza Serikali ifanye haraka kuangalia upya zahanati hizo maana sasa zimeelemewa na idadi ya wagonjwa dawa hazitoshi huduma kwa watoto na akina mama wajawazito hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kuboresha katika kodi ya maendeleo iliyofutwa. Baada ya kupongeza uamuzi wa Serikali wa kufuta kodi sasa tuone namna ya kuzipa fedha Halmashauri kwa ajili ya maendeleo. Badala ya kupendekeza kuwa Halmashauri zipewe fedha kama fidia ya kodi iliyokuwa inalipwa kweli haitakuwa sawa. Zipo Halmashauri maskini ambayo kodi ilikuwa tatizo kulipwa hivyo

ukichukua hesabu hizo, watapata fedha kidogo sana na hivyo itakuwa ni tatizo tena katika maendeleo. Kama Serikali imeamua kufutwa kodi na imeamua kufidia napendekeza fidia hiyo ifuate takwimu za sensa. Takwimu zinazoonyesha kabisa wanaume wazima wenye uwezo wa kufanya kazi na ambao ndiyo ilikuwa walengwe kulipa kodi ndiyo Serikali itoe kwenye Halmashauri husika, vinginevyo kutakuwa na malalamiko tu.

Mheshimiwa Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja hii.

MHE. EDWARD NZIRIYE NDEKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nichangie kwa maandishi hoja hiyo hapo juu. Katika kuchangia hoja hii naomba nijielekeze katika kifungu namba 22 mipango shirikishi jamii na Na. 75 mfuko wa barabara na huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ni hotuba nzuri sana kwa upeo na kina katika maudhui yanayolenga jamii. Nampongeza sana na naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuanzisha mipango shirikishi jamii na kuanza kutekeleza katika Halmashauri mbalimbali chini ya usimamizi wa Wizara ya Serikali ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Sera hii ni muafaka na itasaidia sana katika azma ya utekelezaji miradi ya kijamii na kuondoa umaskini ndani ya jamii.

Mheshimiwa Spika, mpango mzuri huu wa shirikishi jamii si vema ukatekelezwa katika mtindo wa majaribio katika Halmashauri chache za awali zote zinahitaji kupiga hatua hii kwa pamoja kwa sababu malengo ya taifa ya kuondoa umaskini kwa miaka 2015 na 2025 ni kwa Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Kigoma na hususani jimbo langu la Kigoma Kusini tunahitaji mpango huu kuliko labda wenzetu katika Halmashauri na majimbo mengine nchini. Jimbo letu lilikuwa mikononi mwa Upinzani. Kuendelea kulimiliki jimbo hili kutategemea ni jinsi gani tutakavyotekeleza mpango wa aina hii mpango shirikishi. Mpango huu utaleta mshikamano mpya ndani ya jamii na utarejesha imani kwa Serikali, uongozi wa taifa letu na hata chama chetu tawala.

Ni mapendekezo yangu mpango huu tuanze kuutekeleza kwa kutumia mradi wa barabara ya Simbo - Sunuka hadi Kallya km 200. Mradi huu umeanza kutekelezwa hadi Sunuka tu km 50 hivi, chini ya ufadhili wa *TASAF* na nguvu za wananchi. Wananchi katika kata zinazoguswa na barabara hiyo wako tayari kutenda kazi zote zilizoko katika uwezo wao. Kata hizo ni Simbo, Ilagala, Sunuka, Sigunga, Igalula, Buhingu na Kallya.

Utekelezaji wa mradi huu utaleta msisimko wa hali ya juu wa uzalishaji katika kilimo mazao muhimu ya michikichi, maharagwe alizeti, mhogo na pamba. Mazao mengine ni mbao, mifugo, asali na nta, samaki na dagaa.

Mradi wa barabara pia utaimarisha utalii kwa kutumia kwa ukamilifu fursa ya vivutio muhimu vya mbuga maarufu ya taifa ya Wanyama ya Mahale.

Mradi huu vile vile utaimarisha huduma za jamii, elimu, afya na utekelezaji wa miradi ya maji na umwagiliaji. Yapo mabonde mazuri na makubwa yanayofaa kwa umwagiliaji katika Vijiji vya Ilagala, Mgambazi, Nkonkwa, Kallya na Kashagulu.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri inatuthibitishia kifungu cha 75 kwamba Halmashauri ya Kigoma ni miongoni mwa zile ambazo hazikutumia vema mfumo wa barabara. Mpango shirikishi ni suluhisho la upungufu huo.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni sekta ya afya. Uboreshaji wa sekta hii ni pamoja na kutoa usafiri kwenye vituo vya afya. Jimbo la Kigoma Kusini lina jiografia ngumu katika utoaji huduma hasa inapobidi kutegemea uchukuzi kwa njia ya maji boti ambacho ni chombo duni hasa kutolea huduma za dharura kama mama mja mzito au mtu aliyepata ajali.

Kituo cha afya cha Buhingu kiko kilometa zipatazo 150 toka hospitali ya Mkoa wa Kigoma. Boti hutumia saa 12 au zaidi. Barabara ni mkombozi naomba Serikali ichukue hatua za makusudi kutelekeza mradi huo.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maombi kadhaa niliyoyasahau. Kwanza Mamlaka ya Miji Midogo zitakazoanza Januari, 2004 zimepangiwa Bajeti? Ikama zake zikoje?

Pili, je chini mamlaka ya mijini midogo hakuna haja ya kuanzisha mamlaka ambazo siyo vijiji wala mitaa zitakazoitwa *Trading Centre.*

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hoja ya Mheshimiwa Mgana Msindai ulipaji wa Mishahara kupitia *NMB* utaanza mwezi Julai kwa Dar es Salaam. Baadaye tutafanya hatua kwa hatua mikoani ili tusiharibu mambo kwa upapara.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, jimbo langu lina eneo kubwa sana, kuna kilometa za mraba 15,000. Sehemu ya Urambo iliyobakia ni 10,000 kilometa za mraba. Lakini kimaendeleo tuko nyuma sana hususan maendeleo ya barabara kiasi kwamba kuja Makao Makuu ya Wilaya ni tatizo kubwa, hasa katika maeneo mawili Uyowa na Ukumbi Siganga.

Najua huwa mnatuma fedha za barabara kwenye Halmashauri, lakini ombi langu mngetutumia kiasi maalum kikubwa waziwazi kuwa ni cha barabara ya Uyowa Kaliua na Ukumbi Siganga Kaliua. Tukipata milioni 30 kwa kila barabara zinatosha kwani tutajenga na mpango wa kutumia wananchi kama *TASAF* wanavyofanya.

**SPIKA:** Sasa michango ya mawazo na maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge imekamilika. Sasa kama sehemu ya majibu ya Serikali namwita Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu. Kwanza kabisa napenda kusema naunga mkono hoja ya Waziri mwenzangu mtoa hoja kwa asilimia mia moja na napenda nimpongeze sana kwa hoja nzuri iliyowasilishwa vizuri sana. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya kuomba nafasi hii ni kutaka kufanya masahihisho juu ya takwimu za elimu zilizotolewa katika Bunge hili hususan takwimu zilizotolewa jana na Msemaji Mkuu wa Upande wa Upinzani Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ambaye alipokuwa anazungumza alinukuu takwimu kutoka ripoti mbili zilizotolewa na Mashirika ya Kimataifa. Ripoti hizo zilitolewa katika Mkutano uliojulikana kama *Second High Level Group Meeting on Education for all,* uliofanyika huko Abuja tarehe 19 mpaka tarehe 20 Novemba, 2002.

Mheshimiwa Spika, ripoti moja ilikuwa ni ya Benki ya Dunia na ripoti nyingine ilikuwa ni ya *UNESCO.* Mimi nilipata fursa ya kuiwakilisha nchi yetu katika Mkutano huo, kwa hiyo nilikuwepo. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kwanza nikubaliane kwamba takwimu alizonukuu Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kwenye ripoti hiyo ni kweli zilikuwepo. Lakini napenda kuweka rekodi sahihi ya Bunge hili kwamba mimi kama Waziri mwenye dhamana ya takwimu za elimu nilizikanusha zile takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zile zilikuwa ni *projection* zinazozungumzia takwimu za kipindi kijacho na zilitumika takwimu za kipindi kilichopita. Zilitumika takwimu za mwaka kabla ya 2000, namna takwimu zetu za elimu zilivyokuwa katika kipindi cha miaka kumi ya nyuma na namna elimu ilivyoendelea katika miaka hiyo kumi yaani 1990 mpaka 2000. Walizitumia takwimu hizo ku-*project* kipindi kijacho kwamba katika miaka inayokuja hali itakuwa hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa nilisema pale siyo sahihi kufanya *projection* ya namna hiyo kwa sababu Mkutano wa *Education for All*, ile *World Conference* ilikuwa ni mwaka 2000. Kwa hiyo, ili kupata picha sahihi ilitakiwa kutazama utekelezaji wa mwaka 2001 na 2002.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, takwimu zile hazikuwa zimejumlisha katika uchambuzi takwimu zetu za mwaka 2001 na mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ile *Projection* ilikuwa potofu. Kwa hiyo, mimi nilizisahihisha zile takwimu na niliporejea hapa nilichukua fursa ya kuzisahihisha takwimu hizo kwa kuandika barua kwa wahusika waliozitoa hizo takwimu yaani vyombo husika na ili kuweka *record* sahihi, naomba kuisoma moja ya barua hizo nilizoziandika. Ni barua *Reference Number ED/WELL/12/VOL.III/74* ya tarehe 2 Desemba, 2002.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako inasomeka kama ifuatavyo:-

*Mr. Berger Frederick Hernsine,*
*Education Advisory African Region,*
*Washington,*
*United State of America,*
*Fax No.1202477299*

***TANZANIA IS NOT OFF TRACK TO ACHIEVING UPCS***
***(UNIVERSAL PRIMARY COMPLETION BY 2015***

*A World Bank Report entitled Achieving Universal Primary Education by 2015 a chance for every child. A conference edition of which was distributed at the UNESCO's Second High Level Group Meeting on EFA in Abuja on 19th - 20th November, 2002 includes Tanzania among the off track countries for achieving Universal Primary Completion (UPC) by 2015 in table 11 page 120.*

*I strongly object to that classification which is based on Data of prior to the year 2000. In Abuja we were reviewing progress in achieving what was resolved in Dakar in the year 2000.*

*In my opinion classification of on Track and Off Track countries should be base on data for 2001 and 2002. For your information during Dakar 2000 Tanzania's Primary Education net enrolment ratio was 57% and Gross enrolment ration was 70%. While the Net Intake Ratio was 19% and Gross Intake Ratio was 90%.*

*After two years of implementation of Dakar 2000 objectives Tanzania's Primary Education in 2002 has now reached Net enrolment ratio of 80.7%, Gross Enrolment Ration of 98.6%, Net In Take Ratio of 96% and Gross In Take Ratio of 157%. I am confident to achieving both UPE (Universal Primary Education) and UPC (Universal Primary Completion) well before the 2015. (Makofi)*

*Please be guided accordingly to adjust your Projections.*

*Yours Sincerely,*

*Joseph J. Mungai*
*Minister for Education and Culture*
*Tanzania.*

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuiweka *record* ya nyumba hii iwe sahihi katika suala hili la takwimu.

Napenda nimalizie kwa kushauri kwamba katika kuziangalia takwimu za elimu, ningeshauri Waheshimiwa Wabunge tuangalie takwimu zinazotolewa na Wizara katika kitabu kinachoitwa *Best,*

ambacho kila tunapotoa hotuba ya Bajeti hapa huwa kinagawiwa kama kitabu cha nyongeza kwa Waheshimiwa Wabunge na takwimu hizi zitathibitisha hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukuhakikishia kuwa nitampa nakala ya barua hii Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ili aweze kuisoma.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ili kuwapa watoa hoja nafasi nzuri ya kujiandaa kuwasilisha majibu na kuhitimisha hoja yao, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni, ataanza Mheshimiwa Naibu Waziri, atafuata mtoa hoja mwenyewe hatimaye tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima.

*(Saa 06.05 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma A. Akukweti) Alikalia Kiti*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabla sijaanza na mimi kutoa mchango kuhusiana na hoja ya Ofisi yetu, nitumie nafasi hii kwanza kwa kuwapongeza Wabunge wote ambao wamefanikiwa kupita kwenye uchaguzi mdogo na hasa Mbunge wa Mpanda Magharibi ambaye amekamilisha ngwe yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nilitaka vile vile nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Philip Mangula, Katibu Mkuu wa CCM pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Frederick Sumaye kwa kuwa wao ndio walikuja kufanya uzinduzi wa kampeni na mmoja akatufungia kazi ambayo imechangia vizuri sana katika kufanikisha zoezi hili. *(Makofi)*

Lakini vile vile naomba nitume nafasi hii kuwashukuru sana Wabunge wa Mkoa wa Rukwa kwa ujumla ambao wote walishiriki kikamilifu katika uchaguzi, viongozi wangu wa Mkoa, Chama cha Mapinduzi na Wilaya ambao wote kwa pamoja tulifanya kazi kwa mshikamano na ushirikiano mkubwa sana na ukaweza kutupa mafanikio ambayo yametuletea matunda. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa, naomba labda nitangulie kusema kwanza naunga mkono hoja hii moja kwa moja ili nisije nikasahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni mingi, nadhani tutakuwa tumeshafikia karibu idadi ya Waheshimiwa Wabunge kama mia hivi. Kwa hiyo, kwa muda tulionao, sio rahisi kwa kweli kuweza kusema yote. Mimi nitajitahidi kusema yale ambayo Mheshimiwa Waziri alifikiri niyaseme na yeye atasema yale mambo ambayo tumemwachia ayaseme. Lakini kwa ujumla tu, tunachoweza kusema ni kwamba tunafarijika sana na michango mingi ambayo imejitokeza na mingi ambayo imetolewa kwa mfumo wa ushauri, kwa upande wa Wizara itazingatiwa kwa kikamilifu kabisa katika utendaji wa kazi zetu. Lakini iko michango iliyotolewa vile vile ambayo kwa kweli inagusa Sekta nyingine na tutaziwasilisha katika Sekta hizo ili waweze kuzifanyia kazi kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba nijaribu kupitia hoja moja moja kwa zile ambazo nafikiri zinastahili kupewa nafasi katika kikao chako hiki. Nianze na hili la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa linalohusiana na Halmashauri ya Kyela ambayo ilikuwa inazungumzia tenda iliyotolewa ambayo ina thamani ya Sh.4,824,177/=.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tenda hiyo ilitolewa lakini ilitolewa na Halmashauri na haikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na Daktari ambaye ametajwa na baada ya kuwa imetolewa,

taratibu zote zilifuatwa. Isipokuwa, ni kweli kabisa kwamba Mkaguzi alipokuwa anapitia mahesabu, alibaini kwamba kulikuwa na maeneo ambayo bado alitaka kupewa *clarification* na kwa bahati nzuri zoezi hilo lilikamilishwa tukazirudisha kwa Mkaguzi Mkuu na ameshatu-*clear* kwamba zoezi hilo lilikuwa ni barabara kabisa.

Suala lingine ambalo lilijitokeza, lilitoka kwa Mheshimiwa Batenga kuhusiana na Waheshimiwa Wabunge Viti Maalum kupewa Wasaidizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili kwa upande mmoja lina sura mbili. Iko picha ya Waziri Mkuu kwa upande mmoja ambaye ndiye kwa kweli anasimamia suala zima la Bajeti kwa ajili hiyo, lakini kwa upande wetu tunachoweza kusema ni kwamba kuhusiana na Ofisi za Wabunge kwa ujumla, zoezi hilo tutaendelea kulifanyia kazi kwa karibu kabisa kwa kushirikiana na Ofisi zote zinazohusika ikiwa ni pamoja na Ofisi za Wabunge wa Viti Maalum. Hatubagui jambo hili hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la kuanzishwa kwa Wilaya mpya, tumepata michango mingi kuhusiana na eneo hili. Moja ilikuwa ni kutoka kwa Mheshimiwa Laizer, lakini vile vile tulipata kutoka kwa Mheshimiwa Aridi Mwanache Uledi, lakini liko vile vile moja lilitoka kwa Ndugu Chibulunje na ninaweza kusema vile vile maombi mengi tu yanayohusiana na uanzishwaji wa Wilaya katika Ofisi yetu. Tunaloweza kusema hapa ni kwamba ni vizuri tukajua tu kwamba jambo hilo liko chini ya Mamlaka ya Rais ambaye ndiye anaamua wakati gani aunde Wilaya na wakati gani asiunde Wilaya. Lakini hiyo haina maana kwamba tuwanyime nafasi Waheshimiwa Wabunge kuweza kupeleka masuala haya katika ngazi zinazohusika kwa matarajio kwamba Mheshimiwa Rais anaweza akafika mahali akaridhia. Kwa hiyo, kwa kweli tunachowasihi tu ni kwamba kwa wale wanao-*feel very strongly* kwamba wanahitaji maeneo haya, wafuate tu utaratibu. Masuala yawasilishwe katika Wilaya inayohusika, yapitie *RCC*, yakitoka *RCC with recommendation* za Mkoa pale yataletwa katika Ofisi yetu tutayafanyia uchambuzi na hatimaye yatawasilishwa kwa Bwana mkubwa Rais ili aweze kuamua nini afanye.

Lakini ningelipenda vile vile kusisitiza kwamba kwa kweli mwisho wa safari hiyo ndefu, kitakachoamua ni uwezo wa Serikali kwa sababu uanzishwaji wa Wilaya ni gharama kubwa.

Kuhusu kuwapa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na wa Wilaya madaraka zaidi ya uhimili ambayo wengi tumechangia kuonyesha kwamba pengine kwa kutokuwa na madaraka hayo inawezekana tukaleta matatizo, tunachoweza kusema ni kwamba jambo hili tunalifanya kutokana na msingi wa kikatiba. Mkisoma ibara ya 145 na 146 ndiyo inayoelekeza hasa umuhimu na haja ya kupeleka madaraka katika Halmashauri zetu. Sasa inawezekana kabisa kwamba bado yapo mapungufu katika Halmashauri zetu. Lakini hoja si kurudi nyuma, hoja ni kuzisaidia Halmashauri kuzijengea uwezo zaidi ili ziweze kutekeleza majukumu yake inavyotakiwa. *(Makofi)*

Lakini naomba niunganishe hapa pia kwamba kulikuwa na rai kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pengine imekuwa kubwa mno, imebebeshwa mzigo mkubwa mno na nadhani walituheshimu tu ni kama walikuwa wanataka kusema tumeshindwa hata kazi. Lakini ninaloweza kuchangia hapa ni kwamba ni vigumu sana kutenganisha nafasi hizi mbili, Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa kwa maana ya Wakuu wa Mikoa na ma-*DC*. Ni pande mbili za sarafu ile ile. Lakini kwa upande mwingine vile vile ni vizuri mkajua kwamba Ofisi yetu haina tatizo hata kidogo na Wakuu wa Mikoa na Wilaya katika usimamizi wala uendeshaji wa shughuli zao. Si mzigo kwa Ofisi yetu ila tatizo liko katika Halmashauri na sisi bado tunaamini wakuu hawa wanatusaidia sana kusimamia shughuli katika ngazi za Wilaya. Kwa hiyo bado tunadhani kabisa utaratibu uliopo utaendelea kuwepo kwa sababu hatujaona kama una kasoro kubwa ila tutaendelea kuimarisha na kuboresha taratibu na miongozo ili jambo hili liweze kueleweka wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na viwango vya posho za Madiwani kwamba zilingane na kima cha chini. Labda niseme tu kwamba kwa ujumla nadhani Mheshimiwa Waziri wa Nchi, atalitazama hili na kuwapa maelezo mazuri zaidi ili pengine tuweze kupata maelezo ya kina zaidi. Lakini hapa inatosha tu kusema, viwango vilivyowekwa vilizingatia uwezo wa kifedha wakati huo kulingana na uwezo wa kila Halmashauri kwa sababu posho hizi zinatokana na Halmashauri zenyewe. Lakini kwa maana ya michango

tuliyoipata hapa kwa upana wake, Mheshimiwa Waziri wa Nchi atasaidia kuwasaidieni kulielewa kwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ndugai alitoa rai kuhusiana na eneo lile lenye ukame na maamuzi ya Serikali kuhusiana na chaguo la mazao katika maeneo kama haya. Hili tumelipokea na kwa kweli tumesema tutazingatia kwa sababu tutashauriana na Wizara inayohusika ili waweze kutushauri vizuri zaidi namna ya kulifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilikuwepo pia vile vile suala la *TASAF* inavyotekeleza shughuli zake. Kwa sasa ilikuwa imeanza kwa awamu na Mheshimiwa Magayane na hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengine kama mtakumbuka wameona kwamba utaratibu huu pengine ungeweza ukaboreshwa kwa namna nzuri zaidi ili wengi zaidi au Wilaya nyingi zaidi ziweze kunufaika. Mwanzo hili tumelipokea kwa mikono miwili na tumeafiki kabisa kwamba zoezi hili la *TASAF* litapanuliwa ili liweze kuunganisha Wilaya nyingi zaidi na kwa hiyo kunufaisha maeneo mengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Ofisi yetu kuagiza Halmashauri kuingizwa katika mpango wa uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa kwa ujumla wake, hili tumelitazama. Ni kweli tulianza na Halmashauri 38, awamu ya pili tulitegemea Halashauri 45 na awamu ya mwisho tulitegemea tuwe na Halmashauri 31. Lakini baada ya kulitafakari kwa kina katika Ofisi yetu, wote tumeona rai ni ya msingi na tumeona kwamba kwa kweli yapo maeneo ambayo hayana sababu ya kungoja hatua zote 17 na kwa maana hiyo hatuna haja pengine ya kwenda na awamu kama tulivyokuwa tumezifikiria. Kwa hiyo, Serikali imeamua kutekeleza mpango huu kwa Halmashauri zote na maandalizi ya msingi yamekwishaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uondoaji wa watumishi wasiofaa katika Halmashauri zetu na kwamba tujaribu kuweka watu wenye sifa, tunaloweza kusema hapa ni kwamba utaratibu uliopo hivi sasa unatoa maelekezo mazuri sana. Ni msingi wa kisheria, ni kanuni zilizowekwa na kwa hiyo kwa kiasi kikubwa hiyo rai ya Waheshimiwa Wabunge inazingatiwa kwa kiasi kikubwa sana na hawa watumishi wamepangwa vile vile kulingana na viwango vyao kwa maana ya kwamba wanapotenda makosa ni mamlaka gani iweze kushughulikia masuala yao. Kwa hiyo, liko kundi linaloshughulikiwa kama la Mkurugenzi mwenyewe lakini liko kundi linaloshughulikiwa na Halmashauri kwa ujumla na liko kundi ambalo mwenye dhamana sasa ya nidhamu ni Waziri mwenyewe mwenye nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa labda niseme cha ziada tu kwamba kulikuwa na rai kwamba inaonekana pengine Ofisi yetu pengine hatutekelezi wajibu wetu vizuri, tunaachia watu hivi kufanya vitu hovyo hovyo na hatuwachukulii hatua. Naomba tu kutoa taarifa kwamba katika kipindi cha mwaka 2000 wakati ndio Mheshimiwa Waziri Ngwilizi ameshika madaraka katika Ofisi hii mpaka hivi sasa watumishi 23 ama wamefukuzwa kazi ama wameachishwa kazi kutokana na sababu mbalimbali. Wafanyakazi 14 wamevuliwa madaraka, 24 ni wale waliorejeshwa madarakani lakini baada ya kupewa onyo kali na baada ya kuridhika kwamba sababu za kuwafukuza pengine hazikutosheleza. Kwa hiyo tunajitahidi sana kubanana na Watendaji na Halmashauri kwa ujumla.

Lakini hapa labda nigusie kidogo suala la kaka yangu Mheshimiwa Simpasa ambaye nadhani wote mlishuhudia jana alizungumza kwa kweli kwa ukali mpaka nikaogopa na nilipotoka nikasema; Lah, kaka yangu leo naona ulinuia kweli kweli! Lakini nataka nieleze tatizo la Mbozi kidogo ili kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge mwone kilichotokea ni nini.

Mbozi ni kweli tulipeleka Mweka Hazina ambaye alikuwa ametoka Halmashauri nyingine ya Mbarali na kama alivyosema mwenyewe, Mbarali walimpigia simu kwamba umepata Mweka Hazina bomu. Alinifuata na mimi nikamwarifu Waziri lakini tukamsihi sana kwamba wakati mwingine mazingira yanapelekea utendaji mbovu. Hebu mpokeeni, jaribuni kumsaidia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuliamini kwamba katika kauli hiyo tutasaidiana vizuri, lakini haikuwa hivyo. Matokeo yake sasa ni haya mambo aliyoyaeleza kwamba kulibainika kwamba kulikuwa na wizi wa karibu Shilingi milioni moja ambao yeye ndiye alihusika kwa kiasi kikubwa akishiriana na Kaimu Mganga pamoja na Boharia. Sio hilo tu, yale aliyoyasema ya kumkaba koo Mtendaji na kumpiga ngumi ni ya kweli

vile vile na hata hundi ile iliyokuwa imetayarishwa wakati yeye alikuwa hayupo, ni kweli vile vile. Kwa hiyo, kulikuwa na kila sababu kwa Mheshimiwa Simpasa kwa kweli kuona uchungu kwamba jitu kama hili bado tunataka kuliacha acha. Lakini nataka niseme kwamba, mtumishi huyu yuko chini ya Halmashauri ya Mamlaka ya Mbozi. Walimchukulia hatua zote za nidhamu na wakaridhika kabisa kwamba alikosa makosa yote matatu. Lakini kilichonishangaza na nilimwuliza Mheshimiwa Simpasa, ni kwamba walipokutana kwenye kikao cha tarehe 25 Aprili, 2003 Kamati ya Uongozi, Fedha na Mipango wakasema, na hapa naomba tu niseme kwa kifupi walichoamua kwa watu kama hao. "Wajumbe na Madiwani wengine waliohudhuria wote kwa pamoja waliunga mkono hoja iliyotolewa kuwa badala ya kuwafukuza kazi, wahusika wote wapunguziwe adhabu na kupendekeza wachange kurejesha fedha iliyochukuliwa. Bwana Mwalwisi, Dr. Mahungururo wahamishiwe Wilaya nyingine na Bwana Mwangomile apangiwe kazi nyingine."

Huo ndio ulikuwa uamuzi wa Kamati hiyo. Mheshimiwa Simpasa alikuwepo kwenye kikao hicho na Mheshimiwa Halinga alikuwemo kwenye Kikao hicho. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kusema hapa ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge mnapopata bahati nzuri ya kumkaba Mtendaji mbovu kama huyu majibu yake sio haya yaliyofanywa na Kamati. Kweli walitakiwa kuwa wakali zaidi na kwa njia hiyo wangetusaidia. Sasa ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Simpasa, huyu ambaye alidhaniwa kwamba ndiye mkosaji na alistahili kufukuzwa lakini akasamehewa na yeye alitumia njia zake nyingine akapeleka madai kwenye vyombo mbalimbali na aka-*allege* mambo mengi tu dhidi ya uongozi pale kwa ujumla.

Sasa Ofisi yetu tunajitahidi sana kuendesha shughuli zetu kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni, kwa hiyo tusionee mtu. Kwa hiyo, tulikubaliana na ushauri uliotolewa kwenye Ofisi yetu tukaunda timu iende kufanya uchunguzi kuona hii hali imetokana na nini. Kwa kweli mimi nilifurahi sana kwa sababu nilikuwa najiuliza ni kwa nini waovu hawa wamesamehewa? Kuna nini?

Kwa hiyo, tunangojea matokeo ya hiyo taarifa na nilikuwa nimeshamu-*assure* kabisa Mheshimiwa Simpasa kwamba tumefanya jambo hili kwa nia nzuri, tuvumilie tupate matokeo ya timu hiyo tuna hakika tutatenda haki na hatutajali, kama Mkurugenzi katika *implication* zake na yeye ni mwizi, atachukuliwa hatua tu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilifikiri nilieleze hili ili pengine mweze kujua kilichotokea ni nini, lakini naheshimu sana mawazo ya Mheshimiwa Simpasa aliyoyatoa, lakini niliona na mimi nijaribu kuliweka wazi ili tuweze kusaidiana vizuri zaidi huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kasella-Bantu alikuwa katoa rai nzuri tu ya kujenga uwezo wa utendaji katika Halmashauri zetu na sisi tumelipokea hili, kwanza ndio jukumu letu na kwa kweli *basically* ndio kazi tunayojaribu kuifanya kwa hivi sasa. Kwa hiyo, tutalizingatia sana muda wote tunapotekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Benedict Losurutia alitoa rai ambayo tunafikiri ni nzuri. Alikuwa anazungumzia kwamba tutoe maelekezo maalum kwa fedha zitakazotolewa kama fidia ya kufutwa kwa kodi ya maendeleo na jambo hilo tunalizingatia na ndivyo itakavyofanyika ili kusiwe na ubabaishaji katika ngazi hizo za chini.

Kuhusiana na madeni ya nyuma, jambo ambalo vile vile lilizungumzwa na Mheshimiwa Losurutia, ushauri wake kwa kweli tumeuzingatia na tutatoa maelekezo mahususi kabisa ili kubaini madeni ya nyuma ya Watendaji na kuweka utaratibu wa namna ya kulipa hayo madeni ya siku za nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa tena naomba niseme jambo ambalo naona hata yeye alipata taabu kusema, kila akitaka kulisema anaona vigumu na mimi naona vigumu vile vile. Ni suala la mgogoro wa mpaka ambao aliuzungumzia jana kati ya Kondoa na Kiteto.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili lilikwisha na mtakumbuka hata Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna wakati alitoa kauli hapa juu ya jambo hili tukafikiri limekwisha. Lakini leo nimefarijika sana Mheshimiwa Marmo, Mbunge wa Mbulu amejaribu kuliweka vizuri sana.

Wananchi kwa ujumla si wenye tatizo hata la mipaka. Matatizo haya zaidi ni sisi viongozi. Hata katika mgogoro huu tuliwasihi sana viongozi wote wawili kwamba maadam jambo hili linakwenda katika usawa haitasaidia ukisema Kondoa leo walipe milioni 48 mtake msitake, fedha zile walizolipa za kwanza 38 walichota kwenye *Road Fund* kwa sababu Halmashauri haikuwa na uwezo. Kwa hiyo, tulichotegemea ni viongozi kusaidia ku-*calm down* wananchi hawa kuwaeleza, *after all* ndio wamewaweka katika majukumu haya. Kwa hiyo, tukadhani kwamba tungesaidiwa sana na Mheshimiwa Losurutia na viongozi wengine kuzungumza jambo hili vizuri tuone kama linaweza likaishaje. Lakini kama mtakumbuka, jana alikuwa kwa kweli anasema hilo jambo kama litakuwa hivi, basi. Lakini uamuzi wa Serikali ni kwamba ile fidia ya Shilingi milioni 48 haitatolewa hata kidogo kwa sababu tunaona tutaendekeza tu ugomvi wa upande mwingine. Maana ni kugeuza tu upande mmoja unapeleka upande wa pili. Kwa hiyo, tulidhani kwa sasa jambo la kufanya, hapa tulipofika ni kazi yetu kuwasaidia wananchi wajue kwamba jamani mambo haya huwa tunachokozana, unafika mahali mwenzako anashindwa kufanya hili, basi mnazungumza yanakwisha. *(Makofi)*

Lakini jambo lingine ambalo lilijitokeza ni suala ambalo alilizungumza mama Msafiri Mbunge wa Muleba. Katika kuondoa kero mbalimbali za walimu, inaonekana suala la malimbikizo na migogoro inayohusiana na mafao yao bado ni kama vile hatujafanya kitu. Lakini nilitaka niseme hapa kwamba Waheshimiwa Wabunge wote mtakumbuka, Serikali ilifanya uamuzi wa msingi kabisa hasa mwaka 2000 wakati wa uchaguzi kuhakikisha kwamba madeni ya malimbikizo yote wamelipwa na uamuzi ukafanyika wa makusudi kwa upande wa walimu na ilipofika mwaka 2001 walimu waliokuwa wamehakikiwa madeni yao, fedha bilioni nne zikawa zimelipwa kwa ajili hiyo na tukasema kuanzia hapo tusipate tena mgogoro wa malimbikizo ya madeni haya. Lakini kama wote mlivyoshuhudia inaonekana bado tatizo hilo lipo.

Kwa hiyo, tunachoweza kusema tu ni kwamba tutaendelea kukabana koo na Halmashauri zetu ili tuone mgogoro wa malimbikizo mpaka mwaka 2001 unatokana na nini na kwamba kuanzia hapo hali ikoje ili tuweze kuwa na uhakika kabisa kwamba jambo hili linamalizika. Lakini nilitaka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Serikali tangu mwaka 2001 imejitahidi sana kutoa fedha zote zinazotakiwa. Matatizo yako kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala alilolisema Mheshimiwa Mwananzila, suala la upungufu wa magari, tunaomba tu kusema kwamba hili tatizo linaeleweka ni la nchi nzima. Vituo vingi vya Afya, acha Vituo vya Afya, hata Wilaya zenyewe katika Hospitali zake hazina na kama nilivyosema hivi karibuni juu ya swali moja lililoulizwa juu ya jambo hili hili, kwa kweli Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inalifanyia kazi jambo hili kwa nguvu sana. Tunayo matumaini kabisa kwamba tutafika mahali tutapata ufumbuzi wa muda katika jambo hili kwa kujaribu kuona kama tunaweza tukapata usafiri wa kutosha kwa ajili ya Vituo na Wilaya zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ambayo Mheshimiwa Mrope alizungumza jana, ninaloweza kusema tu ni kwamba Ofisi yetu imeunda Tume nyingi tu katika kujaribu kufuatilia migogoro mbalimbali katika Halmashauri zetu, tulifanya hivyo kwa Musoma ambako Mheshimiwa Marwa alikuwa anazungumza, tukafanya Morogoro, Karatu, Arumeru, tumefanya Manispaa ya Arusha, Tanga, Nachingwea, Kilosa, Dodoma, tumefanya hivyo kwa Kondoa, Korogwe, Newala, Tandahimba na hivi sasa bado Tume zinaendelea kwa sababu kwa kweli ni zoezi ambalo tumeona tuendelee nalo mpaka tujiridhishe kwamba likoje. Lakini ninachoweza kusema tu hapa ni kwamba tunafanya kazi hii kwa nia nzuri kabisa na kwa upande wa Masasi labda nimwambie tu Mheshimiwa Mrope, inawezekana wakati huo hukuwepo Jimboni lakini Waziri wa Nchi mwenyewe alikuja mpaka Masasi na akakutana na Madiwani na akatoa taarifa ya Tume iliyokuwa imetumwa kuchunguza mambo katika Halmashauri hiyo. Sasa tunachoweza kuomba tu ni kwamba, kama pengine utaweza kupata details kidogo, hakuna tatizo. Tutakukaribisha Ofisini, labda tunaweza tukakupa maeneo zaidikidogo ambayo yalifikiwa. Lakini taarifa iliwasilishwa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe.

Kuhusu maombi ya kuanzisha Tarafa ya Mnero, hili tulileltewa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo ambaye ni Mbunge wa Nachingwea lakini vile vile Waziri. Ninaloweza kusema hapa ni kwamba, mimi nitoe wito tu kwa ujumla. Tunajua tuna matatizo ya mgao wa Tarafa, Kata, Vijiji kwa upana wake, wacha Wilaya ambazo nimezizungumza. Tunao muda sasa kwa maana ya Vijiji na Kata kwa sababu

uchaguzi ni mwaka kesho. Pengine wale wenye maombi kama haya tungeyapokea tu halafu yafanyiwe kazi halafu tuone lipi linawezekana na lipi haliwezekani. *(Makofi)*

Kuhusu mlolongo wa kodi ambao tulipewa rai na Dr. Masunga Chegeni, ni kweli uko mlolongo mkubwa tu ambao unaweza ukautaja lakini nilitaka tu nitoe taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba kwa kweli kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tumejitahidi sana kupunguza ule mlolongo kutoka kodi sitini mpaka kodi saba, si jambo dogo imefanyika. Ni kazi kubwa sana! Lakini hata ndani ya hizo saba tunafanya kazi sasa ya kujaribu ku-redefine ili kusiwe na mashaka juu ya kodi gani au ushuru gani kwa sababu kunaweza kukawa na watu wana tafsiri jambo lile lile kwa viwango tofauti. Kwa hiyo, hilo tuna hakika kabisa tutalikamilisha na tulishatoa hata Waraka lakini baadaye tumeusitisha ili tuweze kufanya uwe more clearer kuliko ulivyo sasa. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi kubwa kabisa.

Jambo lingine ambalo nilifikiri niseme hapa ni kuhusiana na mafunzo kwa ujumla wake. Tumepata rai nyingi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, najua Mheshimiwa Semindu alisema, Mheshimiwa Kimiti vile vile amesema na wengine kuhusu Mafunzo kwa Watendaji kwa ujumla. Lakini mimi hapa naomba nizungumzie zaidi Watendaji katika ngazi ya Kata pengine na Vijiji. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wote tumejitahidi kutoa taarifa za mara kwa mara, inajitahidi sana kujaribu kutoa mafunzo kwa Watendaji hawa ili kuimarisha utendaji katika ngazi za Wilaya. Lakini bado naomba nitoe rai kwa Halmashauri kwamba kila Halmashauri ichukue initiative vile vile kuwasaidia hata Watendaji wa Kata kuwasomesha ili kuweza kuongeza viwango vyao vya uelewa na bahati nzuri tunacho Chuo cha Mipango hapa Dodoma ambacho kwa kweli historically ni Chuo hasa kwa ajili ya *Rural Development.* Mpanda tumejitahidi, tulipeleka awamu ya kwanza Watendaji tisa, mwaka huu tunao Watendaji tena wengine kama tisa, kwa hiyo tuna uhakika kabisa hata wengine mnaweza kuiga mfano huo mkaanza kupeleka kundi kidogo kidogo. *(Makofi)*

Niseme hili la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kuhusiana na Manispaa ya Shinyanga kama imo katika orodha ya Miji itakayonufaika na mradi wa uboreshaji wa huduma za Mjini. Ukweli ni kwamba haumo, lakini juhudi zinafanywa utakuwemo katika mpango huo kwa njia nyingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani haya yanatoesheleza na kama nilivyosema, mengine yote tutajitahidi kuya-*cover* kadri muda utakavyokuwa unakwenda. Lakini kwa vile nina dakika tatu, naomba niseme mengine machache kabisa. Moja, ni hili alilolisema Mheshimiwa Mzee Makwetta kwamba Vijiji visivyo na ardhi ya kutosha viunganishwe ili kuwatumia vizuri Watendaji wa Vijiji. Ana dhana moja nzuri, anaona *viability* ya baadhi ya Vijiji kwa sababu ya udogo ni kama haipo kiuchumi. Lakini vile vile kiuendeshaji anaona kwamba *it will make more sense* kama eneo likiwa kubwa lina uwezo wa kuzalisha, kwa hiyo Mtendaji anakuwa na kazi ya kufanya. Kwa hiyo, tumelipokea wazo hili na kwa kweli alishalileta siku nyingi na amelirudia tena. Lakini tulitaka tutangulize kusema kwamba kama tutapata maeneo ya Vijiji ambayo yanaona yanaweza yaka-*combine* Vijiji viwili au vitatu kwa rai yao kwa ushirikishwaji wao, mimi nina hakika Ofisi yetu itakuwa tayari kabisa kubariki wazo hilo na kupanua ukubwa wa Kijiji. Lakini Ofisi itaendelea kutazama jambo hili kwa makini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme moja ambalo Mheshimiwa Kigoda alikuwa ameomba tulizungumzie, ni suala la ada ya ardhi ya Sh. 500/= inayotozwa kwa ekari kwa wakulima wanaomiliki mashamba. Suala hili liko Kiteto lakini nadhani liko maeneo mengine. Tumeshatoa maelekezo tayari kwamba jambo hili lifanyiwe marekebisho. *Actually* tumesema yasitishwe kabisa mpaka hapo tutakapokuwa tumetoa maelekezo mengine kama hapana budi. Kwa hiyo, hilo nadhani halina mgogoro.

Kuna wazo lilitoka kwa Mheshimiwa Kidunda ambalo ni zuri tu, nalo alikuwa anataka kujua ni namna gani Chuo Kikuu Kishiriki cha *UCLAS* kinaweza kusaidia katika hizi Wilaya mpya hasa katika uchoraji wa ramani na vitu vingine. Bahati nzuri nimelipata vile vile kutoka kwa Mbunge mwingine na walipokuwa hapa nilizungumza nao. Wako tayari na wanakaribisha na wala sio Wilaya mpya tu, wanakaribisha Halmashauri zote kupeleka mawazo yao juu ya nini wanadhani *UCLAS* inaweza ikasaidia kufanya. Wana uwezo mkubwa na wanaamini kabisa wanaweza kuchangia vizuri sana katika uboreshaji wa mazingira katika Vijiji vyetu. Hili la usimamizi wa mfuko wa pembejeo alilolieleza Mheshimiwa Mollel tutaliwasilisha na tutalizungumza na Wizara inayohusika ili tuweze kuona nini tutafanya.

Lakini liko moja ambalo nadhani nimalizie nalo ni la Mheshimiwa Major Makundi ambalo alitaka kujua kwa nini hawa wazee na wengine waliokamatwa kwa ajili ya kodi na wakafungwa kwa utaratibu wa kisheria wasipewe msamaha? Moja ni kwamba, kufungwa kwao ni halali kabisa kwa sababu sheria ilikuwa inaruhusu na ilimradi hawakukata rufaa, wataendelea kuwemo humo mpaka hapo watakapomaliza kifungo chao. Lakini kinachoweza kufanyika kwa sababu huo utaratibu upo, Rais ndio mwenye madaraka ya mwisho ya kutoa misamaha kama hii na utaratibu upo na una Kamati yake. Kwa hiyo, hawa kama wataona inafaa kwa watu kama hawa mara nyingi ndio wanafanya hiyo kazi ya kumshauri Rais ili aweze kufanya hiyo kazi. Sio Ofisi yetu, kwa sababu hayo mambo yanafanyika kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani na vyombo vingine vinavyohusika.

Labda niseme lingine moja nilitaka kulisahau, hili la Mikoa ya Kilimanjaro, Tabora ambao walikuwa wamefikiria kwamba kutokana na jedwali tulililoletewa Na.21 waliona hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya Ofisi zao. Nataka niwahakikishie kabisa kwamba tume-*cross-check* fedha zipo, Tabora milioni nne, Kilimanjaro nafikiri Sh.2,900,000/= na nadhani hata kuna Wilaya nyingine alikuwa ame-*raise* Mheshimiwa Mbunge mmoja lakini hata hivyo tunajua fedha zake zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudie kusema kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia moja na ninawashukuruni sana. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizokuwa zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, kuhusu makadirio na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2003/2004. Napenda nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote 106 ambao walichangia hoja aidha kwa kusema, ama kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwataje kwanza waliochangia kwa kusema Bungeni, wa kwanza ni Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Makamu Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Pili, ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Peter Slaa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Benedect K. Losurutia, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Esha H. Stima, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mheshimiwa Philip A. Magani, Mheshimiwa Ibrahim W. Marwa, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Lekule M. Laizer, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Dr. Masumbuko R.M. Lamwai, Mheshimiwa Teddy L.Kasela-Bantu, Mheshimiwa Abu T. Kiwanga, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Aridi M. Uledi, Mheshimiwa Prof. Juma M. Mikidadi, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan, Mheshimiwa Christopher S. Wegga, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Mheshimiwa Lediana M. Mung'ong'o, Mheshimiwa Maria D. Watondoha, Mheshimiwa Frank Magoba, Mheshimiwa Hadija K. Kusaga, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa Joseph J. Mungai na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge sabini na nne waliochangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Shamim Parkar Khan, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Lephy B. Gembe, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Leonard N. Derefa, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa George F. Mlawa, Mheshimiwa JumaS. Kidunda na Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo.

Wengine ni Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Omari M. Mwenda, Mheshimiwa Major Jesse J. Makundi, Mheshimiwa Ireneous N. Ngwatura, Mheshimiwa Oscar T. Mloka, Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Dr. Masumbuko R.M. Lamwai, Mheshimiwa Iddi

M. Simba, Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo, Mheshimiwa Salum Omar Ali, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira, Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Mheshimiwa Hasnain M. Murji, Mheshimiwa Profesa Pius P. Mbawala, Mheshimiwa Yete S. Mwalyego, Mheshimiwa Dr. Hussein A. Mwinyi, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Halimenshi K.R. Mayonga, Mheshimiwa Stephen M. Kazi, Mheshimiwa John E. Singo na Mheshimiwa Robert K. Mashala.

Wengine ni Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan, Mheshimiwa Lekule M. Laizer, Mheshimiwa Ally A. Karavina, Mheshimiwa Profesa Henry R. Mgombelo, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa John L. Mwakipesile, Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mheshimiwa Salome J. Mbatia, Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mheshimiwa Abdulkarim E.H. Shah, Mheshimiwa Charles H. Kagonji, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Talala B. Mbise, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Abdula S. Lutavi, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mheshimiwa Emmanuel E. Kipole, Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Jumanne H. Nguli, Mheshimiwa Edward N. Ndeka, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya, na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imezingatia kikamilifu hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika maeneo ya ushauri. Mapendekezo na maoni katika kuboresha utendaji wa Ofisi yangu, napenda kusema kwamba maelezo hayo tumeyazingatia na sasa naomba nitoe maelezo na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Hoja ya kwanza ilihusu Waheshimiwa wapatiwe Ofisi za kufanyia kazi, ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amelieleza na kama alivyosema zoezi hili tunaendelea kulifanyia kazi. Sasa hivi tuna Waheshimiwa Wabunge 165 ambao wana Ofisi, kati ya Wabunge 204. Kwa hiyo, zoezi hili linaendelea mpaka tutakapokamilisha. Kitu ambacho kinatukwaza ni uwezo wa fedha. Hoja nyingine ilikuwa fedha zinazotengwa kupunguza umaskini ni asilimia ndogo sana katika Bajeti yote na katika baadhi ya Wilaya, hakuna kabisa Bajeti ya Maendeleo ya Kilimo wakati gharama za matumizi ya kawaida kama simu na safari zimetengewa fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi fedha za kuondoa umaskini zinajitokeza siyo kwa kuangalia miradi ya maendeleo ya kilimo pekee, bali kwa kuangalia sekta zote za Elimu, Afya, Maji, Barabara na Kilimo kama ilivyoainishwa katika mkakati wa kuondoa umaskini. Aidha kwa upande wa Bajeti za Halmashauri zipo baadhi ya Halmashauri ambazo zimetenga fedha za maendeleo ya kilimo kutokana na vyanzo vyao vya mapato. Fedha nyingine kama ilivyo kwenye sekta za Elimu na Afya zitaonekana kwenye Bajeti za Wizara za Kisekta. Pia baadhi ya wahisani na mashirika yasiyo ya kiserikali yametoa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Halmashauri. Kadhalika Serikali imeondoa ushuru kwenye pembejeo za kilimo ambao ni kwa manufaa ya mkulima moja kwa moja.

Kwa hiyo, fedha za usafiri na simu zinazotengwa na Halmashauri ni kuwezesha utekelezaji wa juhudi hizo zilizoainishwa hapo juu.

Hoja nyingine ni kwamba Mheshimiwa Naibu Spika, ni kuanzishwa programu maalum ya kukabiliana na majanga ya moto na mafunzo yatolewe kwa watumishi. Ofisi ya Waziri Mkuu ina Kitengo kinachoshughulikia maafa yakiwepo majanga ya moto. Aidha, katika kila Mkoa, Halmashauri na Vijiji kuna Kamati za Maafa. Katika Sera ya Maafa iliyoandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu suala la kutoa mafunzo ya namna ya kukabiliana yakiwemo ya moto katika ngazi zote zilizotajwa hapo juu yamezingatiwa.

Kulikuwa na hoja ya kutaka ufafanuzi juu ya ukarabati wa nyumba za Wakuu wa Mikoa na Wilaya zinazokarabatiwa hivi sasa, kwa kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuuza nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni Ikulu Ndogo haziwezi kuuzwa kwa watu binafsi. Naamini kwenye suala hili la nyumba za Serikali zilizouziwa baadhi ya watumishi huenda Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi wakati atakapokuwa anatoa makadirio yake anaweza kulizungumzia kwa kirefu zaidi kwa sababu nyumba hizi ziko chini ya Wizara yake. *(Makofi)*

Kuhusu hoja kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005 uwepo mfumo wa kutoa taarifa unaofanana kwa Mikoa yote kama inavyoelezwa na Hazina. Hoja hii tumeizingatia na Wizara yangu itatoa maagizo kuhakikisha kwamba Mikoa yote inatekeleza agizo hilo. *(Makofi)*

Kulikuwa na hoja kwamba TAMISEMI ionyeshe upungufu wa watumishi katika Mikoa na Halmashauri na hatua zinazochukuliwa kukabili upungufu huo. Upungufu wa watumishi katika Mikoa ni watumishi 481. Kwa upande wa Halmashauri kuna upungufu wa watumishi 5,506. Ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa Wahasibu, Idara Kuu ya Utumishi imetoa vibali vya kuajiri *qualified Accountants 67.* Aidha Wizara ya Fedha imeanza kuwagharamia vijana wenye sifa waliomaliza Kidato cha Sita wapatao 600 kusomea kwenye Vyuo vya Uhasibu *The Institute of Finance Management (IFM), Institute of Accountancy DIA* na *Arusha Institute of Accountancy.*

Hoja nyingine Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba TAMISEMI iandae utaratibu maalum wa kuwaajiri Maafisa Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa. Napenda kuthibitisha kwamba taratibu za ajira kwa watumishi hawa zimeainishwa katika Miundo ya Utumishi wa Kada zao. Kwa mfano, Maafisa Watendaji wa Vijiji wanatakiwa kuwa na elimu ya Kidato cha Nne hadi cha Sita. Na waliohitimu Shahada au Stashahada katika fani yoyote kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kufaulu usaili.

Utaratibu huo unatumika kwa Maafisa Watendaji wa Kata. Ili kuhakikisha haya yaliyoelezwa hapo juu yanatekelezwa Ofisi yangu kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa katika Sera ya Management ya Ajira, katika utumishi wa umma itazielekeza Halmsauri ambazo hazina Bodi za Ajira kuunda Bodi hizo ili ziweze kuwaajiri maafisa Watendaji wa Vijiji, Kata na Mitaa.

Watumishi hao kabla hawajaanza kutekeleza majukumu yao watapewa mafunzo kwenye Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo pamoja na Vyuo vingine vya Maendeleo katika maeneo yao.

Kulikuwa na hoja kwamba Halmashauri zipewe mwongozo kutunga sheria ndogo ndogo. Kama nilivyosema katika hotuba yangu Halmashauri itatoa miongozo na vile vile tumeziagiza kwamba sasa Sheria zote na Sheria Ndogo Ndogo zichapishwe kwa lugha ya Kiswahili ili ziweze kueleweka kwa wananchi. Halmashauri kupewa uwezo wa kusimamia mfuko wa pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuzipa Halmashauri za Wilaya uwezo wa kusimamia mfuko wa pembejeo kwa madhumuni kuwapunguzia wakulima bei ya pembejeo, kimsingi ni zuri. Lakini uzoefu tulionao, unaonyesha kuwa vyombo ambavyo havina mwelekeo wa masuala ya fedha hususan mikopo, zimepata matatizo ya kusimamia urejeshaji wa mikopo. Mfano mzuri ni madeni makubwa yaliyolimbikizwa na vyama vya Ushirika.

Kwa hiyo, suala hili linahitaji maandalizi ya kutosha, kwa maana ya kuangalia uwezo wa taratibu zitakazotumika bila kuziingiza Halmashauri katika madeni kama ilivyokuwa katika vyama vya ushirika.

Kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Dr. Slaa, kwamba Makatibu Tarafa wawe na Vikao vya kisheria vya kuwawezesha kufanya maamuzi ya kisheria katika maeneo haya. Nataka kusema kwamba, Serikali imekwishachukua uamuzi huo na kuwa ajira ya Makatibu Tarafa itaendelea kuwa chini ya Serikali Kuu lakini zoezi la kuweka muundo wa kuwawezesha kufanya kazi chini ya Halmashauri linafanyika. Katika zoezi hili sheria zifuatazo zinafanyiwa marekebisho ili kutambua nafasi na majukumu ya Katibu Tarafa katika Serikali Kuu na katika Serikali za Mitaa. Sheria Na.6 ya 1999, Sheria Na. 7 ya 1982. Sheria Na. 19 ya 1997 na Sheria Na. 8 ya mwaka 2002. *(Makofi)*

Baada ya marekebisho haya, Makatibu Tarafa watakuwa wamejengewa mazingira ya kufanya kazi kwa ufanisi katika mfumo wa Serikali za Mitaa na wakati huo huo kuwa kiungo kati ya Halmashauri na ngazi ya Kata. *(Makofi)*

Vile vile kulikuwa na hoja Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itoe tathmini ya matumizi ya fedha za mfuko wa barabara ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kusimamia na kujua jinsi fedha zilivyotumika. Tathmini ya fedha za mfuko wa barabara katika Halmashauri kwa mwaka 2001/2002 ilifanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na vile vile ukaguzi wa kiufundi *Technical Audit* ulifanywa na Kampuni *ya COWI Consult*. Uchambuzi wa Taarifa hizi unafanywa na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na uchambuzi huu utakapokamilika taarifa kamili zitapelekwa kwenye Halmashauri ili mambo yaliyobainishwa katika taarifa hizi yapate kuzingatiwa na Halmashauri husika. Aidha, Waheshimiwa Wabunge watapatiwa taarifa za uchambuzi wa taarifa hizi ili nao wapate kuzizingatia vilivyo. *(Makofi)*

Kulikuwa na hoja kuhusu hatua gani za kisheria na kinidhamu zilizochukuliwa dhidi ya Halmashauri zilizoshindwa, na zinazotumia vibaya fedha za mfuko wa barabara. Maelezo ni kama yalivyo kwenye hotuba yangu ibara ya 75 ukurasa wa 35. Aidha, katika Halmashauri zilizotumia fedha za mfuko vibaya Watendaji wake wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu. Kwa mfano, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya ya Kibaya na Bagamoyo wameshushwa vyeo na Wahazini wa Halmashauri hizi wamefukuzwa kazi. *(Makofi)*

Zipo Halmashauri nyingi ambazo Watendaji wake ama wamefukuzwa kazi au wamesimamishwa kazi wakisubiri maamuzi ya mashauri yao. Mheshimiwa Dr. Slaa alieleza kwamba hotuba ya Waziri haikugusa lolote juu ya dhana nzima ya mpango wa Elimu kwa wote, *Education for All*. Katika hili napenda tu kusema kwamba hili ni suala la kisera ya elimu yako chini ya Wizara ya Elimu. Lakini hata hivyo, Wizara yangu inatambua fika kwamba elimu ni moja ya vipengele vitano vilivyoainishwa katika mpango wa milenia na maendeleo ya Umoja wa Mataifa unaokusudia kupunguza umaskini kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2015. MMEM ni utekelezaji wa mpango huo unaotokana na maamuzi ya Joint Act na bakaa mwaka 2000. Naamini kwamba Waziri wa Elimu atakapokuwa anawasilisha makadirio yake huenda atapenda kutoa ufafanuzi wa ziada.

Kulikuwa na hoja ya Serikali haikutekeleza ahadi ya kuwasilisha Bungeni Muswada wa Kutunga Sheria *Local Authority Procurement Act* kama ilivyoahidi katika Bunge la 2001/2002 ili kuhuisha utaratibu wa matumizi katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakavyokumbukwa kwamba mwaka 2001 Bunge lako tukufu lilipitisha Sheria ya Manunuzi ya Umma, *The Public Procurement Act No. 3 ya 2001*, ambayo inatumika kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Kama inavyotakiwa na kifungu cha 14 (2) cha Sheria Na.3 ya mwaka 2001, Ofisi yangu imeandaa Kanuni za Manunuzi katika Serikali za Mitaa, *Local Authority Procurement Regulations* ili kuhuisha taratibu za manunuzi na matumizi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Ofisi yangu imetekeleza ahadi hiyo, kwa kuandaa na kuchapisha Kanuni hizo ambayo ni matangazo ya Serikali Na. 48 na 49 ya tarehe 21 *March, 2003*. Katika kutekeleza Kanuni hizo Ofisi yangu pia imeandaa taratibu *Procurement Manuals* za manunuzi ili kuzisaidia Halmashauri katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni hizo. Kulikuwa na hoja kwamba Wizara ifanye tathmini juu ya ubora wa nyumba za walimu, madarasa na vyoo vilivyojengwa katika mpango wa MMEM. Serikali imeandaa Hadidu za Rejea kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango ikiwa ni sehemu ya makubaliano na wahisani kwa kipindi chote cha miaka miwili ya utekelezaji. Pindi tathmini hiyo itakapokamilika taarifa itatolewa na kusambazwa kwa wahusika wote. Aidha, ilitakiwa Wizara itoe ufafanuzi wa jinsi ya kuwapata Wajumbe wa Kamati za Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utaratibu wa kuunda Kamati za Shule ni jukumu la Wizara ya Elimu na Utamaduni, nyaraka zinazozungumziwa katika hoja ya upande wa upinzani zimetolewa na Wizara ya Elimu na Utamaduni. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni atapata nafasi ya kufafanua hoja hii zaidi wakati anawasilisha Bungeni makadirio ya Wizara yake.

Hoja nyingine ilikuwa kwamba kila mhusika afahamu ni kiasi gani cha fedha na vifaa vinavyostahili kupokelewa na pia taarifa waliopewa WaheshimiwaWabunge ili waweze kufuatilia na kusimamia shughuli za MMEM. Napenda kusema kwamba hoja hii imezingatiwa na itatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, iliyomtaka Waziri wa TAMISEMI, nitoe maelezo kuhusu kuondolewa Madiwani katika Bodi ya Zabuni. *(Makofi)*

Msingi wa kuwaondoa Waheshimiwa Madiwani katika Bodi za Zabuni za Halmashauri katika Kanuni zilizopitishwa unazingatia matakwa ya Kifungu cha 14 Kifungu kidogo cha kwanza, cha Sheria Na. 3 ya Mwaka 2001 ambayo Bunge lako Tukufu liliipitisha. Wakati nakabidhiwa kazi hii na Mheshimiwa Rais, niliapa kwamba nitalinda na kutetea Sheria zote zitakazopitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Kwa Taarifa ya Waheshimiwa Wabunge kifungu cha 14 cha Sheria hii ya *The Public Procurement Act 2001* inasema, *"There shall be in each Council a Local Government Authority Tender Board for the Procurement of goods works and services in respect of Council heads, of expenditure falling under Accounting Officers, designated as such in the Local Government Finances Act, 1982. The Composition of a Local Government Authority Tender Board and the method of appointment of the Members and the procedures to be followed by such a Tender Board, shall be as prescribed in the Regulations may pursuant to the provisions of Section 65 of the Local Government Finances Act 1982".* Mwisho wa kunukuu. Na hicho ndicho ilichofanya kwa kuandika *Regulations* ambazo zimetoka katika *GN 48* na 49 za tarehe 21 Machi, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kuwaondoa Waheshimiwa Madiwani kutoka katika Bodi hizo hauwaondolei Waheshimiwa Madiwani jukumu la kusimamia mapato na matumizi ya Halmashauri kupitia Kamati za Kudumu mbalimbali. Kanuni zinazoongoza manunuzi zimeimarisha uwajibikaji wa pande zote mbili, Waheshimiwa Madiwani na Watendaji. Madiwani wanalo jukumu la Kisera la kuidhinisha mipango na bajeti za Halmashauri. Watendaji wanao wajibu wa kutekeleza mipango ya Bajeti kama ilivyoidhinishwa na Madiwani. Bodi ya Zabuni ni chombo kinachotumiwa na Watendaji katika kutekeleza maamuzi ya Baraza la Madiwani ambayo yameidhinishwa katika mpango wa Bajeti husika.

Waheshimiwa Madiwani kupitia kwenye Kamati ya Fedha wanayo nafasi ya kusimamia utekelezaji wa maamuzi hayo. Utaratibu uliyomo katika Kanuni hizi mpya umezingatia checks and balances tangu zabuni inapotangazwa, inapofunguliwa, inapofanyiwa uchambuzi wa kitaalam, inapojadiliwa na Bodi za Zabuni na uamuzi kutolewa hadi kufunga mkataba. Na hatimaye Afisa Mhasibu kwa maana ya Mkurugenzi kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwenye Kamati ya Fedha na mwisho kuwasilishwa kwenye Baraza la Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hili nilijibu kwa kirefu kidogo kwa sababu suala la Zabuni kama sisi tunaofanya kazi Serikali Kuu, kuna Act iliyopitishwa ya Procurement 2003 inahusu Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Hata sisi Waheshimiwa Wabunge hatuko kwenye hizo Bodi za Zabuni. Waheshimiwa Madiwani vile vile wanachotakiwa ni kusimamia. Sasa wakati zabuni zile zinaletwa kwenye Baraza wana nafasi ya kuhoji kama kuna madhambi yoyote ambayo yamejitokeza. Lakini papo hapo Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la posho za Madiwani. Napenda kusema kwamba utaratibu wetu mpaka sasa hapa tulipo unazungumzia kwamba posho za Madiwani zitatokana na fedha zinazotokana na makusanyo ya *tax.* Ndiyo Sheria inavyosema. Ndiyo utaratibu unavyosema. Tunajua hali ilivyo, lakini napenda kusisitiza tu kwamba maombi ya makadirio kwa ajili ya Wizara hii sasa hivi, tunazungumzia fedha ambazo tunaziomba, ambazo zimekwishapitishwa kwa kweli katika Bajeti iliyotolewa hapa na Wizara ya Fedha.

Kwa hiyo, suala hili tutaendelea kulizingatia na hapo itakapoonekana inafaa basi Serikali itatoa uamzi na Waheshimiwa Wabunge watafahamishwa. Kwa hiyo, napenda kusisitiza kwamba posho za Madiwani mpaka hivi sasa zinatokana na *own sources* za *Council* na kama tulivyoona mapato ya *Council* yamekuwa yakizidi kupungua. Haiwezekani tukamega fungu kubwa tukalipeleka kwenye posho wakati fedha hizo hizo ndiyo zinahitajiwa kuwahudumia wananchi kwa ujumla.

Kulikuwa na hoja ya kuimarisha Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, mfuko huu unafanyiwa upembuzi yakinifu ili kujua hali halisi ya mahitaji ya uendeshaji wa Bodi.

Katika kumalizia na kama nilivyosema hoja zote za Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kuzifanyia kazi, ningependa kumalizia kwa kusema yafuatayo. Nisisitize lile ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuhusiana na mipaka ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kusema katika Bunge lako Tukufu kwamba kwa Mtanzania anayo haki na wajibu wa kuzingatia mipaka aina mbili. Mipaka ya nchi ambayo ndiyo inayomfunga asiingie nchi zingine, kwa sababu hahusiki kwenda Uganda na Kenya na mipaka kama ni ya shamba lake ama kiwanja chake. *(Makofi)*

Mipaka ya aina zingine yote ni mipaka ya kiutawala. Watanzania Katiba yetu inatupa ruksa ya kwenda mahali popote ili mradi huvunji sheria. Ndiyo maana wapo Watanzania kutoka Kaskazini wako Kusini, wa Mashariki wako Magharibi. Hata Waheshimiwa Wabunge wa chama cha CHADEMA walikuwa wanazunguka nchi nzima hii kwa sababu wanatumia uhuru wao. Sasa kama mtu kutoka Karatu anakwenda Songea, iweje mwananchi wa kijiji cha karibu aambiwe unakwenda wapi. Naomba kusisitiza yale aliyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, Watanzania waachiwe waishi katika nchi hii mahala wanapopenda. Tusiwavuruge wananchi.

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba kulizungumzwa hapa kwamba labda kuna Watendaji wakubwa wanalindwa. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba katika Wizara hii halindwi mtu inalindwa kazi. Na washukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi walizozitoa kwa Wizara ya TAMISEMI. Nami pia naomba nisiwe mtovu wa fadhila, kwani kazi nzuri hii ambayo wametupongeza ni matokeo ya ushirikiano tulioupata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla na hasa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na pia Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Sisi tunachukulia hoja zote zilizotolewa hapa kwamba siyo lawama bali ni changamoto ili tufanye vizuri zaidi. *(Makofi)*

Katika kusema hivyo, napenda kuwashukuru wenzangu katika Wizara hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watumishi wote wa Wizara, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Viongozi wote wa Halmashauri kwamba haya ni matokeo ya ushirikiano ambao tumeupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kabla hatujafika au sijamwita Katibu atueleze ni hatua gani tunafuatia, tutakapofika kwenye Kamati ili twende kifungu kwa kifungu ili muweze kuweka vitabu vyenu sawasawa mapema zaidi tutaanzia na *Supply Vote* ya Wizara.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

Kifungu 1001 - Administration and General ... Shs. 1,860,832,900/=

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. Kifungu cha 56, programu 10, kasma 1001, kasma ndogo 250100, mshahara wa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitarajii kuchukua shilingi hii moja kwa moja isipokuwa nataka maelezo. Kwanza, maelezo kwa hoja nilizotoa kwa maandishi na zile nilizotoa wakati nikichangia kwa maneno, kwanza kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Januari Mheshimiwa Waziri alitangaza rasmi kwamba tutakuwa na mamlaka ya Miji midogo 88. Lakini jambo hili siyo jambo ndogo linataka maandalizi kwa upande wetu kwa maana ya kuendesha mamlaka hizo na kwa upande wa Serikali nayo inataka maandalizi. Lakini kwa

upande wake sijaona hata mahali pamoja ametenga Bajeti kwa mamlaka hizi 88 ambazo ni muhimu na amesema zitaanza tarehe 1 Januari, 2004 ambapo ni karibu sana. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika kuchangia kwa maneno hapa nilisema kwamba kuna Tarafa kubwa sana ambazo zinashindana kutawalika na maombi ya kuzigawa yalikuwepo Wizarani kwake kwa miaka zaidi ya tisa (9). Kwa hili nisingependa maelezo ya kutokuwa na fedha kwa sababu Tarafa ndogo zaidi ziligawanywa wakati huo na baada ya pale. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuhusu mamlaka ya Miji midogo 88. Tunajua ya kwamba itaanza kazi mwezi Januari, ni kweli. Tumejiandaa, watu tutakaowatumia ni watu ambao tayari wako kwenye ajira ya Serikali, ni katika *deployment* tu. Kwa hiyo, hatuku-*envisage* kwamba kutakuwa na matumizi ya ziada sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii Tarafa ambayo imeombwa igawanywe. Niliwahi kuzungumza na Mheshimiwa Philip Marmo, nikamwambia suala hili nitalifanyia kazi. Ni suala la muda mrefu, ni kweli lakini sasa nitakwenda kulifanyia kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu hicho hicho vote 56, subvote 1001 na hii 250100, mshahara wa Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Naibu wake na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba vile vile maelezo. Ninaelewa kabisa suala la mipaka kama alivyoelezea kuna mipaka ya ndani na kuna mipaka ya nje lakini kila mipaka imechorwa kwa Kisheria na imepitishwa. Nataka maelezo katika mpaka wa Kondoa na Kiteto ambayo imetumia *GN 61* ambayo inaeleweka kama ndiyo imeitumia. Na kutokana na maelezo ya barua kutoka Ofisini kwake kwamba ametumia *GN 161* kwa wapimaji lakini jumlisheni Vijiji vifuatavyo: Kishibro, Katikati, Oruboroti na Machiga katika hiyo *GN*. Je, bado ni *GN* ya mwaka 1961 au ni *GN* mpya? Nataka maelezo.

**NAIBU SPIKA:** Napenda kukumbusha kuwa ni dakika tano ukipigiwa kengele una!

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Haina shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni suala la kufuta machozi ya wananchi wa Katikati. Hili lilikuwa ni Azimio la Kamati ya Ulinzi na Usalama la Mikoa yote miwili ya Dodoma na Arusha. Baada ya kufanya utafiti fedha zilizobaki mmetangaza kwamba wale wananchi hawawezi kupewa tena.

Sasa kama ndivyo hivyo nendeni mkawaambie wenyewe kwamba sasa hatuwapi hizo fedha na wengine mmewapa. Msitupe sisi matatizo nendeni mkawaeleze kwa sababu ninyi ndiyo mliowaahidi kwamba tutawapa, Kamati hizo mbili za Ulinzi na Usalama Mkoa wa Arusha na Dodoma na wakatulia, wakanyamaza, nendeni na ninyi mkahamishe hiyo kitu yenyewe. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tangazo la Serikali Na. 65/61 linatafsiriwa tu katika ardhi na siyo *GN* mpya, wapimaji wanatasfiri mpaka kwenye ardhi tu na siyo kupima mpaka upya. Naomba hilo Mheshimiwa Mbunge alielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hili suala la fidia. Mikoa ilikwishaelezwa hivyo na ninaamini wananchi wamekwishaarifiwa hivyo. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge anasema hawajarifiwa basi tutahakikisha kwamba wanakwenda kuarifiwa. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtu wa uwazi, naomba suala hili na ninaomba Kamati yako, Kamati ya Bunge kwamba ili matatizo haya yaweze kwisha vizuri, naomba Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge iende ikafanye hiyo kazi na kuweza kusaidia katika tatizo hili. Ombi langu ndilo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Sasa sijui kama Mheshimiwa Waziri anaweza kujibu kwa hilo pengine huu ni Utawala wa Bunge. Kwa hiyo, tuseme tu limesikika kuliko kumpa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri hana mamlaka ya kuiamrisha Kamati ya Bunge iende huko. Sijui kama mwenyewe una majibu.

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hiyo *vote 56, program 10, subvote 1001, 250100.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yaliyoulizwa ilihusu suala la Ofisi za Waheshimiwa Wabunge pamoja na hela zinazotumwa pale. Majibu yaliyotoka hayaniridhishi kwa sababu kama Waheshimiwa Wabunge hawana Ofisi na wale wengine ambao wanazo ni ka-chumba tu; na ukizingatia kwamba haya ma-vitabu mnayoturundikia sio mali ya Mbunge, inabidi apeleke kwenye Ofisi yake, kama kuna Kamati aweke ili wapiga kura waweze kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hayo hayapo kiasi kwamba wakati mwingine wapiga kura wanapokuja, huyu amesimama hapa, huyu unafukuzwa aende nje, Katibu wako Msaidizi yuko pale, kwa kweli ni hali ya kudhalilisha kwa sababu hali kama hii hata ndege ana mahali anapolala au sungura ana mahali anakolala. Sasa ninamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze japo kwa kifupi hizo Ofisi zinapaswa kuwa za namna gani kwa sababu Ofisi za watu wengine wote ukiacha Mbunge anayeonekana kama yule Mheshimiwa Rais aliyekuwa anaelezwa anaelea, wala hakuna hivyo viyoyozi wala nini. Si ombi hapa, lakini tunataka iwe ni ya sifa gani? Hilo la kwanza.

Pili, hizo hela kila mwaka wanapeleka pale kwenye Ofisi ya Mbunge, mimi kwenye Ofisi yangu sijawahi kuona hata pini, simu nalipa mimi mwenyewe na pia karatasi nanunua mimi. Sasa nataka kujua kwamba Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutupa maelekezo ya kwamba hizo hela anazozituma zitatumika katika lipi na lipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sitatoa shilingi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zimetengwa kwa kila Mkoa ili tuweze kukarabati Ofisi za Waheshimiwa Wabunge, kitu gani kitakachokuwemo humo, inategemea *equipment list* itakayokuwa imetayarishwa na Kamati ya Bunge lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kusema kwamba sasa hivi fedha tulizoomba ni kwa ajili ya kukarabati na ndiyo hizo ambazo tumeweza kukagawiwa, sasa hivi hatuna uwezo wa kuongeza fungu hilo.

**NAIBU SPIKA:** Sijui hali ya Ofisi ifananeje, ndiyo swali ambalo pia linaulizwa. Chumba cha namna gani kwa ujumla wake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikijibu hapa kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nilisema kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa amekwishatoa maelekezo Mkoani. Tumepata majibu, majibu yana utata kidogo na mimi nikawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira, sasa nimeamua Ofisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu, kulirudisha hili kwenye Tume ili tulizungumze zaidi kwenye upeo wetu kama Waheshimiwa Wabunge, tulipangie utaratibu mzuri zaidi. Ndani ya Serikali kuwe na kasma maalum inayoonyesha ukarabati na ununuzi wa samani za Ofisi za Wabunge, hivi sasa kasma hiyo haipo. Kwa hiyo, nilitaka kwa utaratibu wetu nilirudishe kwenye Tume tuainishe ili tuweze kuishauri Serikali iweke kabisa kwenye kasma ya Mipango ya Maendeleo. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kwa sababu hizi hela tunazogawa siyo zetu ni za walipa kodi na sisi kwa pamoja tunalipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba hizo hela tumetenga kwa ajili ya ukarabati, watakaa huko watajua na sisi kwa *experience* ni kwamba tumeona hakuna wanakokaa, wanakopelekewa wanachukua tu kwa sababu hata Mheshimiwa Mbunge wala hajui zinafanya nini na kwenye Kamati hayumo, wanatumia ovyo ovyo. Maelezo hayo hayatoshi kwa sababu ni lazima kama tumetenga hela za kujenga ukumbi wa Bunge inajulikana na gharama yake inajulikana, tunataka kujua inataka kutengeneza kwenye Ofisi ya nani na wapi siyo kuwapa tu wanatumia ovyo ovyo. Kwa hiyo, maelezo yale mimi siyaafiki na siridhiki nayo na sidhani kama Waheshimiwa Wabunge wanaridhika nayo, tunataka tujue zina karabati nini, huwezi kuwapa shilingi milioni 28 haijulikani ni Ofisi ya nani na ya wapi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi nadhani jibu ambalo amelitoa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba linarudi kwenye Tume, Tume yetu sisi wenyewe itakaa na kuchambua hili halafu tutalifanyia kazi. Mimi nadhani jibu lile lilitosha.

Waheshimiwa Wabunge wakati ule inapotajwa kasma wale ambao wana jambo la kulisema, naomba wasimame ili niwaone kwa ujumla wake ili niweze kupangilia, wakati ule niliwaona hawa ambao niliwapa nafasi. Kwa hiyo, nilimpa nafasi Mheshimiwa Charles Kagonji kuwa wa mwisho na kasma zinazofuata ukiwa na jambo tafadhali tusimame wote ili tujue namna ya kupangilia. Wale ambao wana maneno.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi sina tatizo kubwa katika fungu 56, programu ya 10, kifungu kidogo cha 1001 na kile kidogo zaidi cha mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ningependa maelezo zaidi kuhusiana na matatizo ya mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri ni sawa sawa kabisa, mipaka ya ndani ya Kata, Tarafa na Wilaya kwa kweli isingekuwa ni tatizo kubwa. Lakini nimesikia kauli iliyosemwa hapo ndiyo ninayotaka nipewe ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia ya kwamba wananchi hawana matatizo lakini wenye matatizo ya kugonganisha wananchi ni viongozi. Hili mimi limenikera kidogo kwa sababu tunawapoteza watu, watu wanauana, mali zao zinaharibiwa na kama kweli uchochezi ni wa viongozi mimi naomba maelezo kwamba. Je, Wizara imechukua hatua gani kwa viongozi wanaohusika na kuchonganisha watu na kuleta uhasama na migongano ya Watanzania mpaka wauane na mali zao ziharibike? Ninavyofahamu ni kwamba hakuna aliyeko juu ya Sheria hapa ndani. Tunataka maelezo ni nani hawa wanaowagonganisha watu? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kuhusiana na hoja aliyoitoa Mheshimiwa Charles Kagonji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema wananchi hawana matatizo kwa sababu leo hii Watanzania wanakwenda kila mahala wanapopenda bila matatizo ndiyo maana nikasema wa Kaskazini utawakuta Kusini na wa Mashariki utawakuta Magharibi, hawabaguani. Lakini tunapata matatizo kwa sababu issues hizi mara nyingi tunazihamsha sisi viongozi, ndicho nilichokuwa ninasema. Wananchi wenyewe hawana matatizo, ni kweli watu huwa wanauana lakini mara nyingine chanzo cha kuuana uko ni magomvi ya kawaida ambayo yanatokea katika jamii lakini mara nyingi tunajikuta kwamba tunayastafsiri kwamba ni matatizo ya mipaka. Sisi tunaamini kwamba wananchi Watanzania ikija kwenye suala nani yuko mahala gani hawana matatizo na suala hilo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa*
*na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - Finance and Accounts ....Shs. 164,970,600/=
Kifungu 1003 - Policy and Planning ......Shs. 170,426,000/=
Kifungu 2001 - Regional

Coordination Division ...... Shs. 21,479,252,900/=

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilipenda nipate maelezo ni hatua gani zimechukuliwa kuhusu tatizo la maji katika Mji wa Mwanga.

**NAIBU SPIKA:** Kifungu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu Na. 20, *sub vote* 2001, kifungu 250100. Mji wa Mwanga hauna maji sasa huu mwezi wa tisa (9) tatizo hili limelifikisha Serikalini tangu Oktoba mwaka jana na matatizo haya hayahusiani na kuwepo kwa fedha za Serikali katika kutekeleza majukumu na kuwapa wananchi wa Mwanga Mjini maji, tatizo liko katika utendaji. Ningependa Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ni hatua gani Serikali imezichukua ili kuhakikisha kwamba fedha ambazo tumepewa na Serikali na vifaa ambavyo tumepewa na Serikali sasa vitawapa wananchi wa Mwanga maji leo na baadaye? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Naomba kutoa maelezo kuhusiana na suala hili la maji kwa ajili ya Mji wa Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mawasiliano na Mwanga na bahati nzuri tunaye Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro hapa, maelezo yaliyopo hapa ni kwamba Mkuu wa Mkoa ameongea na *DC* na *DED* Mwanga leo, juu ya hoja ya Mheshimiwa Mbunge hususan utendaji wa Mhandisi wa Maji. *DC* amesema ile taarifa ya timu ya Mkoa iliyochunguza jambo hili itajadiliwa kwenye vikao vyao vya Wilaya na kwa kuanzia Kamati yake ya Ulinzi na Usalama kisha Halmashauri, ameomba wapewe nafasi Wilaya ya Mwanga ishughulikie jambo hili. Ananishauri nikubali Wilaya ilishughulikie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili na fedha hata zilizotolewa kipindi kilichopita zilipelekwa kwenye Halmashauri ya Mwanga, suala hili lipo kwenye mikono ya Halmashauri yenyewe. Kwa hiyo, ili mradi wanakaa wanalizungumza naamini tutapata jibu sahihi kutoka Wilayani Mwanga. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ambayo yametolewa. Lakini ningependa kueleza hapa kwamba Kamati iliyokuwa imeundwa kweli ilifika Mwanga, lakini Kamati iliundwa Desemba, 2002 halafu haikuja Mwanga mpaka ikagonja mtuhumiwa akiwa yeye mwenyewe ndiye Kaimu *DED*, ikaja akaipokea yeye, akaongea nayo yeye mwenyewe, ikaieleza matatizo yeye mwenyewe, ikazunguka, akaisindikiza, ikaondoka, yeye mwenyewe. Sasa ni vipi hata kama Kamati ya Ulinzi na Usalama itajadili, inajadili kitu gani? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mwanga tungependa tupate uhakika kwamba kweli hatua zilizochukuliwa za Serikali zitatupa maji kwa sababu mwanzo tulipoaribikiwa na maji tulipewa hela ya dharura na Serikali, fedha zile zikawa *misused*, siku ile ile pampu ilifungwa waliporudi nyumba ikakatika. Sasa Serikali imenunua pampu mbili, sasa zifungwe na watu wale wale? Ningeomba Serikali iwe inachukua *(Hapa Hakutumia Chombo)* hatua hizi kwa dhati na haraka, kwa kweli hakuna sababu wananchi wakae miezi tisa (9) hawana maji. Dar es Salaam kukikosekana maji siku moja nchi nzima inatetemeka, Mwanga mwezi wa tisa (9) hatuna maji kwa sababu ya uzembe wa watendaji na tukae tukubali kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama ilikuwa hapo kila siku. Kwa hiyo, ningependa nisikie tamko la Mheshimiwa Waziri ambalo linaweza kutatua tatizo hili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo yafuatayo: Kwamba kama nilivyosema awali tatizo hili lilikuwa Mwanga, sasa nimemsikia Mheshimiwa Mbunge, Wizara itafanya kazi yake. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - Local Government Coordination Division ...Shs. 5,706,118,100/=

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Sub Vote 2002*, kifungu kidogo 250100 pamoja na kifungu kidogo 260100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tamko au kauli ya Mheshimiwa Waziri baada ya mimi kuizungumza kwa uchungu mkubwa katika Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na yeye nikamwandikia kwa undani, naomba kusema kwa undani sikuweza kuzungumza katika hadhara, kwa undani kuhusu huyu aliyeteuliwa kuwa Mkusanyaji Ushuru Stendi ya Mailimoja alivyoweza kuwasaliti viongozi wa CCM halafu akarudi akaenda kwenye Halmashauri na Halmashauri wakamkubali ingawa na mabaya yake, nimemwelezea kwa undani.

Naomba kauli yake aniambie kwamba atawatuma watu wake ili twende tukawaone jinsi watu wanavyonyanyasika na kwa nini watu wanamkubali huyu mtu? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo yafuatayo: Ni kweli tatizo hili limeletwa kwetu na sisi tumeiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha na Halmashauri ya Mji mdogo wa Kibaha lishughulikie tatizo hili na kulitanzua. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kuna jibu la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri lakini pia Mbunge wa Jimbo hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Mbunge kuzungumza aliyoyazungumza Bungeni ambapo pia alinihusisha mimi kimakosa kwa sababu sikuisikia kabisa. Nililifuatilia suala hili kama Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha kwa Afisa Mtendaji wa Mji mdogo na pia nililizungumza suala hili kwa ufupi tu na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ambayo nimeyapata na ambayo sasa hivi Afisa Mtendaji wa Mji wa Kibaha amenipa na sasa hivi yeye yuko njiani anakuja Dodoma kuja kumwona Mheshimiwa Waziri, ni kwamba maelezo ya Mheshimiwa Mbunge aliyoyatoa hapa Bungeni hayakuwa sahihi na alishawahi kuyatoa katika Kamati ndani ya Halmashauri ya Mji mdogo akapewa maelezo na yeye kutokana na taarifa niliyopewa; na yeye pia akaandikiwa barua na kwa sababu barua ile hakuipinga, ikachukulika kwamba taarifa zile walizozitoa wao mamlaka ya Mji huo zilikuwa ni sahihi na nilithibitishiwa kwamba wako njiani kuja kumwona Mheshimiwa Waziri kwa sababu Ofisi yake ilishapiga simu Kibaha kutaka maelezo zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani wote mmesema imekwisha hiyo.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeinuka, samahani Mheshimiwa Mwenyekiti.

**NAIBU SPIKA:** Mimi ndiye ninayeongoza kikao utanisikiliza nikupe maelezo halafu kama nikupe ruksa nitakupa ruhusa. Kwa sababu katika maelezo, nimesikiliza sana maelezo nadhani Waheshimiwa Wabunge mmesikia.

Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo anasema suala hili tayari limefika Wizarani na huyu anayehusika anakuja kutaka lipatiwe ufafanuzi. Sasa tulicheleweshe Bunge zima wakati hatua hizo zinaendelea, mimi sioni ni haki kulitendea Bunge hivyo. Lakini haya endelea. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa huruma zako. Napenda kumwambia Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha sikumtaja yeye, samahani kama nimekosea. Lakini naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kibaha kwamba kumtaja yeye sikutaja kwa makosa na nina ushahidi. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Waziri ninakusihi na ninazungumza kama Mbunge wa Viti Maalum, Wanawake wala simwingilii Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msababa kwenye Jimbo lake, lakini kuna wanawake, wananchi, pamoja na mimi mwenyewe binafsi nimeathirika. Ninakuomba ukubaliane kwamba mimi niko tayari kukupa uthibitisho na ninasema kama hili lingetokea Kibaha watu wangeandama kuja hapa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, unachomtaka Mheshimiwa Waziri ni nini? Anachomtaka Mheshimiwa Waziri ili apate kujibu vizuri lieleweke wazi. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ninachomtaka Waziri asimchukue tu *DED* wa Mji Mdogo na Mheshimiwa Msabaha hapa, tunatakiwa twende Kibaha na mimi nikiwemo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ombi ndio hilo, msilimalizie hapa mwende Kibaha. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezingatia agizo lako, Wizara itashughulikia. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie *Sub Vote 2002,* kifungu kidogo cha 250100 ambayo iko kwenye *Local Government Coordination Division.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia ya kuchukua shilingi, lakini nina tatizo la kutoridhika na maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri kuhusu kuwaondoa Madiwani katika *Tender Board*. Kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Waziri kwamba kwa bahati mbaya sheria iliyopitishwa ndani ya Bunge letu ndiyo iliyompa mamlaka. Kwa hiyo, hakutumia mamlaka yake vibaya katika hilo, hilo naomba nilikubali. Lakini kifungu cha 14 cha sheria hiyo kilikuwa kimemtaja tu Mwenyekiti kwamba *Accounting Officer* ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Bodi. Kwa muda mrefu katika nchi yetu tumepiga kelele kuhusu ubadhilifu na matumizi mabaya kwenye Halmashauri. Kanuni iliyotungwa sasa Mwenyekiti ndiyo huyo Mkurugenzi, wajumbe wake ni Mweka Hazina wa Wilaya, Wakuu wa Idara akiwemo Mkuu wa Idara inayohusika na *Procurement* (manunuzi), mtu wa nje pekee ni *DAS* kutoka Ofisi ya *DC*. Mwenyekiti ana uwezo wa kuchagua au kuteua wakuu wengine wawili wa Idara ndio wanafanya *Tender Board* kamili. Ukichunguza katika *document* hii nzima tangu kuanza kuandaa zile *document,* kutangaza tenda, ku-*award tender*, kusimamia kazi, *monitoring* ya kazi yote inafanywa na timu hii chini ya usimamizi wa yule *Accounting Officer.* Kwa bahati mbaya Madiwani iwe wa Kamati ya Fedha au wa *Full Council* hawatajwi mahali popote katika *document* hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka maelezo zaidi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba iwapo hali ndio hivyo na kwa uzoefu tulionao katika vitabu vya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu kwa sasa ambapo matumizi mabaya yametoka katika maeneo haya hasa katika tenda. Sasa tumeruhusu hali hii na Madiwani tumewaweka nje na kifungu kinachofuata nafikiri ni kifungu cha 12 kinamtaka Diwani atakapohitaji *document* yoyote anahitaji na yeye kama mtu mwingine yeyote kwa sababu Diwani hatajwi mahali popote anakuwa kama mtu mwingine yeyote anatakiwa na yeye apate kwanza kibali cha *DED* kupata hiyo *document* na alipie *fee* ili aweze kupata *document* hiyo. Je, tutakuwa tumejenga kweli dhana ya Serikali ambapo tumesema tunataka kujenga uwajibikaji, uwazi, kupiga vita rushwa na ubadhilifu au tutakuwa tumeruhusu haya mambo yote yaweze kufanyika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Madiwani hawatajwi mahali popote isipokuwa Bodi hiyo inapomaliza kazi yake ni lazima ipeleke kwenye Kamati ya Fedha baada ya Kamati ya Fedha inapelekwa kwenye *Full Council.* Wanapokuwa wamekaa pale kwenye *Full Council, Full Council* ina haki ya kuhoji na kutaka *document* yoyote. Isipokuwa Waheshimiwa Madiwani wanatakiwa kufanya hivyo

anapotaka sasa kupata *document* hizo nje ya utaratibu huo ndio anakuwa kama mwananchi wa kawaida lakini *Full Council* ina haki ya kuhoji.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru nia yake njema kama ingekuwa hivyo kisheria kwamba wale jamaa wakimaliza waipeleke kwenye Kamati ya Fedha na *Full Council* kwa *document* hii ni hisani ya hiyo Tenda Bodi siyo kisheria na hakuna mahali popote wanapoambiwa kwamba lazima wai-*submit* kwenye Kamati ile. Watu wanaoambiwa kwamba itakuwa *submitted* ni *Regional Secretariat,* kwa Waziri na kwa *Central Tender Board* hao ndio wanaotajwa na sheria lakini Kamati ya Fedha wala Baraza la Madiwani halipo. Je, Waziri yuko tayari sasa kuweka *amendment* ya sheria hiyo hata kama sio leo lakini atuahidi kwamba ataleta *amendment* ili hayo aliyoyasema yaingizwe katika sheria ili tuweze kuwa na utaratibu huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakwenda kuangalia na ikikamilika basi tutaleta hapa kama ambavyo amependekeza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 56, kifungu kidogo 2002 na Kifungu kidogo zaidi 250100. Napenda Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa sababu asilimia kubwa ya Wabunge waliochangia hoja yake wamezungumza kwa uchungu sana kuhusu viwango vidogo vya posho za Madiwani. Katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri yaelekea kwamba uchungu huu yeye haukumpata vizuri. Ninachoomba kujua au alieleze Bunge lako Tukufu na wananchi kweli kwa jinsi Wabunge walivyolizungumza na sio leo tu ni muda mrefu tangu mwaka jana na mwaka juzi. Je, haoni ipo haja kubwa ya Serikali kuangalia upya Madiwani wakaongezewa posho bila kujali kwamba ni lazima walipwe kutokana na makusanyo ya Halmashauri inayohusika? Maelezo mengi yametolewa katika michango ya Waheshimiwa Wabunge. Nadhani kwa kweli sasa ni wakati muafaka wa kuliangalia suala hili likachukuliwa kama walivyochukuliwa Watendaji wa Kata na vijiji ili Madiwani hawa waweze kuwa katika hali nzuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza, suala la posho za Madiwani na chochote kile ambacho wanatakiwa kupata kwa sasa hivi sheria ilivyo kinatakiwa kitokane na mapato ya *Council* yenyewe. Nimekwishatoa maelezo kwamba sasa hivi tunachokizungumzia ni jinsi gani fedha tunazoziomba kwenye Wizara hii tunaomba zitumike, hatuna fedha za ziada. Kwa hiyo, tulichofanya ni kwamba katika kipindi cha mwaka huu wa Bajeti tutaendelea kulizingatia na itakapoonekana uwezo upo basi Serikali itachukua hatua zinazofaa.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - Institutional Development
Division ................................. Sh.2,911,211,300/=

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 63 - TUMITAA**

Kifungu 1001 - Administration and General ..Sh.681,486,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

**MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA - MIKOA**

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha ................... Sh.13,457,074,100/=
Fungu 71 - Mkoa wa Pwani .................. Sh.11,560,396,800/=
Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma .................. Sh.15,999,206,500/=

Fungu 73 - Mkoa wa Iringa ..................... Sh.16,815,931,600/=
Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma .................. Sh.11,854,188,700/=
Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro .............. Sh. 21,850,846,000/=
Fungu 76 - Mkoa wa Lindi ........................ Sh. 9,538,451,500/=
Fungu 77 - Mkoa wa Mara ....................... Sh. 14,833,966,700/=
Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya ..................... Sh. 21,623,998,800/=
Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro .................. Sh.17,101,141,200/=
Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara ................... Sh.11,323,108,000/=
Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza .................. Sh. 22,633,783,600/=
Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma ................. Sh.13,035,297,000/=
Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga ................ Sh.19,127,821,400/=
Fungu 84 - Mkoa wa Singida .................... Sh.10,770,512,600/=
Fungu 85 - Mkoa wa Tabora ...................... Sh.13,794,994,500/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 86 - Mkoa wa Tanga ....................... Sh.18,607,255,200/=

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* ya 10, *Administration, Sub Vote 1001, Administration and General*, nataka ufafanuzi sio kwa ajili ya Mkoa wa Tanga tu ni kwa ajili ya Mikoa yote. Kuna chombo kiliundwa kisheria hapa katika Sheria ya *Regional Administration, Regional Consultative Council*. Labda pengine Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala imeona katika *memorandum* suala hili limewekewa vifungu isipokuwa hapa halionekani maana yake nimepitia Wizara zote mpaka kufika hapa.

Nimesimama Tanga kwa sababu ndiko ninakotoka lakini nimetazama Mikoa yote sikuona *Regional Consultative Council* zimetajwa mahali popote na hivi ni vyombo vya kisheria. Sasa tunataka maelezo. Tusiwabane ma-*RC* kumbe hakuna kifungu kilichowekwa *specifically* kwa ajili ya hiyo. Wana mambo mengine muhimu kuliko hiyo *Regional Consultative Council*. Kwa hiyo, tunataka maelezo katika hii kwa Mikoa yote *unless* Wabunge wenzangu mmeona katika Mikoa yenu.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu kifungu ulichoulizia ni cha Tanga, basi atajibu lakini jibu linaweza ku-apply kwingine maana vifungu vingine tayari tumepitisha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hapa hakuna fungu linaonekana kwa ajili ya kugharamia RCCs lakini kwa muda wote huu tokea imeanza ilikuwa inagharamiwa kutokana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Sasa tutaangalia inawezekana katika mwaka wa fedha ujao kama upo uwezekano basi itatengewa fedha kwa kibali cha Hazina.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 87 - Mkoa wa Kagera ..................Sh.16,859,200,400/=

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki, kuna wakati nilimwuliza Waziri hasa katika hizi hela nyingi zilizotolewa kwa ujenzi wa barabara na zile *Local Council* ambazo ziko pale.

Kwenye Jimbo langu lenye watu laki mbili na zaidi, Wilaya yenye watu 430,000 hela zote za kitu kinachoitwa *KAHEMP* hawajawahi kutoa pesa kujenga barabara kwenye Jimbo langu. Sasa hata kama Waziri hawezi kujibu hapa yuko tayari kulipokea hilo na kulifanyia uchunguzi kwamba bilioni za hela zimepelekwa pale na wafadhili na kwenye Jimbo langu hawataki kushughulikia barabara yoyote ile?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutengeneza barabara katika Halmashauri, mara nyingi *priorities* zinatolewa na Halmashauri yenyewe na fedha zinatengwa kulingana na *priorities* hizo. Sasa ninachoweza kushauri katika suala hili ni kwamba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu na yeye vile vile ni Mheshimiwa Diwani ahakikishe kwamba barabara hizo anazozizungumzia zinawekwa kwenye *priority* za Halmashauri yake.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaniwia radhi sitaki kuchelewesha kikao chako, lakini ninachojaribu kusema ni kwamba niliuliza swali na alinijibu Mheshimiwa Pinda pale kwamba kule kwangu kuna barabara Kata zote 11 zenye nusu huku Jimbo langu na huku Jimbo langu hela zote wakipata wanatengeneza kwenye Jimbo lao na wanachosema na nilimweleza hapa Waziri akaniambia Serikali haifanyi kazi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini hivyo kwamba Serikali haiwezi kusema pale kuna Mbunge wa Chama kingine, sasa ninachouliza Waziri yuko tayari kufuatilia kwamba hela zote zile hazijawahi kujenga barabara hata moja kule kwenye Jimbo langu? Sio suala la *priority* kwa sababu *priority* haliwezi kuwa kwenye eneo moja la Wilaya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kweli Mheshimiwa Mbunge anavyosema lipo tatizo hilo. Lakini Wizara haiwezi kwenda kuingilia utaratibu wa *Council*, utaratibu unategemea *Council* ina-*lay priority* zake vipi.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam .................. Sh.17,849,403,600/=
Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa ............................ Sh.10,364,391,700/=
Fungu 95 - Mkoa wa Manyara .......................... Sh.10,942,957,600/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 56 - Ofisi ya Rais - TAMISEMI

Kifungu 2002 - Local Government Coordination Division ............. Sh.134,016,701,400/=

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba maelezo, sina sababu ya kuchukua shilingi ya Mheshimiwa Waziri, Kifungu cha 2310, *program 2002, Local Government Coordination Division.*

Katika mchango wangu wa mdogo pamoja na maandishi labda kwa sababu ya muda Waziri hakupata muda wa kufafanua nilitaka kupata uhakika kwamba kwa kuwa Halmashauri nyingi zilikuwa zinategemea fedha zile za kodi baada ya kuzifuta bila shaka kutakuwa na mpango wa kujaza pengo lile, nilitaka uhakika kwamba lile pengo limewekwa kwenye fungu gani kwa sababu nimepitia kitabu cha *supply* na kitabu cha maendeleo sikuona fungu hata moja.

Sasa kwa kuwa hapa ni mahali pa pili labda ningepata tu uhakika kwamba hizi fedha ambazo zitapelekwa zimewekwa kwenye kifungu gani na ni vigezo gani vitatumika katika kupeleka fedha hizo kwenye Halmashauri mbalimbali ziwe za mji, Manispaa au Jiji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kuziba pengo la fedha iliyokuwa ipatikane kutokana na Kodi ya Maendeleo, Serikali imetenga shilingi bilioni nne, uchambuzi bado unaendelea na tunaamini kwamba jinsi tunavyoendelea hali itakuwa inadhibitiwa.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ufafanuzi nilimwandikia Mheshimiwa Waziri ili nipate ufafanuzi wa majengo yaliyojengwa...

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Kifungu cha 6403, *PEDP*.

**MWENYEKITI:** Eeh, maelezo.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Katika majedwali aliandika kwamba Halmashauri ya Monduli majengo ni 24 yaliyokamilika 12 yanayoendelea ni nane.

Ninataka ufafanuzi kwa sababu tumejenga majengo zaidi ya 175 yaliyokamilika ni mengi na ambayo hayajakamilika bado ni mengi. Nashangaa kuona katika majedwali ni tofauti kabisa na kazi iliyofanyika huko kwenye Wilaya yetu. Nataka ufafanuzi kujua *data* hizi zikoje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni matatizo ya takwimu tu, zitarekebishwa.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 3001 - Institutional Development Division ... Sh.100,000,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 70 - Mkoa wa Arusha ..................... Sh.1,667,037,000/=
Fungu 71 - Mkoa wa Pwani ..................... Sh.1,097,657,600/=
Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma ................. Sh.1,170,135,400/=
Fungu 73 - Mkoa wa Iringa ..................... Sh.4,066,954,600/=
Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma .................. Sh. 372,539,800/=
Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro ............ Sh.1,014,790,000/=
Fungu 76 - Mkoa wa Lindi .................... Sh. 928,972,800/=
Fungu 77 - Mkoa wa Mara ..................... Sh.1,139,853,600/=
Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya ................... Sh.3,694,427,800/=
Fungu 79 - Morogoro ............................ Sh.3,644,744,800/=
Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara ................... Sh.1,648,879,200/=
Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza ................ Sh.2,064,613,900/=
Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma ................ Sh.1,286,655,900/=

| | |
|---|---|
| Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga .............. | Sh. 527,718,900/= |
| Fungu 84 - Mkoa wa Singida................... | Shs. 337,495,900/= |
| Fungu 85 - Mkoa wa Tabora .................. | Shs. 621,150,500/= |
| Fungu 86 - Mkoa wa Tanga .................. | Shs. 1,729,627,000/= |
| Fungu 87 - Mkoa wa Kagera.................. | Shs. 5,444,646,600/= |
| Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam ...... | Shs. 240,011,900/= |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa..................Shs. 318,897,300/=

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki *Vote 89, Sub Vote 101.* Mwaka jana nilizungumzia kuhusu suala la Mkoa wa Rukwa kutopata fedha za Maendeleo kama Mikoa mingine na nikaambiwa kwa sababu hatupati fedha za nje. Mimi nilichoomba kama Afisa Mipango katika Mkoa wa Rukwa hana uwezo wa kuandika *project write-ups* kama Mikoa mingine aondolewe. Lakini kama ni kazi ya Wizara ya Mipango kufanya kazi hiyo au Wizara ya TAMISEMI basi na Mkoa huu nao uweze kupatiwa fedha za kutosha. Wakati nikichangia Wizara ya Fedha na wakati nikichangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu suala hili nimelizungumza. Majibu yaliyotokea ni kwamba fedha nyingine zimejificha, hazionyeshwi hapa na mimi nikasema kama katika Mkoa wa Rukwa fedha nyingine zimejificha hata katika Mikoa mingine ambayo fedha zilizoonyeshwa ni bilioni tano au nne, kuna fedha zilizojificha. Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba ni maelezo. Wizara ya TAMISEMI pamoja na Serikali yote inafanya nini ili kuweza kurekebisha tatizo hili siyo katika Mkoa wa Rukwa bali hata Mikoa ya Kigoma, Tabora, Shinyanga pamoja na Mkoa wa Singida.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo ilikwishaelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba sasa hivi timu zitakwenda kwenye Mikoa yote ili kuangalia vigezo vya jinsi gani fedha zitakuwa zinagawanywa kwenye Mikoa. Kwa hiyo, tusubiri timu hiyo itakapotuletea maoni yake.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo ni wazi kwa sababu takwimu zinaonyesha waziwazi. Sasa hii ya kusema tunaunda Tume sijui waende wakaangalie, ni mbinu tu ya kujaribu kutafuta kupoteza muda ili mwakani nianze kuambiwa labda pengine takwimu hizi au Tume haijaleta taarifa. Hili ni jambo la uhakika na ni jambo la uwazi ambalo naomba Serikali itoe tamko hapa ieleze ni kwa nini hatupewi hata fedha za ndani kwa maendeleo. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala nilikuwa sikueleza kwamba kuna fedha zilizojificha. Nilisema tu kuna miradi ambayo haionekani katika vitabu fulani bali zinakuwa katika sekta zile zinazohusika. Lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Bajeti ijayo tutakuwa tumekusanya miradi yote ya kila Mkoa na itaonekana wazi. Kwa hiyo, hili jambo tutalisimamia kikamilifu katika miradi ijayo kama nilivyoeleza hapa, nimesema ni kweli kuna Mikoa ambayo inawezekana fedha zisiwe kidogo kiasi hiki, lakini ni kweli hailingani. Kwa hiyo, tutakwenda kuangalia vizuri zaidi ili tuweze kuweka *balance* nzuri katika maendeleo kwa nchi nzima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwananzila baada ya Serikali yenyewe kutoa maelezo haya bado tena hujaridhika?

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru kwa hayo aliyosema. Lakini nilichozungumza katika suala hili kama Mkoa hauna Maafisa au Wataalam wanaoweza kuandika taarifa za kuweza kuufanya Mkoa uweze kupata fedha za kutosha mbona suala hili hawajataka kulizungumzia au ni Serikali yenyewe ndiyo inafanya kazi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwananzila na Waheshimiwa Wabunge, nadhani hili limeeleweka.

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**MWENYEKITI:** Taratibu, taratibu na mimi ni Mbunge mwenzenu hilo ninajua na mimi natoka huko huko Ruvuma, lakini lazima tuwe wakweli kwamba Serikali inayoongozwa na Waziri Mkuu, imesema italitazama hili kwa upana wake na matatizo yake watajaribu kuyasahihisha. Sasa ni pamoja na Wataalam na nini. Mimi ningemwomba sana Mheshimiwa Mwananzila kwa leo aridhike na jibu hilo ili tuwape nafasi Serikali ifanye kazi yake kwa kuzingatia madai yetu hapa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 95 - Mkoa wa Manyara ...... Shs. 2,474,146,700/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla ya kutoa taarifa nitoe sahihisho kidogo tu kwamba wakati nataja majina ya wachangiaji nililitaja jina la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji kama Haji Mwinyi Haji naomba sahihisho lifanyike ili iwe Dr. Haji Mwita Haji. Baada ya kutoa sahihisho hilo sasa naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia makadirio ya matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makisio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2003/2004 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijaahirisha kikao mpaka Jumatatu nina tangazo moja kutoka kwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, yeye anasema mmepewa Waheshimiwa Wabunge mialiko ya kwenda kwenye Saba Saba na kadi zitatumwa kwenye *pigeon hole*. Zimeanza kugawiwa leo usiku kwa wale ambao watapata nafasi. Huo ni mwaliko kutoka kwa Wizara hiyo. Baada ya tangazo hilo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.10 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 30 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*